Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Tano – Tarehe 10 Mei, 2014**

*(Mkutano Ulianza Saa tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa Zungu Azzan) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA NA MUUNGANO):**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano) kwa mwaka wa Fedha 2014/2015.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa fedha 2014/2015.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. SAID JUMA NKUMBA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha

2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2014/2015 Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu bada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo inayohusu Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, sasa lijadili na kukubali kupitisha makadirio ya matumizi ya kawaida na maendeleo ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, kwa Mwaka 2014/2015.

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa na Afya njema ili tuweze kujadili Bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania ambao wengi wao ni wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze moja kwa moja kuzungumzia hali ya Kilimo na Ushirika ambayo katika hotuba yangu inapatikana kwenye ukurasa wa tano mpaka wa nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni moja ya sekta muhimu katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu kwa kuwa inatoa ajira kwa asilimia 74 ya Watanzania na inachangia zaidi asilimia 100 ya chakula kinachopatikana nchini katika miaka yenye mvua za kutosha. Katika mwaka 2013 sekta ya kilimo ilichangia asilimia 24.7 ya pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 24.8 mwaka 2012. Mchango mkubwa katika pato la Taifa ulitokana na shughuli za huduma ambazo zilichangia asilimia 44.3 ikifuatiwa na sekta ya kilimo. Kwa kuwa asilimia kubwa ya Watanzania wanashiriki katika shughuli za kilimo, mchango huo kwa kiasi kikubwa utachangia katika kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pato la Taifa kwa mwaka 2013 kwa shughuli za kiuchumi za kilimo zinazojumusha mazao, ufugaji, misitu na uuwindaji vimekuwa kwa asilimia 4.3 sawa na ilivyokuwa katika mwaka 2012. Katika ukuaji huo, mchango wa mazao ulikuwa asilimia 4.5 ikilinganishwa na asilimia 4.7 ya mwaka

2012. Katika kipindi hicho uzalishaji wa mazao ya chakula hususan nafaka, uliongezeka kutoka tani milioni 6.7 mwaka 2012 hadi tani milioni 7.6 mwaka 2013, ikiwa ni sawa na ongozeko la asilimia 13.4.

Aidha, uzalishaji wa mahindi uliongezeka kutoka tani milioni 5.1 mwaka 2012 hadi milioni 5.2 mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 2. Uzalishaji wa mchele uliongezeka kutoka tani miloni 1.2 mwaka 2012 hadi tani milioni 1.3 mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile uzalishaji wa mazao ya chakula yasiyo nafaka ulikuwa ni tani milioni 6.8. Uzalishaji huo wa mazao ya chakula wa tani milioni 12.1 katika mwaka 2013/2014 unaonyesha kuwepo kwa ziada ya tani milioni 2.2 za chakula. Ongezeko hilo ambalo limetokana na kuwepo kwa mvua za kutosha na juhudi za Serikali za kuboresha uzalishaji kwa kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima limeleta utoshelevu wa chakula nchini kwa asilimia 118.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji kimechangia asilimia 24 katika utoshelevu huo. Aidha, utoshelevu huo umechangia kushuka kwa bei za vyakula na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza mfumuko wa bei katika bidhaa kutoka asilimia 12.1 mwezi Januari, 2013 hadi 6.1 Mwezi Machi, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Chakula. Kwa ujumla hali ya upatikanaji wa chakula katika mwaka 2013/2014 ilikuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi ya nchi kufuatia mavuno mavuno mazuri ya msimu wa kilimo wa mwaka 2012/2013. Tathimini iliyofanyika mwezi Julai na Agosti, 2013 inaonyesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo 2012/2013 ulikuwa tani milioni 14,383,845 zikiwemo tani milioni 7.6 za nafaka na tani milioni 6.7 za mazao yasiyo nafaka. Kiasi hicho cha chakula kikilinganishwa na mahitaji ya chakula ya tani milioni 12.14 katika mwaka 2013/2014 kinaonyesha kuwepo kwa ziada ya tani milioni 2.2 za chakula. Ziada hiyo ni pamoja na tani 350,000 za mahindi na tani 466,821 za mchele. Kutokana na hali hiyo, Taifa lilijitosheleza kwa chakula kwa asilimia hiyo niliyoitaja 118.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hali ya chakula kuwa ya kurudhisha kulikuwa na baadhi ya maeneo yenye upungufu wa chakula kutokana na kutopatikana kwa mavuno ya vuli, kufuatia mvua za vuli kutonyesha vizuri katika maeneo mengi yanayopata mvua hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathimini ya kina ya hali ya chakula na lishe iliyofanyika Mwezi Oktoba, 2013 ilibaini kuwepo kwa jumla ya watu 828,063

waliokuwa na upungufu wa chakula kiasi cha tani 23,312 za chakula na tayari chakula hicho kimekwishatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuanza msimu 2013/2014, Hifadhi ya Taifa ya Chakula yaani *NFRA* ilikuwa na akiba ya nafaka ya tani 25,455. Katika mwaka 2013/2014, NFRA ilinunua tani 219,377 nakufanya jumla ya akiba ya nafaka kuwa tani 244,830 ambayo inaendelea kugawiwa kwenye maeneo yenye upungufu na taasisi za Umma.

Aidha, katika kipindi cha kuanzia Julai 2013 hadi tarehe 4 Aprili, 2014 *NFRA* imetoa jumla ya tani 32,711 ili kukabiliana na upungufu wa chakula. Tani 14,491 zimeuzwa kwa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani yaani *WFP* na tani 2,881 zimeuzwa kwa taasisi za Umma. Hadi kufika tarehe 2 Aprili, 2014 akiba katika maghala yote ya *NFRA* ni tani 194,747 za nafaka ikiwa na maana kwamba tuna chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mwenendo wa hali ya mvua kuwa nzuri katika msimu wa 2013/2014, katika maeneo mengi ya nchi kuna matarajio ya kupata mavuno mazuri ya mazao ya chakula katika msimu 2014/2015. Hata hivyo, hali halisi ya chakula itajulikana baada ya kufanya tathimini katika mwezi Juni 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za awali zinaonyesha kwamba, mvua zimenyesha vizuri katika nchi nyingine za Ukanda wa Afrika Mashariki, hali hii inaashiria kuwepo kwa mavuno mazuri katika nchi hizo na hivyo kuwepo kwa uwezekano wa kupunguza soko la chakula kinachozalishwa nchini. Hali kama itakuwa hivyo, Serikali inawashauri wakulima na wafanya biashara kutafuta masoko ndani na nje ya nchi na hapa napenda kusisitiza kwamba, Serikali haitawazuia wananchi na wakulima kuza chakula chao ndani na nje ya nchi mradi wafuate sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Ushirika. Kwa ujumla hali ya Ushirika nchini imekuwa siyo ya kuridhisha na hivyo kusababisha wanaushirika na wananchi kwa ujumla kutokuwa na imani nao.

Changamoto za Ushirika ni pamoja na ukosefu wa mitaji, uongozi mbaya, ubadhirifu na upotevu wa fedha za umma. Elimu duni ya ushirika miongoni mwa wana ushirika na udhaifu katika usimamizi wa maendeleo ya ushirika. Kutokana na hali hiyo, Vyama vya Ushirika vimeshindwa kutoa huduma zilizotarajiwa kwa wanachama wake na hivyo kukosa mvuto kwa wananchi wengi kujiunga nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufufua Ushirika katika mwaka 2013/2014 Wizara yangu ilianza kuchukua hatua za muda mfupi na mrefu kukabiliana na matatizo ya Ushirika nchini. Miongoni mwa hatua za muda mfupi zilizochukuliwa ni pamoja na kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa vyama vya ushirika ambapo

Wizara imewapatia mafunzo Maafisa Ushirika 45 na kufanya ukaguzi katika Vyama vya Ushirika vya Msingi 252 na Vyama Vikuu 3 vya Mikoa ya Singida, Tabora na Ruvuma. Hatua za kisheria zimeanza kuchukuliwa dhidi ya wote walkiobainika kufanya ubadhilifu wa mali za vyama. Serikali imewavua madaraka Warajisi Wasaidizi wa Mikoa watatu walioshindwa kutimiza wajibu wao na kuteuwa wengine wapya. Tutaendelea kuwavua wengine wote watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo. Aidha, viongozi wa vyama waliofanya ubadhirifu nao wameamuliwa kufidia hasara walizosababisha katika vyama vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza ufanisi katika ukaguzi wa vyama vya ushirika. Serikali inaendelea kujenga uwezo wa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika yaani *COASCO* kwa kuteuwa bodi mpya ya wakurugenzi na kuongeza idadi ya Wakaguzi 29. Serikali imeanza kumtumia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yaani *CAG* kufanya ukaguzi maalum katika Vyama vya Ushirika wa Tumbaku katika Mkoa wa Tabora hasa niseme tukianza na Mkoa wa Tabora na tutaendela hata Mikoa mingine kuvikagua vyama ambavyo vimedhaminiwa na Serikali kukopa kwenye Mabenki. Matokeo ya Ukaguzi huo wa *CAG* unaendelea yataiwezesha Serikali kuchukua hatua stahiki kwa wale wote watakaobainika kuhusika na ubadhirifu katika Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine zilizochukuliwa na Serikali dhidi ya Wabadhirifu ni kuwafikisha kwenye vyombo vya Sheria baadhi ya Wajumbe na Watendaji wa *Wazalendo SACCOS, Vigen SACCOS, APEX* ya Tumbaku na vyama vya mingi katika Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za muda mrefu ambazo zimechukuliwa ni kutungwa kwa sheria ya vyama vya Ushirika namba sita ya mwaka 2013 ambayo imeanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Sheria hiyo imeanisha majukumu ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika maeneo mawili, yaani eneo la usimamizi ambalo utekelezaji wake utafanywa moja kwa moja na Tume yenyewe, kuanzia ngazi ya Taifa hadi Wilayani na Majukumu ya uhamasishaji ambayo yataelekezwa kwa ushirikiano kati ya Tume na Wizara za kisekta, Halmashauri ya Wilaya, na wadau wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vyama vya Ushirika ambavyo vimeshindwa kutoa huduma kwa wananchama wake katika hali hiyo kukosesha mvuto, vitashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hiyo ya Vyama vya Ushirika imeboreshwa na kuongeza makali ya adhabu kwa wabadhirifu kuondoa mgongano wa maslahi baina ya uongozi wa Ushirika na Uongozi wa Kisiasa na Umma na kurekebisha muda wa uongozi katika Vyama vya Ushirika kutoka miaka tisa hadi

sita. Aidha, Sheria mpya ya Ushirika ilianza kutumika tarehe 1 Januari, 2014. Rasimu ya Kanuni ya kutekeleza sheria hiyo tayari imeandaliwa na kujadiliwa na wadau ili ziweze kutumika na kuanza kutumika rasmi katika mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imefanya tathimini ya hali ya Vyama vya Ushirika nchini na kubaini kuwepo kwa Vyama vya Ushirika Mfu 360 ambavyo vilikuwa havitekelezi majukumu yao kwa mujibu wa Sheria. Vyama hivyo vimefutwa katika daftari la Usajiri ili kukidhi matakwa ya sheria. Ufutaji huo umefanya idadi ya Vyama vya Ushirika kupungua kutoka vyama 9964 mwezi Machi, 2013 hadi vyama 9604 Mwezi Machi, 2014.

Kuanzishwa kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika ambayo kwa mujibu wa Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika, itatekeleza majukumu ya usimamizi mpaka ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mtaa, kutaimarisha usimamizi na udhibiti wa shughuli za vyama vya Ushirika na hivyo kupunguza matatizo yaliyojitokeza hapo awali. Sheria mpya ya Ushirika inaruhusu kuanzishwa kwa vyama vipya vya Ushirika zaidi ya kimoja katika eneo moja ili mradi tu viwe na nguvu ya kiuchumi jambo ambalo litaongeza ushindani katika tasinia hii ya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya *SACCOS* hadi Machi, 2014 ilikuwa 5478 ikilinganishwa na 5559 mwaka 2013. Hivyo kupunguza idadi ya wanachama kutoka 1,153,248 hadi kufikia wanachama 935,121. Katika kupanua kiwango cha huduma za kifedha jumuishi nchini yaani financial inclusion *SACCOS* zimeendelea kuimarishwa ili ziweze kutoa huduma za kifedha kwa wananchi wengi zaidi hususan wale walioko vijijini. Wizara imeandaa mkakati wa kuimarisha *SACCOS* ambao unatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja, yaani financial sector deepening trust na marketing infrastructure value addition. Aidha, hisa, akiba na amana za wananchama zimepungua kutoka bilioni 463.5 kutoka Machi, 2013 hadi shilingi bilioni 451.1 mwezi Machi, 2014 mikopo iliyotolewa kwa wananchama bilioni 778.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza takwimu hizi zinaonyesha kushuka ambayo ndiyo dalili mbaya ya Ushirika kwamba haufanyi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyama vya Ushirika wa Mazao vimeendelea kutoa huduma kwa wakulima zikiwemo huduma za Ugani, Usambazaji wa pembejeo, ukusanyaji na uuzaji wa mazao. Wanachama 45,280 katika mikoa 9 ya Mbeya, Mtwara, Lindi, Mara, Kilimanjaro, Mwanza, Morogoro, Manyara na Singida wameendelea kunufaika na mfumo wa stakabadhi za maghala kwenye mazao ya Mpunga, Mahindi, Korosho, Kahawa, Alizeti kupitia vyama vya Ushirika vya Msingi vya mazao 368 na SACCOS 35. Changamoto kubwa ambayo Serikali inaipata na kuifanyia kazi sasa ni uwezo mdogo wa wanaushirika kuendesha shughuli zao kwa ufanisi ili kurejesha imani ya wanachama katika vyama vyao vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niruhusu nizungumzie matumizi ya fedha katika kipindi cha mwaka 2013/2014, ambayo katika hutuba kubwa yanapatikana kuanzia ukurasa wa 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuri, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu ilikadiria kukusanya mapato ya shilingi bilioni tatu, mia moja sabini na tisa milioni na kumi elfu, kutokana na vyanzo mbalimbali.Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi bilioni moja mia saba na nane milioni, mia moja tisini na mbili elfu, mia tatu sabini na nane, sawa na asilimia 53.73 ya makadirio.

Matarajio ya ukusanyaji wa maduhuli hayataweza kufikia kutokana na kupungua kwa soko la chakula katika nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizoidhinishwa, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu ilitengewa jumla ya shilingi bilioni mia tatu hamsini na tano, sitini na saba milioni mia saba kumi na tatu elfu, kupitia fungu 43 na fungu 24 kama ifuatavyo:-

Fungu 43, zilikuwa shilingi bilioni mia tatu arobaini na tisa, milioni mia mbili themanini na nne, mia sita na nane elfu. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni mia mbili sitini na nane, milioni mia mbili arobaini na nne, mia tatu ishirini elfu, zilikuwa za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni themanini na moja, milioni arobaini, mia mbili themanini na nane elfu zilikuwa fedha za matumizi ya ndani.

Fungu 24, lilitengewa shilingi bilioni tano, milioni mia saba themanini na tatu mia moja na tano elfu, zote zikiwa fedha za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Bajeti ya kawaida, kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa kutoka hazina hadi tarehe 31 machi, 2014 ni shilingi bilioni mia moja sabini na mbili, milioni mia nne hamsini na moja, mia sita tisini na nne elfu mia sita themanini na sita, sawa ma asilimia sitini na tatu ya fedha zilizoidhinishwa.

Matumizi yalifikia shilingi bilioni mia moja sabini na moja, milioni miasana na kumi, mia moja thelathini na nne elfu na mia nane thelathini na nane, sawa na asilimia 99.57 ya fedha zote zilizotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya fedha za bajeti, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu ilitengewa jumla ya shilingi bilioni themanini na moja arobaini milioni mia mbili themanini na nane elfu, kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni ishirini na tatu, mia tisa ishirini na

saba milioni ni fedha za ndani na shilingi bilioni hamsini na saba, mia moja kumi na tatu milioni mia mbili themanini na nane elfu ni fedha za nje.Programna miradi iliyotekelezwa imeonyeshwa katika hutubayangu ndefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014, shilingi bilioni arobaini, mia nane thelathini na moja milioni mia mbili ishirini elfu, mia mbili arobaini na sita, zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo, sawa na asilimia 50.38 ya fedha zilizoidhinishwa.

Matumizi yalifikia shilingi bilioni ishirini na sita, milioni mi atisha sitini na moja mia sita ishirini elfu na themanini na saba, zikiwa ni sawa na asilimia 66.03. matumizi kidogo ya fedha zilizotolewa yamesababishwa na kuchelewa kutolewa fedha kulingana na mpango kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa uniruhusu nizungumzie malengo, mafanikio na changamoto za utekelezaji katika mwaka 2013/2014, ambayo yanapatikana katika hotuba ndefu kuanzia ukurasa wa 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo, utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2013/2014, ulizingatia malengo yaliyomo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa, yaani *Big Results Now (BRN)* na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010.

Malengo hayo yalitekelezwa kupitia kupitia Program ya kuendeleza sekta ya kilimo, *program* ya mageuzi na *Modernization* ya Ushirika na Mpango wa Kukuza Kilimo katika ukanda wa Kusini mwa Tanzania, yaani *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha utekelezaji, Wizara imetekeleza malengo mkakati, yaani *strategic objectives* tisa, kupitia fungu 43 na 24, ambayo yametekelezwa na idara, vitengo, asasi na taasisi za Wizara. Mikakati hiyo na malengo hayo, yameonyeshwa kwa kirefu katika hotuba yangu ndefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie utekelezaji wa malengo ya mikakati hiyo kwa mwaka 2013/2014, ambayo yameonyeshwa kwa ufasaha katika hutuba ndefu, kuanzia ukurasa wa 17 mpaka wa 73.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza tija na uzalishaji wa maza ya kilimo, ili kufikia malengo mkakati yaliyoanishwa katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu ilitekeleza yafuatayo:-

Moja, upatikanaji wa pembejeo za kilimo, makisio yamahitaji ya pembejeo za kilimo za aina mbalimbali, yalikuwa tani mia nne hamsini na mbili

elfu mia mbili na mbili za mbolea, tani elfu sitini za mbegu bora na tani mia tatu ishirini na nane elfu, mia tano themanini na sita elfu za viuatilifu.

Hadi kufikia Aprili, 2014, upatikanaji wa mbolea ulifikia tani mia tatu arobaini na tatu elfu mia sita thamanini na saba, na viuatilifu tani elfu sita mia tano thelathini na nane, na lita themanini na saba elfu mia sita themanini na mbego bora tani thelathini na mbili elfu mia tatu thelathini na tisa nukta tisa.

Kati ya hizo, tani elfu ishirini mia tano kumi na saba, zilizalishwa hapa nchini na tani elfu kumi na moja mia nane ishirini na mbili nukta nane, ziliingizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa pembejeo bado ni mdogo, ikilinganishwa na mahitaji, ili kuongeza upatikanaji wa pembejeo za kilimo, Serikali itaongeza uzalishaji wa mbegu bora katika mashamba yake, na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi kuwekeza katika kuongeza upatikanaji wa pembejeo hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mbmbegu na miche bora, Wizara yangu kupitia wakala wa mbegu za kilimo, yaani *Agricultural Seed Agency, (ASA),* ilizalisha tani elfu tatu mia nne tisini na tano za mbegu bora za nafaka, mikunde na mboga, vipando bora za mhungo milioni kumi na saa mia tano ishilini elfu na miche ya matunda hamsini na tano milioni mia moja sitini na tano elfu mia mbili hamsini na moja, kwa kushirikiana na JKT na Jeshi la Magereza.

Aidha, *ASA,* ilishirikiana na sekta binafsi katika uzalishaji wa mbegu bora tani elfu tatu mia tisa tisini na saba za mbegu za mahindi katika shamba lake la Mbozi. Wizara pia kupitia *ASA,* imezijengea uwezo kampuni binafis za mbegu za kizalendo 14, kwa kuzipatia mafunzo ya teknolojia ya uzalishajiwa mbegu bora kuwezesha kuhudhuria makongamano ya mbegu na kufanya ziara za mafunzo katika nchi za Kenya na Uganda. *ASA* pia imeingia ubia nataasisi ya *Clinton Development Foundation* ya Marekani, katika uzalishaji wa mbegu bora za soya na mahindi kwa kutumia shamba la mbegu la Dabaga. Natumia nafasi hii kuwaomba wadau wote wa tasnia ya mbegu, kutumia fursa hii ya sekta binafsi kuingia ubia na *ASA* Katika miradi ya uzalishaji wa mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia ilisimamia na kufuatilia uzalishaji wa mbegu za daraja la kuazimiwa, yaani *quality declared seeds,* ambapo jumla ya tani mia tatu hamsini na nne za mbeugu bora, zimezalishwa na kuchangia katika upatikanaji. Kazi hii itaendelea katika msimu wa 2014/2014, ambapo tani mia nne hamsini, za mbegu za ubora za kuazimiwa za mahindi, mtama, alizeti, mpunga na maharage zitazalishwa.

Aidha, wakala wa wakulima wadogo wa chai, wamezalisha miche bora ya chai milioni moja nukta saba na taasisi ya utafiti wa kahawa, yaani TaCRI, ilizalisha miche ya kahawa mia tatu hamsini elfu na kuisambaza kwa wakulima kwa utaratibu wa ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu wa 2014/2015, ASA kwa kushirikiana na wakulima wa mkataba, JKT na Magereza, itazalisha tani elfu nne mia mbili za mbegu bora za nafaka, mikunde na mbogamboga, pingili za mhugo milioni 16 na miche bora ya matunda milioni 15.

Aidha *ASA* kwa kushirikiana na sekta binafsi, itazalisha tani elfu nne mia mbili za mbegu za nafaka na tani mia tano kupitia ubea kati ya *ASA* na taasisi hiyo ya *Clinton Development Foundation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu sasa nizungumzie mpango wa ruzuku ya pembejeo, katika mwaka 2013/2014, Wizara ilitoa ruzuku ya pembejeo za kilimo tani mia moja ishirini na nne elfu mia sita themanini na tano za mbolea na tani elfu tisa mia sita ishirini na moja za mbegu kwa kaya mia tisa themanini na mbili elfu na mia moja.

Utaratibu huo umesaidia wakulima kuongeza tija ya uzalishaji wa mahindi kutoka magunia matano kwa ekari hadi wastani wa gunia 15 na mpunga kutoka gunia nne kwa ekari hadi wastani wa gunia 20.

Pamoja namafanikio mazuri ya mpangu wa ruzuku, kumekuwepo na changamoto katika ngazi mbali mbali ikiwemo ubadhirifu, upotevu wa vocha na ucheleweshaji wa vocha, hali iliyosababisha wakulima kushindwa kupata pembejeo mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia changamoto hizo, Serikali katika kuanzia msimu wa 2013/2014, ilibuni utaratibu mpya wa kutoa pembejeo za mbolea, mbegu za mahindi na mpunga, kwa vikundi vya wakulima na Vyama vya Ushirika, kwa kutumi amikopo kupita taasisi za fedha.

Kwa utaratibu huu, Serikali kwa upande wake, ilijipanga kutoa dhamana ya asilimia 50 ya mahitaji ya pembejeo na wakulima walitakiwa kuchangia asilimia 20 awali kama dhamana ya mikopo ili benki nazo ziwakopeshe mara mbili ya dhamana hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huo kwa bahati mbaya haukutekelezwa kutokana na taasisi za fedha, kuweka sharti kwa Serikali, kuweka fedha taslimu kama dhamana kabla ya kutoa mikopo hiyo, jambo ambalo halikuwezekana.

Katika mwaka wa 2014/2015, Serikali itaendelea kufanya mazungumzo na taasisi za fedha zilizo tayari kutekeleza utaratibu huu, ili changamoto zilizojitokeza katika msimu uliopita zisijirudie tena.

Aidha, Wizara inafanya mazungumzo na makampuni ya pembejeo kuangalia uwezekano wa makampuni hayo kuwakopesha wakulima moja kwa moja ili kuongeza upatikanaji wa pembejeo katika msimu 2014/2015. Maana yake, kwa maelezo yangu haya, utaratibu ule wa ruzuku kupitia vocha, sasa tumeuacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa ubora wa mbolea, mamlaka ya udhibiti wa mbolea Tanzania, yaani TFRA, ilisajili na kutoa leseni kwa wafanyabishara mia tano thelathini na tatu wa mbolea na bidhaa zingine zinazohusiana na mbole, kwa msaada wa mradi wa *AGRA*,wakaguzi mia moja wa mbolea kutoka katika mikoa 26, tayari wamepewa mafunzo na kutangazwa katika gazeti la Serikali.

Vilevile mamlaka imefanya ukaguzi wa mbolea katika mikoa ya Ruvuma, Njombe, Iringa, Rukwa, Mbeya, Dar es Salaam na Morogoro na kubaini kuwa tani 36.7 za mbolea zilikuwa chini ya kiwango. Hatua za kisheria zilichukuliwa dhidi ya makampuni yaliyokutwa na mbolea hizo na utaratibu wa kimataifa unaozingatia masuala ya mazingira unafaywa ili kuziteketeza mbolea hizo ambazo ziko chini ya kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti wa ubora wa mbegu, Wizara yangu kupitia taasisi ya udhibiti wa ubora wa mbegu yaani *TOSCI*, ilikagua hekta elfu nane mia moja ishirini za mashamba ya mbegu bora za madaraja yote. Ilipima sampuri elfu moja mia nane na hamsini na kubaini ubora wa mbegu, ilithibitisha vigezo vya aina mpya 64 za nbegu ambapo aina 27 zilipitishwa.

Aidha, ilithibitisha uhalisia wa aina mpya 78 za mbegu na kukagua ubora wa mbegu zilizopo sokoni katika wilaya 32. *TOSCI* pia, imeanzisha imeanzisha udhibiti wa ubora wa mbegu za viazi mviringo, mihogp na kuendeleza udhibiti wa mbegu bora ya pamba ambazo uzalishaji wa aina ya UKM08 iliyopitishwa rasmi unaendelea.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia *TOSCI* itaendelea kudhibiti ubora wa mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nizungumzie udhibiti wa ubora wa madawa, Serikali inaendelea kufuatilia wafanyabiashara wanaozalisha na wanaoingiza madawa, ili kubaini madawa yasiyokidhi viwango vya ubora na

kuchukua hatua kali dhidi yao ikiwa ni pamoja na kuwafungia na kuteketeza mada wa yasiyokidhi ubora kwa kufuata sharia ya mazingira.

Makampuni 195, yalikaguliwakatika mikoa ya Mwanza, Kigoma, Arusha, Dar es Salaam, Mtwara na Shinyanga. Aidha makampuni 719 ya viuatilifu, yalipewa vibali vya kuendesha biashara na vibali 162 vilitolewa kwa ajili ya uagizaji wa viuatilifu. Katika mwaka 2014/2015, wakaguzi kwa kushirikiana na shirikisho la wenye viwanda vya viuatilifu, wataandaa mpango mkakati wa utambuzi wa viuatilifu bandia ili viweze kudhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu sasa nizungumzie uzalishaji wamazao makuu ya asili ya biashara. Katika mwaka 2013/2014, uazlishaji wa mazao ya pareto, korosho, sukari, tumbaku na mkonge, umeongezeka kwa viwango tofauti ili hali uzalishaji wa mazao ya pamba, kahawa na chai, ulishuka kidogo kama inavyoonyeshwa katika jedwali namba moja. Nimeeleza sababu zakushuka na kupanda kwa uzalishaji wa mazoa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko ya wazalishaji wa sukari nchini, kuhusu changamoto wanazokabiliana nazo juu ya kushindwa kuuza sukari katika soko la ndani, kutokana na hisia kuwa kiasi kikubwa cha sukari kimeingizwa inchini bila kuidhinishwa na Serikali.

Kutokana na changamoto hiyo, Wizara na wadau wa sukari, waliazimia kuundwa kwa kikosi kazi kitakachotafiti na kutoa mapendekezo ya mfumo mzuri wa uagizaji wa sukari, ambao hautaathiri uzalishaji wandani na upatikanaji wa sukari. Kikosi kazi hicho kimeundwa na kinajumuisha wazalishaji wa sukari nchini, wakulima wa miwa, wataalam wa sukari, wawakilishi kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi, Viwanda na Biashara na Wizara yangu ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu wa 2013/2014, kumekuwepo na changamoto ya kutokuota kwa mbegu ya pamba tani 1,088, isiyokuwa na manyoya iliyotayarishwana kampuni ya *Quton* ambayo ilisambazwa kwa wakulima.

Wizara ilifanya tathimini ya mbegu yote iliyoharibika katika maeneo iliyoharibika katika maeneo yaliyoathirika na wakulima walipewa mbegu mbadala. Aidha Wizara haitalipa kampuni ya *Quton,* shilingi bilioni 1.7 ya ruzuku ya mbegu ambayo haikuota. Vilevile, vilevile Wizara yangu, imepanga kuktana na waklulima wa pamba, ili kujadili changamoto za tasnia ya pamba mara baada ya mkutano huu wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mazao ya bustani, wenyewe umeongezeka hasa katika scheme za umwagiliaji, ambapo mazao ya vitunguu,

njengere, kabichi na nyanya yamekuwa yakizalishwa. Mwenendo wa uzalishaji huu ni kama inavyoonekana katika jedwali namba mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta. Sekta binafsi imeendelea kuimarika katika sekta ndogo ya mazao ya mafuta, hususan zao la alizeti na hivyo kuifanya sekta hii kuendelea kukua na kuongeza uzalishaji kama inavyoonyesha katika jedwali namba tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie umwagiliaji, katika mwaka 2013/2014, Wizara iliendelea na ujenzi na ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye *Schemes 37* zenye hekta 19,890 za wakulima wadogo, kama inavyoonyeshwa katika kiambatanisho namba moja. Ujenzi unaendelea katika mabwawa ya Nala, manispaa ya Tabora, Kasuga katika wilaya ya Kakonko, Mahiga huko Kwimba, Mesaga huko Serengeti, Rwanye - Mbarali na Dongobeshi - Mbulu. Aidha ujenzi wa Bwawa la Itagata - Manyoni na Bwawa la Misozo - Mheza umekamilika. Hata hivyo pia tunafanya juhudi za kukarabati Bwawa la Hidagababeshi, lakini hili liko huko Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mpango wa tekeleza kwa matokeo makubwa sasa *(BRN) Schemes 78* za Maendeleo ya Kilimo cha mpunga, zinaendelezwa ambapo hadi mwezi Machi, 2014, vyama vya wamwagiliaji katika Schemes 76 vimesajiliwa kati ya schemes 78 za utekelezaji wa Big Results Now.

Utafiti wa awali umefanyika katika schemes 78 ili kupata taarifa za msingi kabla ya ujenzi. Wizara imepata watoa hudma wawili watakaofanya kazi kwenye schemes 30 za Wilaya ya Iringa, Iringa Vijijini, Mbarali na Kyela, kuendesha *schemes* hizo kitaalam na kujenga uwezo wa vyama vya wamwagiliaji ili viweze kujiendesha kibishara.

Mafunzo ya kilimo shabibi, yaani *systemes of rice Intensification,*cha mpunga na kanuni za kilimo bora kwa wagani 78 na wakulima 240 katika *schemes 78* na mafundi sanifu wa umwagiliaji 11, kwa ajili ya kuandaa mashamba darasa na mafunzo, tayari yamekwisha kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya umwagiliaji, itakarabati schemes 22 katika mpango wa Big Results Now, itajenga na kuboresha maghala matano na kuweka watoa huduma binafsi kwenye Schemes hizo, ili kuziwezesha kujiendesha kitaalam na kuboresha barabara za kutoka vijijini kwenda mashambani katika schemes za Big Results Now, kama ilivyo katika kiambatanisho namba nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya umwagiliji katika ukanda wa *SAGCOT,* katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendeela kutekeleza miradi ya umwagiliaji katika ukanda wa *SAGCOT,* ya Itete, yenye ukubwa wa hekta 1000, Sonjo,

hekta 1,340, Lupilo hekta 4000, Mpang'angalimila hekta 31,500,000 mkoani Morogoro.

Mradi wa kuendeleza wakulima wadogo kwenye Bonde la Rufiji chini wa hekta 4000, nao umeanza kutekelezwa. Katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia Tume ya Umwagiliaji, itaendelea kutekeleza miradi mingine 39 ya umwagiliaji katika ukanda huu wa *SAGCOT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza miradi 23 ya umwagiliaji ambayo ilianzishwa chini ya DASIP, katika mikoa ya Geita, Mwanza, Kagera, Shinyanga, Mara na Kigoma.

Aidha Serikali itaendelea kutekeleza miradi hii kwa kutumia vyanzo vingine pamoja na vyanzo kama Food Aid Counterpart Fund na vyanzo vingine ambavyo havitakuwa vimekasimiwa katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza mradi wa PHRD ili kuongeza uzalishaji wa mpunga katika skimu 20 za umwagiliaji maji masambani kwa kutumia teknolojia ya kilimo Shabidi cha mpunga, yaani systems of rice intensification. Maelezo ya kina yametolewa katika hotuba yangu ndefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 Wizara itaendelea kutekeleza mradi wa *PHRD,* kwa kuanza kuzalisha mpunga kibiashara kwa kuzingatia mnyororo wa thamani. Aidha Wizara itatekeleza mradi wa kuongeza uzalishaji wa mpunga, yaani *Expanded Rice Production Project* unaofadhiliwa na mfuko wa *Global Agriculture and Food Security* katika skimu tano za Mbogo, Kigugu, Msolwa Ujamaa, Njage na Mvumi katika mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nizungumzie kidogo kuhusu kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabia nchi yanayoathiri shughuli za Kilimo. Serikali imetoa kipaumbele cha kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji mashambani ambapo Imetunga sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Namba Tano (5) ya Mwaka 2013. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine inataka kuanzishwa kwa Tume ya Umwagiliaji na Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji.

Tume itaweza kudhibiti na kusimamia uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji. Mfuko huo wa Umwagiliaji ambao utachangiwa n a Serikali Kuu na wadau nwengine nao utasaidia kuongeza kasi ya ujenzi wa miradi midogo midogo pamoja na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji inayoharibika. Aidha rasimu za kanuni za Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji na mapendekezo ya Muundo wa Tume tayari vimeandaliwa. Vile vile rasimu ya kanuni ya kutekeleza

sheria hiyo zimeandaliwa na kujadiliwa na wadau ili ziweze kukamilishwa na kuanza kutumika katika mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie upatikanaji wa zana za kilimo. Wizara iliendelea kuhimiza matumizi ya zana bora za kilimo na kuhamasisha sekta binafsi kuingiza nchini zana hizo kwa lengo la kuongeza upatikanaji wake. Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba, 2013 sekta ya binafsi iliingiza matrekta makubwa 916 na matrekta madogo 828. Aidha Wizara kupitia mradi wa *DASIP* imenunua na kusambaza mashine za kupandikiza mpunga katika skimu 27 za umwagiliaji ili kuwapunguzia wakulima harubu ya kupanda mpunga kwa mkono na kuwawezesha kupanda kwa wakati. Vile vile mradi umenunua matrekta ya mkono 70 na kuyasambaza kwa wakulima katika wilaya 11.

Katika mwaka 2014/2015 Wizara yangu itatathmini utendaji kazi wa zana za kilimo zilizonunuliwa kupitia mradi wa DASIP, DADIPS, AFSP, SUMA JKT kwa mkopo kupitita Agricultura Inputs Trust Fund katika kanda saba za kilimo ili kutambua changamoto zilizopo na kuchukua hatua za kuboresha mfumo wa upatikanaji wa pembejeo hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie uendelezaji wa kilimo hifadhi. Mabadiliko ya tabia nchi yanayosababisha ukame, mtawanyiko mbaya wa mvua na mafuriko yameanza kuleta hasara kiuchumi nchini ambapo takriban asilimia moja ya pato la taifa hupotea na kuathiri maisha ya watu. Ili kukabiliana na hali hiyo Wizara inaendelea kusisitiza matumizi ya kilimo hifadhi ambacho kinazingatia kupanda mbegu bora bila kukatua, kufunika ardhi kwa kutumia mazao funika yanayorutubisha ardhi na uchaguzi mzuri wa mzunguko wa mazao ambao utaweza kudhibiti wadudu na magonjwa ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie Mfuko wa Taifa wa Pembejeo. Hadi tarehe 15 Aprili, 2014 mfuko wa pembejeo ulikuwa umetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 3,843,344,468 kwa ajili ya ununuzi wa matrekta makubwa 65, matrekta madogo 15, zana za umwagiliaji 2, mashine za uvunaji 2, mashine za usindikaji 2 na pembejeo za kilimo na mifugo. Katika mwaka 2014/2015 mfuko wa pembejeo umepanga kutumia shilingi 6,300,000,000 kwa ajili ya kutoa mikopo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa visumbufu vya mazao na mimea. Katika mwaka 2013/2014 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ilidhibiti visumbufu vya milipuko kwa kununua na kusambaza lita 7,000 za kiwatilifu cha kudhibiti kwelea kwelea, lita 14,000 za kiwatilifu za kudhibitiviwavijeshi, lita 2,500 za kiwatilifu za kudhibiti nzige wekundu na lita 400 za kiwatilifu cha kudhibiti panya. Vile vile Wizara imeendelea na kukagua mazao yanayoingizwa nchini na yanayosafirishwa nchi za nje katika vituo vya

mipakani, kusajili viwatilifu, kusajiri na kukagua wafanyabiashara wa viwatilifu na kutoa vibali vya kuingiza viwatilifu nchini. Katika mwaka 2014/2015 Wizara itaendelea kuchunguza na kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea na kudhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie huduma za ugani. Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI iliendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa kuboresha uenezaji wa teknolojia za kisasa katika kilimo kwa kutumia mbinu shirikishi ambapo mashambadarasa yameongezeka kutoka 16,330 yenye wakulima 344,986 katika mwaka 2012/2013 hadi 16,512 yenye jumla ya wakulima 345,106 katika mwaka 2013/2014 katika mikoa 25 nchini. Aidha wakulima 21,604 wamepatiwa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga, muhogo na ngano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 Wizara imepanga kuanzisha mashamba darasa na mashamba ya mfano 20,000 yenye wakulima 500,000 yakiwemo mashamba darasa 117 ya zao la mpunga, kwenye skimu za umwagiliaji 30 zinazotekeleza Big Results Now. Aidha Wizara kwa kupitia *PHRD* itawezesha wakulima wa mpunga 5,000 wakiwemo vijana kutoka mikoa ya Mbeya, Morogoro  na Iringa na kuwaunganisha kwenye vikundi ili waweze kuzalisa kibiashara kwa kuwafundisha mbinu bora za uzalishaji, usindikaji na utafutaji wa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014 Serikali ilitoa kibali cha ajira kwa sekta ya kilimo chenye nafasi 1804. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2014 Sekretarieti ya Ajira ya Utumishi imeweza kuwapanga wataalam 1,382 na kuwapeleka kwa waajiri ambapo kati ya hao wa Astashahada ni 881, Stashahada 284 na Shahada 217.

Aidha wahitimu 422 bado hawajaajiriwa. Wizara inaendelea kuwasiliana na Sekretarieti ya ajira ili ikamilishe kuwaajiri wahitimu hao waliosalia kulingana na kibali cha ajira kilichokwishatolewa. Iwapo nafasi zote za kibali ngazi ya kijiji zitajazwa itaongeza idadi ya wagani walio kwenye ajira kufikia 9,558. Hii itakuwa ni sawa na kubakiwa na upungufu wa maafisa ugani 5,524 ili tufikie lengo la 15,082. Serikali inaendelea kufanya juhudi kuwaajiri wagani hawa ili tuweze kufikia malengo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti. Katika mwaka 2013/2014 Wizara iliidhinisha aina mpya 13 za mbegu za mazao ya maharage ya soya, njugu mawe mahindi viazi vitamu, na aina mpya 14 za mbegu za mazao ya  mtama, mahindi tumbaku na kahawa kutoka kwenye taasisi za binafsi kama inavyoonekana katika kiambatisho namba 6. Wizara pia ilizalisha jumla ya kilo 217,860 za mbegu mama ili kukidhi mahitaji ya *Agricultural Seeds Agency.* Wizara pia imegundua mbinu za uzalishaji wa miche bora kwa kutumia chupa,

yaani tissue culture ambapo kwa mazao ya migoma, mihogo viazi vitamu na viazi mviringo vyenye ubora tayari vimeanza kuzalishwa.

Aidha katika mwaka 2014/2015 Wizara kwa kushirikiana na Sekta binafsi itaendelea na utafiti wa kugundua mbegu bora za mazao , kuzalisha mbegu mama tani 18 kwa mazao ya nafaka, mikunde mboga  mboga na mbegu za mafuta pamoja na pingili milioni mbili za mazao ya mizizi. Vile vile wizara yangu itaendelea na juhudi za kutekeleza mikakati ya kutokomeza magonjwa ya mazao, hususan ugonjwa wa unywanjano katika zao la migomba, batobato na michirizi ya kahawia katika zao la muhogo na ugonjwa wa mnyauko wa zao la mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie program ya kuendeleza sekta ya kilimo *(ASDP)*. Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa wa ASDP iliyoanza Julai, 2006 ilikamilika mwezi Juni, 2013.

Mwaka 2013/2014 ni kipindi cha mpito ambapo kazi muhimu ambazo hazikukamilika ndizo zinazoendelea kutekelezwa wakati Wizara za sekta ya kilimo zikiendelea mchakato wa pili wa *ASDP*.taarifa rasmi ya kutathmini kuhusu utekelezaji wa *ASDP* nchini kote, yaani implementation completion report iliyoganyika kati ya mwezi Desemba 2013 hadi Februari, 2014 imeonesha mafanikio ya kuridhisha katika utekelezaji wa program hiyo.

Jumla ya skimu 1,325 za umwagiliaji maji mashambani zilikarabatiwa nakujengwa.  Maafisa ugani 6,785 walipatiwa mafunzo. Mashamba darasa 64,469 yalianzishwa, wakuilima 774,156 walipewa mafunzo na watoa huduma za ugani binafsi 441 walipewa mikataba. Aidha jumla ya magari 100, pikipiki 1,613 na baiskeli 3,3389 zilisambazwa katika halmashauri 85 kwa ajili ya kuwezesha maafisa ugani kufanya ufuatiliaji na usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya rasilimali vya kata 166 vilianzishwa, na kompyuta 475 na printers zake zilinunuliwa kwa ajili ya ofisi za maafisa ugani. Jumla ya kilometa 31,817 za barabara za vijijini vilikarabatiwa na kujengwa maghala 698 ya kuhifadhi mazao. Masoko ya msingi 395 yalijengwa, masoko madogo ya mifugo 46 yalijengwa na mabanda 336 ya kuanika na kukausha ngozi ya mifugo yalijengwa. Aidha malambo 108 na visima vya maji 80 vilijengwa, matrekta makubwa 65 matrekta madogo 1,972 na plau 1,321 vilipatikana. Vile vile vituo vya maksai 105 vilianzishwa, maabara za wanyama 104 na majosho 2,394 yalijengwa.

Pia, mashine za kusagisha 13, 525 zilipatikana pamoja na mashine 626 za kukamua mafuta. Vile vile maghala 170 yanayotumia mfumo wa stakabadhi

yalianzishwa katika halmashauri 26. *ASDP two* itandeleza mambo yaliyokwisha anza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie mashamba ya kilimo cha kibiashara kwa mazao ya mpunga na miwa. Katika kuwezesha kupatikana kwa mashamba makubwa ya uwekezaji kupitia mpango wa tekeleza matokeo makubwa sasa hatua iliyofikiwa ni kama ifuatavyo.

Moja, mashamba mawili kati ya saba, yaani Bagamoyo Eco-energy ya Mkulazi yamepatiwa hati miliki, mbili shamba la Bagamoyo eco-energy kwa ajili ya kilimo cha miwa limezinduliwa tarehe 15 Machi, 2014 na mwekezaji tayari ameanza kazi, tatu shamba la Mkulazi limegawanywa katika maeneo ya uzalishaji wa mpunga na miwa na taratibu za kupata wawekezaji zinaendelea. Nne, mashamba ya Ngalimila, Lukulilo, Rufiji Delta yamefikia hatua ya kuhaulishwa kutoka ardhi ya kijiji kwenda ardhi ya kawaida.

Mashamba mawili yaliyobaki ya Muhoro na Tawi katika Wilaya ya Rufiji yapo katika hatua za upimaji ili yaweze kuendelea na taratibu za kupatiwa Hatimiliki.

Tano, taratibu za kuwahusisha wakulima wadogo na vijiji vinazunguka katika mashamba ya Ngalimila, Lukulilo na Bagamoyo tayari zimefanyika kwa kuwawezesha wakulima hao kutengeneza mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na kuwapatia hati miliki za kimila. Vijiji hivyo ni kipugila, Kipo, Naminywili na Ndundunyikanza katika Wilaya za Rufiji, vinavyozunguka shamba la Lukulilo. Vijiji vingine ni Ngalimiala, Mpanga, Kamwene, Utengule, Ipugasa, Mlimba, Igwindembo, Matema, Viwanja Sitini, Miembeni, Msola, Nangombo ambavyo vinazunguka shamba la Ngalimila.

Sita, kukamilisha mipango ya kina ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vya Wilaya za Rufiji na taratibu za kutangaza katika gazeti la serikali kwa mashamba ya Tawi hekta 9,395, na Muhoro hekta 3,915 tayari imekamilika.

Shamba la Mkongo jumla ya hekta 5,510 zimepatikana kwa ajili ya uwekezaji ambapo kampuni ya Frontline Development Partners imeonesha nia ya kuwekeza katika eneo hilo.

Shamba la Muhoro-Rufiji tayari zimepatikana hekta 3,915 kwa ajili ya uwekezaji ambapo kampuni ya Agro-forestry imeonesha nia ya kuwekeza; na kwa upande wa bonde la Malagarasi mashamba mawili yamepatikana katika maeneo ya Kasulu hekta 47,000 na Kibondo hekta 25,000 ambapo kampuni ya Kigoma Sugar imeonesha nia ya kuwekeza katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kambi ya vijana ya kilimo huko Mkongo Rufiji. Serikali ilianzisha kambi ya mafunzo ya kilimo kwa vijana kwa

kukarabati majengo 11 katika eneo la Mkongo Wilayani Rufiji ikiwa na lengo la kuhamasisha vijana kushiriki katika kilimo cha Umwagiliaji cha kibiashara. Kambi hiyo ilizinduliwa rasmi tarehe 5 Oktoba, 2013 na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kambi hiyo imeshatoa mafunzo ya kilimo kwa vijana 50.

Wizara yangu kupitia *RUBADA* itaendeleza vijana kwenye kituo cha kilimo katika kambi ya Mkongo Rufiji na kujenga miundombinu katika mashamba ya vijana katika kituo hicho katika mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuongezeka na upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo. Katika hotuba ndefu iko katika ukurasa wa 62.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa masoko ya mazao ya kilimo unakabiliwa na kukosekana kwa taarifa sahihi za bei na miundombinu mibovu. Ili kuhakikisha wakulima wanapata bei nzuri ya mazao Serikali katika mwaka 2013/2014 ilifanya mambo yafuatayo.

Moja, wizara kwa kushirikiana na wadau wa mazao husika inaandaa utaratibu wa kuandaa mfuko maalum wa kufidia bei ya mazao, yaani price stabilization fund kwa ajili ya kusaidia wakulima pindi bei ya mazao inaposhuka katika soko la dunia. Katika mwaka 2014/2015 Wizara itawasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya kuanzisha Mfuko wa kufidia bei za Mazao.

Mbili, Wizara inashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuanzisha soko la bidhaa na masoko ya mazao yaani *Commodity Exchange*. Ili kufanikisha mfumo huo utakapoanza Wizara kupitia *Big Results Now* imeanza mpango wa kujenga na kukarabati maghala 275 ya mahindi katika awamu tatu kama ilivyo katika jedwali namba saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa maghala mawili ya *NFRA* ya Songea na Mbozi yenye uwezo wa kuhifadhi tati 5,000 kila moja yapo katika hatua mbalimbali na yanaendelea. Aidha Wizara inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya masoko ya kimkakati, yaani *strategic markets* matano ambayo yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi katika maeneo ya Busoka - Kahama, Kabanga - Ngara, Sirari - Tarime, Nkwenda na Mrongo huko Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa nafaka kupitia Wakara wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula. Katika mwaka 2014/2015 *NFRA* imepanga kununua jumla ya tani 200,000 za nafaka zikiwemo tani 190,000 za mahindi na tani 10,000 za mpunga ili kuongeza wigo wa uhifadhi wa mazao ya chakula na kuchangia katika kupunguza mfumuko wa bei za vyakula katika masoko ya mijini. Wakala pia utaendelea na mipango ya kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao ya

chakula kwa kujenga ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 za nafaka katika kanda ya Songea.

Ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, *NFRA* imepanga kuanzisha kanda mpya ya Kigoma itakayohudumia mikoa ya Kigoma, Kagera, Geita na Tabora ili kupunguza majukumu katika kanda ya Shinyanga katika hali hiyo ya kununua mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha uongezaji wa thamani na usindikaji wa mazao. Wizara yangu imeainisha vikundi 10 vyenye jumla ya wakulima 390 vya wasindikaji wadogowadogo wa mbegu za mafuta ya alizeti kutoka katika kanda 390 za wasindikaji wadogo wa mbegu za mafuta ya alizeti kutoka katika halmashauri za Wilaya za Iramba, Manyoni, Mkalama, Singida Ikungi na Manispaa ya Singida katika mkoa wa Singida na kuwapatia mashine 10 za kukamua na kusafisha mafuta ili kuongeza ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, uhifadhi, uchambuzi na usambazaji wa takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naomba wajumbe wako wasome katika hotuba yangu ndefu ambayo iko katika ukurasa kuanzia kati ya ukurasa wa 63 na kuendelea mpaka 67. Naomba nizungumzie kwa haraka haraka, kusimamia sera, sheria na mikakati katika sekta ya kilimo ambayo inapatikana katika hotuba ndefu ukurasa wa 67.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya kilimo ya 2013 imeandaliwa na kusambazwa kwa wadau wa kilimo. Sera hiyo inalenga katika kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo kwa kuongeza tija na uzalishaji wa mazao mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha usalama wa chakula na ziada kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi. Mkazo umewekwa katika kuongeza matumizi ya pembejeo na matumizi ya teknolojia za kisasa pamoja na kushirikisha sekta binafsi kama muhimili katika kuongeza ukuaji katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie kuboresha uratibu katika sekta ya kilimo.Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na wadau inaandaa mfumo wa kuboresha uratibu katika sekta utakaotumika katika utekelezaji wa *ASDP two;* ambao mfumo wake wa utaratibu utakuwa mpana zaidi kuweza kuratibu miradi mingi zaidi pamoja na wahifadhi wake katika sekta ya kilimo, ikiwemo jata miradi ambayo haiendeshwi kwa fedha za umma.

Katika mwaka 2014/2015 Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta ya kilimo pamoja na wabia wa maendeleo itakamilisha maandalizi ya awamu ya pili ya *ASDP two* ili program hiyo ianze kutekelezwa katika 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie kidogo sheria ya kulinda ardhi ya kilimo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri omba pesa muda wako umeshakwisha. Omba hicho kifungu.

**WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina eneo la hekta milioni arubaini na nne zinazofaa kwa kilimo, kati ya hizo hekta milioni kumi na tatu nukta tisa sawa na ailimia thelathini na moja nukta sita ndizo zinazolimwa.

Hali hiyo ya kutokuwepo sheria inayotambua na kulinda ardhi ya kilimo imechangia matumizi ya arhdi yasiyo endelevu na kwa matumizi yasiyo ya kilimo hivyo kupungua kwa ardhi yenye rutuba inayofaa kwa kilimo. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na TAMISEMI inaandaa mapendekezo ya sheria ya kulinda ardhi ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Naomba sasa nishukuru kwa haraka haraka wale wote ambao wametusaidia katika kutekeleza mambo haya ambayo ni Mashirika yafuatayo.

Napenda kuzishukuru nchi za Japan, Ireland, China, India, Israel, Indonesia, Korea Kusini, Marekani, Uingereza, Misri, Ubelgiji, Malaysia, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil na Uholanzi. Nashukuru pia mashirika ya taasisi za kimataifa ambayo ni Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, SIMIT, IKRISAD, ASARECA, USAID, COICA, IKRAF, ITA, IRA, CFC, AVRDC, AGRA,* na *WARDA, Bill and Melinda Gates Foundation* ambao wote kwa pamoja wametusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, maombi ya fedha. Kabla sijaomba fedha naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wote wananchi na wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Napenda kumshukuru kipekee Naibu Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, Katibu Mkuu Bibi Sophia Elias Kaduma, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Yamungu Kyandabira, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Raphael Daruti, Wakurugenzi wote na Wakuu wa Idara ambao wamefanikisha maandalizi ya Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka 2014/2015. Kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa, naomba sasa Bunge lako Tukufu kwa Fungu la

43 liidhinishe Shilingi 317,738,678,000 kwa ajili ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika Fungu 43 kwa Mwaka 2014/2015. Kati ya fedha hizo Shilingi 271,658,404,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 47,080,270,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida Shilingi 230,970,391,380 ni kwa ajili ya Matumizi Mengine, Shilingi bilioni ishirini na sita, milioni mia tisa arubaini na sita elfu na arubaini na saba, mia nane, ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara na Shilingi 13,741,968,820 ni Mishahara ya Bodi na Taasisi. Kati ya fedha za Bajeti ya Maendeleo Shilingi 25,000,000,000 ni fedha za ndani na 22,080,270,000 ni fedha za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 24, katika mwaka 20114/2015, Wizara yangu kupitia Fungu 24 inaomba shilingi 6,685,413,000 kwa ajili ya shughuli za kuendeleza Ushirika nchini. Kati ya fedha hizo shilingi 4,500,000,000 ni kwa ajiili ya Matumizi Mengine na shilingi 779,566,000,000 ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 5. Katika Mwaka 2015/2015 Wizara yangu kupitia Fungu 5 inaomba Shilingi 29,408,021,000 kwa ajili ya kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji hapa Nchini. Kati ya fedha hizo Shilingi 47,000,000 ni kwa aili ya matumizi mengine na Shilingi 28,933,021,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo Bajeti ya Maendeleo ni 10,000,0000,000 na fedha za ndani ni 18,933,021,000. *(Makofi)*

Mheshimniwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA, MHE. MHANDISI CHRISTOPHER KAJORO CHIZA (MB.) KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA KWA MWAKA 2014/2015**

**UTANGULIZI**

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Maji na Mifugo inayohusu Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, sasa lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya

Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika siku ya leo tukiwa na afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania ambao wengi wao ni wakulima.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kuwashukuru viongozi wetu wa ngazi za juu wa Serikali kwa kukipa kilimo msukumo mpya. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, amekuwa mstari wa mbele katika kusimamia utekelezaji wa nguzo kubwa ya dhana ya Kilimo Kwanza. Aidha, Mhe. Rais anasimamia na kutoa maelekezo moja kwa moja katika utekelezaji wa Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) katika Sekta ya Kilimo ili kuwezesha ushiriki wa Sekta za umma na binafsi katika kukuza kilimo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nitumie fursa hii kumpongeza Mhe Rais kwa kuanzisha mchakato wa kupata katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kipekee namshukuru Mhe. Rais kwa kuteua wawakilishi wa wakulima kushiriki katika Bunge Maalum la Katiba lililoanza tarehe 18 Februari 2014. Ni matarajio yangu kwamba ushiriki wao utachangia kuipata katiba ambayo itaweka mazingira bora na endelevu yatakayojibu changamoto za wakulima na kutumia fursa zilizopo katika kukuza Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal ambaye pamoja na majukumu yake mengi amekuwa akitenga muda wa kutosha kufuatilia maendeleo ya Sekta ya Kilimo, ikiwemo kukagua na kuhamasisha shughuli za kilimo na kutoa maagizo mbalimbali kuhusu kilimo kinachozingatia utunzaji wa mazingira. Wizara yangu inaendelea kutekeleza maagizo hayo kwa kuandaa miongozo mbalimbali na mapendekezo yatakayowezesha kutungwa kwa Sheria ya Kusimamia Rasilimali za Kilimo. Aidha, Wizara yangu imeendelea kuhimiza Halmashauri zote nchini kutunga sheria ndogo za kuwafanya wadau wa kilimo kufanya shughuli zao katika namna ambayo inaleta mageuzi ya kilimo bila kuathiri mazingira.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.) kwa kusisitiza umuhimu wa kuendeleza kilimo cha kisasa, kibiashara na chenye tija. Aidha Mhe. Waziri Mkuu (almaarufu mtoto wa mkulima) amekuwa mfano wa kuigwa katika kuhimiza kilimo cha kisasa kwa vitendo, ambapo mashamba yake yamekuwa yakitumika kama mashamba darasa. Vilevile, napenda kumshukuru Mhe. Waziri Mkuu kwa kutumia sehemu ya muda wake kufuatilia changamoto nyingi wanazozipata wakulima ikiwemo migogoro ya makundi mbalimbali katika Sekta ya Kilimo na kuipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo Maji na Mifugo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Peter Mahamud Msolla, Mbunge wa Kilolo, kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2014/2015 bila kuchoka. Pia naishukuru Kamati kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina taarifa ya utekelezaji ya Wizara yangu ya mwaka 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2014/2015 katika vikao vyake vilivyofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 29 Aprili, 2014, na tarehe 01 na 03 Mei 2014. Napenda kuihakikishia Kamati pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa yamezingatiwa katika bajeti hii.

Natoa shukrani na pongezi za pekee kwa wananchi wa Jimbo langu la Buyungu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Nawapongeza kwa juhudi wanazofanya katika kujiletea maendeleo yao ya kilimo hususan kilimo cha kahawa, mpunga, alizeti n.k. Pia nawashukuru kwa uvumilivu wao wanaponikosa ninapokuwa nje ya Jimbo nikitimiza majukumu mengine ya kitaifa. Kipekee nawapongeza kwa kuwa kwa miaka mingi wamekuwa wakizalisha chakula cha kujitosheleza na kuuza ziada. Nataka pia niwapongeze, na kwa niaba yao, nimshukuru Mhe. Rais kwa kuwasogezea karibu huduma za Serikali kwa kuwapatia Wilaya na Halmashauri mpya ya Kakonko.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.) kwa hotuba yake ambayo ilielezea kwa muhtasari hali ya kilimo chetu ilivyo kwa hivi sasa na mwelekeo kwa mwaka ujao. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge waliotumia mijadala hiyo kutoa michango ya namna ya kuendeleza Sekta ya Kilimo. Wizara yangu imezingatia mawazo yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014 Bunge lako tukufu lilipata msiba wa kuondokewa na Mheshimiwa William Augustao Mgimwa aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mbunge wa Kalenga, Mheshimiwa Saidi Bwanamdogo Mbunge wa Chalinze na Mheshimiwa Salum Hemedi Khamisi Mbunge wa Chambani. Nawapa pole ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu hao, Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema peponi roho za marehemu hao.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mhe. Dkt Asha Rose Migiro kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Mbunge na kisha kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Nawapongeza pia wote walioteuliwa kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, akiwemo Mhe. Godfrey Weston Zambi (Mb), Naibu Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika. Napenda pia kuchukua fursa hii kuwapongeza Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze, Mhe. Godfrey William Mgimwa kuwa Mbunge

wa Jimbo la Kalenga na Mhe. Yussuf Salim Hussein kuwa Mbunge wa Jimbo la Chambani. Naahidi kushirikiana nao katika kuiletea nchi yetu maendeleo.

## HALI YA KILIMO NA USHIRIKA

### Hali ya Kilimo

Mheshimiwa Spika, kilimo ni moja ya Sekta muhimu katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu kwa kuwa inatoa ajira kwa asilimia 74 ya Watanzania na inachangia zaidi ya asilimia 100 ya chakula kinachopatikana nchini kwa miaka yenye mvua za kutosha. Katika mwaka 2013, Sekta ya Kilimo ilichangia asilimia 24.7 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 24.8 mwaka 2012. Mchango mkubwa katika Pato la Taifa ulitokana na shughuli za huduma ambazo zilichangia asilimia 44.3 ikifuatiwa na Sekta ya Kilimo. Kwa kuwa asilimia kubwa ya Watanzania wanashiriki katika shughuli za kilimo, mchango huo kwa kiasi kikubwa utachangia katika kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Pato la Taifa kwa mwaka 2013, kwa shughuli za kiuchumi za kilimo zinazojumuisha mazao, ufugaji, misitu na uwindaji limekua kwa asilimia 4.3 sawa na ilivyokuwa katika mwaka 2012. Katika ukuaji huo, mchango wa mazao ulikuwa asilimia 4.5 ikilinganishwa na asilimia 4.7 ya mwaka 2012. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa mazao ya chakula, hususan nafaka uliongezeka kutoka tani milioni 6.7 mwaka 2012 hadi tani milioni 7.6 mwaka 2013 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 13.4.

Aidha, uzalishaji wa mahindi uliongezeka kutoka tani milioni 5.1 mwaka 2012 hadi tani milioni 5.2 mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 2. Uzalishaji wa mchele uliongezeka kutoka tani milioni 1.2 mwaka 2012 hadi tani milioni 1.3 mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 11. Vilevile, uzalishaji wa mazao ya chakula yasiyo nafaka ulikuwa tani milioni 6.8. Uzalishaji huo wa mazao ya chakula wa tani milioni 12.1 katika mwaka 2013/2014 unaonesha kuwepo kwa ziada ya tani milioni 2.2 za chakula.

Ongezeko hilo, ambalo limetokana na kuwepo kwa mvua za kutosha na juhudi za Serikali za kuboresha uzalishaji kwa kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima, limeleta utoshelevu wa chakula nchini kwa asilimia 118. Kilimo cha umwagiliaji kimechangia asilimia 24 katika utoshelevu huo. Aidha, utoshelevu huo umechangia kushuka kwa bei za vyakula na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza mfumuko wa bei za bidhaa kutoka asilimia 12.1 Januari, 2013, 9.8 Machi, 2013, hadi 6.1 Machi, 2014.

### Hali ya Chakula

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya upatikanaji wa chakula katika mwaka 2013/2014 nchini ilikuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi ya nchi kufuatia

mavuno mazuri ya msimu wa kilimo wa mwaka 2012/2013. Tathmini iliyofanyika mwezi Julai na Agosti, 2013, inaonyesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2012/2013 ulikuwa tani 14,383,845 zikiwemo tani 7,613,221 za nafaka na tani 6,770,624 za mazao yasiyo ya nafaka. Kiasi hicho cha chakula kikilinganishwa na mahitaji ya chakula ya tani 12,149,120 katika mwaka 2013/2014 kinaonyesha kuwepo kwa ziada ya tani 2,234,726 za chakula. Ziada hiyo ni pamoja na tani 354,015 za mahindi na tani 466,821 za mchele. Kutokana na hali hiyo, Taifa lilijitosheleza kwa chakula kwa asilimia 118. Pamoja na hali ya chakula kuwa ya kuridhisha, kulikuwa na baadhi ya maeneo yenye upungufu wa chakula kutokana na kutopatikana kwa mavuno ya vuli kufuatia mvua za vuli kutonyesha vizuri katika maeneo mengi yanayopata mvua hizo. Tathmini ya Kina ya Hali ya Chakula na Lishe iliyofanyika mwezi Oktoba/Novemba 2013 ilibaini kuwepo kwa jumla ya watu 828,063 walikuwa na upungufu wa tani 23,312 za chakula na tayari chakula hicho kimetolewa.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuanza msimu wa 2013/2014 Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) ilikuwa na akiba ya nafaka tani 25,453. Katika mwaka 2013/2014 NFRA ilinunua tani 219,377 na kufanya jumla ya akiba ya nafaka kuwa tani 244,830, ambayo inaendelea kugawiwa kwenye maeneo yenye upungufu na taasisi za umma. Aidha, katika kipindi cha kuanzia Julai 2013 hadi Aprili 2014 NFRA imetoa jumla ya tani 32,711 ili kukabiliana na upungufu wa chakula. Tani 14,491 zimeuzwa kwa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) na tani 2,881 zimeuzwa kwa taasisi za umma. Hadi kufikia tarehe 02 Aprili 2014 akiba katika maghala yote ya NFRA ni tani 194,747 za nafaka.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mwenendo wa hali ya mvua kuwa mzuri katika msimu wa 2013/2014 katika maeneo mengi ya nchi, kuna matarajio ya kupata mavuno mazuri ya mazao ya chakula katika msimu wa 2014/2015. Hata hivyo, hali halisi ya chakula itajulikana baada ya kufanya tathmini katika mwezi Juni 2014.

Mheshimiwa Spika, taarifa za awali zinaonesha kwamba mvua zimenyesha vizuri katika nchi nyingine za Afrika Mashariki, hali inayoashiria kuwepo kwa mavuno mazuri katika nchi hizo na hivyo kuwepo kwa uwezekano wa kupunguza soko la chakula kinachozalishwa nchini. Hali ikiwa hivyo, Serikali inawashauri wakulima na wafanyabiashara kutafuta masoko ndani na nje ya nchi. Napenda kusisitiza kwamba Serikali haizuii uuzaji halali wa chakula cha ziada nje ya nchi.

**Hali ya Ushirika**

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya ushirika nchini imekuwa siyo ya kuridhisha na hivyo kusababisha wanaushirika na wananchi kwa ujumla kutokuwa na imani nao. Changamoto za ushirika ni pamoja na ukosefu wa

mitaji, uongozi mbovu, ubadhirifu na upotevu wa fedha za wanachama, elimu duni ya ushirika miongoni mwa wanaushirika na udhaifu katika usimamizi wa maendeleo ya ushirika. Kutokana na hali hiyo, vyama vya ushirika vimeshindwa kutoa huduma zilizotarajiwa kwa wanachama wake na hivyo kukosa mvuto kwa wananchi wengine kujiunga.

Mheshimiwa Spika, ili kufufua ushirika, katika mwaka 2013/2014 Wizara yangu ilianza kuchukua hatua za muda mfupi na mrefu kukabiliana na matatizo hayo katika ushirika. Miongoni mwa hatua za muda mfupi zilizochukuliwa ni pamoja na kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa vyama, ambapo Wizara imewapatia mafunzo Maafisa Ushirika 45 na kufanya ukaguzi katika vyama vya ushirika vya msingi 252 na vyama vikuu vitatu (3) katika mikoa ya Singida (47), Tabora (193) na Ruvuma (15). Hatua mbalimbali za kisheria zimeanza kuchukuliwa dhidi ya wote waliobainika kufanya ubadhirifu wa mali za vyama. Serikali imewavua madaraka Warajis Wasaidizi wa Mikoa watatu walioshindwa kutimiza wajibu wao na kuteua wapya. Aidha, viongozi wa Vyama waliofanya ubadhirifu wameamriwa kufidia hasara walizosababisha katika vyama vyao.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi katika ukaguzi wa Vyama vya Ushirika Serikali inaendelea kujenga uwezo wa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) kwa kuteua Bodi Mpya ya Wakurugenzi na kuongeza idadi ya Wakaguzi 29. Aidha, Serikali imeanza kumtumia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum katika Vyama vya Ushirika wa Tumbaku katika Mkoa wa Tabora ambavyo vimedhaminiwa na Serikali kukopa kwenye mabenki. Matokeo ya ukaguzi huo unaoendelea yataiwezesha Serikali kuchukua hatua stahiki kwa wote watakaobainika kuhusika na ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa na Serikali dhidi ya wabadhirifu ni kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria baadhi ya wajumbe/watendaji wa Wazalendo *SACCOS, Vision SACCOS, Apex* ya Tumbaku , *WETCU* na Vyama vya Msingi mkoani Pwani.

Mheshimiwa Spika, hatua za muda mrefu ambazo zimechukuliwa ni kutungwa kwa Sheria ya Vyama vya Ushirika Namba 6 ya Mwaka 2013 ambayo imeanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Sheria hiyo imeainisha majukumu ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika maeneo mawili yaani eneo la usimamizi ambalo utekelezaji wake utafanywa moja kwa moja na Tume yenyewe kuanzia ngazi ya Taifa hadi wilayani na majukumu ya uhamasishaji ambayo yatatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Tume na Wizara za ki-Sekta, Halmashauri za Wilaya na wadau wengine.

Pia Sheria hiyo imeboreshwa kwa kuongeza makali ya adhabu kwa wabadhirifu, kuondoa mgongano wa maslahi baina ya uongozi wa ushirika na

uongozi wa kisiasa na Umma na kurekebisha muda wa uongozi katika vyama vya Ushirika kutoka miaka tisa hadi sita. Sheria mpya ya Ushirika ilianza kutumika tarehe 1 Januari 2014. Aidha, rasimu ya kanuni za kutekeleza sheria hiyo zimeandaliwa na kujadiliwa na wadau ili ziweze kukamilishwa na kuanza kutumika rasmi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya tathmini ya hali ya vyama vya ushirika nchini na kubaini uwepo wa vyama vya ushirika mfu 360 ambavyo vilikuwa havitekelezi majukumu yao kwa mujibu wa sheria. Vyama hivyo vimefutwa katika Daftari la Usajili ili kubakiza vyama vinavyokidhi matakwa ya sheria. Ufutaji huo umefanya idadi ya vyama vya ushirika kupungua kutoka vyama 9,964 mwezi Machi 2013 hadi vyama 9,604 mwezi Machi 2014. Kuanzishwa kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika ambayo, kwa mujibu wa sheria mpya ya vyama vya ushirika, itatekeleza majukumu ya usimamizi mpaka ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutaimarisha usimamizi na udhibiti wa shughuli za vyama vya ushirika na hivyo kupunguza matatizo yaliyojitokeza hapo awali. Aidha, Sheria mpya ya Ushirika inaruhusu kuanzishwa kwa vyama vipya vya Ushirika zaidi ya kimoja katika eneo moja ili mradi viwe na nguvu ya kiuchumi, jambo ambalo litaongeza ushindani.

Mheshimiwa Spika, idadi ya *SACCOS* hadi Machi 2014 ilikuwa 5,478 ikilinganishwa na 5,559 mwaka 2013 hivyo kupunguza idadi ya wanachama kutoka 1,153,248 hadi kufikia wanachama 935,121. Katika kupanua kiwango cha huduma za kifedha jumuishi nchini (Financial Inclusion), *SACCOS* zimeendelea kuimarishwa ili ziweze kutoa huduma za kifedha kwa wananchi wengi zaidi hususan waliopo vijijini. Wizara imeandaa mkakati wa kuimarisha *SACCOS* ambao unatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja na *Financial Sector Deepening Trust (FSDT)* na Markerting Infrastructure Value Addition and Rural Finance (MIVARF). Aidha, hisa, akiba na amana za wanachama zimepungua kutoka Shilingi bilioni 463.5 Machi 2013 hadi Shilingi bilioni 451.1 Machi 2014. Mikopo iliyotolewa kwa wanachama ilifikia Shilingi bilioni 778.4.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika wa Mazao (Agricultural Marketing Cooperative Societies – AMCOS) vimeendelea kutoa huduma kwa wakulima zikiwemo za ugani, usambazaji wa pembejeo, ukusanyaji na uuzaji wa mazao. Wanachama 45,028 katika mikoa tisa ya Mbeya, Mtwara, Lindi, Mara, Kilimanjaro, Mwanza, Morogoro, Manyara na Singida wameendelea kunufaika na Mfumo wa Stakabadhi za Maghala kwenye mazao ya mpunga, mahindi, korosho, kahawa na alizeti kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi vya Mazao 368 na *SACCOS 35*. Kupitia Vyama vya Ushirika, pembejeo za kilimo zilisambazwa kwa wakulima zikiwemo mbolea, vifungashio na madawa ya kuua wadudu hususan kwa mazao ya tumbaku na korosho, mbegu na miche ya kahawa, miti na matunda. Changamoto kubwa ambayo Serikali inaifanyia kazi ni uwezo mdogo wa wanaushirika kuendesha shughuli zao kwa ufanisi ili kurejesha imani ya wanachama kwa Vyama vya Ushirika.

**MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA KIPINDI CHA 2013/2014**

**Makusanyo ya Maduhuli**

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2013/2014 Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi 3,179,010,000 kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi 1,708,192,378.56 sawa na asilimia 53.73 ya makadirio. Vyanzo vikubwa vya maduhuli ni ada za ukaguzi wa mazao yanapopitishwa mipakani na mauzo ya nyaraka za zabuni. Kutokana na kupungua kwa soko la chakula katika nchi jirani, matarajio ya ukusanyaji wa maduhuli hayatafikiwa.

**Fedha Zilizoidhinishwa**

Mheshimiwa Spika katika mwaka 2013/2014 Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ilitengewa fedha kama ifuatavyo:

(a) Fungu 43: Shilingi 349,284,608,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 268,244,320,000 zilikuwa za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 81,040,288,000 zilikuwa fedha za Matumizi ya Maendeleo.

(b) Fungu 24: Shilingi 5,783,105,000 ni fedha za Matumizi ya Kawaida.

(c) Hivyo jumla ya fedha zote zilizotengwa kwa Wizara ni Shilingi 355,067,713,000.

**Matumizi ya Bajeti ya Kawaida**

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa kutoka Hazina hadi tarehe 31 Machi, 2014 ni Shilingi 172,451,694,686.19 sawa na asilimia 63 ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi ni Shilingi 171,710,134,838.75 sawa na asilimia 99.57 ya fedha zilizotolewa. Kati ya matumizi ya kawaida, jumla ya Shilingi 208,054,897,400 ni fedha zinazolindwa *(ring fenced)* ambazo zinatumika kwa maeneo muhimu ya ununuzi wa nafaka Shilingi 109,656,840,000 na ruzuku ya pembejeo ni Shilingi 97,011,057,400 na michango kwa Mashirika ya Nje ni Shilingi 1,387,000,000. Fedha za matumizi kwa majukumu mengine ya Wizara ni Shilingi 23,271,045,600 tu.

**Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo**

Katika mwaka wa 2013/2014, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ilitengewa jumla ya Shilingi 81,040,288,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 23,927,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 57,113,288,000 ni fedha za nje. Programu na miradi iliyotekelezwa ni:-

(i) Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme – ASDP);*

(ii) Programu ya Kilimo ya Kuendeleza Tija na Uzalishaji katika Mashariki mwa Afrika *(Eastern Africa Agricultural Productivity Program - EAAPP);*

(iii) Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga *(Japan Policy and Human Resources Development – PHRD);*

(iv) Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani *(District Agricultural Sector Investiment Project – DASIP);*

(v) Programu ya Kuongeza Usalama wa Chakula *(Accelerated Food Security Programme – AFSP);* na

(vi) Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT).*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014 Shilingi 40,831,220,246 zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo sawa na asilimia 50.38 ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi ni Shilingi 26,961,620,087 sawa na asilimia 66.03 ya fedha zilizotolewa. Matumizi kidogo ya fedha kidogo zilizotolewa yamesababishwa na kuchelewa kutolewa fedha kulingana na mpango kazi.

## MALENGO, MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI MWAKA 2013/2014

### Malengo

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2013/2014, umezingatia malengo yaliyomo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Mkubwa Sasa *(Big Resuts Now - BRN)* na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Malengo hayo yalitekelezwa kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Program – ASDP),* Programu ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika *(Cooperative Reform and Modernization Program - CRMP)* na Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT).*

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji, Wizara imetekeleza Malengo Mkakati *(Strategic Objectives)* tisa (9) kupitia Fungu 43 na 24 ambayo

yametekelezwa na Idara, Vitengo, Asasi na Taasisi za Wizara. Malengo Mkakati hayo ni:-

(i) Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo;

(ii) Kuwezesha Upatikanaji wa Masoko ya Bidhaa za Kilimo;

(iii) Kuwezesha Uongezaji wa Thamani ya Mazao ya Kilimo;

(iv) Kuwezesha na Kuimarisha Ushirika na Asasi za Wananchi katika Kilimo na Sekta nyingine za Kiuchumi;

(v) Kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji, Uhifadhi, Uchambuzi na Usambazaji wa Takwimu;

(vi) Kusimamia Sera, Sheria na Mikakati katika Sekta ya Kilimo;

(vii) Kuboresha Uratibu katika Sekta ya Kilimo;

(viii) Kuboresha Uwezo wa Wizara wa kutoa Huduma; na

(ix) Kuzingatia Masuala Mtambuka katika Kilimo.

**Utekelezaji wa Malengo Mkakati kwa Mwaka 2013/2014**

**Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo**

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo mkakati yaliyoainishwa, katika mwaka 2013/2014 Wizara yangu ilitekeleza yafuatayo:-

**Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo.**

Mheshimiwa Spika, makisio ya mahitaji ya pembejeo za kilimo za aina mbalimbali kwa mazao ya kilimo yalikuwa tani 452,202 za mbolea, mbegu bora tani 60,000 na viuatilifu tani 328,586. Hadi kufikia Aprili, 2014 upatikanaji wa mbolea ulifikia tani 343,687 na kusambazwa kwa wakulima. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2014 upatikanaji wa mbegu bora umefikia tani 32,339.9. Kati ya hizo tani 20,517.11 zilizalishwa hapa nchini na tani 11,822.79 ziliingizwa kutoka nje ya nchi. Kiasi hicho cha upatikanaji wa mbegu bora kimeongezeka kwa asilimia 30.7 ikilinganishwa na upatikanaji wa mwaka 2012/2013. Hadi mwezi Aprili, 2014 upatikanaji wa viuatilifu ulifikia tani 6,538.15 na lita 87,680.

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa pembejeo bado ni mdogo ikilinganishwa na mahitaji. Ili kuongeza upatikanaji wa pembejeo za kilimo, Serikali itaongeza uzalishaji wa mbegu bora katika mashamba yake na kuhamasisha ushiriki wa Sekta binafsi kuwekeza katika kuongeza upatikanaji wa pembejeo hizo.

***Uzalishaji wa Mbegu na Miche Bora***

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo (*Agricultural Seed Agency - ASA*) ilizalisha tani 3,495 za mbegu bora za nafaka, mikunde na mboga mboga, vipando bora vya muhogo 17,520,000 na miche ya matunda 55,165,251 kwa kushirikiana na JKT na Jeshi la Magereza. ASA pia ilishirikiana na Sekta Binafsi katika uzalishaji wa mbegu bora kwa kutumia mashamba yake ya mbegu ambapo *Suba Agro-Trading & Engineering Company* na *Meru Agro-Tours & Consultancy Limited* yalizalisha tani 3,997 za mbegu za mahindi katika Shamba la Mbozi. Aidha, Wizara kupitia *ASA* imezijengea uwezo kampuni binafsi za mbegu za kizalendo 14 za *Highland Seed Growers Company Ltd*. ya Mbeya, *Northern Seed Company Ltd*. ya Moshi, *Aminata Quality Seeds and Consultancy Ltd* ya *Tanga, Kibo Seed Company (T) Ltd* ya *Arusha., Meru Agro-Tours & Consultants Co. Ltd* ya *Arusha, Alpha Seed Company Ltd* ya *Moshi., Suba Agro Trading and Engineering Co. Ltd., Itente Company Limited* ya Kagera, *IFFA Seed Company (T) Limited* ya Arusha na *Kipato Seed Limited* ya Njombe, *Agriseed Technologies Ltd ya Morogoro, Namburi Agricultural Company* Ltd ya Arusha na Jambe Agro Company ya Korogwe.

Kampuni hizo zilipewa mafunzo ya teknolojia ya uzalishaji wa mbegu bora, ziliwezeshwa kuhudhuria makongamano ya mbegu na kufanya ziara za mafunzo nchini Kenya na Uganda. *ASA* pia imeingia ubia na taasisi ya *Clinton Development Foundation* ya Marekani katika uzalishaji wa mbegu bora za soya na mahindi kwa kutumia Shamba la Mbegu la Dabaga. Natumia nafasi hii kuwafahamisha wadau wa tasnia ya mbegu kutumia fursa hii kwa Sekta Binafsi kuingia ubia na ASA katika miradi ya uzalishaji mbegu.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara pia ilisimamia na kufuatilia uzalishaji wa Mbegu za Daraja la Kuazimiwa (*Quality Declared Seed - QDS*) ambapo jumla ya tani 354 za mbegu bora zimezalishwa na kuchangia upatikanaji. Pia Halmashauri za Wilaya 18 za Morogoro, Mvomero, Kilosa, Kilombero na Ulanga (Morogoro), Bahi, Kondoa, Mpwapwa na Kongwa (Dodoma), Iringa na Mufindi (Iringa), Njombe, Ludewa na Makete (Njombe), Ruangwa na Nachingwea (Lindi), Mtwara na Masasi (Mtwara) zimewezeshwa kwa kupatiwa mashine za kutayarisha mbegu kwa lengo la kuhakikisha uwepo wa mbegu bora kwa wakulima. Kazi hii itaendelea katika msimu wa 2014/2015, ambapo tani 450 za daraja la kuazimiwa za mahindi, mtama, alizeti, mpunga na maharage

zitazalishwa. Aidha, Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai (*Tanzania Smallholder Tea Development Agency – TSHTDA*) ulizalisha miche bora ya chai milioni 1.7. Vilevile, Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (*Tanzania Coffee Research Institute – TaCRI*) imezalisha miche ya kahawa 350,000 na kuisambaza kwa wakulima katika maeneo mbalimbali kwa utaratibu wa ruzuku.

**Mheshimiwa Spika,** katika msimu wa 2014/15, ASA itawezeshwa kuzalisha tani 4,200 za mbegu bora za nafaka, mikunde na mboga mboga, pingili za muhogo 16,000,000 na miche bora ya matunda 15,000,000 katika mashamba yake na pia kupitia ushirikiano na wakulima wa mkataba wakiwemo JKT na Magereza. ASA pia itaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika uzalishaji wa mbegu. Vilevile, ASA itashirikiana na makampuni ya *Suba Agro-Trading & Engineering Company* na *Meru Agro-Tours & Consultancy Limited* katika uzalishaji wa mbegu ambapo jumla ya tani 4,200 za mbegu za nafaka zitazalishwa katika shamba la Mbozi. Aidha, ubia kati ya ASA na taasisi ya *Clinton Development Foundation* utaweza kuzalisha tani 500 katika shamba la Dabaga.

**Mpango wa Ruzuku ya Pembejeo**

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya pembejeo za mbegu bora na mbolea kwa wakulima kwa utaratibu wa vocha kama ifuatavyo: mwaka 2008/2009 kaya 737,000; 2009/2010 kaya 1,500,000; 2010/2011 kaya 2,011,000; 2011/2012 kaya 1,780,000 na 2012/2013 kaya 940,783. Aidha, katika mwaka 2013/2014 Wizara ilitoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa kaya 932,100 ambazo zilitumia tani 124,685 za mbolea na tani 9,621 za mbegu. Utaratibu huo umesaidia wakulima kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao ya mahindi na mpunga. Uzalishaji wa mahindi umeongezeka kutoka magunia 5 kwa ekari hadi wastani wa gunia 15 kwa ekari na mpunga umeongezeka kutoka gunia 4 kwa ekari hadi wastani wa gunia 20 kwa ekari.

Aidha utoshelevu wa chakula ulioongezeka kutoka asilimia 103 mwaka 2009/2010 hadi kufikia asilimia 118 mwaka 2013/2014. Pamoja na mafanikio mazuri ya mpango wa ruzuku, kumekuwepo na changamoto katika ngazi mbali mbali ikiwemo ubadhilifu, upotevu wa vocha na ucheleweshaji wa vocha hali iliyopelekea wakulima kushindwa kupata pembejeo mapema.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, Serikali kuanzia msimu wa 2013/2014 ilibuni utaratibu wa kutoa pembejeo za mbolea, mbegu za mahindi na mpunga kwa vikundi vya wakulima na vyama vya ushirika kwa kutumia mikopo kupitia Taasisi za Fedha. Serikali kwa upande wake ingetoa dhamana ya asilimia 50 ya mahitaji ya pembejeo na wakulima kutoa asilimia 20 ya awali kama dhamana ya mikopo ili Benki ziwakopeshe mara mbili ya dhamana.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua juhudi kubwa za maandalizi zilizofanywa na vikundi vya wakulima waliohamasika kutekeleza utaratibu huu ikiwa ni pamoja na kuchangia asilimia 20 ya gharama za mikopo ya pembejeo lakini kwa bahati mbaya utaratibu huu haukutekelezwa kutokana na Taasisi za Fedha kuweka sharti kwa Serikali kuweka fedha taslimu kama dhamana kabla ya kutoa mikopo hiyo, jambo ambalo halikuwezekana. Katika mwaka wa 2014/2015, Serikali itaendelea kufanya mazungumzo na Taasisi za Fedha zilizo tayari kutekeleza utaratibu huu ili changamoto zilizojitokeza katika msimu uliopita zisijirudie tena. Aidha, Wizara inafanya mazungumzo na makampuni ya pembejeo kuangalia uwezekano wa makampuni hayo kukopesha wakulima moja kwa moja ili kuongeza upatikanaji wa pembejeo.

**Mheshimiwa Spika,** ruzuku ya madawa ya korosho tani 6,538.15 na lita 87,680 imetolewa kwa wakulima. Ruzuku pia ilitolewa kwa ajili ya uzalishaji wa miche bora ya chai milioni 1.7 itakayosambazwa kwa wakulima katika msimu wa 2014/2015. Miche milioni 1.6 ya chai iliyozalishwa katika msimu wa 2012/2013 ilisambazwa na kupandwa katika mashamba mapya (hekta 100 sawa na miche milioni 1.343) na miche 257,000 katika mashamba ya zamani. Pia miche bora ya kahawa 350,000 ilizalishwa kwa mpango wa ruzuku.

Kwa msimu wa 2014/2015 ruzuku ya viuatilifu vya korosho itakayotolewa ni tani 892.9 na dawa za maji lita 167,000. Aidha, ruzuku ya viuatilifu vya pamba ni paketi za ekari 1,625,000; ruzuku ya mbegu za pamba ni tani 8,000; ruzuku ya miche ya chai ni miche 3,000,000; na ruzuku ya miche ya kahawa ni miche 800,000.

*Udhibiti wa Ubora wa Mbolea*

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania *(Tanzania Fertilizer Regulatory Authority - TFRA)*, ilisajili jumla ya Wafanyabiashara wa Mbolea 533 na kuwapa leseni za kufanya biashara ya mbolea na bidhaa zingine zinazohusika na mbolea. Aidha vibali vya kuingiza mbolea nchini 203 na 163 vya kutoa mbolea nje ya nchi vilitolewa. Kwa msaada wa mradi wa *AGRA,* jumla ya wakaguzi 100 wa mbolea wamefanyiwa mafunzo na kutangazwa katika gazeti la serekali, wakaguzi hao wapo katika Mikoa 26 ya Tanzania. Mamlaka imefanya mafunzo juu ya Sheria ya Mbolea ya 2009 kwa Mawakala wa Mbolea 240 katika Mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Iringa, Katavi na Njombe.

**Mheshimiwa Spika, k**atika kuhakikisha mbolea inayouzwa kwa wakulima ipo katika ubora unaotakiwa, Mamlaka imefanya ukaguzi wa mbolea katika maghala na maduka ya mbolea ya mikoa ya Ruvuma, Njombe, Iringa, Rukwa, Mbeya, Dar es-salaam na Morogoro. Katika Ukaguzi huo Mamlaka ilibaini jumla

ya tani 36.7 za mbolea zilikuwa chini ya kiwango na hatua za kisheria zilichukuliwa dhidi ya makampuni yaliyokutwa na mbolea hizo.

**Udhibiti wa Ubora wa Mbegu**

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu - *TOSCI* imetekeleza kazi zifuatazo: kukagua mashamba yenye ukubwa wa hekta 8,120 yanayozalisha mbegu bora za madaraja yote zikiwemo mbegu za daraja la kuazimiwa *(QDS);* kupima sampuli 1,850 katika maabara kubaini ubora wa mbegu; kuthibitisha vigezo vya aina mpya 64 vya mbegu ambapo aina 27 zilipitishwa; kuthibitisha uhalisia *(Distinctiveness Uniformity and Stability - DUS)* wa aina mpya 78 za mbegu; na kukagua ubora wa mbegu iliyopo sokoni katika wilaya 32. Aidha, *TOSCI* imeanzisha udhibiti wa ubora wa mbegu za viazi mviringo, mihogo na kuendeleza udhibiti wa mbegu ya pamba ambapo uzalishaji wa aina ya UKM08 iliyopitishwa rasmi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kukabiliana na changamoto ya kuwepo kwa mbegu zisizokidhi viwango vya ubora katika soko. *TOSCI* inakagua na kuchukua hatua za kisheria kwa makampuni na mawakala wanaosambaza mbegu zisizo na ubora, ikiwa ni pamoja na kufuta mashamba ya mbegu yasiyokidhi viwango (field standards) na kusimamisha mauzo ya mbegu zisizokidhi viwango vya ubora *(stop sale orders)*.

Kwa mfano, baadhi ya mashamba ya makampuni ya *Kibo Seed, Quton, Aminata Seed Quality, Beula Seed Company na Agriseed Company* yalikataliwa na hivyo kuamriwa kuvuna na kuuza kama nafaka ya kawaida.

Mheshimiwa Spika,*TOSCI* imefanya ukaguzi wa mashamba na mbegu katika mikoa 19 kati ya mikoa 24 ya Tanzania Bara. Mikoa iliyofanyiwa ukaguzi ni pamoja na Tabora, Kigoma, Kagera, Manyara, Rukwa, Ruvuma, Njombe, Iringa, Mbeya, Mtwara, Dodoma, Morogoro, Mwanza, Arusha, Kilimanjaro, Singida, Tanga, Simiyu na Geita. Aidha, makampuni 27 ya mbegu na vituo 7 vya utafiti vinavyozalisha mbegu mama vilifanyiwa ukaguzi katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia TOSCI itaendelea kuthibiti ubora wa mbegu, kuajiri na kutoa mafunzo kwa rasilimali watu ili kutoa huduma bora. Aidha, TOSCI itakagua hekta 10,000 za mashamba yanayozalisha mbegu za madaraja yote ikiwemo QDS. Vile vile, itachukua sampuli 2,500 kutoka katika aina mpya 65 za mbegu na kupima ubora wake; kuthibitisha vigezo na sifa za aina mpya za mbegu; itakagua ubora wa mbegu iliyopo sokoni katika wilaya 40 na kuhamasisha utambuzi wa ubora wa mbegu kufuatilia ukaguzi wa mbegu katika wilaya 180.

**Udhibiti wa Ubora wa Madawa**

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufuatilia wafanyabiashara wanaoingiza madawa ili kubaini madawa yasiyokidhi viwango vya ubora, kuchukua hatua kali dhidi yao ikiwa ni pamoja na kuwafungia na kuteketeza madawa yasiyokidhi ubora kwa kufuata Sheria ya Mazingira. Aidha, watengenezaji wameanza kuweka alama za siri kwenye vibandiko na viwekeo vya viuatilifu ambazo zinatambuliwa na Ofisi ya Msajili wa Viuatilifu na kutumiwa na wakaguzi katika utambuzi wa viuatilifu bandia na visivyo bandia. Katika kipindi husika jumla ya makampuni 195 yalikaguliwa katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Mwanza (85), Kigoma (22), Arusha (35), Dar es Salaam (41), Mtwara (7), Shinyanga (5) makampuni 719 ya viuatilifu yalipewa vibali vya kuendesha biashara zao. Makampuni hayo ni wauzaji wa viuatilifu 449, waagizaji 41, wachanganyaji 2 na wafukizaji 227. Aidha, vibali 862 vilitolewa kwa ajili ya uagizaji wa viuatilifu.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha udhibiti wa ubora wa viuatilifu, katika mwaka 2014/2015, wakaguzi kwa kushirikiana na Shirikisho la Wenye Viwanda vya Viuatilifu Tanzania (CropLife-Tanzania) wataandaa mpango mkakati wa utambuzi wa viuatilifu bandia. Aidha, Wizara yangu itafanya ukaguzi wa maduka yanayouza viuatilifu na kuhakiki ubora wake kabla havijapelekwa kwa wakulima.

**Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Asili ya Biashara**

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Wizara ilisimamia na kufuatilia utendaji wa kazi wa Bodi za Mazao ya Chai, Sukari, Tumbaku, Pamba, Pareto, Mkonge, Kahawa, Korosho na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa lengo la kuhakikisha kuwa kila Bodi ina Mkakati wa kuendeleza zao husika kwa mujibu wa Sheria. Uzalishaji wa mazao ya pareto, korosho, sukari, tumbaku na mkonge umeongezeka kwa viwango tofauti. Hadi mwezi Aprili 2014, uzalishaji wa pareto ulikuwa tani 6,500. Uzalishaji wa zao hilo unatarajiwa kufikia tani 7,000 ifikapo mwezi Juni 2014 kutokana na kuongezeka kwa tija hadi kilo 1,100 kwa hekta. Uzalishaji wa korosho umeongezeka kufikia tani 127,939.419 ikilinganishwa na tani 121,703.811 za mwaka 2012/2013.

Uzalishaji wa Sukari katika viwanda vya Kilombero, Mtibwa, *TPC* na Kagera hadi tarehe 31 Machi 2014 ulikuwa tani 293,011, sawa na asilimia 99.91 ya malengo. Ongezeko hilo linatokana na sababu za kuwepo kwa mvua za kutosha, hususan katika maeneo ya Kilombero na Kagera; kupanua miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji katika mashamba ya kampuni ya Sukari Kagera; kutumia mbegu bora za miwa ambazo ni mpya aina ya *N19* na N25, na ukarabati wa viwanda vya Kilombero na *TPC*.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko ya wazalishaji wa Sukari nchini kuhusu changamoto wanazokabiliana nazo juu ya kushindwa kuuza

sukari katika soko la ndani kutokana na hisia kuwa kiasi kikubwa cha sukari kimeingizwa nchini bila kuidhinishwa na serikali. Kutokana na changamoto hiyo Wizara na wadau wa sukari waliazimia kuundwa kwa kikosi-kazi kitakachotafiti na kutoa mapendekezo ya mfumo mzuri wa kuagiza sukari ambao hautaathiri uzalishaji wa ndani na upatikanaji wa sukari. Kikosi-kazi kimeundwa na kinajumuisha wazalishaji wa sukari nchini, wakulima wa miwa, wataalamu wa sukari, wawakilishi kutoka Wizara za Fedha, Viwanda na Biashara, na Kilimo Chakula na Ushirika. Hadidu za rejea za Kikosi-kazi hicho ni:-

(a) Kupendekeza mfumo bora utakaotumika katika zoezi zima la uagizaji wa Sukari nje ya nchi kwa matumizi ya kawaida.

(b) Kupendekeza utaratibu wa ushirikishwaji wa wakulima wadogo katika upimaji wa utamu wa sukari (renderment).

(c) Kupendekeza mfumo bora wa tozo itakayotumika kwa ajili ya sukari inayoingizwa nchini.

(d) Kupendekeza mfumo bora wa kiasi cha tozo kwa zao la miwa kwenye Halmashauri za Wilaya ambazo zao la miwa linalimwa ikiwa ni pamoja na ada zingine zinazotozwa.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa zao la mkonge uliongezeka kutoka tani 23,344 mwaka 2012/2013 hadi tani 41,104 mwaka 2013/2014. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa bei katika soko la dunia kutoka wastani wa Dola za Marekani 1,458 mwaka 2012/2013 hadi Dola za Marekani 1,460 kwa tani ya singa mwaka 2013/2014 (Februari 2014) baada ya kuweko kwa mahitaji makubwa kwenye nchi za Saudi Arabia, Uingereza, Hispania, Nigeria, Ujerumani, Syria, China, Japan, Kenya na Kuwait ambako kumehamasisha wakulima kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na tathmini iliyofanywa mwezi Machi 2014, uzalishaji wa tumbaku unatarajiwa kupanda kutoka tani 74,240 mwaka 2012/2013 hadi tani 100,000 mwaka 2013/2014 kwa sababu ya ongezeko la bei katika soko la dunia. Kumekuwa na changamoto za zao la tumbaku zinazotokana na mfumo wa upatikanaji wa pembejeo ambao umewasababishia wakulima kupata hasara zilizotokana na mfumo mbovu wa kukopeshwa pembejeo. Serikali imeelekeza uagizaji wa pembejeo ufanywe na Vyama vya Msingi ili kuondoa ukiritimba na gharama zisizo za lazima.

Aidha, Mkutano Mkuu wa wadau wa sekta ndogo ya Tumbaku uliofanyika tarehe 4 Februari 2014 mkoani Tabora uliazimia, pamoja na mambo mengine, kwamba mfumo wa ukopaji usiendeshwe kwa makundi pekee bali wakulima wanaoweza kujidhamini waruhusiwe kununua pembejeo zao

wenyewe. Vilevile, Serikali iliagiza *WETCU Ltd.* ilipe madeni yote ya wakulima wa tumbaku kwa kukatwa ushuru wake wa tumbaku na kwamba kuanzia msimu ujao, wakulima wa tumbaku walio chini ya *WETCU Ltd.* wasikatwe fedha kwa ajili ya ushuru wa *WETCU Ltd.* kwa kuwa bado wanaidai *WETCU Ltd.*

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa pamba mbegu katika mwaka 2013/2014 ulifikia tani 246,767 ikilinganishwa na tani 351,151 za mwaka 2012/2013 ikiwa ni pungufu kwa asilimia 31. Sababu kuu iliyochangia kushuka kwa ununuzi wa pamba katika msimu wa soko wa 2013/2014 ni kushuka kwa bei ya pamba kwa mkulima katika mwaka 2012/2013. Matarajio ya uzalishaji kwa mwaka 2013/2014 yanaonesha kuongezeka. Changamoto zilizojitokeza katika zao hili ni pamoja na kuvurugika kwa mfumo wa upatikanaji wa pembejeo hususan mbegu na viuatilifu kupitia Vyama vya Ushirika, kutokana na kuwepo kwa mapungufu katika utekelezaji wa kilimo cha mkataba; bei ndogo kwa mkulima iliyosababishwa na kushuka kwa bei katika soko la dunia. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kutoa elimu ya kilimo cha mkataba kwa wakulima wa pamba ili kuhakikisha wanapata weledi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine iliyojitokeza katika msimu wa 2013/2014 ni tani 1,088 za mbegu ya pamba isiyokuwa na manyoya inayotayarishwa na kampuni ya Quton zilizosambazwa kwa wakulima kutokuota. Wizara ilifanya tathmini ya mbegu yote iliyoharibika katika maeneo yaliyoathirika na wakulima walipewa mbegu mbadala. Aidha, Wizara haitailipa kampuni ya Quton Shilingi bilion 1.7 ya ruzuku ya mbegu ambayo haikuota. Vile vile, Wizara yangu imepanga kukutana na wakulima wa pamba ili kujadili changamoto za tasnia ya pamba mara baada ya mkutano wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya kahawa na chai ulipungua katika mwaka 2013/2014 kutoka tani 71,200 hadi 48,599 na 33,700 hadi 33,000 mwaka 2012/2013 mtawalia. Kushuka kwa uzalishaji wa zao la kahawa kumetokana na mzunguko wa uzaaji wa mibuni, matumizi duni ya pembejeo na bei isiyotabirika.

Aidha, uzalishaji wa chai kavu umepungua kutokana na kupungua kwa uzalishaji katika nusu ya kwanza ya mwaka (Julai hadi Desemba 2013) ambapo katika msimu huo uzalishaji wa chai kavu ulikuwa ni tani 12,751 ikilinganishwa na tani 14,033 zilizozalishwa Julai hadi Desemba 2012. Upungufu huo ulisababishwa na uhaba wa mvua hususan katika mwezi wa Agosti, Oktoba na Desemba 2013. Katika kukabiliana na changamoto za soko la kahawa Serikali imeunda kikosikazi kinachoongozwa na Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mbunge wa Muleba Kusini, kutathmini mwenendo wa soko la kahawa ya Tanzania.

Uzalishaji wa mazao makuu ya biashara ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 1.**

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Biashara 2012/2013 hadi 2013/2014 na Matarajio 2014/2015**
**(Tani)**

| Zao | Uzalishaji 2012/2013 | Uzalishaji 2013/2014 | Matarajio 2014/2015 |
|---|---|---|---|
| Pamba | 351,151 | 246,767 | 250,000 |
| Kahawa | 71,200 | 48,599 | 61,000 |
| Chai | 33,700 | 33,000 | 35,000 |
| Pareto | 6,100 | 7,000 | 7,500 |
| Tumbaku | 74,240 | 100,000 | 113,600 |
| Korosho | 121,704 | 127,939 | 120,000 |
| Mkonge | 23,344 | 41,104 | 43,400 |
| Sukari | 286,380 | 293,011 | 320,000 |

Chanzo: Bodi za Mazao

***Uzalishaji wa Mazao ya Bustani***

**Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa mazao ya bustani umeongezeka hasa katika skimu za umwagiliaji maji ambapo mazao ya vitunguu, njegere, kabichi na nyanya yamekuwa yakizalishwa. Mwenendo wa uzalishaji huo ni kama ilivyo katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani)**

| Zao | 2011/2012 | 2012/2013 | 2013/2014 | |
|---|---|---|---|---|
| Matunda | 3,938,730 | 4,096,280 | 4,416,690 | |
| Mbogamboga | | 901,680 | 937,750 | 1,005,305 |
| Maua | 9,850 | 10,200 | 10,790 | |
| Viungo | 7,370 | 8,125 | 8,377 | |

Chanzo: Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika

***Uzalishaji wa Mazao ya Mbegu za Mafuta***

**Mheshimiwa Spika,** Sekta binafsi imeendelea kuimarika katika sekta ndogo ya mazao ya mafuta, hususan zao la alizeti na hivyo kuifanya Sekta hii kuendelea kukua na kuongeza uzalishaji kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 3**. Uwekezaji mkubwa umekuwa katika viwanda vidogo na vya kati vya kusindika mafuta na hivyo kuhamasisha uzalishaji zaidi katika mikoa ya Manyara, Dodoma, Njombe, Mbeya, Rukwa na Kigoma inayozalisha zao hilo. Aidha, mkoa wa Singida umebaki kuwa kinara katika uzalishaji wa zao la alizeti.

**Jedwali Na. 3: Uzalishaji wa Mbegu za Mafuta (Tani)**

| Na. | Zao | 2011/2012 | 2012/2013 | 2013/2014 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Alizeti | 1,125,000 | 2,625,000 | 2,755,000 |
| 2 | Karanga | 810,000 | 1,425,000 | 1,635,735 |
| 3 | Ufuta | 456,000 | 1,050,000 | 1,113,892 |
| 4 | Mawese | 24,880 | 40,500 | 41,000 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika

***Umwagiliaji***

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014 Wizara iliendelea na ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye skimu 37 zenye hekta 19,890 za wakulima wadogo. Ujenzi wa mabwawa saba ya umwagiliaji umefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo: Inala (Manispaa ya Tabora) –asilimia 57; Kasuga (Kakonko) asilimia 100; Mahiga (Kwimba) - asilimia 95; Mesaga (Serengeti) asilimia 30; Lwanyo (Mbarali) asilimia 60; na Dongobesh (Mbulu) asilimia 85.

Aidha, ujenzi wa bwawa la Itagata (Manyoni) na Bwawa la Misozwe (Muheza) umekamilika. Wizara pia ilisimamia ukamilishaji wa skimu 14 zenye jumla ya hekta 4,186 zinazogharamiwa na *Food Aid Counterpart Fund (FACF)* na skimu sita zenye hekta 390 zilitekelezwa kwa fedha za *District Agricultural Development Plans (DADPs)* na Taasisi nyingine katika Halmashauri za Kilombero, Mbeya, Njombe na Iringa**.** Aidha, Wizara iliendelea kufuatilia na kusimamia ujenzi na ukarabati wa skimu 38 zenye hekta 2,220 katika Halmashauri mbalimbali nchini kwa kutumia fedha za *District Irrigation Development Fund (DIDF)*

**Mheshimiwa Spika,** kupitia Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa skimu 78 za maendeleo ya kilimo cha mpunga zinaendelezwa, utekelezaji hadi mwezi Machi 2014 ulikuwa kama ufuatavyo:

(i) Vyama vya wamwagiliaji katika skimu 76 vimesajiliwa kati ya skimu 78 za utekelezaji wa *BRN*.

(ii) Utafiti wa awali umefanyika katika skimu zote 78 ili kupata taarifa za msingi za ujenzi.

(iii) Wizara imepata Watoa huduma wawili ambao watafanya kazi kwenye skimu 30 za Wilaya ya Iringa Vijijini, Mbarali na Kyela kuendesha skimu hizo kitaalamu, kujenga uwezo wa Vyama vya Wamwagiliaji kujiendesha kibiashara.

(iv) Mafunzo ya Kilimo Shadidi cha Mpunga na Kanuni za Kilimo Bora kwa wagani 78 na wakulima 240 katika skimu 78 na Mafundi Sanifu wa Umwagiliaji 11 kwa ajili ya kuandaa mashamba darasa na mafunzo kwa wakulima yametolewa.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itakarabati Skimu 22 kati ya 39 zilizolengwa katika mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN); itajenga na kuboresha maghala 5 kati ya 39 yaliyolengwa katika skimu za *BRN* na kuweka Watoa Huduma Binafsi kwenye skimu hizo ili kuziwezesha kujiendesha kitaalamu; na kuboresha barabara za kutoka vijijini kwenda mashambani katika skimu za *BRN*.

***Miradi ya Umwagiliaji Ukanda wa SAGCOT***

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014 Wizara inaendelea kutekeleza miradi ya umwagiliaji katika Ukanda wa *SAGCOT* kama ifuatavyo:-

(i) **Mradi wa Umwagiliaji – Itete, Morogoro wa Hekta 1,000** umelenga kuendeleza kilimo cha umwagiliaji wa zao la mpunga kwa wakulima wadogo. Hadi Machi 2014 ujenzi wa banio umefikia asilimia 60; ujenzi wa ofisi ya mradi umekamilika na ujenzi wa mfereji mkuu wa kushoto na kulia umekamilika kwa asilimia 50 na 15 mtawalia.

(ii) **Mradi wa Umwagiliaji Sonjo – Kilombero, Morogoro wa Hekta 1,340:** ilipangwa kufanya usanifu, kuandaa michoro na kuanza ujenzi wa skimu. Hadi kufikia Machi 2014 usanifu ulikuwa umefikia asilimia 80 na kazi bado inaendelea.

(iii) **Mradi wa Umwagiliaji – Lupiro, Ulanga, Morogoro wa Hekta 4,000:** upo katika eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji cha mpunga. Kazi zilizopangwa ni pamoja na kukamilisha upembuzi yakinifu, usanifu na kuanza ujenzi. Hadi Machi 2014 upembuzi yakinifu umekamilika na usanifu kufikia asilimia 45.

(iv) **Mradi wa Umwagiliaji – Mpanga - Ngalimila Kilombero, Morogoro wa Hekta 31,500;** ni mradi mkubwa kwa ajili ya kilimo cha mpunga. Upembuzi yakinifu na tathmini ya mazingira inaendelea. Upimaji wa sura ya ardhi kwa kutumia ndege umefanyika na taarifa kutoka kwa mkandarasi zimepatikana na uchambuzi wa takwimu *(data processing)* unaendelea. Aidha, upimaji wa udongo hatua ya awali *(initial reconnaissance soil survey*) umefanyika Desemba 2013 na upimaji wa kina (*detailed soil survey*) unatarajiwa kuanza baada ya msimu wa mvua kwisha. Vilevile, tathmini ya awali ya mahitaji muhimu ya maji ya mazingira *(Rapid Environmental Flows Assessment - REFA*) imefanyika.

(v) **Mradi wa kuendeleza Wakulima Wadogo kwenye Bonde la Rufiji Chini wa Hekta 4,000:** Kazi ya kuandaa hati za kimila katika shamba la Lukuliro ilianza katika kijiji cha Kipo. Wakulima wamepimiwa maeneo yao na eneo la Hekta 75 limeshapimwa na kugawanywa katika mashamba madogo yenye ekari 2.5, 5 na 50. Kazi hiyo inaendelea katika vijiji vya Ndundunyikanza, Nyaminywili na Kipugira.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea kutekeleza miradi 39 ya umwagiliaji katika Ukanda wa Kilimo Kusini mwa Tanzania – *Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT.*

**Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutekeleza miradi 23 ya umwagiliaji ambayo ilianzishwa chini ya DASIP. Utekelezaji wa Miradi ya Lwenge (Geita), Bigombo (Ngara), Mgondogondo (Kibondo), Miyogwezi (Ukerewe), Mwagwila (Meatu), Kyakakera (Missenyi), Luhala (Kwimba), Mkuti (Kigoma Vijijini), Lutubiga (Busega) na Kyamyorwa (Muleba) umefikia zaidi ya asilimia 95 na inatazamiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2014. Aidha, utekelezaji wa miradi ya Kahanga (Kahama), Nampangwe (Bukombe), Mwiruzi (Biharamulo), Igenge (Misungwi), Kinamwigulu (Maswa), Rabuor (Rorya) umefikia zaidi ya asilimia 75 na miradi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2014.

Vile vile, utekelezaji wa miradi ya Isholelo (Shinyanga), Mwasubuya (Bariadi), Masinono (Butiama), Sukuma (Sengerema), Kisangwa (Bunda), Nyisanzi (Chato) na Nyamititа (Serengeti) umefikia kati ya asilimia 20 na 60. Miradi hii haikufikia hatua ya juu ya utekelezaji kutokana na sababu mbalimbali zikiwa ni pamoja na migogoro ya ardhi na uwezo mdogo wa wakandarasi. Serikali itaendelea kutekeleza miradi hii kutoka katika vyanzo vyake pamoja na vyanzo vingine ikiwemo FACF.

**Mradi wa *Policy and Human Resource Development – PHRD***

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia PHRD ililenga kuongeza uzalishaji wa mpunga katika skimu mbalimbali kwa kutumia teknolojia ya Kilimo Shadidi cha Mpunga (*Systems of Rice Intensification - SRI)*. Kazi zilizofanyika ni pamoja na:-

(i) Kuanzisha maeneo ya kutoa mafunzo ya Kilimo Shadidi cha Mpunga (SRI) kwa wakulima katika skimu 14 za Mkula (Kilombero), Mkindo (Mvomero), Uturo, Madibira, Mbuyuni/Kimani na Ipatagwa (Mbarali), Lekitatu (Arumeru), Musa Mwinjanga (Hai), Kivulini (Mwanga), Mawemairo (Babati), Mwamapuli (Igunga), Ruvu Rice Farm, Nakahuga (Songea) na Kilangali (Kilosa);

(ii) Kutoa mafunzo kwa Wakulima Viongozi 33 na wakulima wengine 600 kuhusu matumizi bora ya maji, miundombinu ya umwagiliaji na matumizi ya Mwongozo wa Uendeshaji na Matengenezo (Operation and Maintenance Manual) katika skimu 20 za *PHRD* **(Kiambatisho 5);** na

(iii) Kutoa mafunzo kuhusu masoko na usindikaji wa mpunga kwa vikundi 20 vya vijana vyenye vijana 22 kila kimoja katika skimu 11. Vilevile, mafunzo kuhusu masoko na usindikaji wa mpunga yalitolewa kwa maafisa ugani 20 na wakulima 20 kutoka skimu 20.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea kutekeleza mradi wa *PHRD* kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija ya zao la mpunga na kuwezesha wakulima katika Skimu 20 za umwagiliaji kuanza kuzalisha mpunga kibiashara kwa kuzingatia mnyororo wa thamani. Aidha, kupitia msaada wa Serikali ya Japan *(Japan International Cooperation Agency – JICA),* Wizara imeanza utekelezaji wa mradi wa kuendeleza skimu za umwagiliaji za wakulima wadogo *(Small Scale Irrigation Development Project - SSIDP)* katika skimu 19 kupitia Mfuko wa *DIDF*.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, Wizara itatekeleza Mradi wa kuongeza uzalishaji wa mpunga *(Expanded Rice Production Project* - ERPP) unaofadhiliwa na Mfuko wa *Global Agriculture and Food Security Program - GAFSP* katika skimu tano za Mbogo, Kigugu, Msolwa Ujamaa, Njage na Mvumi katika mkoa wa Morogoro. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Ushirikiano Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Initiatives*) kupitia mradi wa "*Irrigation Development and Watershed Management Project in the Lake Victoria Basin side of Tanzania*" imetenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kufanya tathmini ya kimazingira na kijamii (*Environmental and Social Impact Assessment- ESIA*) katika miradi ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 20,229 katika ukanda wa Ziwa Viktoria.

*Kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji*

**Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi yanayoathiri shughuli za kilimo, Serikali imetoa kipaumbele cha kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji mashambani ambapo Bunge limetunga Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 5 ya mwaka 2013. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine inataka kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji. Tume itaweza kudhibiti na kusimamia uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji.

Mfuko huo utakaochangiwa na Serikali Kuu na wadau wengine utasaidia kuongeza kasi ya ujenzi wa miradi midogomidogo pamoja na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji inayoharibika.

Aidha, rasimu ya Kanuni za Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji na mapendekezo ya Muundo wa Tume zimeandaliwa. Aidha, rasimu ya kanuni za

kutekeleza sheria hiyo zimeandaliwa na kujadiliwa na wadau ili ziweze kukamilishwa na kuanza kutumika katika mwaka 2014/2015.
*Zana za Kilimo*

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuhimiza matumizi ya zana bora za kilimo na kuhamasisha Sekta Binafsi kuingiza nchini zana hizo kwa lengo la kuongeza upatikanaji wake. Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2013, Sekta Binafsi iliingiza jumla ya matrekta makubwa 916 na matrekta ya mkono 828. Aidha, baada ya SUMA JKT kuuza matrekta yote 1,846 yaliyoingizwa nchini kwa mkopo nafuu kutoka Serikali ya India, sehemu ya fedha iliyopatikana imetumika kuagiza matrekta mengine 268 kutoka India yenye thamani ya Shilingi bilioni 7.02.

Mwezi Desemba 2013, matrekta 228 (210 aina ya New Holland na 18 Farmtrac) yenye thamani ya shilingi bilioni 6.086 yaliingizwa nchini, ikiwa ni sehemu ya matrekta 268 yaliyoagizwa. Matrekta hayo yanauzwa kwa wakulima, vikundi vya wakulima na Vyama vya Ushirika kwa fedha taslimu au mkopo. Hadi kufikia tarehe 18 Aprili 2014, matrekta 71 yalikuwa yameuzwa kwa walengwa. Upatikanaji wa zana hizo umewezesha kuongezeka kwa eneo linalolimwa kwa kutumia matrekta kutoka asilimia 10 mwaka 2006 hadi asilimia 14 mwaka 2013. Aidha, matumizi ya jembe la mkono yamepungua kutoka asilimia 70 hadi asilimia 62 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mradi wa DASIP imenunua na kusambaza mashine za kupandikiza mpunga katika skimu 27 za umwagiliaji ili kuwapunguzia wakulima harubu ya kupanda mpunga kwa mkono na kuwawezesha kupanda kwa wakati. Mashine hizo zimegawiwa moja kwa kila wilaya za Kibondo, Bukombe, Kahama, Ngara, Geita, Chato, Kwimba, Kigoma, Sengerema, Shinyanga, Maswa, Meatu, Bariadi, Magu, Bunda, Musoma, Tarime, Rorya, Misenyi, Muleba, Biharamulo, Serengeti, Misungwi, Ukerewe, Kasulu na mbili kwa Wilaya ya Kakonko. Vilevile Mradi umenunua *Power tiller* 70 na kuzisambaza kwa wakulima katika wilaya za Kwimba (11), Mbogwe (15), Bukombe (6), Misungwi (11), Magu (11), Kahama (4), Shinyanga (5), Misenyi (1), Muleba (1), Biharamulo (1), Ngara (1), Mugumu (1), Meatu (1) na Kakonko (1).

**Mheshimiwa Spika,** kupitia Mradi wa Usalama wa Chakula (*Accelerated Food Security Project - AFSP*), Wizara imevijengea uwezo vikundi vya wakulima katika Halmashauri 18 za Morogoro Vijijini, Mvomero, Kilosa, Kilombero na Ulanga (Mkoa wa Morogoro), Bahi, Kondoa, Mpwapwa na Kongwa (Dodoma), Iringa Vijijini na Mufindi (Iringa), Njombe, Ludewa na Makete (Njombe), Ruangwa na Nachingwea (Lindi) na Mtwara Vijijini na Masasi (Mtwara) kwa kuvipatia kila kimoja seti ya mashine nne za kupiga mpunga, kumenya na kupukuchua mahindi, kupanga madaraja na kuweka mbegu dawa. Mashine hizo zitawezesha vikundi kuzalisha mbegu za *QDS.*

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, Wizara itatathmini utendaji kazi wa zana za kilimo zilizonunuliwa kupitia miradi ya *DASIP, DADPs, AFSP, SUMA JKT* na kwa mkopo kupitia AGITF katika kanda 7 za kilimo ili kutambua changamoto zilizopo na kuchukua hatua za kuboresha mfumo wa upatikanaji wa zana bora za kilimo nchini.

*Uendelezaji wa Kilimo Hifadhi.*

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha ukame, mtawanyiko mbaya wa mvua na mafuriko, yameanza kuleta hasara kiuchumi nchini ambapo takriban asilimia moja ya pato la Taifa hupotea na kuathiri maisha ya watu. Ili kukabiliana na hali hiyo, Wizara inaendelea kusisitiza matumizi ya Kilimo Hifadhi ambacho kinazingatia kupanda mbegu bora bila kukatua, kufunika ardhi kwa kutumia mazao funika yanayorutubisha ardhi na uchaguzi mzuri wa mzunguko wa mazao ambao utaweza kudhibiti wadudu na magonjwa ya mazao.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Vituo vya Utafiti vya Uyole, Mlingano na Selian ilisambaza teknolojia ya Kilimo Hifadhi katika Halmashauri 27 za wilaya za Meru, Arusha, Hanang, Morogoro, Kilosa, Babati, Karatu, Kongwa, Kiteto, Simanjiro, Moshi, Mtwara, Lindi, Bukoba, Bunda, Magu, Serengeti, Meatu, Maswa, Sengerema, Geita, Urambo, Uyui, Igunga, Nzega, Singida na Mbeya ambapo wakulima 10,000 wanalima takriban ekari 14,200 kwa kuzingatia kanuni za kilimo hifadhi. Aidha, Kilimo Hifadhi kimeongeza tija katika zao la mahindi kutoka magunia 3 mwaka 2005 hadi wastani wa magunia 20 kwa ekari katika mwaka 2013. Wadau wengine wanaohamasisha Kilimo Hifadhi nchini kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ni Asasi Zisizo za Kiserikali (AZAKI) za *ACT, WADEC, RECODA, CPAR, Gatsby Trust,* LIMAC, *Aga Khan Foundation* na CARE International ambao huwapatia wakulima mafunzo na zana.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu wa Kilimo Hifadhi, Tanzania ilishiriki kwenye Kongamano la Kwanza la Afrika la Kilimo Hifadhi (*1st Africa Congress on Conservation Agriculture*) lililofanyika Lusaka nchini Zambia tangu tarehe 18 hadi 21 Machi 2014. Kongamano liliandaliwa na Mtandao wa Kilimo Hifadhi wa Afrika (*African Conservation Tillage Network*) ambao Tanzania ni mwanachama. Kongamano lilitoa maazimio 10 yanayolenga kuzihamasisha nchi za Afrika kuwekeza kwenye kukuza na kuendeleza Kilimo Hifadhi na kuweka lengo la kuwafikia angalau wakulima milioni 25 katika Bara la Afrika ifikapo mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na COMESA na FAO imeunda Kikosi-kazi cha kitaifa cha kuendeleza Kilimo Hifadhi (*National Conservation Agriculture Task Force*) kinachojumuisha wadau toka Serikalini, AZAKI, Sekta Binafsi na wakulima. Majukumu ya kikosi kazi hicho ni kubuni mikakati ya kukuza Kilimo Hifadhi nchini, kuhamasisha wakulima kubadili mtazamo na kuondokana na mazoea ya kukatua na kwenda kwenye mtazamo mpya wa kuzalisha kiendelevu kwa kuzingatia Kanuni za Kilimo Hifadhi.

***Mfuko wa Taifa wa Pembejeo***

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka wa Fedha 2013/2014 Mfuko ulipanga kutumia Shilingi 7,102,800,000 ili kutoa mikopo ya matrekta mapya 107, matrekta madogo ya mikono 26, mikopo ya thamani ya Shilingi 1,134,000,000 kwa ajili ya pembejeo za Kilimo na Mifugo na vifungashio, mikopo 8 kwa ajili ya zana za umwagiliaji maji na mikopo 5 kwa ajili ya mashine za usindikaji. **Jedwali Na. 4** linaonyesha mikopo iliyotolewa hadi tarehe 15 Aprili, 2014.

**Jedwali Na. 4: Mikopo iliyotolewa katika kipindi cha 1/7/2013 hadi 15/4/2014**

| **Na.** | **Aina ya Mkopo** | **Utekelezaji** | | **Thamani ya Mikopo** |
|---|---|---|---|---|
| | | **Lengo** | **Halisia** | |
| 1 | Matrekta mapya makubwa | 107 | 65 | 2,623,174,468 |
| 2 | Matrekta ya mkono (Power Tillers) | 26 | 15 | 105,218,000 |
| 3 | Pembejeo za Kilimo/Mifugo | | 20 | 851,550,000 |
| 4 | Zana za Umwagiliaji maji | 8 | 2 | 63,902,000 |
| 5 | Mashine za uvunaji (Combine harvester) | | 2 | 142,000,000 |
| 6 | Mashine za Usindikaji | 5 | 2 | 57,500,000 |
| | **JUMLA** | | | **3,843,344,468** |

Chanzo: Mfuko wa Pembejeo

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Pembejeo umepanga kutumia Shilingi 6,342,800,000 kwa ajili ya kutoa mikopo mbalimbali katika msimu wa 2014/2015.

Fedha hizo ni jumla ya Shilingi 1,940,000,000 kutoka Hazina na Shilingi 4,402,800,000 zitakazotokana na marejesho ya mikopo kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 5.**

**Jedwali Na.5: Mikopo Itakayotolewa Katika Mwaka 2014/2015**

| Na. | Aina ya Mkopo | Idadi ya Mkopo Bajeti 2014/2015 | Thamani (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Matrekta mapya makubwa | 84 | 3,992,000,000.00 |
| 2. | Matrekta ya mkono *(Power tillers)* | 22 | 276,000,000.00 |
| 3. | Pembejeo za Kilimo/Mifugo | | 1,134,800,000.00 |
| 4. | Zana za Umwagiliaji | 8 | 320,000,000.00 |
| 5. | Mashine za uvunaji *(Combine Harvester)* | 2 | 300,000,000.00 |
| 6. | Mashine za Usindikaji | 8 | 320,000,000.00 |
| | **JUMLA** | | **6,342,800,000.00** |

*Udhibiti wa Visumbufu vya Mazao na Mimea*

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, ilidhibiti visumbufu vya milipuko (Viwavijeshi, Kwelea kwelea na Panya) kwa kununua na kusambaza lita 7,000 za kiuatilifu cha kudhibiti kwelea kwelea, lita 14,000 za kiuatilifu cha kudhibiti viwavijeshi, lita 2,500 za kiuatilifu cha kudhibiti nzige wekundu na lita 400 za kiuatilifu cha kudhibiti panya.  Milipuko hiyo ilitokea na kudhibitiwa katika Wilaya za Singida

Vijijini, Mkalama, Ikungi, Dodoma Mjini, Mpwapwa, Kongwa, Bahi, Chamwino, Kilosa, Mvomero, Morogoro Mjini, Kilindi, Kibaha, Handeni, Njombe, Ruangwa, Mkuranga, Bagamoyo, Kisarawe, Rufiji, Lindi na Kilwa. Wilaya nyingine ni Nzega, Igunga, Shinyanga Vijijini, Kishapu, Moshi, Rombo, Hai, Siha, Arumeru, Karatu, Hanang, Simanjiro, Monduli na Mbulu.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea na ukaguzi wa mazao yanayoingizwa nchini na yanayosafirishwa nchi za nje katika vituo vya mipakani; kusajili viuatilifu; kusajili na kukagua wafanyabiashara wa viuatilifu; na kutoa vibali vya kuingiza viuatilifu nchini. Kazi nyingine ni pamoja na kudhibiti visumbufu vipya (*invasive species*) ikiwemo kudhibiti mdudu hatari anayeshambulia matunda (nzi wa matunda – *Bactrocera invadens*) ambapo lita 400 za kivutia wadudu zilinunuliwa. Vilevile Wizara imeendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya viuatilifu na kueneza mbinu mbalimbali za Udhibiti Husishi. Kazi ya kusambaza wadudu walawangi (*biological control agents*) ambao hudhibiti visumbufu kibaiyolojia ilifanyika.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuchunguza na kudhibiti milipuko ya wadudu, nzige, kwelea kwelea, panya, viwavi jeshi na magonjwa ya mimea. Aidha, Wizara itaandaa na kueneza teknolojia ya kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao *(Integrated Pest Management)* ya mahindi, mpunga, pamba, kahawa, mboga na viazi katika Halmashauri 20. Wizara pia, itaviwezesha vituo 20 vya mipakani vya sehemu ya Afya ya Mimea kuweza kukagua kwa ufanisi mazao yanayopitishwa. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kwa Wakaguzi 50 na Wakufunzi 50 juu ya viwango vya kimataifa kuhusu usafi wa mazao na jinsi ya kudhibiti visumbufu vipya *(Invasive Species Pest Management - ISPM)*.

***Huduma za Ugani***

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI iliendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa kuboresha uenezaji wa teknolojia za kisasa katika kilimo kwa kutumia Mbinu Shirikishi ambapo Mashamba Darasa yameongezeka kutoka 16,330 katika mwaka 2012/2013 yenye wakulima 344,986 hadi 16,512 mwaka 2013/2014 yenye jumla ya wakulima 345,106 katika mikoa 25 nchini. Mafunzo kupitia Shamba Darasa yalilenga kuwapatia wataalamu wa kilimo na wakulima mbinu za kilimo bora na teknolojia mbalimbali kwa mazao yanayolimwa katika maeneo yao. Mbinu hii imewawezesha wataalamu wa ugani kuwafikia wakulima wengi kwa wakati mmoja.

**Mheshimiwa Spika,** wakulima 21,604 wamepatiwa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga, muhogo na ngano. Mafunzo yalihusu: kanuni za kilimo bora; kilimo shadidi cha mpunga (SRI); uzalishaji wa mbegu bora za mpunga za QDS;

kilimo cha kibiashara; usindikaji; upatikanaji wa masoko; mikopo na mbinu za uendeshaji wa vikundi. Mafunzo yalitolewa kwa njia za ziara za mafunzo; mashamba ya maonyesho; majukwaa ya ubunifu na siku ya mkulima shambani.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara iliingia mikataba na Shirika la Utangazaji la Tanzania (TBC), Radio Binafsi saba na kampuni ya mawasiliano ya *NURU Infocom* katika kurahisisha ufikishaji teknolojia na upatikanaji wa taarifa za masoko kwa wakulima kwa ufanisi zaidi. Jumla ya vipindi vya radio 122 vilirushwa kupitia TBC Taifa (52) na radio binafsi za jamii (70) kuhusu kanuni za kilimo bora. Aidha, wakulima 36 kutoka Halmashauri za Wilaya za Kilombero, Mvomero na Kilosa walifundishwa na *NURU Infocom* namna ya kutumia simu za viganjani katika kupata taarifa za kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015 Wizara imepanga kuanzisha mashamba darasa na mashamba ya mfano 20,000 yenye wakulima 500,000 yakiwemo mashamba darasa 117 ya zao la mpunga kwenye skimu za umwagiliaji 30 zinazotekeleza BRN. Wizara kwa kupitia PHRD itawezesha wakulima wa mpunga 5,000 wakiwemo vijana kutoka mikoa ya Mbeya, Morogoro na Iringa na kuwaunganisha kwenye vikundi ili waweze kuzalisha kibiashara kwa kuwafundisha mbinu bora za uzalishaji, usindikaji na utafutaji wa masoko. Wizara pia itahamasisha vikundi 20 vya vijana kushiriki katika kilimo cha kibiashara, uanzishaji na uendelezaji wa vikundi vya usindikaji katika mazao na itaendelea kuwezesha vijana waliopatiwa mafunzo ili kila mmoja ashiriki kikamilifu katika kilimo cha kibiashara. Vilevile, Wizara itaandaa mitaala ya kufundishia wakulima wadogo wa nje (*outgrowers*) wanaozunguka mashamba ya wakulima wakubwa (*nucleus farmers*) kwa mazao ya mpunga, miwa na mahindi.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa kutumia mkulima kiongozi kuwafundisha wakulima wenzake (*Farmer-to-Farmer Extension*) kwa kutoa mafunzo kwa wakulima ili waweze kusimamia uzalishaji wa mpunga katika skimu 39 za umwagiliaji katika mikoa 10 ya BRN na wakulima wa mazao ya mahindi, muhogo, ngano, matunda, mbogamboga na mazao ya mbegu za mafuta. Wizara kupitia EAAPP na PHRD itatoa mafunzo kwa wakulima wawezeshaji 850 na wataalam wa ugani 384 ambao nao wataweza kuwafundisha wakulima wengine.

***Mafunzo kwa Wakulima Wawezeshaji na Maafisa Ugani***

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014 Wizara ilitoa mafunzo maalum kwa wakulima wawezeshaji kuhusu kilimo bora cha zao la mpunga kupitia miradi ya EAAPP na PHRD. Jumla ya wakulima wawezeshaji 710 na Maafisa Ugani 76 kutoka katika Halmashauri za Wilaya za Kyela, Kilombero,

Mbarali, Kilosa, Mvomero, Bunda na Sengerema walipatiwa mafunzo hayo ili waweze kufundisha wakulima wengine. Aidha, Wizara kupitia miradi hiyo imehamasisha jumla ya vijana 432 kutoka katika Mikoa ya Morogoro, Mbeya, Mwanza, Katavi, Iringa na Pwani kushiriki katika kilimo cha kibiashara. Uteuzi wa vijana ulizingatia maeneo ya BRN na ushiriki wao katika kilimo, lengo likiwa ni kubaini mahitaji ya vijana katika kilimo cha mpunga, changamoto na kutafuta ufumbuzi kwa kushirikiana na uongozi katika Halmashauri na vijiji husika.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha na kurahisisha mfumo wa upelekaji teknolojia kwa wakulima, Wizara inajenga Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata 319 katika Halmashauri 106 kwenye mikoa 20. Kati ya Vituo hivyo, 224 vimekamilika na vimeanza kutoa mafunzo kwa wakulima na wafugaji. Wizara pia kupitia *EAAPP* imeviwezesha vituo sita vya Kiberege - Morogoro, Kajunjumele - Kyela, Msanzi -Rukwa, Sadani - Iringa, Nyakasungwa - Mwanza na Kisangwa - Mara kwa kuvipatia vitendea kazi vya ofisi. Aidha, vituo vingine vinaendeshwa na Sekta Binafsi chini ya Programu ya ONE-UN katika mkoa wa Lindi na taasisi za VECO ya Chunya, *PAFOEL – Ukerewe, CoRDS – Longido na Concern* iliyoko Kilolo ambapo jumla ya wakulima 31,640 wamepatiwa mafunzo ya kilimo cha mazao, mifugo na uvuvi kwenye vituo hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, Wizara ilishiriki kikamilifu katika sherehe za Nane Nane 2013 Kikanda na Kitaifa. Katika sherehe za kitaifa Wizara ilipata ushindi wa nafasi ya Pili katika kundi la Sekta ya **Uchumi na Uzalishaji.** Wizara na taasisi zake za ASA na Bodi za Chai, Korosho na Kahawa pamoja na Kampuni za Mbolea za *YARA Tanzania Ltd*. na *Minjingu Mines & Fertiliser Co* walitoa zawadi kwa washindi Wakulima Bora wa Mazao watatu na Wamwagiliaji Bora watatu zenye thamani ya Shilingi 15,833,000 ikiwa ni fedha taslimu, mbolea, mbegu, vifaa vya umwagiliaji pamoja na vikombe.

**Mheshimiwa Spika,** mwaka 2007/2008 Wizara ilifanya tathmini ya Maafisa Ugani na kubaini kuwa walikuwepo Maafisa Ugani 3,379 ambapo mahitaji halisi yalikuwa jumla ya maafisa ugani 15,082. Kati ya hao, maafisa ugani 2,855 walihitajika katika ngazi ya Kata na 12,227 katika ngazi ya kijiji. Katika kukabiliana na upungufu huo Wizara iliandaa Mpango wa Kuimarisha Huduma za Ugani, ambao ulijumuisha kusomesha na kuajiri Maafisa ugani, ili ifikapo mwaka 2015 kila kijiji kiwe na Mtaalam wa Kilimo (Afisa Ugani). Katika kutekeleza mpango huo Wizara ilijiwekea mkakati wa kuongeza udahili wa wanafunzi wa ngazi ya Astashahada na Stashahada katika vyuo vya Kilimo. Hadi kufikia Juni 2013 wataalam waliohitimu mafunzo ya Kilimo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ni 8,659.

Kati ya hao walioajiriwa ni 4,595 sawa na asilimia 53. Kwa ajira hizo idadi ya Maafisa ugani nchi nzima ni 7,974, bado kuna upungufu wa Maafisa Ugani 7,108 kufikia lengo la 15,082, kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 6.**

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**Jedwali Na. 6: Idadi ya Maafisa Ugani Nchini hadi Juni 2013**

| Na. | Kada | Vituo | Mahitaji | Waliopo | Upungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Astashahada | Vijijini | 12,227 | 5,119 | 7, 108 |
| 2 | Stashahada | Kata | 2,855 | 2,855 | 0 |
| | **Jumla** | | **15,082** | **7,974** | **7, 108** |

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Serikali ilitoa kibali cha ajira kwa Sekta ya Kilimo chenye nafasi 1,804. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2014 Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imeweza kuwapanga wataalam 1,382 kwa waajiri ambapo kati ya hao wahitimu wa Astashahada ni 881, Stashahada 284 na Shahada 217.

Aidha, wahitimu 422 hawajaajiriwa. Wizara inaendelea kuwasiliana na Sekretarieti ya Ajira ili ikamilishe kuajiri wahitimu waliosalia kulingana na kibali cha ajira kilichotolewa. Iwapo nafasi zote za kibali ngazi ya Kijiji zitajazwa itaongeza idadi ya wagani walio kwenye ajira kufikia 9,558, hii ni sawa na kubakiwa na upungufu wa Maafisa Ugani 5,524 ili tufikie lengo.

**Utafiti**

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Wizara iliidhinisha aina mpya 13 za mbegu za mazao ya maharage ya soya (2); njugumawe (4); mahindi (3) na viazi vitamu (4) ambazo zimegunduliwa katika Vituo vya Utafiti vya Umma vya Uyole, Ilonga na Ukiriguru. Aidha, aina mpya 14 za mbegu za mazao kutoka Taasisi binafsi zinazojishughulisha na utafiti wa kilimo zimeidhinishwa. Mbegu hizo ni mtama (2) , mahindi (4), tumbaku (4) na kahawa (4). Wizara pia ilizalisha jumla ya kilo 217,860 za mbegu mama *(pre - basic seeds)* kukidhi mahitaji ya ASA ili kuweza kuzalisha mbegu za msingi (basic seeds) kwa lengo la kuzipatia kampuni za mbegu kuzalisha mbegu zilizoidhinishwa *(certified seeds)* kwa ajili ya matumizi ya wakulima. Mbegu mama zilizozalishwa ni: ngano kilo 16,100; mpunga kilo 1,500; mahindi kilo 127,460; maharagwe kilo 1,380; kunde kilo 3,320; pamba kilo 14,400; njugumawe kilo 800; ufuta kilo 2,000; dengu *(chickpeas)* kilo 900; na korosho (*polyclonal seeds*) kilo 50,000. Vilevile, vipando bora vimeendelea kutolewa na kusambazwa kwa wakulima kwa mazao ya: korosho *(grafts)* miche 120,000; pingili za muhogo 1,598,867; marando ya viazi vitamu 177,832; zabibu vipando 200,000; viazi mviringo vipando 14,102 na miche ya migomba 7,650.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara pia imetoa teknolojia za agronomia katika udhibiti wa magugu ya majani mapana na membamba katika kilimo cha mpunga ambazo ni kwa kutumia viuagugu vya *tillergold* kwa kiwango cha lita moja (1) kwa hekta na *solito* kwa kiwango cha lita moja na nusu (1.5) kwa hekta zote kwa kunyunyuziwa baada ya majani na mazao kuota. Katika maendeleo ya matumizi ya bayoteknolojia Wizara imegundua mbinu za uzalishaji wa miche bora kwa kutumia chupa *(tissue culture and micropropagation)* ambazo zimewezesha uzalishaji wa miche mama ya migomba, muhogo, viazi vitamu na viazi mviringo vyenye ubora. Pia bayoteknolojia imeongeza ufanisi wa uchunguzi wa magonjwa ya mimea na kuharakisha uchunguzi wa uhakika wa magonjwa ya batobato na michirizi ya kahawia kwenye muhogo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014 utafiti wa mizania ya mazao (*farm budgets*) ulifanyika kwa wakulima wa Kanda za Mashariki, Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini. Utafiti huo ulibaini kwamba wakulima waliopanda mbegu bora za mahindi na kuzingatia kilimo cha kitaalamu katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini walipata faida ya Shilingi 1,238,000 kwa hekta ambayo ni mara 3.8 zaidi ya wale wasiozingatia kilimo cha kitaalam. Vilevile, wakulima waliopanda mbegu bora za mpunga kwa maeneo ya umwagiliaji na kuzingatia ushauri wa kitaalamu walipata faida ya Shilingi 3,361,000 kwa hekta mara 3.3 ya mavuno kwa wasiozingatia utaalamu.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia Mradi wa Uzalishaji wa Uongezaji Tija katika Kilimo Mashariki ya Afrika (EAAPP), utafiti wa mnyororo wa thamani ya zao la mpunga uliendelea kufanyika katika Kanda za Ziwa (Rorya na Maswa), Mashariki (Mvomero na Kilombero) na Nyanda za Juu (Mbarali na Kyela). Mafunzo yalitolewa kwa wadau 388 (Wanaume 272 na Wanawake 116) kuhusu namna ya kuongeza faida, ubora wa mpunga, kupata masoko na kilimo biashara. Aidha, vikundi 69 vya wakulima 1,380 vilianzishwa na kusajiliwa. Vilevile, uboreshaji wa Kituo cha KATRIN kuwa Kituo Mahiri cha Mpunga katika Ukanda wa Mashariki ya Afrika umefikia asilimia 61. Watafiti 16 wameendelea na mafunzo ya Shahada za Juu za uzamivu – *Ph.D. 11* na uzamili – *MSc. 5* katika Vyuo Vikuu mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuwaongezea uwezo katika fani na kuwa mahiri katika utafiti wa kilimo. Aidha, kwa kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* jumla ya watafiti 17 wamechaguliwa kuanza masomo ya shahada za juu – *Ph.D. 1; MSc. 16.*

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015 Wizara itaendelea na utafiti wa kugundua mbegu bora za mazao, kuzalisha mbegu mama *(pre-basic seed)* za mazao kiasi cha tani 10 kwa mazao ya nafaka, mikunde, mbogamboga na mbegu za mafuta pamoja na pingili 2,000,000 za mazao ya mizizi. Aidha tani 8 za mbegu mama za mpunga zitazalishwa kutoka kituo cha KATRIN ili ziweze

kutumika katika uzalishaji wa mbegu bora na kusambazwa kwa wakulima kupitia Taasisi za Umma na binafsi zinazozalisha mbegu nchini kwa madhumuni ya kukidhi mahitaji katika maeneo yaliyobainishwa katika Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)*.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mradi wa '*Expanded Rice Production Project'* ilihakiki mbegu mpya 13 za mpunga pamoja na teknolojia nyingine 5. Uhakiki huu utafanyika katika skimu za umwagiliaji 40, maeneo yenye mvua za uhakika na kupeleka mpunga unaozalishwa katika maeneo ya miinuko. Aidha kwa kushirikiana na Serikali ya Ireland Wizara yangu itajenga uwezo katika usimamizi wa taarifa na usambazaji wa teknolojia za kilimo kupitia vitengo unganishi vya utafiti ugani na wakulima vya Kanda (ZIELUs) kwa lengo la kufikisha teknolojia za Kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015 Wizara itafanya utafiti kwa mtazamo wa mnyororo wa thamani ili kutathmini aina ya mazao mapya yanayoibuka kwa biashara kama vile kakao, matofaa, maparachichi ili kuweza kupata aina zinazofaa kwa wakulima katika kanda za uzalishaji za ikolojia za kilimo hapa nchini. Utafiti wa kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa mazao utaendelea ili kuhakikisha kuwa mazao yanayozalishwa na wakulima wetu yanakuwa na ubora unaotakiwa na kukidhi mahitaji ya soko. Aidha mazao yatakayotiliwa mkazo ni yale ya migomba, muhogo, mahindi na minazi.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu itaendelea na juhudi za kutekeleza mikakati ya kutokomeza magonjwa ya mazao hususan ugonjwa wa unyanjano katika zao la Migomba, batobato na michirizi ya kahawia katika zao la muhogo na MLND katika zao la mahindi. Aidha, ili kutokomeza ugonjwa wa unyanjano katika zao la migomba mkoani Kagera Wizara yangu kupitia Kituo cha Utafiti Maruku itaendelea kushirikiana na uongozi wa mkoa wa Kagera katika kampeni yake ya "TOKOMEZA UGONJWA WA MNYANJANO MKOANI KAGERA"

**Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya vipando bora visivyo na vimelea vya ugonjwa ni moja ya njia muhimu za kuthibiti maambukizi katika mashamba ya migomba. Kwa hiyo, Wizara yangu kupitia Vituo vyake vya Utafiti itashirikiana na maabara ya Tishu ya binafsi ya *"Crop Bioscience Solution Limited"* ya Arusha ili kuzalisha miche ya migomba bora kwa njia ya tishu (tissue culture) na kuisambaza kwa wakulima wa mkoa wa Kagera kwa ruzuku. Miche hiyo ni ya aina ya migomba ya ndizi zinazopendwa na walaji wa Mkoa wa Kagera kama vile Enshakala na Enyoya.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa magonjwa ya muhogo ya Batobato na Michirizi ya kahawia. Wizara kwa kuvitumia Vituo vyake vya Utafiti itaendelea kuzalisha vipando vya muhogo visivyo na magonjwa hayo (clean

planting cuttings) vya mbegu ya muhogo aina ya *Mkombozi* na kuvisambaza kwa wingi katika maeneo makubwa katika Wilaya za Mkoa wa Mara ambako mashambulizi ya magonjwa haya ni makubwa. Kazi hii itafanyika kwa kutumia uzoefu uliopatikana Wilaya ya Ukerewe ambapo magonjwa hayo sasa yametokomezwa. Aidha, Wizara yangu itaendelea kufanya Utafiti wa uhandisi jeni ili kuziwekea ukinzani aina za muhogo zinazopendwa na walaji. Vile vile Utafiti kwa njia za kawaida utaendelea ili kutoa mbegu zaidi zenye ukinzani wa magonjwa hayo muhimu katika zao la muhogo.

Katika Mwaka wa 2014/15, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)* itatekeleza Mradi wa Kudhibiti Ugonjwa wa *Maize Lethal Necrotic Disease* katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara wenye thamani ya Dola za Kimarekani *(USD)* 103,000. Mikoa hii ndiko ambako ugonjwa umeanza kuonekana na ni mikoa muhimu kwa uzalishaji wa mbegu za mahindi nchini. Lengo kubwa ni kuudhibiti na kuzuia ugonjwa huu usienee katika mikoa mingine. Kazi zitakazofanyika katika mradi huu ni pamoja kuunda kikosi kazi cha kusimamia udhibiti, kutengeneza mkakati na muongozo wa pamoja wa kitaifa wa kudhibiti ugonjwa, mpango kazi wa udhibiti ngazi ya Wilaya na usimamizi wa Sheria na Kanuni za udhibiti.

Sambamba na mradi huu, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la *Centre for Agricultural Biosciences International (CABI)* inatekeleza pia Mradi wa Zahanati ya Afya ya Mimea *(Plant Clinics)* ikiwa ni hatua muhimu ya kusogeza huduma za kuwafundisha wakulima kutambua matatizo ya kiafya ya mazao yao na njia za kuyatatua kwa haraka zaidi katika mashamba yao. Hadi sasa mradi unatekelezwa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Tanga (Lushoto), Pwani, Dar-es-salaam, Morogoro, Dodoma na Iringa. Pamoja na jitihada hizi, Wizara inasisitiza kuwa wakulima watumie mbegu zilizothibitishwa ubora na TOSCI.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara pia itafanya utafiti wa rutuba ya udongo, kilimo mseto na kurekebisha ramani zilizoko kwenye mfumo wa kijiografia (*GIS*) ili ziweze kusaidia wadau kuwekeza katika kilimo hapa nchini. Vilevile Wizara kupitia Mradi wa *EAAPP* itaendelea kuimarisha uzalishaji wa teknolojia za mpunga, muhogo na ngano na kuhakikisha kuwa teknolojia hizo zinasambazwa katika nchi zingine zilizoko katika mradi huo ikiwa ni pamoja na Kenya, Uganda na Ethiopia. Aidha, chini ya mradi huu, teknolojia zitakazozalishwa katika nchi hizo, vile vile zitaletwa hapa nchini kwa matumizi ya wakulima na wadau wengine.

*Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo – ASDP.*

**Mheshimiwa Spika,** awamu ya kwanza ya utekelezaji wa ASDP iliyoanza Julai 2006 ilikamilika mwezi Juni 2013; na mwaka 2013/2014 ni kipindi cha mpito ambapo kazi muhimu ambazo hazikukamilika ndizo zinazoendelea kutekelezwa

wakati Wizara za Sekta ya Kilimo zikiendelea na mchakato wa kuandaa awamu ya pili ya ASDP. Taarifa rasmi ya kutathmini kuhusu utekelezaji wa ASDP nchini kote; yaani *Implementation Completion Report* (*ICR*) iliyofanyika kati ya mwezi Desemba 2013 hadi Februari 2014 imeonesha mafanikio ya kuridhisha katika utekelezaji wa programu hiyo. Jumla ya skimu 1,325 za umwagiliaji zilikarabatiwa na kujengwa, Maafisa ugani 6,785 walipata mafunzo, mashamba darasa 64,469 yalianzishwa, wakulima 774,156 walipewa mafunzo na watoa huduma za ugani binafsi 441 walipewa mikataba. Jumla ya magari 100, pikipiki 1,612 na baiskeli 3,389 zilisambazwa katika halmashauri 85 kwa ajili ya kuwezesha maafisa ugani kufanya ufuatiliaji na usimamizi.

**Aidha,** Vituo vya Rasilimali vya Kata vya Kilimo 166 (*Ward Agricultural Resource Centres – WARC*) vilianzishwa na kompyuta 475 na *printers* zake zilinunuliwa kwa ajili ofisi za maafisa ugani. Jumla ya kilometa 31,813 za barabara za vijijini zilikarabatiwa na kujengwa, maghala 698 ya kuhifadhi mazao yalijengwa, masoko ya msingi 365 yalijengwa, masoko madogo ya mifugo 46 yalijengwa na mabanda 336 ya kuanika na kukausha ngozi za mifugo yalijengwa. Aidha, malambo 1,008 na visima vya maji 80 vilijengwa, matrekta makubwa 65, matrekta madogo ya mkono 1,972 na plau 1,321 yalipatikana. Vilevile, vituo vya maksai 105 vilianzishwa, maabara za wanyama 104 na majosho 2,364 yalijengwa. Pia mashine za kusagisha 13,525 zilipatikana pamoja na mashine 626 za kukamua mafuta. Maghala 170 yanayotumia mfumo wa stakabadhi yalianzishwa katika Halmashauri 26 na idadi ya makampuni yanayotumia *Tanzania GS1 barcode system* yaliongezeka kutoka 120 hadi 515. Aidha, bidhaa zilizosajiliwa zinazotumia *barcode* ziliongezeka kwenye soko kutoka 2,200 hadi 9,942.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa yote yaliyotajwa hapo juu umewezesha kufikiwa kwa kiwango kikubwa malengo makuu mawili ya ASDP ambayo ni (i) kuwezesha wakulima kupata na kutumia elimu ya kilimo, teknolojia, mfumo wa masoko na miundombinu ambavyo vyote vinachangia katika kuongeza tija, faida na kipato, na (ii) kuhamasisha uwekezaji binafsi katika kilimo pamoja na mazingira bora ya sera na sheria katika kilimo. Kwa mfano asilimia ya wakulima wanaofikiwa na huduma bora za kilimo na miundombinu imeongezeka kutoka 35 hadi 45, ushauri wa mifugo kutoka 16 hadi 21 na matumizi ya umwagiliaji kutoka 8 hadi 10. Aidha, uwekezaji binafsi katika kilimo umekuwa ukikua kwa wastani wa asilimia 5 kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya mafanikio hayo, utekelezaji wa ASDP ulikabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo za kutokukamilika kwa miradi mingi ya ujenzi wa skimu za umwagiliaji; kuwepo fedha ambazo hazijatumika kwa muda mrefu kutokana na ukosefu wa wataalam wa kusanifu na kujenga miradi; viwango hafifu vya ujenzi vinavyosababisha miradi kukarabatiwa mara kwa mara; wanufaika kushindwa kuchangia gharama za uendeshaji na

ukarabati; kutokuhifadhiwa kwa vyanzo vya maji; usanifu wa ujenzi unaozingatia mikoa badala ya kanda za ekolojia na usimamizi hafifu wakati wa ujenzi wa miundombinu ya skimu za umwagiliaji. Maeneo hayo yanaendelea kutekelezwa katika kipindi hiki cha mpito mwaka 2013/2014 na yatasimamiwa kikamilifu wakati wa utekelezaji wa awamu ya pili ya ASDP.

***Mashamba ya kilimo cha kibiashara kwa mazao ya mpunga na miwa***

Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha kupatikana kwa Mashamba Makubwa ya uwekezaji kupitia Mpango wa Tekeleza Matokeo Makubwa Sasa, hatua iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Mashamba mawili (2) kati ya saba (7) yaani *Bagamoyo Eco-Energy* na Mkulazi yamepewa hati miliki (*Title Deeds*) kutoka Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

(ii) Shamba la *Bagamoyo Eco-Energy* kwa ajili ya kilimo cha miwa limezinduliwa tarehe 15/03/2014 na mwekezaji ameanza kazi.

(iii) Shamba la Mkulazi limegawanywa katika maeneo ya uzalishaji wa mpunga na miwa na taratibu za kupata wawekezaji zinaendelea.

(iv) Mashamba ya Ngalimila, Lukulilo na Rufiji Delta yamefikia hatua ya kuhawilishwa kutoka ardhi ya kijiji kwenda ardhi ya kawaida. Mashamba mawili (2) yaliyobaki Muhoro na Tawi ya Wilaya ya Rufiji yapo katika hatua za upimaji ili yaweze kuendelea na taratibu za kupatiwa hati miliki.

(v) Taratibu za kuwahusisha Wakulima Wadogo na vijiji vinavyozunguka katika mashamba ya Ngalimila, Lukulilo na Bagamoyo zimefanyika kwa kuwawezesha wakulima hao kutengeneza mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na kuwapatia Hati za Kimila *(Customary Certificates of Rights of Occupancy - CCRO)*. Vijiji hivyo ni Kipugila, Kipo, Nyaminywili na Ndundunyikanza katika Wilaya ya Rufiji, vinavyozunguka shamba ya Lukulilo. Vingine ni Ngalimila, Mpanga, Kamwene, Utengule, Ipugasa, Mlimba, Idwindembo, Matema, Viwanja Sitini, Miembeni, Msolwa na Ngombo vinavyozunguka shamba la Ngalimila.

(vi) Kukamilisha mipango ya kina ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vya Wilaya ya Rufiji na taratibu za kutangaza katika gazeti la Serikali kwa mashamba ya Tawi hekta 9,365.59 na Muhoro hekta 3,915.85.

(vii) Shamba la Mkongo jumla ya hekta 5,510.89 zimepatikana kwa ajili ya uwekezaji ambapo kampuni ya *Frontline Development Partners* imeonesha nia ya kuwekeza katika eneo hilo.

(viii) Shamba la Muhoro Rufiji zimepatikana hekta 3,915.85 kwa ajili ya uwekezaji ambapo Kampuni ya *Agroforestry* imeonesha nia ya kuwekeza.

(ix) Kwa upande wa bonde la Malagarasi, mashamba mawili yamepatikana katika maeneo ya Kasulu hekta 47,000 na Kibondo hekta 25,000 ambapo Kampuni ya Kigoma Sugar imeonesha nia ya kuwekeza katika eneo la Kasulu. Aidha, taratibu muhimu za kuhaulisha eneo la Kasulu kutoka ardhi ya kijiji kuwa ardhi kwa ajili ya uwekezaji zinaendelea.

***Kambi ya Vijana ya Kilimo Mkongo, Rufiji***

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilianzisha kambi ya mafunzo ya kilimo kwa vijana kwa kukarabati majengo 11 katika eneo la Mkongo, Wilayani Rufiji ikiwa na lengo la kuhamasisha vijana kushiriki katika Kilimo cha umwagiliaji kibiashara. Kambi hiyo ilizinduliwa rasmi tarehe 5 Oktoba, 2013 na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kambi hiyo imeshatoa mafunzo ya kilimo kwa vijana 50. Wizara kupitia RUBADA itaendeleza vijana kwenye Kituo cha Kilimo katika kambi ya Mkongo, Rufiji na kujenga miundombinu katika mashamba ya vijana katika kituo hicho katika mwaka 2014/2015.

**Kuongeza Upatikanaji wa Masoko ya Mazao ya Kilimo.**

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo umekuwa ni changamoto kubwa katika kuchochea uzalishaji endelevu. Aidha, mfumo wa masoko ya mazao ya kilimo unakabiliwa na kukosekana kwa taarifa sahihi za bei na miundombinu mibovu. Ili kuhakikisha wakulima wanapata bei nzuri ya mazao, Serikali katika mwaka 2013/2014 ilifanya yafuatayo:-

(i) Katika kukabiliana na changamoto ya kupanda na kushuka kwa bei za mazao ya biashara katika Soko la Dunia, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa mazao husika inaandaa utaratibu wa kuanzisha Mfuko Maalum wa Kufidia Bei za Mazao (*Price Stabilization Fund)* kwa ajili ya kusaidia wakulima pindi bei ya mazao inaposhuka katika Soko la Dunia. Katika mwaka 2014/2015 Wizara itawasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya kuanzisha Mfuko wa Kufidia Bei za Mazao.

(ii) Wizara inashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuanzisha Soko la Bidhaa na Masoko ya Mazao *(Commodity Exchange)*. Aidha, ili kufanikisha

mfumo huo utakapoanza, Wizara kupitia BRN imeanza mpango wa kujenga na kukarabati maghala 275 ya Mahindi katika awamu tatu (3) kama Jedwali Na. 7 linavyoonyesha. Maghala hayo yataunganishwa na Soko la Bidhaa na Masoko ya Mazao

**Jedwali Na. 7: Mpango wa Maghala 275 ya Mahindi 2013/2014-2015/2016**

| **Mwaka wa Fedha** | **2013 /2014** | **2014 /2015** | **2015 /2016** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Maghala Yatakayojengwa/ kukarabatiwa | 30 | 145 | 100 | 275 |

**Mheshimiwa Spika,** maeneo ya utekelezaji katika miaka mitatu (3) hadi kufikia 2015/16, Idadi ya Maghala kwa kila Mkoa na Wilaya ni kama inavyooneshwa kwenye**.** Tathmini ya maghala 275 katika mikoa 6 na wilaya 12 kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 7 imekamilika. Mpango wa ukarabati wa Maghala 30 umeanza katika Mkoa wa Mbeya kwenye Wilaya za Mbozi (maghala 26 katika vijiji 26) na Momba (maghala 4 katika vijiji 4). Aidha, Mtoa Huduma *(Service Provider)* ambaye atafanya kazi na wakulima katika vijiji 30 vilivyochaguliwa katika Wilaya hizo amepatikana na ameingia mkataba na kuanza kazi mwanzoni mwa mwezi Mei, 2014.

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa maghala mawili ya NFRA ya Songea na Mbozi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 kila moja unaendelea. Aidha, Wizara inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya Masoko ya kimkakati (*Strategic Markets*) matano ambayo yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi katika maeneo ya Busoka (Kahama), Kabanga (Ngara), Sirari (Tarime), Nkwenda na Murongo (Karagwe).

***Ununuzi Kupitia Wakala wa Hifadhi wa Taifa ya Chakula***

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, *NFRA* imepanga kununua jumla ya tani 200,000 za nafaka zikiwemo tani 190,000 za mahindi na tani 10,000 za mpunga ili kuongeza wigo wa uhifadhi wa mazao ya chakula na kuchangia katika kupunguza mfumuko wa bei za vyakula katika masoko ya mijini. Wakala pia utaendelea na mipango ya kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao ya chakula kwa kujenga ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 za nafaka katika kanda ya Songea.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, NFRA imepanga kuanzisha kanda mpya ya Kigoma itakayo hudumia mikoa ya Kigoma, Kagera, Geita na Tabora kupunguza majukumu kwa Kanda ya Shinyanga ambayo kwa sasa inahudumia mikoa minane ya Kanda ya Ziwa. Wakala pia umepanga pindi barabara ya lami kutoka Songea hadi Mtwara itakapokamilika, mikoa ya Lindi na Mtwara itapata huduma zake kutoka katika Kanda ya Songea badala ya Kanda ya Kipawa (Dar es Salaam).

***Kuimarisha Uongezaji wa Thamani na Usindikaji wa Mazao ya Kilimo***

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza lengo mkakati hilo, katika mwaka 2013/2014, kazi zilizopangwa kutekelezwa zinajumuisha kuboresha teknolojia za usindikaji na uhifadhi wa mavuno (*post harvest handling/technologies)*; ufungashaji na kujenga vituo vya kuhifadhi na kukusanya mboga na matunda. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na *Tanzania Horticultural Association* (*TAHA*) ilijenga na kukarabati miundombinu ya kukusanya na kuhifadhi mazao ya bustani katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro. Vituo vilivyojengwa ni pamoja na Midawe (Arusha), Kikas (Hai), Makiba (Arumeru) na Mabilioni (Same). Vituo vya Rundugai na Kawaya (Hai) vilikarabatiwa.

**Mheshimiwa Spika,** katika mpango wa kuwawezesha wakulima wa mboga na matunda kupunguza upotevu, kuongeza thamani, kupata bei nzuri za mazao yao na kuongeza uhakika wa chakula, Wizara pia imejenga jengo la kuhifadhia mbogamboga na matunda *(packhouse)* na kuwapatia *kontena* la baridi *(refrigerated container)* la kuhifadhia mbogamboga na matunda vikundi 81 vya wakulima wa mbogamboga na matunda katika Halmashauri za Wilaya za Lushoto na Korogwe katika Mkoa wa Tanga. Aidha, Wizara imetoa mafunzo ya hifadhi bora na usindikaji wa mazao hayo kwa wawakilishi wa vikundi vya wakulima 200 katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeainisha vikundi 10 vyenye jumla ya wakulima 360 vya wasindikaji wadogo wa mbegu za mafuta ya alizeti kutoka katika Halmashauri za Wilaya za Iramba, Manyoni, Mkalama, Singida, Ikungi na Manispaa ya Singida katika Mkoa wa Singida na kuwapatia mashine 10 za kukamua na kusafisha mafuta ili kuongeza ubora. Vilevile, Wizara imetoa mafunzo kwa wanavikundi hao kuhusu hifadhi bora na usindikaji wa zao la alizeti. Chama Kikuu cha Ushirika cha Tandahimba na Newala *(TANECU)* kinajenga ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 15,000 za korosho. Ujenzi huo umefikia hatua ya kuezeka na kusakafia. Upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kubangulia tani 30,000 za korosho kwa mwaka umefanywa na *African Cashew Alliance*.

***Kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji, Uhifadhi, Uchambuzi na Usambazaji wa Takwimu***

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Misaada la Japan *(Japan International Cooperation Agency - JICA)* imeendelea kutekeleza mfumo ulioboreshwa wa ukusanyaji wa takwimu za kilimo. Chini ya mpango huo, wataalamu 8,723 wa kilimo na mifugo katika ngazi

ya vijiji na kata wamefundishwa namna bora ya kukusanya takwimu kwa kutumia fomu maalumu. Wataalamu 504 wa ngazi ya Wilaya na 50 wa Mkoa wamepewa seti 184 za kompyuta na mafunzo ya jinsi ya kutumia, kutunza, kuchambua na kusambaza takwimu. Aidha, wataalamu wa Halmashauri wamepewa pikipiki 178 kwa ajili ya kuwezesha usimamizi. Mpango huo umeanzisha mfumo unaowezesha takwimu kusafirishwa kutoka wilayani mpaka makao makuu kwa njia ya TEHAMA. Wizara inaendelea kukusanya na kuweka takwimu kwenye mfumo wa kompyuta unaojulikana kama *Tanzania Countrystat* ili kuwezesha takwimu kutunzwa vizuri kwa njia endelevu na kusambazwa dunia nzima kwa njia ya TEHAMA.

**Kusimamia Sera, Sheria na Mikakati Katika Sekta ya Kilimo**

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Taifa ya Kilimo 2013, imeshachapishwa na kusambazwa kwa wadau wa kilimo kutoka sekta ya umma na sekta binafsi ikiwa ni pamoja na wakulima, Viongozi wa Serikali, washirika wa Maendeleo na Waheshimiwa Wabunge. Sera hiyo inalenga katika kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo kwa kuongeza tija na uzalishaji wa mazao mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha usalama wa chakula na ziada kwa ajili yakuuzwa nje ya nchi. Mkazo umewekwa katika kuongeza matumizi ya pembejeo na matumizi ya teknolojia za kisasa pamoja na kushirikisha Sekta Binafsi kama mhimili katika kuongeza ukuaji wa sekta ya kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** maeneo mengine yaliyopewa umuhimu ni pamoja na usindikaji wa mazao ili kuyaongezea thamani, jinsi ya kukabiliana na athari mbalimbali katika kilimo *(risk management);* uimarishaji wa Vikundi vya Wakulima na Ushirika, uboreshaji wa masoko ya kilimo na ugharamiaji wa kilimo *(agriculture financing).* Kwa kuwa kilimo chetu kinategemea sana nguvu kazi ya wazee na wanawake, sera imeweka matamko ya sera yenye lengo la kuhamasisha vijana kujishughulisha na kilimo. Kilimo cha kibiashara kimewekewa mkazo, hususan kutekeleza masuala yatakayomsaidia mkulima mdogo au vikundi vya wakulima kuboresha kilimo ili kiwe cha kisasa na cha kibiashara; mawasiliano na matumizi ya TEHAMA katika kilimo, mbinu za ushiriki wa pamoja katika kutoa huduma zimepewa umuhimu; mfano, mfumo wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi - *Public-Private Partnerships* katika kutoa huduma za ugani na utafiti, na dhana ya Shamba Darasa *(Farmer Field Schools).*

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kutungwa kwa Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na.5 ya mwaka 2013, Wizara imeandaa mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Mbegu Na. 18 ya mwaka 2003; Sheria ya Hifadhi ya Mimea *(Plant Protection Act)* Na. 13 ya mwaka 1997; Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu vya Kitropiki *(Tropical Pestcides Research Institute Act, ya 1979 Cap. 161. R.E. 2002)*; Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Pembejeo Na. 9 ya mwaka 1994 *(Agricultural Inputs Trust*

*Fund Act)*; na Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji (*Rufiji Basin Development Authority – RUBADA Act)* Na. 5 ya mwaka 1975.

**Kuboresha Uratibu katika Sekta ya Kilimo**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inaratibu maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta *(Agricultural Sector Lead Ministries - ASLMs)* ambazo ni Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Viwanda na Biashara; na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Uratibu huo unahusisha pia utekelezaji wa ASDP ambayo inagharamiwa kupitia michango ya Washirika wa Maendeleo kwenye Kapu la Pamoja (*ASDP Basket Fund – ASDP BF*).

Pamoja na *ASDP* ipo miradi inayotekelezwa nje ya mfumo wa kapu. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na wadau inaandaa mfumo wa kuboresha uratibu katika sekta utakaotumika katika utekelezaji wa ASDP II ambayo mfumo wake wa uratibu utakuwa mpana zaidi kuweza kuratibu miradi mingi zaidi pamoja na wafadhili wake katika Sekta ya Kilimo ikiwemo hata miradi ambayo haiendeshwi kwa fedha za umma. Katika mwaka 2014/2015 Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Sekta ya Kilimo pamoja na Wabia wa Maendeleo itakamilisha maandalizi ya awamu ya pili ya ASDP ili Programu hiyo ianze kutekelezwa katika mwaka 2015/2016. Kuboresha Uwezo wa Wizara kutoa Huduma

**Mafunzo katika Vyuo vya Kilimo**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imedahili wanafunzi 2,485 (astashahada 1,858 na stashahada 627) katika mwaka wa 2013/2014. Kozi wanazosoma ni astashahada na stashahada ya kilimo mseto, stashahada ya umwagiliaji, uzalishaji chakula na lishe, matumizi ya zana katika kilimo, uzalishaji wa mazao, mboga, maua na matunda. Aidha, wanafunzi 784 (astashahada 500, stashahada 284) wanaendelea na mafunzo ya mwaka wa pili na watahitimu mwezi Juni 2014. Katika mwaka 2014/2015 Wizara itafundisha vijana 2,500 wa ngazi ya astashahada na stashahada kwa ajili ya kuongeza maafisa ugani.

***Kilimo Mtandao***

**Mheshimiwa Spika,** matumizi ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yameenea hadi vijijini kupitia simu za viganjani. Teknolojia hizi zinawezesha kutumika katika ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa habari na taarifa mbalimbali za mnyororo wa thamni kwa wadau, zikiwemo zinazohusu mbinu za uzalishaji, usindikaji na upatikanaji wa masoko kwa urahisi na haraka. Tayari yapo makampuni binafsi ambayo kwa kupitia makampuni ya simu *(TiGO,* Vodacom na Zantel) yameweka mifumo ya kusambaza taarifa za masoko ya mazao kwa wadau kwa kulipia fedha kidogo. Serikali inatambua na kuthamini mchango wao. Wizara pia inaendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa

matumizi ya TEHAMA katika kilimo, ambapo katika mwaka wa 2014/2015 imepanga kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuandaa mfumo (system) wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za kilimo katika skimu za umwagiliaji zilizomo katika Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN),* ambao utawezesha ubadilishanaji wa taarifa za kilimo baina ya wadau kwa kutumia simu za kiganjani. Katika mfumo huo, ubadilishanaji wa taarifa mbalimbali kati ya wadau (wakulima, wataalamu, wafanyabishara) utawezeshwa kwa kutumia simu za viganjani.

(ii) Kuandaa mfumo wa TEHAMA kuunganisha maghala yaliyoainishwa katika BRN (COWABAMA), ikiwa ni sehemu ya ujengaji wa mfumo mkubwa wa masoko ya kilimo kama ilivyoainishwa katika mkakati wa TEHAMA.

(iii) Mifumo hii ni mwanzo wa uwekaji wa mfumo mkubwa wa TEHAMA *(Agricultural Information System)* unaohusu kuwezesha matumizi *(leveraging)* ya TEHAMA katika mlolongo wa thamani katika kilimo kama ulivyainishwa katika mkakati wa TEHAMA katika kilimo ili kuongeza tija.

(iv) Kuandaa mfumo wa ardhi ya kilimo *(Geographical Information System)* katika maeneo ya Matokeo Makubwa Sasa – *SAGCOT*. Hii pia ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa TEHAMA.

(v) Kuendelea kuboresha zaidi Tovuti ya Wizara kwa kuweka taarifa zaidi za kilimo.

***Migogoro ya Wakulima na Wafugaji.***

**Mheshimiwa Spika,** katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji, pia wakulima na wawekezaji kutokana na ongezeko la idadi ya watu na kupanuka kwa mahitaji ya ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na ukosefu wa malisho na miundombinu ya kunywesha mifugo. Mipango ya matumizi bora ya ardhi pamoja na ujenzi wa miradi ya umwagiliaji wa mazao na malisho ya mifugo inaweza kuwa suluhisho la kudumu la kuondoa migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Kwa hiyo, kuanzia mwaka 2014/2015 Wizara itashirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, TAMISEMI na wadau wengine katika kubuni, kupanga na kuanzisha miradi hiyo.

**Kulinda Ardhi ya Kilimo**

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ina eneo la hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo. Kati ya hizo, hekta milioni 13.92 sawa na asilimia 31.6 ndizo zinazolimwa. Hali ya kutokuwepo sheria inayotambua na kulinda ardhi ya kilimo imechangia

matumizi ya ardhi yasiyo endelevu na kwa matumizi yasiyo ya kilimo, hivyo kupungua kwa ardhi yenye rutuba inayofaa kwa kilimo. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na TAMISEMI inaandaa mapendekezo ya Sheria ya Kulinda Ardhi ya Kilimo.

*Ujenzi wa Mabwawa ya Umwagiliaji na Udhibiti wa Mafuriko*

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mabadiliko ya tabianchi, tumeshuhudia maeneo mengi ya nchi hususan mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Kigoma, Mbeya, Arusha na Mara, yakikumbwa na mafuriko ya mara kwa mara ambayo husababisha uharibifu wa miundombinu, ikiwemo reli, barabara, makazi, madaraja, mashamba na kugharimu maisha ya watu na mali zao. Athari nyingine za mafuriko ni pamoja na njaa, milipuko ya magonjwa, gharama za kuhamisha na kuwatunza waathirika. Mafuriko yanayosababisha athari zote hizo yanaletwa na mito ambayo ikijengewa mabwawa makubwa kwenye maeneo yanayofaa, maji yake yanaweza kudhibitiwa na hivyo kupunguza madhara hayo *(flood control)* wakati huo huo yakatumika katika kilimo cha umwagiliaji wa mazao na malisho ya mifugo na matumizi mengine. Aidha, miradi mikubwa kama hiyo inaweza kutoa fursa kubwa ya kutatua migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Katika kukabiliana na hali hiyo, Wizara itashirikiana na Wizara za Maji, Mifugo na Uvuvi, Uchukuzi, Ujenzi na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira katika kubuni, kupanga mkakati wa pamoja wa kuanzisha miradi ya namna hiyo.

***Vyombo vya Habari na Kuhamasisha Kilimo***

**Mheshimiwa Spika,** Vyombo vya habari hususan vituo vya redio, televisheni na magazeti vimekuwa na mchango mkubwa katika kuhabarisha na kuwafikishia wananchi taarifa za maendeleo ya kilimo nchini. Mapinduzi ya Kilimo yatafikiwa ikiwa wananchi na wadau wa Sekta ya Kilimo watapata taarifa sahihi zinazohusu fursa mbalimbali zikiwemo kilimo biashara, uwekezaji, masoko na matumizi ya teknolojia za kisasa kama vile zana bora, pembejeo na matumizi salama ya viuatilifu. Aidha, vyombo vya habari vikitumiwa ipasavyo vina nafasi ya kuchangia ufikiwaji wa teknolojia sambamba na uboreshaji wa huduma za ugani. Wizara itaimarisha matumizi ya vyombo vya habari na kushirikiana na waandishi wa habari kama wadau muhimu katika kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu sera, programu na huduma mbalimbali za kuendeleza kilimo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, Wizara imedhamiria kuhamasisha waandishi wa habari za kilimo ili waanzishe Jukwaa la Waandishi wa Habari za Kilimo *(Agricultural Journalists Forum)* ambao watajengewa uwezo na uelewa wa kutosha wa masuala ya kilimo ili waweze kuandika habari zitakazochochea maendeleo ya kilimo. Msukumo utakuwa kuongeza matumizi

ya vyombo vya habari vya kijamii *(community media)* ambavyo vinapatikana na kusikika katika maeneo ya vijijini ambako hasa ndiko waliko wakulima na Watanzania walio wengi.

**Kuzingatia Masuala Mtambuka katika Kilimo**

***Mazingira***

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza Mpango Kazi wa Kimazingira wa Sekta ya Kilimo, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, *Department for International Development - DFID* na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine *(SUA)* ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha Mpango Kazi wa kuhimili na kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwa Sekta ya Kilimo. Kazi hii itakamilika ifikapo tarehe 31 mwezi Mei, 2014.

Aidha, katika kutekeleza mpango wa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN),* Wizara imefanikiwa kutengeneza Mipango ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii *(ESMPs) 14* kwa kusudi la kupunguza uharibifu wa mazingira katika vijiji vinavyozunguka mashamba ya uwekezaji ya Mpanga-Ngalimila na Lukulilo. Pia Wizara imefanikiwa kutoa mafunzo kwa Maafisa 32 wa Halmashauri 9 zinazotekeleza mpango wa BRN juu ya matumizi bora ya kemikali za kilimo, uharibifu katika vyanzo vya maji, uharibifu wa miundombinu ya umwagiliaji unaosababishwa na uingizwaji wa mifugo katika miundombinu hiyo, na teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone. Wataalamu hao ni kutoka Halmashauri za Kyela na Mbarali (Mbeya), Kilosa, Morogoro, Kilombero na Mvomero (Morogoro) Mpanda na Mlele (Katavi), na Iringa (Iringa).

***VVU na UKIMWI***

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea na jitihada za kupambana na UKIMWI na maambukizi mapya ya VVU mahali pa kazi kwa kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari na kuendelea kuwawezesha kupata dawa na vyakula vyenye virutubisho watumishi 18 wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

***Jinsia***

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na *ASARECA* ilitoa mafunzo ya Jinsia kwa watumishi (watafiti, wagani na mwakilishi wa masuala ya Jinsia Wizarani) 37 kati yao wanawake walikuwa 20 na wanaume 17, ili kuhakikisha kuwa teknolojia za kilimo zinazalishwa na kusambazwa kwa wakulima kwa kuzingatia mahitaji yao kijinsia.

**SHUKRANI**

**Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie nafasi hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Kwanza napenda kuzishukuru nchi za Japan, Ireland, China, India, Israel, Indonesia, Korea ya Kusini, Marekani, Uingereza, Misri, Ubelgiji, Malaysia, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil na Uholanzi. Nayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, CFC, AVRDC, AGRA, WARDA, Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust*, *Rockfeller Foundation* na *Unilever*. Ushirikiano na misaada ya nchi na mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki; Katibu Mkuu Bibi Sophia Elias Kaduma; Naibu Katibu Mkuu Dkt. Yamungu Kayandabila, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Raphael Daluti; Wakurugenzi wa Idara; Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara; watumishi wote wa Wizara; na wadau mbalimbali wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2013/2014 kama nilivyofafanua katika hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba, Wizara itaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2014/2015. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa hotuba hii.

## MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2014/2015

### FUNGU 43

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe Shilingi **318,738,678,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika Fungu 43 kwa mwaka 2014/2015. Kati ya fedha hizo, Shilingi **271,658,408,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **47,080,270,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, Shilingi **230,970,391,380** ni kwa ajili ya Matumizi Mengine *(OC)*, Shilingi **26,946,047,800** ni kwa ajili ya Mishahara *(PE)* ya Wizara na Shilingi **13,741,968,820** ni Mishahara *(PE)* ya Bodi na Taasisi. Kati ya fedha za bajeti ya maendeleo, Shilingi **25,000,000,000** ni fedha za ndani na Shilingi **22,080,270,000** ni fedha za nje.

### FUNGU 24

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu kupitia Fungu 24 inaomba Shilingi **6,855,413,000** kwa ajili ya shughuli za kuendeleza Ushirika

nchini. Kati ya fedha hizo, Shilingi **4,500,000,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengine *(OC)* na Shilingi **779,566,000** ni kwa ajili ya mishahara *(PE)* ya Watumishi wa Tume na Shilingi **1,575,847,000** ni kwa ajili ya mishahara *(PE)* ya Taasisi.

**FUNGU 5**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2014/2015 Wizara yangu kupitia Fungu 05 inaomba Shilingi **29,408,021,000** kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji hapa nchini. Kati ya fedha hizo, Shilingi **475,000,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Mengine (OC) na Shilingi **28,933,021,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha za bajeti ya Maendeleo Shilingi **10,000,000,000** ni fedha za ndani na Shilingi **18,933,021,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**MHE. SAID JUMA NKUMBA- MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9), Kanuni za Bunge Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 29 Aprili, 2014, tarehe 1 Mei, 2014 na tarehe 3 Mei, 2014 Kamati ilikutana na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ili kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara, Maoni na Ushauri wa Kamati Kuhusu Makisio ya Mwaka wa Fedha 2013/2014. Pamoja na Malengo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupita na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa Serikali imeyafanyia kazi Maoni ya Kamati. Kwa ujumla Kamati imeridhika na utendaji wa Wizara isipokuwa maeneo ambayo utekelezaji wake ulikwamishwa na ucheleweshaji au ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara ilikumbana na changamoto zifuatazo:-

(a) Ufinyu wa Bajeti na mtiririko wa fedha usioridhisha uliochangia kutofikiwa kwa malengo katika kipindi husika. Kwa mfano fedha zilizopokelewa

hadi kufikia mwezi Machi, 2014 ilikuwa shilingi bilioni 210.5 ambazo ni sawa na asilimia 63 kati ya bilioni 349.23.

(b) Upatikanaji mdogo wa fedha za mikopo ya mfuko wa pembejeo. Kwa mfano mfuko wa pembejeo ulitengewa kiasi cha shilingi bilioni tatu (bilioni 3) tu ukilinganisha na mahitaji halisi ya Shilingi bilioni nane (Bilioni 8) kwa mwaka.

(c) Uchache wa maafisa Ugani, maafisa Ushirika, mafundi mchundo na wakaguzi wa mazao ukilinganisha na mahitaji halisi.

(d) Elimu na ufahamu mdogo wa wahusika na wananchi kwa ujumla Kuhusu Ushirika na hivyo kusababisha kuwa na idadi ndogo ya wananchama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukamilisha utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele yaliyowekwa kwenye mpango wa Bajeti kwa mwaka 2013/2014 Kamati inashauri Wizara ya fedha itoe fedha zote zilizobaki kwa Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ili kutekeleza mpango wa Bajeti wa mwaka 2013/2014. Maombi ya fedha na malengo ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu yake, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika chini ya fungu 43 inaomba jumla ya Shilingi 318,738,678,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 271,658,408,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 47,080,270,000 ni kwa Miradi ya Maendeleo.

Fungu 24, Ushirika, inaomba jumla ya shilingi 6,855,413,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na fungu 5 Tume ya Taifa ya umwagiliaji inaomba shilingi 29,408,021,000 ambapo kati ya fedha hizo Shilingi 475,000,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 28,933,021,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazoombwa na Wizara zinakusudia kutkeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo, kuwezesha upatikanaji masoko ya bidhaa za kilimo, kuwezesha uongezaji wa thamani wa mazao ya kilimo, kuwezesha na kuwezesha ushirika na asasi za wananchi katika kilimo na skta nyingine za kiuchumi, kufanya utafiti wa mazao yenye thamani kubwa na magonjwa ya mazao, kuimarisha mipango ya matumizi bora ya ardhi ya kilimo. Kuongeza uwezo wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula, kutoa ruzuku za pembejeo za kilimo ana kuimarisha Ushirika na vyama vya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka wa Bajeti 2014/2015. Baada ya kueleza utekelezaji wa maoni ya Kamati changamoto na maeneo ya utekelezaji kwa mwaka 2013/2014, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa kamati kwa Bajeti ya mwaka 2014/2015 kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati Kwa Wizara Kwa Mwaka wa Bajeti 2014/2015: Baada ya kueleza utekelezaji wa maoni ya Kamati changamoto na maeneo ya utekelezaji kwa mwaka 2013/2014, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa Bajeti ya Mwaka 2014/2015 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara hiii imendelea kuwa ndogo na ni sababu kubwa ya Sekta hii kushindwa kuchangia kwa kiasi cha kutosha katika pato la Taifa. Katika mwaka 2009/2010 Sekta ya Kilimo ilichangia asilimia 26 tu pato la taifa, licha ya ukweli kwamba Watanzania wanaokadiriwa kufikia asilimia 80 wanajishughulisha na Kilimo.

Aidha, ukuaji wa Kilimo unashuka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2008/2009, Kilimo klikuwa kwa asilima nne (4.6%). Mwaka 2010kwa asilimia 4.2. Mwaka 2011 kilikuwa kwa asilimia 3.6 tu. Wakati huo huo, idadi ya watu inakuwa kwa asilimia 2.9.

Aidha, Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Sekta ya Kilimo, imekuwa haitabiriki. Kama inavyoonyeshwa katika Jedwali lifuatalo. Kiasi cha Bajeti ya Sekta ya Kilimo ambacho kimekuwa kikitengwa. Mwaka 2008/2009 asilimia 6.4. Mwaka 2009/2010 asilimia 7.0. Mwaka 2010/2011 Asilimia 6.7, mwaka 2012/2013 asilimia 7.4 na mwaka 2013/2014 asilimia 5.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtiririko huu usio tabirika wala kuridhisha. Kamati inaishauri Serikali ifanye uamuzi wa makusudi ili Bajeti ya Sekta ya Kilimo, ifikie angalao kiwango kilichokubaliwa na nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *SADC* cha asilimia 10 ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyeki, Maombi ya Fedha za Nyongeza: Mpango wa utekelezaji wa Bajeti ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa mwaka 2014/2015, umezingatia malengo yaliyomo kwenye mpango wa Maendeleo wa miaka mitano na Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa sasa, *Big Result Now BRN*. Aidha, Kamati imeridhika kwamba Mpango wa 2013/2014, umehusisha masuala muhimu na ambayo ni ya Kipaumbele katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haikuridhishwa na Kiwango cha Fedha kinachotengwa kutekeleza majukumu mbali mbali ya kipaumbe yaliyoainishwa, kwenye mpango wa mwaka 2014/2015. Pamoja na kwamba Kilimo kinataajwa kwamba kama ni uti wa Mgongo wa Taifa, na kinachangia sehemu kubwa katika pato la Taifa. Bado fedha zibnazotengwa kwa ajili ya Kilimo hazitoshi ikilinganishwa na umuhimu wake. Baadhi ya maeneo ya kipaumbele yaliyotengewa fedha pungufu ukilinganisha na mahitaji na ambayo Kamati inayaombe fedha ya nyongeza ili kuiwezaesha Wizara kutekelza kwa ufanisi ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Moja, (Mfuko wa Taifa wa Pembejeo) Idadi ya Wakulima wanaomba Mikopo wa kununu zana za kilimo kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Ambapo mfuko umekuwa ukipokea maombi ya mikopo ya kati ya Shilingi Bilioni 6 – 9 kwa msimu. Ikilinganishwa na wastani wa shilingi bilioni 2.5 mpaka 3, zinazotengwa na Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu mwaka 2013/2014, Mfuko ulipokea maombi ya mikopo wenye dhamani ya shilingi bilioni 8.87, ambapo mikopo yenye dhamani ya shilingi biloni 6.o6 iliidhinishwa na kutokewa kwa waombaji. Hata hivyo kutokana na uwezomdogo wa fedha, mikopo iliyotolewa ni yenye dhamani shilingi bilioni 3.28 tu. Mikopo ambayo haikuweza kutolewa ni shilingi bilioni 2.77.

Kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014 Mfuko ulitengewa shilingi bilioni 2.81 na mpaka Machi, 2014 umepokea shilingi bilioni 1.56 na umeweza kutoa mikopo ya zana za kilimo. Umwagiliaji na Usindikaji wa Mazao yenye dhamani ya shilingi 3.28 kutokana na marejesho ya Mikopo iliyoiva.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na fedha kidogo, unazotenga Mfuko, uwezo wake wa kutoa mkopo kukithi mahitaji ni mdogo, ili mfuko huu uweze angalau mkopo wa Matrekta 300 na Zana nyingine za Kilimo kwa Wakulima, Kamati inashauri kuongeza shilingi bilioni 15, ili kufikika lengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi Za Mazao ni Taasisi zinazodhibiti na kuhamisha uzalishaji Mazao husika. Hata hivyo Bodi hizo zimekuwa hazipati fedha za kutosha ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hali inayosababisha uzalishaji na ubora wa mazao kuwa hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tangu mwaka 2006/2007, utekelezaji wa majukumu ya Bodi ya Tumbaku unakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa fedha hivyo Bodi hiyo imekuwa inashindwa kusimamia Sheria katika maeneo ya Ubora, Mazingira na Kanuni za Kilimo. Hali hiyo imesababisha kushukuka kwa ubora wa zao na hivyo wakulima kupara bei ndogo na pia kupotea kwa zao zaidi ya asilimi 30 wakati wa ukaushaji na kutokana kukosa mafunzo na ufutiliaji wa uzingatiaji wa sheria na Kanuni.

Mheshmiwa Mwenyekiti, kukosa fedha za kufanya kazi ya uteuzi wa Tumbaku na usimamizi wa Masoko na hivyo miaka mingine kupelekea kuomba michango, kutoka kwa Makampuni yanayonunu Tumbaku na hivyo kushusha hadhi ya bodi kufanya kazikwa uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuiwezesha Bodi ya Tumbaku iweze kutekeleza majukumu yake ya kisheria ipasavyo. Kamati inapendekeza Bodi ipewe

nyongeza ya fedha kwa kiasi shiilngi bilioni 1.2. Aidha, kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Bodi ya mazao Mchanganyiko. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali iiweezeshe Bodi hiyo ili iweze kuanza kuekeleza Wajibu wake mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 10, kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa sasa. Kiasi ambacho hakitoshelezi kulingana na shughuli muhimuza Wizara. Kiasi kilichotengwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015, cha shilingi biloni 30, hakitoshi kutokana na umuhimu wa Wizara hii ambayo imelenga kuzalisha ziada ya Sukari tani 150, mahindi tani 100,000. Mchele tani 290,000. Kamati inapendekeza kuwa malengo ya Usalama wa Chakula na hata kuuza ziada nje ya nchi, Wizara iongezewe kiasi cha shilingi bilioni 30 ili iweze kutekeleza malengo yake katika Mpango huu wa Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utafiti wa kilimo ni muhimu kwa sababu ndio njia pekee ya kugundua njia mpya za kukabili matatizo ya uzalishaji. Kwa kufanya utafiti katika kilimo teknolojia mpya hugunduliwa na kutumiwa na wakulima ili kuongeza tija kwa kiasi kikubwa. Teknologia hizo ni pamoja na mbegu bora. Njia bora za ukuwaji wa mazao. Udhibiti wa wadudu waharibifu na magonjwa ya
Mazao. Urutubishaji wa udongo na matumizi ya sayansi jamii na mifumo ya Kilimo. Aidha, miundombinu ya taasisi za mafunzo ya Kilimo na utafiti imechakaa sana na inahitaji ukarabati mkubwa.

Mhehimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha miundombinu ya Taasisi za Utafiti na Mafunzo na shughuli za Utafiti, katika Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika. Kamati inapendekeza ipewe nyongeza ya fedha kiasi cha shilingi bilioni 7,256,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kurejesha imani kwa wananchi kuhusu Maendeleo ya Ushirika Nchini. Serikali kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipitisha sheria ya Vyama Ushirika Namba 6 mwezi Agosti, 2013. Utekelezaji wa sheria hii katika Vyama vya Ushirika, utasimamiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria hiyo, ili kuhakikisha usimamzi bora na utekelezaji wa sheria hii, Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliandaa Bajeti yake ya mwaka 2014/2015, lakini Bajeti hiyo haikuwa na Fungu la shughuli ya Maendeleo. Hali hii imelazimisha baadhi ya Majukumu ya Maendeleo kuweka ndani ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida OC. Aidha kwa ufinyu wa ukomo uliotolewa kwa Tume. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida pia haikuwa na uwiano na hali halisi ya mahitaji ya Tume, hususan katika mwaka wa fedha wa uanzishwaji wake.

Mheshimwia Mwenyekiti, Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika Namba 6 ya 2013, imetangazwa kuanza kufanya kazi kuanzia tarehe 1 Januari, 2014. Hata hivyo utekelezaji wa kazi za Tume utaanza katika mwaka wa 2014/2015. Kwa mujibu wa Sheria hiyo Tume ya Mendeleo ya Ushirika, imepewa Mjukumu Makuu mawili ambayo ni:-

· Kusimamia na kukagua shughuli za Vyama vya Ushirika Nchini, kuanzia ngazi ya tawi, ya taifa hadi katika ngazi ya Wilaya.

· Kusimamia na kuratibu uhamasishaji. Uanzishaji na uendelezaji wa Vyaa vya Ushirikiana kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza kikamilifu majukumu haya Kamati inapendekeza Wizara kupewa nyongeza ya kiasi cha shilingi bilioni 10,000,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya kilimo kwanza haijatoa matunda ambayo yalitarajiwa. Kamati imebadini kwamba pamoja na kuwepo kwa mikakati ya Kilimo kwanza utekelezaji wake hauko dhahiri. Kamati inashauri Serikali ifanye tathmini juu ya mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa azma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba Serikali haina mipango dhabiti kuhusu utafiti na Maendeleo. Licha ya nia nzuri iliyoonyeshwa na Serikali mwaka 2008 ya kuanza kutenga fedha kwa ajili ya utafiti na maendeleo, ili hatimaye kufikia lengo asilimia moja la pato ghafi la taifa kama ilivyokubaliwa kwenye nchi za Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali iendelee kutenga fedha za kutosha kwaajili ya Utafiti na Maendeo. Ili vituo vyaUtafiti vitekeleze majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na rasilimai za kutosha za kuweza kutengeneza mbolea ya kutosheleza hapa nchini, Kamati haijaridhika na kasi ya uzalishaiji wa mbolea. Kamati inashauri Serikali kufanya utafiti na tathmini ili kuona ni kwa nini mbolea ya Minjingu Mazao inafaa katika baadhi ya maeneo tu. Aidha Kamati inashauri pawepo na maabara ndogo katika kila kanda ya kupima udongo *(Soil Profile)* ili kujua ni mbolea ya aina gani inafaa katika maeneo hayo.

Kwa mfano vituo ambavyo vinaweza kutumika kwenye kanda baada ya kuboreshwa ni *SUA,* Mlingano, Tumbi, Uyole, Ilonga, Naliendele, Maruku na Ukiliguru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu ni pembejeo muhimu katika Kilimo, ili kuwezesha wakulima kuzalisha mazao ya biashara nay a chakula cha kutosha na kuhakikisha kunakuwepo na usalama wa chakula. Kamati inashauri Serikali kuweka mikakati na kuhakikisha kuwa madawa yanayosambazwa kwa wakulima yawe ni yale ambayo yanafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya ushauri uliotolewa na Kamati mara kadhaa, nchi yetu bado inaagiza 75% ya mbegu kutoka nje jambo ambalo linaweza kuwa chanzo cha kuingiza magonjwa mapya nchini. Kamati inazidi kusisitiza kuwa Serikali kwa kushirikiana na taasisi nyingine kama vile JKT, Magereza na hata watu binafsi kuzalisha mbegu za kutosha kukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mazao mengi yakiwemo ya chakula na biashara kushambuliwa na wadudu waharibifu na kwa kuwa kuna malalamiko kuwa baadhi ya dawa zinazosambazwa haziangamizi wadudu, Kamati inashauri Serikali iweke mikakati ya kuhakikisha kwamba madawa yanayosambazwa kwa wakulima ya kuzuia wadudu waharibifu yawe ni yale ambayo yanafaa. Utafiti wa kutumia viuatilifu vya kipaumbele vya kimaumbile yaani biological control uendelee ili wakulima wavipate kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na migogoro mingi inayohusu matumizi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji, wakulima na wawekezaji, wananchi na mamlaka za hifadhi za taifa, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

Moja, Serikali iweke juhudi za makusudi kupima maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi.

Pili, Serikali isisitize kuchukua hatua kwa wawekezaji waliochukua maeneo makubwa ya ardhi na hayaendelezwi mpaka sasa na kuwapa wananchi kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo na ufugaji.

Tatu, kwa upande wa migogoro ya wananchi, wafugaji na hifadhi za taifa Serikali ifanye tathmini ya kina kina kuona kama maeneo hayo bado yanastahili kutumika kama hifadhi na kwamba katika maeneo ambayo hayana sifa hizo Serikali iwagawie wananchi kwa matumizi ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji mifuko ya kuhimili mitikisiko ya bei za mazao. Kamati inasisitiza uanzishwaji wa mfumo ambao utamlinda mkulima kutokana na mtikisiko wa bei ya mazao. Aidha, Serikali iwe makini katika kuagiza chakula kutoka nje kabla ya kufanya tathmini ya kiasi cha chakula kilichopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya kilimo. Kamati inaendelea kusisitiza mchakato wa uanzishwaji wa benki ya Kilimo uharakishwe na kukamilishwa ili wakulima waweze kufaidika na mikopo ya riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za ugani. Kamati inatambua umuhimu wa huduma za ugani katika kuhakikisha Kilimo kinakuwa na tija. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza udahili katika vyuo vya Kilimo. Kamati inasisitiza huduma za ugani ziboreshwe ili kuhakikisha yafutayo yanatekelezwa:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2013/2014 Serikali imetoa kibali cha ajira kwa sekta ya Kilimo chenye nafasi 1,804 kati ya nafasi hizo watakaoajiriwa ngazi ya kijiji ni 1,484 na nafasi 320 wataaajiriwa katika Wizara za Kisekta. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2014 Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imeweza kuwapanga wataalamu 1,382 kwa waajiri, kati ya hao wahitimu wa Stashahada yaani Cheti ni 881, Stashahada ya Diploma ni 284 na Shahada 217. Hata hivyo, nafasi 422 hazijapangiwa waajiriwa. Iwapo nafasi zote za kibali ngazi ya kijiji zitajazwa itaongeza idadi ya waghani walio kwenye ajira kufikia 9,558, hii ni sawa na kubakiwa na upungufu wa Maafisa Ughani 5524 ili tufikie lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuwaajiri Maafisa Ughani 4,988 waliopo sokoni waajiriwe ili tuweze kufikia lengo la kuwa na Afisa Ughani katika kila Kata na kila Kijiji. Sekta ya Kilimo inahitaji kupewa kipaumbele katika ajira za Waghani ili tuweze kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa kwa ufanisi. Sekta hii ipewe kipaumbele cha ajira kama ilivyo kwenye Wizara za Elimu na Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ajira za Maafisa Ughani Wizara kupitia Fungu 24 Tume ya Ushirika inaomba ajira za Maafisa Ushirika 150 kupitia fungu 5, Tume ya Umwagiliaji inaomba ajira ya Maafisa Wahandisi 150 na Fundi Sanifu 95 yaani technicians.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa masoko, stakabadhi ghalani. Mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani umekuwa ukiwanufaisha wakulima kwa utaratibu uliopo wa utunzaji na uuzaji wa mazao ya Kilimo. Mfumo huu una changamoto nyingi ambazo Kamati inashauri yafuatayo ili kuboresha.

Sheria ya leseni za maghala ina upungufu na hivyo ipitiwe upya. Idara ya masoko ya bidhaa za kilimo ipo kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara wakati bidhaa za kilimo zipo kwenye Wizara ya Kilimo. Jambo hili limekuwa gumu katika utekelezaji na Serikali inashauriwa kuliangalia upya.

Serikali izingatia muda wa kuwalipa wakulima mazao yao ili kuepuka kuwavunja moyo wakulima kutokana na kutolipwa fedha zao kwa wakati na kabla ya msimu mpya wa Kilimo kuanza.

Kwa kuwa Tanzania ina maghala mengi na ina mpango wa kujenga maghala mengine zaidi ya 145 na kwa kuwa mawasiliano ya kielektoniki nchini yameendelea kuboreshwa, Kamati inashauri Serikali kuanzisha mfumo wa

bidhaa za mazao yaani Comodity Exchange Market ili kuhakikisha uhakika wa masoko kwa mazao yetu na uhakika wa bei za mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Taifa. Kutokana na Bajeti ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula kuwa ndani ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika wakati wa mgawo wa ukomo wa Bajeti, Wizara huathirika kwa kuonekena imepewa fedha nyingi za matumizi ya kawaida ambapo fedha hizo ni kwa ajili ya matumizi maalumu ya kiusalama.

Aidha, wakati wa utekelezaji wa Bajeti mara zote kipaumbele kitaifa huwekwa katika hifadhi ya chakula na hivyo kuathiri upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu mengine ya msingi ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hili, Kamati inapendekeza kwamba lianzishwe fungu jipya ndani ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa ajili ya Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula, pembejeo na kulipia michango kwa Mashirika ya Nje. Utaratibu huu pia utaongeza uwajibikaji katika taasisi hiyo kwa mujibu wa kifungu 44(2)(b) cha kanuni za fedha za mwaka 2001 kama zilivyorekebishwa mwaka 2004. Pia, utaratibu huo utaimarisha mfumo wa usimamizi katika matumizi ya fedha za ununuzi wa chakula cha Hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Umwagiliaji. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Tume ya Umwagiliaji. Tume hii muhimu itasaidia kuharakisha mpango kabambe wa umwagiliaji, ambao unaonyesha kuwa Tanzania ina eneo lenye ukubwa wa hekta milioni 29.4 linalofaa kwa Kilimo cha umwagiliaji. Hadi kufikia Aprili, 2014 takwimu zinaonyesha kuwa eneo lililoendelezwa ni hekta 461,326 sawa na 1.6% ya eneo lote linalofaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji.

Kamati inaamini kuwa hali hii imetokana na uwekezaji mdogo katika sekta ya mwagiliaji, hivyo Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

Moja kuona umuhimu wa kuitengea Bajeti ya kutosha sekta hii na kuachana na kutegemea kilimo cha mvua kisicho na uhakika na kujielekeza katika Kilimo cha Umwagiliaji.

Mbili, kuongeza Bajeti kwa ajili ya kuanzisha scheme ndogo, za kati na kubwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Tatu, kuainisha na kuyatumia mabonde mengi ya maziwa na mito kwa ajili ya Kilimo cha Umwagiliaji.

Nne, kuviongezea uwezo wa kiutendaji vituo vya Kanda vya Umwagiliaji ikiwa ni pamoja na kuboresha na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji katika scheme za wakulima wadogo na kujenga scheme mpya katika maeneo yanayofaa kuendelezwa ili kuweza kuwahudumia wananchi na Halmashauri za Wilaya kwa wingi na kuongeza idadi ya wataalamu wa umwagiliaji na kuwaajiri katika Halmashauri za Wilaya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushuru wa Mazao. Kwa muda mrefu sasa wakulima wamekuwa wakitozwa ushuru wa mazao yao wanapoyatoa shambani na kuyapeleka nyumbani. Ushuru huu kwa kiasi kikubwa ndiyo sababu ya kupanda kwa bei ya chakula. Kamati inaendelea kusisitiza yafuatayo:-

Serikali ione umuhimu wa kuondoa ushuru wa mazao ili kumpunguzia mlaji makali wa bei na mbili, ushuru wa 2% wa zao la Tumbaku ambao Serikali iliahidi ni vema ukazingatiwa kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Mbunge na Naibu Waziri Waziri Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge, kwa ushirikiano wao mzuri katika kipindi chote cha utekelezaij wa majukumu ya kikanuni na kisheria ya Kamati.

Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Ndugu Sophia Kaduma na Manaibu Katibu Wakuu Dkt. Yamungu Kayandabila na Engineer Raphael L. Daluti pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Elieka Saanya na Angellina Sanga, kwa kuihudumia vizuri Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika Fungu 43 kwa mwaka 2014/2015, jumla ya shilingi bilioni 318,738,678,000/=, Fungu 24 shilingi bilioini 6,855,413,000/= na Fungu 5 shilingi bilioni 29,408,021,000/= pamoja na nyongeza ya fedha iliyoombwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Umesoma vizuri sana na sasa namwita Msemaji Mkuu wa Upinzani wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

**MHE. PAULINE PHILIPPO GEKUL (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatolewa chini ya Kanuni ya 99 toleo la Mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunitia nguvu na afya njema niweze kusimama mahali hapa nisome taarifa hii. Lakini kwa namna ya pekee na kwa heshima kubwa naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa uteuzi wa Baraza jipya la kivuli uliofanywa na kiongozi wa Kambi ya Upinzani hapo jana, nasema kazi ndiyo imeanza rasmi leo hadi huko tunakoelekea hakuna kulala hadi kieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mujibu wa *instrument* inatekeleza majukumu yafuatayo ili kufikia dira ya kufanikisha dhima ya Serikali katika sekta hiyo. Nasoma machache na kwa sababu ya muda naomba hotuba yote iingie kwenye Hansard na Waziri apatie ufafanuzi baadaye na majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu hayo ni:-

1. Kubuni na kuratibu utekelezaji wa sera ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

2. Kuratibu Matumizi bora ya ardhi katika Kilimo, kusimamia sekta binafsi, kuwekeza katika kilimo na umwagiliaji, kusimamia Bodi ya Asasi zilizo chini ya Wizara, kubuni mifumo ya utoaji wa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima wadogo na mengineyo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufisadi na udhaifu unaathiri sekta ya kilimo. Stimulus Package ilikuwa *EPA* nyingine, usiri kuhusu orodha ya matokeo ya ukaguzi wa *CAG* kwa makampuni yaliyonufaika ukomeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaingia kwa undani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa Fedha 2014/2015. Naomba nifanye Mapitio ya utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 kwa kutaka majibu juu ya suala moja muhimu la Stimulus Package. Suala hili limekuwa tukihoji kwa nyakati mbalimbali bila ya hatua za

maana kuchukuliwa hivyo kutokana na unyeti wake tunasisitiza kwamba maswali tunayohoji juu ya jambo hili yapatiwe majibu kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyakati mbalimbali kati ya mwaka 2009/2013 Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilihoji kuhusu fedha za *Stimulus Package* kabla ya mpango huo kabla ya fedha kutolewa na hata baada ya fedha hizo kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashaka ya Kambi Rasmi ya Upinzani yalithibitishwa na msingi wake wa report ya Mkaguzi Mkuu wa *Report* ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baadaye ambapo alieleza bayana kwamba hakukabidhiwa nyaraka na orodha ya walionufaika na kiasi cha jumla ya shilingi bilioni 48 za Stimulus Package kilichotolewa kwa ajili ya kuchochea ukuaji wa uchumi kutoka Benki Kuu ya Tanzania katika juhudi za kukabiliana na msukosuko wa uchumi ulioikumba dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha ya makampuni hayo iliombwa Bungeni na Mheshimiwa Spika mwenyewe aliajiza kwamba Waziri wa Fedha awasilishe orodha hiyo mpaka ninaposoma report hii sijapokea au Kambi Rasmi ya Upinzani haijapokea orodha ya makampuni yaliyonufaika ambayo kwa sehemu kubwa yalikuwa ni kutoka Sekta ya Kilimo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwasilishe Bungeni orodha hiyo ya makampuni hayo kwa kila sekta ili wakulima na Watanzania kwa ujumla wafahamu ni akina nani hasa walinufaika.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni kasoro zipi zilibainika katika ukaguzi huo hatua ambazo zimechukuliwa kushughulikia udhaifu uliojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kilimo nchini. Kilimo nchini kimeendelea kutawaliwa na wakulima wadogo wadogo takribani 70% ya kilimo kinategemea jembe la mkono na 20% jembo la kukokotwa na Ng'ombe na 10% matumizi ya…………

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaomba utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. PAULINE PHILIPO GEKUL (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2001 hadi 2013 Bajeti nzima ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikitolewa na wahisani kutoka nje, maana yake ni washirika wa Kimataifa wa Maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 pekee fedha zilizochangwa na Washirika wa Maendeleo yaani wafadhili kwa ajili ya sekta ilifikia 88.45% na kwa mwaka

2013/2014 fedha za ndani zilizotengwa kwa maendeleo zilikuwa ni 9.5% na fedha za wafadhili zilikuwa ni 70.45%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia Miradi ya Maendeleo iliyokusudiwa ni dhahiri kwamba fedha zilizotolewa ambazo ni Tshs. Bilioni 40.8 ambazo ni 50.3% ya fedha za Maendeleo tena ni fedha kutoka kwa wahisani na kati ya fedha hizo zilizotumika ni shilingi bilioni 26.9 mchango wa fedha za ndani bado hatujauweka, hadi lini kilimo chetu kitaendeshwa na Wahisani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya hivi karibuni iliyotolewa na NSAF inaonyesha kwamba Bajeti kwa sekta ya kilimo kwa sekta ya kilimo kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita imekuwa ikiongezeka sana kutoka shilingi bilioni 84.5 kati ya mwaka wa fedha 2002/2003 hadi shilingi bilioni 926.0 kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Hii inaonyesha ni kwa jinsi gani hiki kidogo tulichonacho kinavyogawanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi ni kwa nini licha ya kiasi hicho kutengwa kwa sekta hiyo lakini ukuaji wa sekta ya kilimo umekuwa ni mdogo wa wastani wa 4% kwa mwaka licha ya ongezeko la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania ambao ndiyo wanaolipa kodi, hapa kuna nini? Au fedha zinazotengwa zinaondolewa na kuingizwa kwenye matumizi ambayo hayaelezeki? Tunaomba ufafanuzi wa kina katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, taarifa hiyo ya uchambuzi wa Bajeti ya *NSAF* inaeleza kuwa ukuaji mdogo wa sekta ya Kilimo inawezekana ni raslimali zinazotengwa kwa sekta hiyo ya Kilimo haitumiki kimkakati ili matokeo kuonekana au raslimali zinazotengwa hazitumiki kwa matumizi lengwa kutokana ubadhilifu uliokithiri katika taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inakubaliana kabisa na uchambuzi huo kwani kuna taarifa kwamba baadhi ya Mawaziri waliokuwa na dhamana ya Wizara hiyo wakati wa kuhamishwa Wizara walijimilikisha magari ya Wizara na kujiuzia kwa bei karibu na bure na wapo hapa Bungeni. Kwa njia hii ni kwa vipi tija inawezekana kupatikana? Sekta ya Kilimo imekuwa ni shamba la Bibi au kichwa cha mwendawazimu kama alivyowahi kusema Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili kuhusu soka la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Afrika kupitia NEPADS waliasisi program ya kuendeleza kilimo mwaka 2003 CAADP kwa kikao kilichofanyika Maputo nchini Msumbiji kwa viongozi wa nchi za Afrika kukubaliana na kuchukua dhamana ya kutoa utaalamu na msaada wa fedha kwa sekta ya

kuendeleza kilimo kwa nchi zao kwa kutenga 10% ya Bajeti ya nchi zao kuelekezwa kwenye sekta ya Kilimo na Maendeleo Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawo katika sekta ya Kilimo umekuwa ukiongezeka kwa tarakimu tu lakini fedha halisi zinazotolewa bado ni kidogo. Serikali yetu bado ina safari ndefu katika kutimiza matakwa ya kutenga 10% kila mwaka kwa sekta hii. Takwimu zinaonyesha kwamba Bajeti ya kilimo ilipanda kutoka 3.8% mwaka 2000 hadi 6.1% mwaka wa fedha 2007/2008 hadi 2010. Lakini fedha halisi zinazotolewa kwa kipindi hicho kilichofanyiwa utafiti kuwa ni 2.3% na 4.9% tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza Bunge kwa miaka minne iliopita kila mwaka ni asilimia ngapi za fedha hizo zinatengwa na kutolewa kwa mwaka kwa sekta hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine muhimu ambalo kwa mujibu wa taarifa ya utafiti wa NSAF ni muhimu Watanzania na hasa wadau wa Kilimo kuielewa ni kwamba mgawo wa sekta ya Kilimo kama asilimia ya Bajeti Kuu ya Serikali umeendelea kuwa mdogo ukiwa ni wastani wa 5.2% kwa kipindi chote toka Tanzania kuridhia Azimio la Maputo ambapo Serikali iliridhia kutenga si chini ya 10% ya Bajeti ya nchi kwa Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, punguzo hilo la matumizi kwa sekta ya Kilimo maana yake ni kwamba, huduma za Kilimo nazo zinasimama au kupungua kwa kiwango kikubwa, miundombinu ya barabara, masoko nayo pia ilizidi kuwa tatizo kwa maeneo mengi ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mfumo wa vocha, pembejeo za mazao. Kuanzia kipindi cha mwaka 2008/2009 Serikali ilianzisha rasmi mpango wa ruzuku ya mbolea (uliolenga kusambaza tani 155,000 na tani 65 za mbegu kuwafikia wakulima milioni saba katika mikoa 10 kwa mwaka 2009/2010 mpango uliolenga kuwafikia wakulima milioni 1.5. Aidha, mwaka wa uchanguzi 2010 mpango wa ruzuku ulipanua wigo wa kufikia wilaya 74 na mikoa 20 ukilenga kuwafikia wakulima milioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtafiti anayeandaa taarifa hiyo anaeleza kuwa mpango wa ruzuku kwenye pembejeo ulikuwa ni mkakati wa kisiasa ili kushinda uchaguzi na hilo linaonekana wazi maeneo ya vijijini ijapokuwa hilo lilikuwa kinyume na matakwa ya sera za wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi rasmi ya upinzani inasema kuwa utafiti huo unaweza kuwa ni ukweli kwani kama kungekuwa na upembuzi yakinifu

kabla ya kuanzisha mfumo huo wa kutoa vocha za pembejeo ni dhahiri wizi na ubadhirifu unaoendelea leo usingekuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo imeelezwa hapo juu CAG anasema kuwa, mfumo wa ruzuku kwenye pembejeo hauna mwongozo na hivyo unafanyika kisiasa zaidi na mwishowe unawanufaisha viongozi wa kisiasa na siyo wakulima. (Makofi)

Pia utafiti wa kutosha wa aina za udongo kutokufanyika kabla ya utoaji wa hati za mbolea ili kuhakikisha pembejeo zinatolewa unaendana na aina ya udongo wa mahali husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubadhirifu katika usambazaji wa pembejeo za ruzuku limekuwa ni tatizo kubwa duniani. Hapa Tanzania inakadiriwa kwamba, 40% - 70% ya pembejeo za ruzuku haiwafikii walengwa. Kwa takwimu za 2010/2011 upotevu huu ni sawa na Tsh. Bilioni 58.4 hadi Tsh. Bilioni 102.2 na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kupitia program ya *EPNAV* kimefanya utafiti wa kina juu ya tatizo hili na kupendekeza mfumo wa kielektroniki wa kusambaza pembejeo za kilimo na ruzuku ambazo kama utatumika utaondoa kwa kiasi kikubwa upotevu wa pembejeo.

Mheshimikwa Mwenyekiti, imekuwa ni kawaida sana katika Bunge lako Tukufu kusikia Wabunge wakilalamikia wizi wa pembejeo za kilimo kama mbolea na mbegu katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Tatizo hili limekuwa sugu sana, lakini Serikali katika maeneo husika imeacha kuwachukulia hatua stahiki wale wote wanaotuhumiwa kuhusika na hujuma hizo. Kwa mfano; huko wilayani Kasulu katika kijiji cha Ruhita takribani kilomita 20 hivi kutoka Kasulu Mjini kumetokea wizi wa mbolea kiasi cha kutisha kulingana na kiwango au kiasi cha mbolea iliyotarajiwa kupelekwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko Kasulu mbolea aina ya Minjingu Kamati ya pembejeo ya kijiji ilipokea mifuko 100 tu badala ya mifuko 500. Urea mifuko 80 badala ya mifuko 500. Wanakijiji wanaeleza kwamba mifuko ya mbolea ilikuwa ikishushwa njiani katikati ya eneo la chuo cha kilimo Mubondo na kijiji cha Ruhita na hivyo kusababisha kupokea mifuko pungufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ukaguzi wa CAG inaonesha tuhuma za wizi wa vocha za pembejeo ambazo hazikupelekewa kwa walengwa katika wilaya ya Chato zenye thamani ya Tsh. Bilioni 1.16 hazikutumika.

Je, hapa si inaonesha mfumo huu ni wa kuwanufaisha watu fulani katika mfumo wa Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni. Huwezi kuamini sehemu nyingine nyaraka za vocha za pembejeo zinajazwa bila pembejeo kufika vijijini, vibali vya kupeleka pembejeo bila kuthibitishwa na Afisa Kilimo vimetolewa kwa Mawakala kuthibitisha kwamba pembejeo zimepelekwa wakati hazikufika kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi ni kwamba kila mwaka pembejeo zimekuwa zikichelewa Wilayani Kasulu na maeneo mengine nchini na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla wake, mathalani wakulima wa Mkoa wa Kigoma huanza kupanda mazao mwezi Oktoba kila mwaka, lakini pembejeo zinaletwa mwezi miezi ya Desemba, Januari hadi Februari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla matatizo haya yanajitokeza kwa sababu Mkuu wa Wilaya ya Kasulu hayuko makini na maendeleo ya Wakulima wa wilaya ya Kasulu. Kambi rasmi ya Upinzania inaona kuwa hii ni hujuma kwa wakulima na hii ni hatari kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandiko yanaendelea kuonesha kwamba matumizi ya pembejeo za kisasa kwa wakulima imekuwa ni tatizo kubwa sana hasa matumizi ya mbolea. Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa mwaka 2006 na Benki ya Dunia na Prof. Andrew Temu na Serikali yenyewe ni kwamba, yako chini ya asilimia 15. Hivyo basi, tija katika uazalishaji imekuwa chini sana na kama matumizi bora ya pembejeo hayatazingatiwa wastani wa uzalishaji kwa hekta moja unaweza kuwa ni kati ya tani 3.5 hadi 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la pembejeo hasa mbegu limekuwa ni kubwa sana kutokana na ukweli kwamba kuna wamiliki wa kampuni zinazozalisha au kusambaza mbegu ni viongozi waandamizi wa Serikali au ni viongozi wa juu katika siasa. Jambo hili limeendelea kulalamikiwa sana na wakulima lakini hakuna hatua zozote zinazochukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa karibu nusu ya wakulima wilayani Hai wameathirika kutokana na utoaji wa mbegu za mahindi zilizosambazwa na kampuni ya *SIDCO* Na. 513 na 625 zilizoota chini ya asilimia 20. Wakulima waliathirika sana ni kutoka katika Kata ya Rundugai hasa kijiji cha Kawaya, Kata ya Masama, Kata ya Machame, Weruweru, vijiji vya Batakero, Nguseru, Longoi, kwa tatizo hilo zaidi ya ekari 1000 zimeathirika.

Pia kuna mbegu za nyanya aina ya Rio grand, ambazo wakala wake ni Dollad Enterprises. Wakulima wanaolima bustani wameathirika sana hasa wale wa Hai mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya malalamiko hayo kutoka kwa wakulima Halmashauri ilikiri kuwepo kwa tatizo hilo na kuahidi kulifanyia kazi kwani wamejiridhisha hasa kwamba mbegu hizo hazikuota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti unaofanywa na muunganiko wa vikundi vya wakulima Tanzania (MVIWATA) wilayani Babati ulibaini kwamba wakulima waliathirika sana na hawakuelewa maisha yao yatakuwaje kwani Serikali pamoja na kuelewa uwepo wa ugonjwa huo hadi sasa haijawahi kuwaeleza wakulima walioathirika na wanaoendelea kuwa wahanga wa ugonjwa huo wa mlipuko kwenye zao la mahindi ujulikanao kwa jina la kitaalam maize lethal necrosis disease.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, utafiti wa MVIWATA uligundua kuwa wakulima wadogo wadogo wengi hawakuwa na taarifa kuhusiana na ugonjwa huo na hivyo waliendelea na shughuli zao za kilimo kama kawaida kwa kutumia mbegu zilezile japokuwa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara ilitoa taarifa kwa Wakurugenzi wa wilaya zote za Mkoa wa Manyara tarehe 6 Desemba, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo lilifanywa na Serikali ni kusimamia ufyekwaji wa mashamba ya mahindi na kuchomwa moto kwa maeneo ambayo yalikua yameathirika na mbegu zenye ugonjwa bila ya kuwapa wakulima nini wafanye kwa hasara iliyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi rasmi ya Upinzani inauliza ni kwanini Serikali imeshindwa kuwataarifu wakulima wakati ikielewa madhara ya ugonjwa huo? Je, hii si hujuma kwa wakulima hao?

Je, kampuni iliyozalisha mbegu hizo inawajibika vipi kwa hasara waliyoipata wakulima hao wa mkoa wa Manyara? Aidha, kwa mujibu wa CAG, mbegu bandia zilizosambazwa kwa walengwa katika vijiji vya Mpanda, Kaisho, Nyambishenge katika Wilaya ya Karagwe na kijiji cha Idunda katika Wilaya ya Ulanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kambi rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wananchi wealioathirika na tatizo hilo wanafidiwaje na lini kwani hasara tayari imeishaingia na msimu wa sasa umepita na kwa suala kama hili ni dhahiri kwamba wakulima toka mikoa mbalimbali wanaathirika na tatizo hili la kutoota kwa mbegu, lakini Serikali inakaa kimya, kwa njia hii ni kwa vipi kilimo chetu kinaweza kuwa cha kisasa, endelevu na cha biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pamba na umuhimu wake kwa Taifa. Pamba inachangia asilimia 24 ya mauzo yote ya bidhaa za kilimo nje ya nchi na inachangia asilimia 4 ya mauzo yote nje ya nchi. Takribani hekta 400,000

zinatumika kwa ajili ya kilimo cha Pamba kwenye Wilaya zaidi ya 40 za Mikoa 13 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Wakulima wa Pamba Tanzania *(TACOGA)* kilifanya utafiti katika matao yote mawili yanayolima Pamba nchini. Utafiti huu unatumia mbinu shirikishi ya majadiliano katika vikundi na ulishirikisha jumla ya wakuma 800.

Mheshimiwa Mwenykiti, katika utafiti huu masuala kadhaa yaliibuliwa kama changamoto za Kilimo cha Pamba kama ifuatavyo:-

Moja, bei ndogo ya Pamba, Mbili ni tija ndogo na tatu ni kuharibiwa kwa makusudi kwa mizani kwa lengo la kumuibia mkulima. Pia ushuru mkubwa unaoongeza mzigo kwa mkulima, uwezo hafifu wa viwanda vya kuchambua Pamba, ruzuku ndogo kutoka katika Bajeti ya Taifa, ushindani usiozingatia kanuni, kulegea kwa miongozo na Kanuni za zao la Pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikosi kazi cha wadau wa Pamba ambacho kilifanya utafiti huu kilikuja na mapendekezo ambayo kambi rasmi ya Upinzani inapenda kuitaka Serikali kuyatekeleza ili kuondokana na mvutano usio wa lazima na usiomalizika kati ya wakulima wa Pamba na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo hayo ni pamoja na:-

(i) Ruzuku maalum ya Pamba kutoka katika Bajeti ya Taifa;
(ii) Wazawa wamiliki mashine za kuchambua Pamba;

(iii) Wamiliki wa mashine za kuchambua Pamba watengeneze nyuzi;

(iv) Wawekezaji wa Viwanda vya nguo wasichambue Pamba na badala yake wabaki na viwanda vya nguo na wanunue malighafi za nyuzi kutoka kwenye viwanda vya wazawa;

(v) Uchambuzi huru wa ukokotoaji wa bei ya Pamba;

(vi) Mamlaka ya Wakala wa Vipimo na Mizani kufanya ukaguzi wa mizani kwa kushirikiana na Mkaguzi wa Pamba;

(vii) Mikataka yote iwe standard na ifanyike kwa wazi; na
(viii) Sheria na Kanuni zitoe adhabu za kifungo na kusitisha leseni kwa wahusika wanaohujumu Mizani na sekta ya Pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uzalishaji wa Miwa Mtibwa. Mtibwa Tuliani ni pamoja na maeneo yaliyoathirika sana na uwekezaji kwenye kilimo ambapo

inaonesha wazi kuwa wawekezaji wanapambana na wakulima wadogo wadogo badala ya kusaidia na kuongeza uzalishaji kwa kuinua tija katika kilimo. Kwa mfano; uzalishaji wa miwa kwa wakulima wa nje wakati wa kabla ya uzalishaji kiwanda cha Mtibwa mwezi wa Nane 1998 wakulima walizalisha 92 ya Miwa yote iliyotumiwa na Kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada tu ya ubinafsishaji siyo tu kuwa uzalishaji umekuwa ukiyumba sana, bali pia umepungua hadi kufikia 35% mwaka 2001. Pamoja na juhudi za zima moto za Serikali na kujituma kwa wakulima binafsi na umoja wao wa wakulima *(MOA)* na kufanikiwa kuinua uzalishaji hadi 56% mwaka 2004 hadi 2005 bado uzalishaji umeendelea kuathirika na sasa umekwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa sababu zilizoelezwa na wakulima na kubainishwa na taasisi huru za utetezi wa kilimo na wakulima ni pamoja na hizi zifuatazo:-

1. Usimamizi mbaya wa kilimo na biashara ya miwa;

2. Mfumo wa utaratibu mbaya wa uvunaji wa miwa ya wakulima wa nje jambo linalopelekea wakulima kupata hasara kubwa kwani miwa mingi huachwa mashambani na hata iliyovunwa haifiki kiwandani;

3. Kwa kipindi cha 2002 hadi 2013 inakadiriwa zaidi ya tani 40,000 huachwa kila mwaka bila kuvunwa mashambani; na

4. Kusitishwa kwa utaratibu wa wawekezaji kutoa huduma za mashambani bila utaratibu mbadala kuwekwa na hivyo kuwaathiri sana wakulima ikiwamo upatikanaji wa mbegu za miwa, vifaa vya uvunaji, mbolea na pembejeo nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huu Serikali inaua kilimo cha miwa na wakulima wa miwa nchini kwa kuneemesha wawekezaji ambao siku moja wataamua kufunga uwekezaji wao bila manufaa yoyote kwa nchi. Hii pia inatoa picha kuwa iwapo uwekezaji utaendelezwa namna hii basi hautakuwa na manufaa yoyote kwa nchi na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya Bajeti kwa mwaka 2014/2015. Kwa mwaka huu wa fedha Wizara hiyo yenye Mafungu 43, 24 na 5 imetengewa jumla ya Tsh. Bilioni 355 na kati ya fedha hizo Tsh. Bilioni 279 ni fedha za Matumizi ya Kawaida na Tsh. Bilioni 79 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida kwa Fungu 43 Wizara imepanga kutumia Tsh. Bilioni 271.6 kati ya fedha hizo Tsh. Bilioni 2.8 zimepangwa kutumika kwa ajili ya usafiri tu, hii ni pamoja na Tsh. Milioni 877.2 kwa ajili ya ununuzi wa magari na pikipiki, Tsh. Milioni 994.9 kwa ajili ya ununuzi wamafuta na vilainishi, huku Tsh. Milioni 893 zikipangwa kutumika kwa ajili ya nauli za ndege kwa ajili ya watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa safari kwa Watumishi kama njia mojawapo ya utendaji wao, lakini ikumbukwe kwamba Wizara hii ina safari chache sana kuwafikia walengwa (Wakulima), hivyo pamoja na haja ya kuongezeka kwa Bajeti kwenye sekta hii ya kilimo, ni vyema fedha zielekezwe eneo lenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ni muhimu kwa watendajina wataalam, lakini msingi mkuu wa wataalam kwa Wizara hii ni kuwawezesha wakulima kupata na kutumia utaalam kwa tija. Wizara hii imepanga kutumia Tsh. Milioni 804.4 kwa ajili ya mafunzo ya semina, kati ya fedha hizo Tsh. Milioni 71.3 tu ndizo zinazolenga wakulima ambao ni sawa na 9% ya fedha za mafunzo, huku zaidi ya Tsh. Milioni 700 ambazo ni zaidi ya 90% ya fedha za mafunzo zikielekezwa kwenye mafunzo ya semina za watendaji wa Wizara. Aidha, Tsh. Bilioni 1.3 zimetengwa kwa ajili ya mafunzo kwenye fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kambi rasmi ya Upinzani inauliza hivi wizara hii mteja wake ni nani na anayetakiwa kuwezeshwa ni nani? Swali kuu la kujiuliza ni je, watumishi wanaoajiriwa na Wizata hii hawana sifa kiasi cha kuhitaji mafunzo kila mwaka? Ni lini hali hii itabadilika kwa kila mwaka mafunzo kwa watendaji wa Wizara? Huu ni muda mwafaka ka Serikali kubadilika na kuangalia ni jinsi gani sekta binafsi inavyofanya kazi na raslimali watu inatumika vipi katika sekta hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Bunge hili lilitunga sheria ya kuanzisha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji mwaka 2013 ili kuweza kusimamia uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji. Kutokana na uanzishwaji wa Tume, Idara ya umwagiliaji na huduma za ufundi katika bajeti ya mwaka huu haikutengewa hata senti moja kwani kazi zake zimehamishiwa kwenye tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika randama ya Wizara ukurasa wa 24 inasema rasimu za kanuni za sheria ya umwagiliaji na mapendekezo ya muundo wa tume zimeandaliwa lakini hadi sasa hazijawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuidhinishwa na kutolewa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza inakuwaje kanuni bado hazijapitishwa ni kwa vipi Tume hii inapewa kazi wakati mwongozo wa kufanyia kazi bado haujatolewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu Wizara kupitia Tume ya Umwagiliaji, Fungu 5 imepangiwa Tsh. Milioni 475 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Tsh. Bilioni 28.9 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, lakini kutokana na umuhimu wake tume imeanza vibaya kwa muktadha wa matumizi ya fedha. Tume imepanga kutumia Tsh. Milioni 227 kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi, Tsh. Milioni 69 zikielekezwa kwenye kuwezesha watumishi kuhudhuria Maonesho ya Kilimo, Tsh. Milioni 61 ni kwa ajili ya stahili za watumishi na zaidi ya Tsh. Milioni 88 ni kwa ajili ya ufuatiliaji, tathmini na mambo mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na fedha hizi tume inapanga kutumia zaidi ya Tsh. Bilioni 7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, uendeshaji kati ya Tsh. Bilioni 28 zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mchanganuo ni kwa programu 4486 Mradi Na. CO3CO1, programu 4496 miradi Namba CO4CO1, Kifungu 1004 na miradi mingine hapo chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 2002 Programu 4486 Mradi DO1DO1 kifungu cha 2004 programu na miradi mingine. Aidha, Tsh. Bilioni 1 zimepangwa kununua magari 16 kwa ajili ya matumizi ya tume huku zaidi ya Tsh. Bilioni 3.1 ni kwa ajili ya watoa huduma binafsi. Miradi mingine imeelezwa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kambi rasmi ya Upinzania inaitaka Serikali ieleze kama tayari imekwishapanga kutumia Tsh. Milioni 227 kwenye fedha za matumizi ya kawaida ni kwa vipi tena matumizi ya kawaida yanawekwa kwenye fedha za Miradi ya Maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla inaonesha kwamba tume hii imeundwa kwa kuwa huru kiutendaji lakini inaweza kutumika kuwa kichaka cha ufisadi mkubwa na hivyo tija kushindwa kuonekana. Mfano ni matumizi ya fedha tajwa kwa ajili ya washauri tu. Hoja nyingine ni kwamba, tume inashindwa ku- consolidate fedha za wahisani na wao wakapanga matumizi kulingana na hali halisi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali halisi bajeti ya maendeleo ya tume ya umwagiliaji ni Tsh. Milioni 567.8 tu ambayo inaenda kwa wakulima, japokuwa Tsh. Milioni 350 hazina uhusianio wa moja kwa moja na umwagiliaji kama jukumu la msingi la tume linavyohitaji. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge kuna haja gani ya kuwa na tume ya taifa iwapo miradi iliyo chini yake inaendeshwa na watu binafsi? Mpango huu unaonekana kuwa dhamira yake si kuendeleza sekta, bali ni kutafuta fedha kwa ajili kundi fulani kwenye mchakato wa uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache sasa kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. *(Makofi)*

**HOTUBA YA UPINZANI KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA MHESHIMIWA ROSE KAMILI SUKUM (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014**
**(Inatolewa Chini ya Kanuni ya 99(9) toleo la mwaka 2013)**

**UTANGULIZI**

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, kwa mujibu wa "instruments" inatekeleza majukumu yafuatayo ili kufikia Dira na kufanikisha Dhima ya Serikali katika sekta hiyo:-

(i) Kubuni na kuratibu utekelezaji wa sera za kilimo,chakula na ushirika;

(ii) Kuratibu matumizi bora ya ardhi katika kilimo;

(iii) Kujenga uwezo wa Halmashauri za Wilaya katika kutoa huduma za ugani,umwagiliaji na ushirika kwa wakulima;

(iv) Kufanya utafiti wa kilimo;

(v) Kusimamia usalama wa chakula;

(vi) Kudhibiti magonjwa, wadudu, ndege na wanyama waharibifu wa mazao;

(vii) Kuendeleza raslimali watu katika fani ya kilimo na ushirika;

(viii) Kusimamia na kuratibu program ya kuendeleza sekta ya kilimo (ASDP);

(ix) Kusimamia na kuratibu program kabambe ya mageuzi na modernization ya ushirika;

(x) Kusimamia sekta binafsi kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji;

(xi) Kusimamia Bodi na Asasi zilizo chini ya Wizara;

(xii) Kubuni mifumo ya utoaji wa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima wadogo;

(xiii) Kuendeleza ushirika na vikundi vya uzalishaji;

**UFISADI NA UDHAIFU UNAATHIRI SEKTA YA KILIMO**

Stimulus Package ilikuwa *"EPA"* nyingine; usiri kuhusu orodha na matokeo ya Ukaguzi wa CAG kwa makampuni yaliyonufaika ukomeshwe

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia kwa undani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka fedha 2014/2014, naomba nifanye mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa kutaka majibu juu ya suala moja muhimu la "stimulus package". Suala hili tumekuwa tumelihoji kwa nyakati mbalimbali bila ya hatua za maana kuchukuliwa. Hivyo, kutokana na unyeti wake tunasisiza kwamba maswali tutakayoyahoji juu ya jambo hilo yapatiwe majawabu kwa ukamilifu. Kwa nyakati mbalimbali kati ya mwaka 2009 mpaka 2013, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilihoji kuhusu fedha za "Stimulus Package" kabla ya Mpango huo kabla ya fedha kutolewa na hata baada ya fedha hizo kutolewa.

Mheshimiwa Spika; mashaka ya Kambi Rasmi ya Upinzani yalithibitishwa msingi wake na Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali baadaye ambapo alieleza bayana kwamba hakukabidhiwa nyaraka na orodha ya walionufaika na kiasi cha jumla ya Sh. bilioni 48 (Stimulus package) kilichotolewa kwa ajili ya kuchochea ukuaji wa uchumi toka Benki Kuu ya Tanzania katika juhudi za kukabiliana na msukosuko wa uchumi ulioikumba dunia.

Orodha ya makampuni hayo ilipoombwa bungeni wewe mwenyewe uliagiza kwamba Waziri wa Fedha awasilishe orodha hiyo. Mpaka ninaposoma ripoti hii, sijapokea orodha ya kampuni yaliyonufaika ambayo kwa sehemu kubwa yalikuwa ni kutoka Sekta ya Kilimo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwasilishe bungeni orodha hiyo ikianisha makampuni kwa kila sekta ili wakulima na watanzania kwa ujumla wafahamu ni wa kina nani hasa walinufaika.

Mheshimiwa Spika; Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza sababu zilizofanya nyaraka hizo zisikabidhiwe na na kutoa taarifa ya kina ya kueleza iwapo nyaraka zote kwa sasa zimewasilishwa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni kasoro zipi zilibainika katika Ukaguzi huo na hatua ambazo zimechukuliwa kushughulikia udhaifu uliojitokeza.

**HALI YA KILIMO HAPA NCHINI**

Mheshimiwa Spika, Kilimo nchini kimeendelea kutawaliwa na wakulima wadogo wadogo; karibu asilimia 70 ya kilimo kinategemea jembe la mkono, asilimia 20 jembe la kukokotwa na ng'ombe na asilimia 10 matumizi ya trekta.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2001/02 -2012/13, bajeti nzima ya maendeleo ya sekta ya kilimo kwa kiasi

kikubwa imekuwa ikitolewa na wahisani toka nje i.e. Washirika wa kmataifa wa maendeleo1. Kwa mwaka wa fedha 2012/13 pekee, fedha zilizochangwa na washirika wa maendeleo (Wafadhili) kwa ajili ya sekta ilifikia asilimia 88.45. Na kwa mwaka 2013/14 fedha za ndani zilizotengwa kwa maendeleo zilikuwa ni asilimia 29.5 na fedha za wafadhili zilikuwa ni asilimia 70.452.

Mheshimiwa Spika, kwa kuangalia miradi ya maendeleo iliyokusudiwa ni dhahiri kwamba fedha zilizotolewa ambazo ni Tshs 40,831,220,246 ambazo ni asilimia 50.38 ya fedha za maendeleo tena ni fedha kutoka kwa wahisani na kati ya fedha hizo zilizotumika ni shilingi 26,961,620,087. Mchango wa fedha za ndani bado hatujaweka. Hadi lini kilimo chetu kitaendeshwa na wahisani?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kanuni za uwezeshaji ni zile zile hata kwa nchi wahisani, hakuna nchi yoyote au mtu yeyote anayeweza kukuwezesha ili nawe uweze kushindana nae. Hoja ni je kama sisi tukiwa imara kesho si tutashindana nao? Hivyo jambo la msingi ni sisi kuangalia ni kwa vipi tunatokaje hapa tulipo, na hivyo ni uwajibikaji tu, jambo ambalo serikali ya CCM imeshindwa kulisimamia na hivyo kupoteza uhalali wa uwepo wake, hasa kwa wadau wa sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo ndiyo iliyobainishwa kuwa sekta muhimu katika kukuza uchumi. Sekta ya Kilimo ni sekta ambayo inazungumzwa sana kama sekta kiongozi katika Maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na mipango mbalimbali inayoandaliwa na Serikali kuhakikisha kwamba Kilimo kinakuwa cha kisasa na hivyo kuzalisha chakula cha kutosha na pia mazao mengi ya biashara hivyo kuongeza kipato kwa mwananchi mmoja mmoja, kukuza pato la Taifa na kuongeza thamani ya mauzo yetu nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejaribu kuhamasisha kilimo cha kibiashara kwenye ngazi ya sera, lakini ni dhahiri kwamba utekelezaji wa sera hizo umekuwa ni jambo lisilotekelezeka. Na sababu kubwa zimekuwa ni za kiutendaji zaidi zinazohusu kushindwa kusimamia raslimali zilizopo ili ziendane na maandiko yaliyopo na hakuna hatua za kinidhamu zinazochukuliwa au raslimali kidogo zinazopatikana zinagawanywa sana na hivyo kuwapa mwanya watumishi wasio waaminifu kuchepusha fedha hizo kwa matumizi yasiyokusudiwa mwisho ni kutoonekana matokeo yoyote ambayo yangelingana na kiasi cha uwekezaji uliowekwa.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kuwa kwa miaka kumi iliyopita sekta ya kilimo ilikuwa inakuwa kwa asilimia 4.5 kwa mwaka, na hivyo kuchangia robo ya pato la taifa na vile vile kuchangia asilimia 34 ya fedha za kigeni.Kwa mujibu wa taarifa ya hivi karibuni iliyotolewa na ANSAF inaonyesha kwamba bajeti kwa sekta ya kilimo kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita imekuwa ikongezeka sana kutoka shilingi bilioni 84.5 katika mwaka wa fedha

2002/2003 hadi shilingi bilioni 926.0 kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Hii inaonyesha ni kwa jinsi gani hiki kidogo tulichonacho kinavyogawanywa. Hoja ya msingi ni kwa nini licha ya kiasi hicho kutengwa kwa sekta hiyo lakini ukuaji wa sekta ya kilimo umekuwa ni mdogo wa wastani wa asilimia 4 kwa mwaka licha ya ongezeko la Bajeti?

Mheshimiwa Spika,Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze watanzania ambao ndio walipa kodi hapa kuna nini? Au fedha zinazotengwa zinaondolewa na kuingizwa kwenye matumizi ambayo hayaelezeki? Tunaomba ufafanuzi wa kina katika hili.

Mheshimiwa Spika, aidha, taarifa hiyo ya uchambuzi wa bajeti ya ANSAF inaelezea kuwa ukuaji mdogo wa sekta ya kilimo inawezekana ni raslimali zinazotengwa kwa sekta hiyo ya kilimo haitumiki kimkakati ili matokeo kuonekana au raslimali zinazotengwa hazitumiki kwa matumizi lengwa kutokana na ubadhirifu uliokithiri katika taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inakubaliana kabisa na uchambuzi huo kwani kuna taarifa kwamba baadhi ya Mawaziri waliokuwa na dhamana ya Wizara hiyo wakati wa kuhamishwa Wizara walijimilikisha magari ya Wizara kwa kujiuzia kwa bei karibu na bure na wapo hapa Bungeni. Kwa njia hii ni kwa vipi tija inawezeka kupatikana? Sekta ya kilimo imekuwa ni shamba la bibi au kichwa cha mwenda wazimu kama alivyowahi kusema Rais Msataafu wa Awamu ya Pili kuhusu soka la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya hivi karibuni iliyotolewa na Serikali inaonyesha kwamba Sekta ya Kilimo haijakua kiasi cha kutosha na kuweza kupunguza umasikini wa Watanzania! Taarifa ya Umasikini na Maendeleo ya mwaka 2011 inasema kwamba mchango wa sekta ya Kilimo katika Pato la Taifa (GDP) umeporomoka kutoka asilimia 29 mwaka 2001 mpaka asilimia 24 mwaka 2010.

Kuporomoka huku yawezekana kunachangiwa na kukua kwa sekta nyingine kama ile ya huduma au uzalishaji viwandani katika kipindi hicho. Hata hivyo kasi ya ukuaji wa Sekta ya Kilimo katika kipindi cha muongo huo (2001 – 2010) ilikuwa ni asilimia 4.3 chini kabisa ya kiwango kilicholengwa katika Mkakati wa kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA).

Mheshimiwa Spika, Kutokana na kuwapo kwa utofauti wa hali ya hewa kikanda, uwepo wa maji ya kutosha kwa umwagiliaji na mifugo, kuwepo kwa ardhi kubwa ifaayo kwa kilimo, Tanzania imekuwa na fursa nzuri ya kuzalisha mazao mbalimbali, mifugo, na mazao mbalimbali ya misitu.

Mheshimiwa Spika, Kupitia utekelezaji wa Mkukuta, Serikali iliweka lengo la kukuza pato la taifa kuwa kati ya asilimia 6-8 kwa mwaka kati ya mwaka 2005/06 and 2009/10. Lakini mahususi, mchango wa sekta ya kilimo kupanda kutoka asilimia 5 hadi asilimia 10 kwa mwaka 2010. Mheshimiwa Spika huu ni mwaka 2014, je lengo hili limefanyiwa tathmini?

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2005 inatamka kuwa "Kilimo cha Kisasa ndiyo Msingiwa Uchumi wa Kisasa". Ili Uchumi wa Nchi yetu ukue kwa kiwango cha asilimia 10 ifikapo 2010 lazima Kilimo kifikie ukuaji wa angalau asilimia 20 ifikapo mwaka 2010"

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 Tanzania ilikuwa na program ya kuendeleza kilimo ambayo ilikuwa itekelezwe kwa muda wa miaka 7 iliyojulikana kama (ASDP). Programe ilianza kwa kusuasua kutokana na kutokuwepo kwa makubaliano kati ya Serikali na mashirika ya wafadhili na nchi washirika wetu wa maendeleo kupitia mikopo ya Benki ya Dunia kwa mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wa wafadhili na washirika wetu wa maendeleo ni kwamba mkakati huo wa kuendeleza sekta ya kilimo ulikuwa umejikita zaidi katika kuendeleza mali ya umma kwa raslimali nyingi kuelekezwa upande huo wa Serikali kuu wakati huohuo wahusika wakuu walikuwa ni wazalishaji katika sekta ya kilimo ambao ni watu binafsi kwa tafsiri pana kwa kuanzia na uzalishaji hadi masoko3.

Mheshimiwa Spika, umoja wa Afrika kupitia NEPAD's waliasisi program ya kuendeleza Kilimo mwaka 2003 (CAADP) kwa kikao kilichofanyika Maputo nchini Msumbiji kwa Viongozi wa nchi za Afrika kukubali na kuchukua dhamana ya kutoa utaalamu na msaada wa fedha kwa sekta ya kuendeleza kilimo kwa nchi zao kwa kutenga asilimia 10 ya bajeti ya nchi zao kuelekezwa kwenye sekta ya kilimo na maendeleo vijijini.

Mheshimiwa Spika, mgawo katika sekta ya kilimo umekuwa ukiongezeka kwa tarakimu tu lakini fedha halisi zinazotolewa bado ni kidogo. Serikali yetu bado ina safari ndefu katika kutimiza matakwa ya kutenga asilimia 10 kila mwaka kwa sekta hii. Takwimu zinaonyesha kwamba bajeti ya kilimo ilipanda kutoka 3.8% mwaka 2000 hadi 4.6% na 6.1% kwa mwaka wa fedha 2007/08 na 2009/10, lakini fedha halisi zilizotolewa kwa kipindi kicho kilichofanyiwa tafiti ilikuwa ni 2.3% na 4.9% tu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge kwa miaka minne iliyopita kila mwaka ni asilimia ngapi za fedha zinatengwa na kutolewa kila mwaka kwa sekta hii ya kilimo. Aidha, ukweli ni kwamba biashara katika sekta hii imeendelea kuwa na vikwazo vingi katika mkakati mzima wa kuiendeleza.

Mheshimiwa Spika, suala lingine muhimu ambalo kwa mujibu wa taarifa ya utafiti ya *ANSAF* ni muhimu watanzania hasa wadau wa kilimo kulielewa ni kwamba mgawo wa sekta ya kilimo kama asilimia ya bajeti kuu ya serikali umeendelea kuwa mdogo ukiwa ni wastani wa asilimia 5.2 kwa kipindi chote toka Tanzania kuridhia azimio la Maputo, ambapo Serikali iliridhia kutenga si chini ya asilimia 10 ya bajeti ya nchi kwa sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba uongezaji wa fedha na uwajibikaji wa utendaji kwa fedha za umma kwenye sekta ya kilimo ni dhahiri ukuaji wa uchumi ni rahisi kuonekana. Nchi ambazo zimetumia angalau asilimia 10 ya bajeti ya nchi zao uchumi umepanda, nchi hizo ni pamoja na Malawi, Ethiopia na Cape Verde 4.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji zaidi kwenye kilimo kiuchumi unatija kwa sababu kubwa kwamba kilimo ndio sekta kiongozi katika kutoa ajira na ni ukweli kwamba zaidi ya asilimia 90 ya wananchi wanaishi vijijini na wanaendesha maisha yao kupitia kilimo, aidha kilimo kinachangia zaidi ya asilimia 50 ya pato la nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kilichofanyiwa tafiti, yaani 2005-10 matumizi kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya kilimo(mafunzo, utafiti na ugani) yalikuwa ni takriban asilimia 60 ya matumizi yote na asilimia iliyobaki yalielekezwa zaidi kwa malipo kwa wakulima na mawakala wa pembejeo na matumizi haya kwa kipindi cha mwanzo cha utafiti. Kuanzia mwaka 2009 kulikuwa na ongezeko kwa matumizi kwa wazalishaji kupitia mfumo wa ruzuku na matumizi ya sekta yalipungua hadi kuwa chini ya asilimia 50. Punguzo hilo la matumizi kwa sekta ya kilimo maana yake ni kwamba huduma za kilimo nazo zimesimama au zilipungua kwa kiwango kikubwa, miundombinu ya barabara na masoko nayo pia ilizidi kuwa tatizo kwa maeneo mengi ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya uwekezaji Tanzania ya mwaka 2012 iliyotolewa Novemba 2013, inasema kwamba, nanukuu "kilimo ambacho kina mchango mkubwa kwenye pato la taifa kiliendelea kuwa na kiwango kidogo cha uwekezaji kutoka nje. Pamoja na ongezeko la uwekezaji katika shughuli za kilimo kuwa zaidi ya asilimia 50.0 kati ya 2008 na 2011, thamani ya uwekezaji wake ilikuwa ndogo ikilinganishwa na uwekezaji kwenye shughuli nyingine kama vile uchimbaji madini na mawe, uzalishaji viwandani, fedha na bima; na habari na mawasiliano"

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo inatoa ushauri ambao tumekuwa mara zote tunautoa kuhusu jinsi ya kuongeza uzalishaji vijijini, nanukuu "Jitihada za kufanya sekta ya kilimo kuwavutia wawekezaji wengi, Jitihada hizo ni pamoja na; kuwekeza kwenye miundombinu vijijini, miradi ya umwagiliaji, upatikanaji wa umeme vijijini kwa ajili kuwezesha usindikaji wa mazao pamoja na uchoraji wa ramani zenye mgawanyo wa matumizi ya ardhi nchi nzima".

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2003 hadi 2013, sekta ilipangiwa bajeti ya kiasi cha asilimia 6.2 ambayo ilichangia kiasi cha asilimia 4 kwenye maendeleo ya sekta kwa mwaka, tofauti na bajeti ya maendeleo ya sekta ya taifa ambayo ina kiasi cha asilimia 8. Jambo la msingi ni kutambua kwamba asilimia 80 ya jumla ya watu wanaoishi vijijini huishi kwa kutegemea kilimo. Matumizi ya fedha yamekuwa yakirudishwa nyuma na ucheleweshwaji wake. Mbali na hilo, ushinikizaji wa serikali katika kuweka bajeti kubwa kwenye sekta ya kilimo, ongezeko hilo linaweza lisilete matokeo mazuri katika kufanikisha malengo yaliyokusudiwa, bila kutafuta ufumbuzi wa masuala mengine 5. Katika Mamlaka ndogo za Serikali imegundulika kwamba sekta ya kilimo inachangia kuingiza pato kwa Mamlaka hizo lakini zinapata kiwango kidogo cha uwekezaji kutoka kwenye vyanzo yake.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Serikali katika chapisho la utafiti la Fao kwa kushirikiana na Serikali lililotolewa Julai 2013 zinaonyesha kuwa "wakati bajeti ya kilimo inayopitishwa na Bunge ikikua hadi asilimia 53 kati ya mwaka 2007 hadi 2011, kiulinganisho kwa matumizi ya serikali ni kuwa ilishuka kutoka takriban asilimia 13 mwaka 2007 hadi asilimia 9 mwaka 2011 Matumizi halisi kwenye kilimo yaliongezeka kidogo sana kwa kipindi tajwa hapo juu. Kwa kuangalia azimio la Maputo matumizi yalikuwa ni zaidi ya lengo la asilimia 10. Katika nusu ya kipindi kilichofanywa utafiti, maendeleo vijijini yalitumia asilimia 72 ya bajeti nzima na nusu ya pili matumizi yalishuka hadi kufikia asilimia 456.

Mheshimiwa Spika, aidha, nyaraka zinaendelea kuonyesha kwamba kwa mwaka wa fedha 2008/09 karibia ya asilimia 25 ya bajeti ilitengwa kwa ajili ya shughuli za kiutawala. Bajeti hii kwa miaka ya nyuma ilikuwa inatumiaka kwa shughuli zinazosaidia maendeleo ya sekta ya kilimo, jambo ambalo kwa sasa halitiliwi mkazo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuangalia bajeti ya Wizara ya kilimo upande wa matumizi ya kawaida na upande wa matumizi ya maendeleo ni kwamba kwa mwaka wa fedha 2000/01 matumizi ya kawaida yalikuwa asilimia 39.5 kwa mwaka 2008/09 ya kawa asilimia 82.4 na kwa mwaka 2011/2012 yakashuka na kuwa asilimia 59 na mwaka 2013/14 yakawa asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo huo ni kwamba uwiano kati ya matumizi ya kawaida na maendeleo mizani imelalia eneo moja Mwaka 2000/01 ilikuwa asilimia 60.5 na mwaka 2013/14 ni asilimia 257. Kwa tafsiri rahisi ni kwamba Serikali bado haijatambua umuhimu wa sekta ya kilimo japokuwa inatoa kauli mbiu kila kuchapo.

**MFUMO WA VOCHA ZA PEMBEJEO ZA MAZAO**

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba ruzuku kwenye mbolea ilirejeshwa na Serikali mwaka 2003 wakati Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kipindi hicho alipokuwa anawasilisha bajeti yake Bungeni. Kwa kipindi hicho kurejesha ruzuku kwenye mbolea ilikuwa ni kwenda kinyume na matakwa ya wahisani.

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2003/04, ruzuku yenye thamani ya shilingi bilioni 2 ilitolewa na ruzuku iliendelea kupanda hadi shilingi bilioni 32 kwa mwaka 2008/2009. Katika kipindi hicho mbolea ya ruzuku ilikuwa ni kwa mazao ya mahindi, tumbaku na Kahawa tu. Kwa mkopo wa Benki ya Dunia wa shilingi bilioni 138 mwaka 2009/10 mfumo wa ruzuku uliongeza wigo na kuingiza zao la Mpunga.

Mheshimiwa Spika, kuanzia kipindi cha mwaka 2008/2009 Serikali ilianzisha rasmi mpango wa ruzuku ya mbolea - *National Agricultural Input Voucher Scheme (NAIVS)* ulilenga kusambaza tani 155,000 za mbolea na tani 65,000 za mbegu kuwafikia wakulima 7000,000 katika mikoa 10 na kwa mwaka 2009/10 mpango ulilenga kuwafikia wakulima milioni 1.5.8 Aidha kwa mwaka wa uchaguzi 2010, Mpango wa ruzuku ulipanua wigo na kufikia wilaya 74 za mikoa 20 ikilenga wanufaikaji 2,000,000.9

Mheshimiwa Spika, mtafiti aliyeandaa taarifa hiyo anaeleza kuwa mpango wa ruzuku kwenye pembejeo kupanua wigo ilikuwa ni mkakati wa kisiasa ili kushinda uchaguzi na hilo lilionekana wazi maeneo ya vijijini japokuwa hilo lilikuwa ni kinyume na matakwa ya sera za wahisani10

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa utafiti huu unaweza kuwa ni ukweli kwani kama kungekuwa na upembuzi yakinifu kabla ya kuanzisha mfumo huu wa kutoa vocha za pembejeo ni dhahiri wizi na ubadhirifu unaoonekana leo usingekuwepo, lakini kwakuwa jambo lenyewe lilikuwa ni la zima moto ndio madhara yake tunayaona leo, ya pembejeo za ruzuku kutokupatikana kwa wakati au kuchakachuliwa wakati serikali tayari imekwishalipia mbolea na hivyo mfumo huu wa ruzuku ya pembejeo kuwanufaisha wafanyabiashara badala ya wakulima ambao ndio walengwa.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo imeelezwa hapo juu, CAG anasema11 kuwa mfumo wa ruzuku kwenye pembejeo hauna mwongozo na hivyo unafanyika kisiasa zaidi na mwishowe kuwanufaisha viongozi wa Kisiasa na sio wakulima. Pia utafiti wa kutosha wa aina za udongo kutokufanyika kabla ya utoaji wa hati za mbolea ili kuhakikisha pemebejo zinazotolewa unaendana na aina ya udongo wa mahali husika.

Mheshimiwa Spika, Ubadhirifu katika usambazaji wa pembejeo za ruzuku limekuwa ni tatizo kubwa duniani. Hapa Tanzania inakadiriwa kwamba asilimia 40-70 ya pembejeo za ruzuku haifiki kwa walengwa. Kwa takwimu za 2010/11 upotevu huu ni sawa na shilingi za Tanzania bilioni 58.4—102.2. Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, kupitia program ya EPINAV, kimefanya utafiti wa kina juu ya

tatizo hili na kupendekeza mfumo wa kielektroni wa kusambaza pembejeo za ruzuku, ambao kama utatumika utaondoa kwa kiasi kikubwa upotevu wa pebejeo12.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida sana katika Bunge lako tukufu kusikia Wabunge wakilalamikia wizi wa pembejeo za kilimo kama mbolea na mbegu katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Tatizo hili limekuwa sugu sasa, lakini serikali katika maeneo husika imeacha kuwachukulia hatua stahiki wale wote wanaotuhumiwa kuhusika na hujuma hizo. Kwa mfano Huko Wilayani Kasulu katika Kijiji cha RUHITA takribani Km 20 hivi kutoka KASULU mjini kumetokea wizi wa mbolea kiasi cha kutisha kulingana na kiwango au kiasi cha mbolea iliyotarajiwa kupelekwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, huko Kasulu, Mbolea aina ya MINJINGU: Kamati ya pembejeo ya kijiji ilipokea mifuko 100 tu badala ya 500; UREA Mifuko 80 badala ya 500; wanakijiji wanaeleza kwamba mifuko ya mbolea ilikuwa ikishushwa njiani katikati ya eneo la Chuo cha kilimo Mubondo na Kijiji cha Ruhita na hivyo kusababisha kupokea mifuko pungufu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ukaguzi wa CAG inaonyesha tuhuma za wizi wa vocha za pemebejeo ambazo hazikupelekwa kwa walengwa katika wilaya ya CHATO zenye thamani ya shilingi bilioni 1.16 hazikutumika na hazikutumika. Je, hapa si inaonyesha mfumo huu ni wa kuwanufaisha watu Fulani katika mfumo wa Serikali?

Mheshimiwa Spika, Hakika, ukistaajabu ya Musa utayaona ya firauni, huwezi amini sehemu nyingine nyaraka za Vocha za pembejeo zinajazwa bila pembejeo kufika vijijini; Vibali vya kupeleka pembejeo bila kuthibitishwa na Afisa Kilimo vimetolewa kwa mawakala kuthibitisha kwamba Pembejeo zimepelekwa wakati hazikufika kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Mbaya zaidi ni kwamba kila mwaka Pembejeo zimekuwa zikichelewa Wialayani Kasulu na Mkoa wa kigoma kwa ujumla wake, mathalani wakulima wa mkoa wa kigoma huanza kupanda mazao mwezi OKTOBA Kila mwaka lakini pembejeo zinaletwa mwezi Desemba, January na February.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla matatizo hayo yanajitokeza kwa sababu Mkuu wa wilaya ya Kasulu hayuko makini na maendeleo ya wakulima wilayani Kasulu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa hii ni hujuma kwa wakulima, na hii ni hatari kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, maandiko yanaendelea kuonyesha kwamba matumizi ya pembejeo za kisasa kwa wakulima limekuwa ni atatizo kubwa sana, hasa matumizi ya mbolea kwa mujibu wa taarifa ya zilizotolewa mwaka

2006 na Benki ya Dunia, Prof. Andrew Temu na Serikali yenyewe ni kwamba yako chini ya asilimia 15.

Hivyo basi, tija katika uzalishaji umekuwa chini sana, na kama matumizi bora ya pembejeo yatazingatiwa wastani wa uzalishaji kwa hekta moja unaweza kuwa ni kati ya tani 3.5 hadi 4.

Mheshimiwa Spika, tatizo la pembejeo hasa mbegu limekuwa ni tatizo sana kutokana na ukweli kwamba kuna wamiliki wa makampuni yanayozalisha au kusambaza mbegu ni viongozi waandamizi wa Serikali au ni viongozi wa juu katika siasa, jambo hili limeendelea kulalamikiwa sana na wakulima lakini hakuna hatua zozote zinazochukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa karibu nusu ya wakulima wilaya ya Hai wameathirika na kwa uotaji wa mbegu za mahindi zilizosambazwa na kampuni ya SEED CO namba 513 na namba 625, zilizoota chini ya asilimia 20, Wakulima waliothirika zaidi ni kutoka kata za Rundugai hasa kijiji cha Kawaya, Kata ya Masama na Kata ya Machame weruweru Vijiji vya Mbatakero, Ngusero na longoi, Kwa tatizo hilo zaidi ya Ekari elfu moja zimeathirika.

Pia kuna mbegu za nyanya aina ya RIO GRAND ambapo wakala wake ni DOLADAE ENTERPRISES wakulima wanaolima bustani wameathirika sana hasa wale wa Hai mjini.

Mheshimiwa Spika, baada ya malalamiko haya kutoka kwa wakulima Halmashauri ilikiri uwepo watatizo hilo na kuahidi kulifanyia kazi kwani wamejiridhisha hasa kuwa mbegu hazioti.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na muungano wa vikundi vya wakulima Tanzania-MVIWATA wilaya ya Babati ulibaini kwamba wakulima waliathirika sana na hawakuelewa maisha yao yatakuwaje kwani Serikali pamoja na kuelewa uwepo wa ugonjwa huo hadi sasa haijawahi kuwaeleza wakulima walioathirika na wanaendelea kuwa wahanga wa ugonjwa wa mlipuko kwenye zao la Mahindi ujulikanao kwa jina la kitaalam "Maize Leathal Necrosis Diseases" –(MLND).

Mheshimiwa Spika, aidha, utafiti wa MVIWATA uligundua kuwa wakulima wadogo wadogo wengi hawakuwa na taarifa kuhusiana na ugonjwa huo na hivyo waliendelea na shughuli zao za kilimo kama kawaida kwa kutumia mbegu zile zile, japokuwa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara ulitoa taarifa kwa Wakurugenzi wa Wilaya zote za Mkoa wa Manyara tarehe 6 Desemba, 201213.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo liliofanywa na Serikali ni kusimamia ufyekwaji wa mashamba ya mahindi na kuyachoma moto kwa maeneo ambayo yalikuwa yameathirika na mbegu zenye ugonjwa bila ya kuwapa wakulima nini wafanye kwa hasara iliyopatikana.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza ni kwanini Serikali imeshindwa kuwaataarifu wakulima wakati ikielewa madhara ya ugonjwa huo? Je hii si hujuma kwa wakulima hao? Je, Kampuni inayozalisha mbegu hizo inawajibika vipi kwa hasara waliyoipata wakulima hao wa Mkoa wa Manyara?

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa CAG mbegu bandia zilisambazwa kwa walengwa katika vijiji vya Mpanda, Kaisho na Nyabishenge wilaya ya Karagwe na Kijiji cha Idunda wilaya ya Ulanga.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wananchi walioathirika na tatizo hilo watafidiwa je na lini? Kwani hasara tayari imeishaingia na msimu kwa sasa umepita na kwa suala kama hili ni dhahiri kwamba wakulima toka mikoa mbalimbali wanaathirika na tatizo hili la kutoota kwa mbegu lakini Serikali inakaa kimya. Kwa njia hii ni kwa vipi kilimo chetu kinaweza kuwa cha kisasa endelevu na cha kibiashara?

**PAMBA NA UMUHIMU WAKE KWA TAIFA**

Mheshimiwa Spika, Pamba inachangia asilimia 24 ya mauzo yote ya bidhaa za kilimo nje ya nchi na inachangia asilimia 4 ya mauzo yote nje ya nchi. Takribani hekta 400, 000 zinatumika kwa ajili ya kilimo cha pamba kwenye wilaya zaidi ya 40 za mikoa 13 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, zao la pamba ni la pili kwa uingizaji wa fedha za kigeni baada ya zao la kahawa, likichangia asilimia 40 ya ajira nchini, limekuwa likikabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo tija ndogo, bei ndogo ya mbegu na pamba yenyewe, kilimo cha mkataba na stakabadhi maghala (ambavyo pia havijaeleweka vizuri kwa wakulima), uchafuzi wa pamba, uuzaji nje wa pamba ghafi kwa asilimia 75, zana na pembejeo duni, utegemezi wa mvua, mabadiliko ya tabia nchi, udanganyifu (wizi) katika mizani na kutokuwa na taarifa zinazohusu mabadiliko ya bei. Chama cha Wakulima wa Pamba Tanzania *(TACOGA)* kilifanya utafiti ulifanyika katika matao yote mawili yanayolima pamba nchini; tao la mashariki linalojumuisha wilaya za Bagamoyo, Lushoto, Same, Kilosa na Ulanga; na tao la magharibi katika wilaya za Maswa, Bariadi, Chato, Bunda, Manyoni, Iramba, Bukombe, Geita na Meatu. Utafiti huu ulitumia mbinu shirikishi ya majadiliano katika vikundi na ulishirikisha jumla wa wakulima mia nane (800).

Katika utafiti huu masuala kadhaa yaliibuliwa kama changamoto za kilimo cha pamba, kama yafuatayo:-

(i) Bei Ndogo ya Pamba;

(ii) Tija ndogo;

(iii) Kuharibiwa kwa makusudi kwa mizani kwa lengo la kumuibia mkulima;

(iv) Ushuru mkubwa unaoongeza mzigo kwa mkulima;

(v) Uwezo hafifu wa viwanda vya kuchambua pamba;

(vi) Ruzuku ndogo kutoka katika bajeti ya Taifa;

(vii) Ushindani usiozingatia Kanuni; na

(viii) Kulegea kwa Miongozo na Kanuni za zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, kikosi kazi cha wadau wapamba ambacho kilifanya utafiti huu, kilikuja na mapendekezo, kwayo Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuitaka Serikali kuyatekeleza ili kuondokana na mvutano usio malizika kati ya wadau wa Pamba na Serikali. Mapendekezo hayo ni kuwa iandikwe Sera (muongozo) ya Kitaifa ya Pamba ambayo pia itaainisha ukokotozi wa bei.

Pia muongozo huo uzingatie pendekezo la ulazima wa kuongeza thamani ya zao la Pamba hivyo kukabiliana na bei ya soko la dunia, kama ifuatavyo:-

1. Ruzuku maalum ya pamba kutoka katika bajeti ya taifa.

2. Wazawa wamiliki mashine za kuchambua pamba.

3. Wamiliki wa mashine za kuchambua pamba watengeneze nyuzi.

4. Wawekezaji viwanda vya nguo wasichambue pamba, badala yake wabaki na viwanda vya nguo na wanunue malighafi za nyuzi kutoka kwenye viwanda vya wazawa.

5. Mchambuzi huru wa ukokotozi wa bei ya pamba.

6. Mamlaka ya wakala wa vipimo na mizani kufanya ukaguzi wa mizani kwa kushikiriana na mkaguzi wa pamba.

7. Mikataba yote iwe standard na ifanyike kwa uwazi.

8. Sheria na Kanuni zitoe adhabu ya kifungo na kusitisha leseni. kwa wahusika wanaohujumu mizani na sekta ya pamba.

**UZALISHAJI WA MIWA-MTIBWA**

Mheshimiwa Spika, Mtibwa Turiani ni moja ya meneo yaliyoathirika sana na uwekezaji kwenye kilimo ambapo inaonesha wazi kuwa wawekezaji wanapambana na wakulima wadogo badala ya kusaidia na kuongeza uzalishaji kwa kuinua tija katika kilimo. Kwa mfano, uzalishaji wa miwa wa wakulima wa nje wakati kabla ya ubinafsishaji kiwanda cha Miwa Mtiba (August 1998) wakulima walizalisha 62% ya miwa yote iliyotumiwa na kiwanda.

Mheshimiwa Spika, baada tu ya ubinafsishaji, sio tu kuwa uzalishaji umekuwa ukiyumba sana bali pia umepungua hadi kufikia 35% mwaka 2001. Pamoja na juhudi za zimamoto za serikali, na kujituma kwa wakulima binafsi na Umoja wao wa wakulima *(MOA)* na kufanikiwa kuinua uzalishaji hadi 56% mwaka 2004/05 bado uzalishaji umeendelea kuathirika na sasa umekwama.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa sababu zilizoelezwa na wakulima na kubainishwa na taasisi huru za utetezi wa kilimo na wakulima ni pamoja na:-

(a) Usimamizi mbaya wa kilimo na biashara ya miwa;

(b) Mfumo na utaratibu mbaya wa uvunaji miwa ya wakulima wan je, jambo linalopelekea wakulima kupata hasara kubwa kwani miwa mingi huachwa mashambani na hata iliyovunwa haifiki kiwandani;

(c) Kwa kipindi cha 2002 hadi 2013 inakadiriwa zaidi ya tani 40,000 huachwa kila mwaka bila kuvunwa mashambani;

(d) Kusitishwa kwa utaratibu wa mwekezaji kutoa huduma za mashambani bila utaratibu mbadala kuwekwa na hivyo kuwaathiri sana wakulima ikiwemo upatikanaji wa mbegu za miwa, vifaa vya uvunaji, mbolea na pembejeo nyingine.

Mheshimiwa Spika, Sababu hizi pamoja na udhaifu wa serikali kusimamia sekta hii, ikiwa ni pamoja na kushindwa kusimamia soko la miwa na hivyo kumuacha muwekezaji akiwaathiri wakulima wa nje, uzalishaji wa miwa umeshuka toka tani 275,000 mwaka 2001/2002 hadi tani 70,247.5 kati ya tani 286,179.68, huku mwekezaji akizalisha tani 215,932.18.

Mheshimiwa Spika**,** kwa utaratibu huu serikali hii inauwa kilimo cha miwa na wakulima wa miwa nchini kwa kuneemesha wawekezaji ambao siku moja wataamua kufunga uwekezaji wao bila manufaa yoyote kwa nchi. Hii pia inatoa picha kuwa iwapo uwekezaji utaendelezwa namna hii, basi hautakuwa na manufaa yoyote kwa nchi na wananchi.

**TAKWIMU KATIKA SEKTA YA KILIMO**

Mheshimiwa Spika, watafiti wote duniani hutumia takwimu zilizofanyika nyuma na kueleza ni nini kifanyike kuboresha zaidi huduma au kukuza uchumi wa nchi kwa manufaa ya umma. Kitaalamu hakuna takwimu ambazo zinapitwa na wakati. Hivyo takwimu huwa hazipitwi na wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida utafiti huu unatakiwa kufanyika kila baada ya miaka mitano kama nchi itaweza kumudu gharama zake. Utafiti wa kwanza ulifanyika mwaka 1971/1972, wa pili ulifanyika kwa mikupuo miwili (1993/94 na 1994/1995), wa tatu mwaka 2002/2003 (ulihusu kilimo na mifugo) na wa nne mwaka 2007/2008 (ulihusu kilimo na mifugo).

Mheshimiwa Spika, utafiti wa sensa ya Kilimo na Mifugo uliofanyika mwaka 2002/03 ripoti ya matokeo yake ya awali ilitoka mwaka 2007. Matokeo ya awali yalitoka baada ya miaka mitano na machapisho mengine ya kina (further analysis) yalitoka kuanzia mwaka 2008 kwa ushirikiano na mtaalamu mshauri kutoka *FAO*. Halikadhalika Utafiti wa Sensa ya Kilimo na Mifugo ya Mwaka 2007/08 matokeo ya awali yalitoka tarehe 16 Machi, 2011.

Mheshimiwa Spika, takwimu za Utafiti wa Sensa ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 2002/2003 Takwimu zake ziliendelea kutumika katika bajeti ya mwaka 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010 na 2010/2011. Matokeo ya Utafiti wa Sensa ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 2007/2008 yamenza kutumika katika bajeti ya mwaka 2011/2012 na yataendelea kutumika katika bajeti zijazo na pia kwenye Sera ya Kilimo na Mifugo hadi utafiti mwingine wa Sensa ya Kilimo na Mifugo utakapofanyika nchini mwaka 2013/2014.

**USHIRIKA**

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika huanzishwa na kuandikishwa kwa kuzingatia Sheria ya Ushirika ya Mwaka 2003, ambayo mwaka 2013 sheria hii ilibadilishwa na kutungwa upya kwa kuanzisha tume ya Ushirika ili iendane na utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini (CRMP) iliyobuniwa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, vyama vya ushirika ni mkombozi wa wakulima katika kuboresha kilimo chenye tija na ufanisi na katika utafutaji wa masoko na masoko, hivyo basi vipewe mikopo na mabenki ili viweze kujiendesha vyenyewe kuliko mtindo wa sasa wa serikali wa kupitia makampuni hasa kwenye sera ya Kilimo cha mkataba kwamba badala ya kutegemea makampuni kwenye usambazaji wa mikopo, pembejeo na mbegu basi vyama vya ushirika ndivyo vitumike hiyo itasaidia hata pia kuvinufaisha vyama vyenyewe na kuondoa riba kubwa anayokatwa mkulima na makampuni hayo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Idara ya Ushirika fungu 24 inaonyesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/15 idara imetengewa jumla ya shilingi 6,855,413,000.00 kama matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 4.5 ni matumizi mengine. Aidha, kifungu 4003 Sehemu ya Benki za Ushirika na Uwekezaji, kimetengewa jumla ya shilingi170,515,000.00.

Mheshimiwa Spika, Randama ya Ofisi ya Waziri Mkuu fungu 37 taarifa ya Mhe. Waziri wa Uwekezaji na Uwezeshaji uk. 40 inaonyesha kuwa benki za CRDB na NMB zilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 37.169 kwa SACCOS 192 na vikundi 86 na Wajasiriamali 44,224.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, kwa kuwa SACCOS ziko chini ya Idara ya Ushirika, hivyo basi ni vyema tukaelezwa uhusiano uliopo kati ya taasisi hizi kiutendaji kuhusiana na uratibu wa SACCOS na Benki za Ushirika.

**MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2014/2015**

Mheshimiwa Spika, kwamwaka huu wa fedha, wizara yenye mafungu 43, 24 na 05 imetengewa jumla ya shilingi 355,002,111,000/- na kati ya fedha hizo shilingi 278,988,821,000/- ni fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi 76,013,290,000/- ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida kwa fungu 43, wizara imepanga kutumia shilingi bilioni 271.6, kati ya fedha hizo shilingi 2,765,100,000/- zimepangwa kutumika kwa ajili ya usafiri tu. Hii ni pamoja na shilingi milioni 877.2 kwa ajili ya ununuzi wa magari na pikipiki, shilingi milioni 994.9 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta na vilainishi. Huku shilingi milioni 893 zikipangwa kutumika kwa ajili ya nauli za ndege na mabasi kwa ajili ya watumishi wa wizara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu kwa safari za watumishi kama njia mojawapo ya utendaji wao, lakini ikumbukwe kuwa Wizara hii ina safari chache sana kuwafikia walengwa, yaani wakulima. Hivyo pamoja na haja ya kuongeza bajeti kwenye sekta ya kilimo, ni vyema fedha zielekezwe eneo lenye tija.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ni muhimu kwa watendaji na wataalam, lakini msingi mkuu wa utaalam kwa wizara hii ni kuwezesha wakulima kupata na kutumia utaalam kwa tija. Wizara hii imepanga kutumia shilingi milioni 804.44 kwa ajili ya mafunzo na semina, kati ya fedha hizi shs milioni 71.34 tu ndizo zinazolenga wakulima, ambazo ni sawa na asilimia 9 ya fedha za mafunzo. Huku zaidi ya shilingi milioni 733 ambazo ni zaidi ya asilimia 90 ya fedha za mafunzo zikielekezwa kwenye mafunzo na semina za watendaji wa Wizara, aidha shilingi bilioni 1.37 zimetengwa kwa ajili ya mafunzo kwenye fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, hivi wizara hii mteja wake ni nani? Na anaetakiwa kuwezeshwa ni nani? Na swali kuu la kujiuliza ni je, watumishi wanaoajiriwa na wizara hii hawana sifa kiasi cha kuhitaji mafunzo kila mwaka? Ni lini hali hii itabadirika kwa kila mwaka mafunzo kwa watendaji wa wizara. Huu ni muda mwafaka kwa serikali kubadilika na kuangalia kwanini sekta binafsi inavyofanya kazi na raslimali watu inatumika vipi.

**TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI**

Mheshimiwa Spika, Bunge hili lilitunga sheria ya uanzishaji wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji mwaka 2013, ili kuweza kudhibiti na kusimamia uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji. Kutokana na uanzishwaji huo wa Tume, idara ya umwagiliaji na huduma za ufundi katika bajeti ya mwaka huu haikutengewa hata senti moja kwani kazi zake zimehamishiwa kwenye Tume.

Mheshimiwa Spika, katika Randama ya Wizara uk.24 inasema Rasimu za Kanuni za Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji na mapendekezo ya muundo wa Tume zimeandaliwa lakini hadi sasa hazijawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuidhinishwa na kutolewa kwenye Gazeti la Serikali. Mhe. Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza inakuwaje kanuni bado hazijapitishwa ni kwa vipi Tume hiyo inapewa kazi wakati mwongozo wa kufanyia kazi bado haujatolewa?

Mheshimiwa Spika, mwaka huu Wizara, kupitia tume ya Umwagiliaji (Fungu 05) imepangiwa shilingi milioni 475 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha shilingi bilioni 28.93 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Lakini kutokana na umuhimu wake tume imeanza vibaya kwa muktadha wa matumizi ya fedha. Tume imepanga kutumia shilingi milioni 227 kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi tu, shilingi milioni 69 zikielekezwa kwenye kuwezesha watumishi kuhudhuria maonyesho ya kilimo, shilingi milioni 61 ni kwa ajili ya stahili za watumishi na zaidi ya shilingi milioni 88 ni kwa ajili ya ufuatiliaji,tathmini na mambo mtambuka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na fedha hizi, tume imepanga kutumia zaidi ya shilingi bilioni 7.083 matumizi ya kawaida/uendeshaji kati ya shilingi bilioni 28.9 zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mchanganuo ni kwamba Programu 4486 mradi namba: CO3CO1, Programu 4496 miradi namba: CO4CO1; CO4CO1; Kifungu 1004 CO3SO1; Kifungu 1007 Programu CO2DO1; Kifungu 2001 Programu 4486 miradi: CO3CO1;CO3CO2;CO3CO3;CO3CO4;CO4CO2.

Kifungu 2002 programu 4486: DO1DO1; Kifungu 2004: Programu 4486: EO2SO1. Vifungu hivyo vipo kwenye bajeti ya maendeleo lakini ni matumizi ya Kawaida.

Aidha, shilingi bilioni 1 zimepangwa kununua magari 16 kwa ajili ya matumizi ya tume, huku zaidi ya shilingi bilioni 3.1 kwa ajili ya watoa huduma binafsi.

Mheshimiwa Spika, mradi namba CO3CO1 umetengwe shilingi 1,566,148,676.00 zimetengwa kuajiri mshauri mwelekezi kwa ajili ya kusimamia uendeshaji wa skimu ndogo za umwagiliaji kupitia mradi wa SSIDP unaofadhiriwa na JICA. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza kama fedha hizo kwa mwaka ni kwa mshauri mwelekezi ambayo kwa mwezi ni shilingi milioni 130.5. Aidha mradi namba DO1SO2 kumuajiri mtoa huduma wa binafsi kwa ajili ya skimu 78 za BRN shilingi 1,455,000,000.00 sawa na shilingi milioni 121.25 kwa mwezi. Je kwa matumizi haya Tume itakuwaje na tija kwa Watanzania?

Mheshimiwa Spika, mradi namba CO3CO4 kununua pikipiki 80 kwa ajili ya ofisi za umwagiliaji katika halmashauri, shilingi 248,000,000.00 ambayo ni sawa na shilingi milioni 3.1 kwa kila pikipiki. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua hiyo pikipiki inayonunuliwa kwa shilingi milioni 3.1 ni ya aina gani na inatoka nchi gani? Tunachoelewa ni kwamba kadri zinavyonunuliwa kwa wingi na bei yake inapungua.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi inaitaka Serikali ieleze kama tayari imekwishapanga kutumia shilingi milioni 227 kwenye fedha za matumizi ya kawaida, ni kwa vipi tena matumizi ya kawaida yanawekwa kwenye fedha za miradi ya maendeleo?

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla inaonyesha kwamba Tume hii imeundwa kuwa huru kiutendaji lakini inaweza kutumika kuwa kichaka cha ufisadi mkubwa sana na hivyo tija kushindwa kuonekana. Mfano ni matumizi ya fedha tajwa kwa kuajiri washauri tu. Hoja nyingine ni kwanini tume inashindwa ku-consolidate fedha za wahisani na wao wakapanga matumizi kulingana na hali halisi ya nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, kwa hali halisi ya bajeti ya maendeleo ya Tume ya Umwagiliaji ni shilingi milioni 567.8 tu, ambayo inaenda kwa wakulima, japokuwa shilingi milioni 350 hazina uhusiano wa moja kwa moja na umwagiliaji kama jukumu la msingi la Tume linavyohitaji.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge, kuna haja gani ya kuwa na Tume ya Taifa iwapo miradi iliyo chini yake inaendeshwa na watu binafsi? Mpango huu unaonekana kuwa dhamira yake si ya kuendeleza sekta bali ni kutafuta fedha kwa ajili ya kundi fulani kwenye mchakato wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

……………………………………….
Rose Kamili Sukum (Mb)
K.n.y Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani - Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.
10.5.2014

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitatangaza orodha ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; Wageni wa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa *Engineer* Christopher Kajoro Chiza ni Wakuu wa Idara na Bodi za Mazao na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo, wakiongozwa na Bibi Sophia E. Kaduma, Katibu Mkuu wa Wizara.

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa *Engineer* Christopher K. Chiza, ambao ni Bibi Gloria Chegeni Chiza, mke wa Waziri na Bwana William Chiza, mtoto wao.

Wageni 40 wa Mheshimiwa Godfrey Zambi, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kutoka Jimbo la Mbozi Mashariki wakiongozwa na Ndugu Aloyce Lavuma, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbozi. Karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Mgeni mwingine wa Mheshimiwa Godfrey Zambi ni Bibi Mkesa Zambi, mke wake. Karibu sana Mama Zambi. *(Makofi)*

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 142 kutoka Chuo cha Mipango Dodoma na wanafunzi 87 na walimu 3 kutoka Shule ya Msingi Chidachi.

Tangazo la kikao cha Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara: Mwenyekiti anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuwa leo tarehe 10 Mei, 2014 saa 5.00 asubuhi kutafanyika Kikao cha Kamati ya Wizara ya Fedha na Uchumi katika Ofisi ya Hazina Ndogo Dodoma, Ukumbi Na. 136; tunaomba mmalize upesi mrudi jioni kupitisha bajeti.

Mheshimiwa Ngeleja, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, anawatangazia Wajumbe wake kwamba leo tarehe 10 Mei, 2014 saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi wa Hazina Ndogo Na. 125.

Mheshimiwa Peter Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuwa kesho Jumapili tarehe 11 Mei, 2014 saa 5.00 asubuhi kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi Na. 136 uliopo Hazina Ndogo.

Mheshimiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuwa kesho tarehe 11 Mei, 2014 saa 5.00 asubuhi, kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi Na. 229 Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge sasa tunaingia kwa wachangiaji; tuna wachangiaji leo kama 28, ninategemea kuwamaliza wote. Tunaanza na Mheshimiwa Hezekiah Chilubunje.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu naitwa Hezekiah Chibulunje. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Hivyo hivyo.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia hoja hii ya Hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika ambayo naiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla, kwa kukamilisha mchakato wa kutungwa kwa Sheria mbili muhimu Na. 5 na 6 za mwaka jana ambazo zinatoa nafasi ya kuanzishwa kwa Tume kuu mbili; Tume ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika ambazo zote zina lengo la kuharakisha maendeleo ya kilimo na ushirika kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la umwagiliaji, ningependa kusema kwamba katika maeneo kame kama Mkoa wetu wa Dodoma, kilimo cha mvua ni kilimo cha kubahatisha sana. Kwa hiyo, niiombe Wizara ihakikishe katika mipango yake ya umwagiliaji inajielekeza katika kutoa kipaumbele katika maeneo kame ukiwepo Mkoa wetu wa Dodoma. Kipekee, nimwombe Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa kututengea fedha katika kilimo cha umwagiliaji katika shamba letu la zabibu pale Chinangali, lenye ekari 250, ziongezwe mpaka ekari 400 ili Mradi huu uweze kuwanufaisha wakulima wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na Mradi huu, lakini kwenye Jimbo langu la Chilonwa kuna miradi mingine ya umwagiliaji ambayo ni Skimu ya Bwigiri, Skimu ya Bwawa la Ikowa katika Kijiji cha Chalinze ambayo kwa sasa hivi kusema kweli inahitaji tu ukarabati ili iweze kufanya shughuli za umwagiliaji kwa mwaka mzima, badala ya hali ya sasa ambapo umwagiliaji unafanyika katika kipindi kifupi sana cha mwaka. Sambamba na Miradi hii miwili, uko Mradi mpya ambao unaanzishwa katika Bonde la Bwawa la Dabalo kwa ajili ya kilimo cha miwa. Naomba Serikali ianze kutenga fedha kwa ajili ya kuanzishwa kwa Mradi

huu. Haya yote yakifanyika, itatuondoa katika kilimo cha kutegemea mvua ambacho ni cha kubahatisha sana ili wakulima wetu waweze kujiongezea kipato na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la ushirika, naishukuru sana Wizara kwa jitihada ambazo zimefanyika katika kuunusuru ushirika kwenye matatizo mengi. Kama alivyokiri Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwamba moja ya matatizo au sababu zinazosababisha kuzorota kwa ushirika ni ukosefu wa usimamizi kwa karibu; na hapa nijikite katika suala zima la ukaguzi yaani *Cooperative Inspectorate*. Kada hii ya Ukaguzi wa Ushirika imezorota kwa muda mrefu sana, lakini nashukuru sasa Tume imeundwa; kwa hiyo, ningeomba Tume hii ianze kazi yake kwa kujielekeza katika kufufua kada ya *Cooperative Inspection* ambayo naomba kwanza ianze kwa kuajiri watumishi wengi wa kutosha na kuwapa mafunzo.

Kwa hiyo, niiombe Wizara kwa kushirikiana na Chuo chetu Kikuu cha Ushirika Moshi, kuweza kuandaa Programu Maalum ambayo itawezesha kuwapa mafunzo hawa Wakaguzi wa Ushirika, kwa sababu sekta hii imeshazorota kwa muda mrefu, ili waweze kupata ujuzi na uwezo wa kuweza kusimamia na kukagua Vyama vya Ushirika katika sehemu za Wilaya. Kwa kweli ningesisitiza Wakaguzi hao wasambazwe Wilayani ambako ndiyo kuna kazi ya kusimamia Vyama vya Ushirika.

Sambamba na hilo, niiombe Wizara iimarishe Shirika la Ukaguzi la Vyama vya Ushirika *(COASCO)*. Mambo mengi yanayojitokeza hapa katika kuzorota kwa ushirika nchini ni kutokana na kukosekana na ukaguzi. Shirika la Ukaguzi la *COASCO* halina uwezo wa kutekeleza majukumu yake ipasavyo na ndiyo maana hata hapa kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri zile kazi ambazo zinatakiwa zisimamiwe na *COASCO* kwa karibu, sasa zinaelekezwa kwa *CAG*. *CAG* ambaye ana kazi nyingi sana za kukagua Mashirika ya Umma na Idara za Serikali, kwa hiyo, tukiimarisha Shirika hili la *COASCO* litaweza kusimamia hivi Vyama vya Ushirika ambavyo Mheshimiwa Waziri amekiri katika hotuba yake kwamba vimezorota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, sambamba na uzalishaji wa mazao ambayo tunayazalisha katika hizi skimu za umwagiliaji. Mheshimiwa Waziri anajua ya kwamba, katika ile skimu yetu ya umwagiliaji ya pale Chinangali tuna tatizo kubwa sana la soko; zabibu zinazalishwa pale lakini upatikanaji wa soko ni shida sana. Hivi sasa ninapozungumza, zabibu tulizozivuna mwezi Februari mpaka sasa wakulima hawajalipwa. Hii inatokana na kuwa na mnunuzi mmoja tu, ambaye anashikilia ukiritimba na kwa hiyo anafanya jinsi anavyotaka. Kwa hiyo nadhani Serikali ikisimamia shughuli hizi za uzalishaji katika skimu hizi za uzalishaji hususan katika ile skimu yetu ya

umwagiliaji ya Chinangali sambamba liwepo na suala zima la kutuletea soko ambalo litakuwa la uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependekeza kwamba, zabibu ni zao la biashara ambalo litakuwa la uhakika katika Mkoa wetu wa Dodoma. Pengine ni vizuri basi ikaundwa Bodi Maalum ambayo inaweza kusimamia kusukuma masoko ya zao hili, maana tunashuhudia kwamba mazao ambayo yana usimamizi wa soko, matatizo haya hayajitokezi kama ambavyo yanajitokeza katika eneo letu hili. Kwa hiyo, wakulima wangependa sana suala hili la soko la zabibu likatiliwe mkazo na hatimaye wakulima waweze wakanufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nimkumbushe tu Waziri kwamba, katika mazao mengine kuna ruzuku za pembejeo, lakini zao letu la biashara kwa hapa Dodoma ni zabibu. Kwa hiyo, nianze kuomba zao hili lianze kufikiriwa kuingizwa katika ruzuku ili kuwawezesha wakulima wapate kipato cha kuwawezesha kuondoa umaskini. Tukifanya hivyo tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana ya kuwasimamia wakulima wetu na hatimaye na wao waweze kujikomboa katika matatizo ya kujiondolea umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema, katika sekta hii ya ushirika tusipoimarisha ukaguzi, hizi shughuli zingine zote zitakuwa zinagonga ukuta kwa sababu watu watakuwa wanakula fedha bila woga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo, machache nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa ningemwita Mheshimiwa Azza, lakini nitampa Mheshimiwa Genzabuke kwa sababu anawahi kwenye Kamati, Mheshimiwa Azza atafuatia baada ya Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa rehema zake nyingi, kunijalia kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa Hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kwamba, mwaka huu tumejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 18. Ninawapongeza Wakulima wa Tanzania kwa kazi kubwa ya uzalishaji kwa kuweza kufikia kiwango hicho. Naomba niwapongeze Wakulima wa Mkoa wa Kigoma kwa juhudi za kuweza kuzalisha chakula kwa kiasi kikubwa. Kwa kumbukumbu zangu, Mkoa wetu wa Kigoma sijawahi kusikia tukipelekewa chakula cha njaa. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa juhudi wanazozifanya. Tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu, aendelee kutujalia tuwe na nguvu, tutunze mazingira kwa

sababu ardhi yetu ni nzuri, mvua ni za kutosha ndiyo maana tunapata chakula cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya nchi nzima kuhusu chakula wakati mwingine imekuwa ni ya wasiwasi kwa sababu ya mvua. Mwaka huu mvua zimekuwa nzuri, kwa hiyo, najua tutaendelea kupata chakula kwa kiasi kikubwa, naomba Serikali ijiandae kuhakikisha inanunua chakula cha Wananchi watakachokuwa wamekizalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbolea iliyokuwa ikipelekwa kwa Wananchi; naipongeza Serikali kwa kuondoa utaratibu wa njia ya vocha. Mkoa wa Kigoma hususan katika Wilaya ya Kasulu, tumekuwa tukiathirika sana kwa mbolea hii. Wananchi wamekuwa wakipata shida, imekuwa ikiwanufaisha watu wachache, maskini wakibaki wanapata shida. Hii ni sera ya Chama cha Mapinduzi kwamba wakulima watasaidiwa pembejeo kupitia kwenye Sera yetu ya Chama cha Mapinduzi. Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ilisema kwamba, Wananchi watasaidiwa, lakini Wananchi wamekuwa hawanufaiki wamekuwa wakinufaika watu wachache. Maeneo mengine utaratibu huu umekuwa ukiwasaidia, lakini kwa Kasulu imekuwa kilio badala ya furaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani utaratibu huu kupitia vikundi tutaweza kufanya vizuri, kwa sababu mimi ni Mbunge wa Viti Maalum, lakini ni Mwenyekiti wa UWT wa Mkoa. Nimekuwa nikipita kuwahamasisha wanawake na wanawake wamejiunga kwenye vikundi wameanzisha *SACCOS,* kwa hiyo, nina imani kwa utaratibu huu watapata mbolea na watakuwa wazalishaji wakubwa sana. Utaratibu huu wa mbolea kwa njia ya vocha ni ukweli usiopingika, wapo watu ambao walikuwa Viongozi lakini walikuwa wanafanya ubadhirifu wa namna hii. Kwa kweli ninaishukuru Serikali kwa kuondoa utaratibu huu na kuanza utaratibu mpya, nina imani vikundi vitaweza kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NFRA* imeanza kuja Kigoma kununua mazao, naomba hifadhi ya chakula iongeze bidii sasa kuhakikisha inakwenda kunununua mazao kwa sababu Kigoma mazao yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na migogoro mikubwa sana baina ya wakulima na makundi mbalimbali; mfano, wakulima na Hifadhi za Taifa na wakulima na wafugaji. Kwa mfano, katika Wilaya ya Kasulu eneo la Kagerankanda, watu hawa wanapakana na Hifadhi ya Taifa. Ninaomba Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Waziri wa Maliasili na Utalii wakae wote kwa pamoja waangalie ni jinsi gani watawasaidia Wananchi hao ambao wamepakana na Hifadhi ya Taifa. Ikiwezekana, Sheria iletwe Bungeni ifanyiwe marekebisho ili mipaka isogezwe Wananchi wapate maeneo ya kulima. Vilevile watu wa *game reserve,* waangalie maeneo ambayo hayatumiki wayapime upya ili Wananchi wapate

maeneo ya kulima kwa sababu tunasema kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo na wananchi bila ya kulima hawawezi kunufaika. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie utaratibu wa kurudisha Sheria Bungeni, ifanyiwe marekebisho, mipaka isogezwe Wananchi wapate maeneo ya kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya nchi nzima ya wafanyakazi, maafisa ugani, ni 15,082 ili kijiji na kata kipate afisa ugani mmoja. Mwaka 2013/2014, Serikali ilikubali kuajiri watu 1,804, walioajiriwa ni 1,382 na waliobaki ni 422. Naomba Serikali iwaajiri hao 422 waliobaki ili iongeze ajira na tuweze kufikia lengo letu la wafanyakazi 15,082. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, naomba nikushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa Mheshimiwa Azza Hillal, ajiandae na Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. AZZA HILLAL HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuweza kunipa afya ya kutosha na hatimaye nimesimama ndani ya ukumbi wako nikiwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Naibu Waziri wa Chakula, Kilimo na Ushirika, kaka yangu Zambi, mara baada ya kuteuliwa ametembelea Mkoa wa Shinyanga na amejionea hali halisi ya Miradi ya Umwagiliaji iliyopo Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri alitembelea Mradi wa Itilima uliopo Kishapu, Mradi wa Ishololo uliopo Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga na Mradi wa Masengo uliopo Halmshauri ya Wilaya ya Shinyanga. Bado nimwombe kuna mradi mmoja wa Kahanga ambao hata kwenye taarifa ya Waziri umeonekana naomba mkaungalie ili uweze kukamilika mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite katika Miradi ya Umwagiliaji tu kwa siku ya leo. Mradi wa Umwagiliaji wa Ishololo uliopo Halmashauri ya Shinyanga, Naibu Waziri ameuona, mkataba ulisainiwa mwaka jana mwezi Februari na mradi ulikuwa ni mkopo kutoka *IDB* kupitia *DASIP,* shilingi milioni 748 na Halmashauri ilichangia shilingi milioni 200 ikawekwa kwenye akaunti ya *DASIP*. Kama tunavyojua *DASIP* muda wake umekwisha 2013 Desemba. Cha kushangaza na cha kusikitisha, Mradi huu haujakamilika, ulikuwa ukamilike mwaka jana mwezi Agosti, Mkandarasi akaongezewa muda lakini bado mpaka hivi ninavyoongea, ukifika *site* hakuna vifaa na hakuna kitu chochote kinachoendelea, lakini Mkandarasi huyo alishalipwa shilingi milioni 250.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa natapa tabu; MKATABA ulisainiwa Wizarani na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mkoa haujui, Halmashauri haijui, Ofisi ya Kanda haijui! Mimi najiuliza hii mikataba inayokuwa inasainiwa Wizarani wana mpango gani na Miradi yetu ya kwenye Halmashauri; kwa sababu ukimfuata Mkandarasi anakwambia mimi Halmashauri sihusiki kwenu wala mkoa sihusiki kwenu nahusika na Wizara! Mimi naomba hawa watendaji wanaotumia madaraka yao vibaya hebu Serikali iwaangalie; kwa sababu mkandarasi huyu sasa anafanya mwenyewe anavyojua, hana mtu wa kumwuliza. Wananchi mwaka jana hawakuweza kulima, mwaka huu hawakuweza kulima na bado maji waliyokuwa wanategemea kuvuna hawakuweza kuyavuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata tabu, kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa sababu Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wamejipanga vizuri kwa Mradi huu, nategemea wakisimama hapa wataniambia Mradi wa Isholol0 unamalizwa kwa staili gani? Kwa sababu *DASIP* ilishakwisha muda wake lakini bado nilikuwa naomba nipewe majibu zile shilingi milioni 200 ambazo zilichangiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga na zikaingia kwenye akaunti ya *DASIP* zipo wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipewe majibu tunazihitaji shilingi milioni 200 zetu zilizokwenda kwenye akaunti *DASIP*. Nimwombe sana Waziri, akisimama awaambie Wananchi wa Shinyanga, Mradi wa Ishololo hatima yake ni nini, bila ya kusema hayo siwezi kumwelewa Waziri. Naomba awaambie Wananchi wa Shinyanga kinachoendelea katika Mradi wa Ishololo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie katika Mradi wa Umwagiliaji wa Masengwa. Mheshimiwa Naibu Waziri Zambi, amefika katika Mradi wa Umwagiliaji Masengwa na toka nimechaguliwa kuwa Mbunge hakuna siku ambayo nimesimama bila kusemea Masengwa.

Mimi naomba kuuliza; hivi hizi ahadi mpaka ufanye nini ndiyo zitekelezwe kwa sababu hii ni ahadi ya Serikali toka mwaka 2007? Leo naelekea kumaliza miaka mitano Mradi huu haujatekelezwa. Mimi naomba kuambiwa kama Mradi huu hautekelezwi mtuambie, Waziri ukisimama hapo naomba uniambie ili Wananchi wa Masengwa wajue kama mradi unatekelezwa au hautekelezwi. Siku zote tunasema, aliyekuwa Waziri Mkuu mstaafu wakati huo Mheshimiwa Lowassa, alifika kuuzindua Mradi ule na akaahidi kuchimba bwawa katika Mradi ule, lakini zimekuwa ni ngonjera tu. Serikali ipo, ofisi ipo, kigugumizi kiko wapi? Kwa nini mnatutesa Wananchi wa Shinyanga? Ahadi mlitoa wenyewe Serikali, lakini kutimiza ule MRADI imekuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ahadi hii haitekelezwi, tuambieni watu wa Shinyanga tujue tutafute namna nyingine ya kufanya kuliko kukaa tunajua kuna Mradi ambao tuliahidiwa na Serikali na ipo siku utatekelezwa, miaka inakwenda hatimaye hatujui hatima ni nini.

Mheshimiwa Zambi umefika pale, umewasikia Wananchi walivyokulalamikia. Sikutegemea kutouona Mradi wa Masengwa kwenye Hotuba ya Waziri. Nimwombe Waziri akisimama hapa, awaambie Wananchi wa masengwa ahadi hiyo itatekelezwa lini, kwa sababu bila kuwaambia sidhani kama wanaweza kutuelewa na wala mimi siwezi nikaelewa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ukisimama useme na nadhani hili sasa limekuwa kero hata humu ndani, kila nikisimama nalisema lakini utekelezaji wake bado ni sifuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii pia kuishauri Serikali iweze kuongeza bajeti katika Wizara ya Kilimo ili kuondokana na kilimo ambacho kinategemea mvua. Tukishakuwa na Miradi mingi ya Umwagiliaji, nina hakika suala la chakula litakuwa ni la uhakika na si kama ambavyo sasa hivi tunakwenda kwa kutegemea mvua ambazo hazitabiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mafuriko makubwa yanayotokea, maji yanapotea hayana sehemu ya kwenda. Hivi tunashindwa nini kuyavuna yale maji na hatimaye watu wetu wapate maji kwa ajili ya kumwagilia mazao, bustani na maji kwa ajili ya mifugo? Nina hakika kabisa kama Serikali itaongeza bajeti Wizara ya Kilimo, hakuna linaloshindikana. Kama kweli tunasema kilimo ni uti wa mgongo, hebu Serikali iangalie basi Wizara ya Kilimo iweze kuongezewa fedha waweze kutekeleza yale ambayo tunayahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema tena, namwomba sana Mheshimkiwa Waziri, akisimama hapa aniambie hatima ya Mradi wa Ishololo na hatima ya Mradi wa Masengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndassa, jiandae Mheshimiwa Silinde.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono Hotuba ya Waziri, lakini nina mambo mawili makubwa.

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ni shahidi, nimekuwa nikimwomba mara kwa mara kuhusu ghala la chakula pale Bukwimba, Nkalalo. Alipokuja wakati wa uzinduzi wa mbegu za *quton* pale Kata ya Mwandu, nilimwambia na bahati nzuri alipita eneo hilo akaona. Miundombinu iliyoko pale inajitosheleza kabisa kabisa kuhifadhi mahindi pale au nafaka mbalimbali.

Ninaomba niulize; katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri sijaona, sasa ni vizuri akatuambia kama inawezekana au haiwezekani, kuliko kukaa kila siku tunaomba. Mama Hewa juzi katika swali lake la nyongeza aliuliza, ukasema kitabu changu kwenye bajeti nitalisemea, sijaona. Ukipeleka hifadhi ya chakula kwenye eneo lile, Wananchi wa Mikoa ya Simiyu, Mara na Mwanza, watachukulia pale badala ya kwenda kuchukua chakula Shinyanga ambako ni mbali. Gharama inakuwa kubwa zaidi kwa sababu kutoka Mara kwenda Shinyanga ni mbali, kutoka Simiyu kwenda Shinyanga ni mbali. Kutoka Kalalo, Bukwimba ni karibu zaidi, ipo reli, ipo barabara na maghala yapo. Mnang'ang'ania kwenda kujenga mengine ili kuongeza gharama! Naomba Mheshimiwa Waziri, alijibu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuhusu mbegu za pamba za *quton*, Wakulima wa Mikoa wa Mwanza, Shinyanga wameathirika sana na mbegu hizi, lakini amesema kwamba, hawatapeleka fedha zote bilioni 10, watapeleka shilingi ngapi, wanajua wenyewe. Huyu mkulima aliyeathirika na mbegu hizi yeye anafidiwa na nani? Amenunua mara ya kwanza akapanda hazikuota, akaenda kununua mara ya pili akapanda hazikuota, ina maana kwa mwaka huu wa msimu wa kilimo hana pamba tena; nani atamfidia?

Tunaomba Mheshimiwa Waziri hili nalo mlione, kwa sababu yeye huyu mkulima wa pamba hana kosa hata kidogo, kosa liko kwenye mbegu zenu mlizozipigia debe. Ulikuja Mwandu pale mkazipigia debe, Mwenyekiti wa Bodi ya Pamba yeye ndiye akawa *sales and marketing manager* wa kubeba mpaka ule mfuko, mbegu nzuri, mbegu nzuri, kumbe mbegu zenyewe hazioti. Sasa mkulima huyu wa pamba amepata hasara. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atuambie huyu mkulima aliyeathirika atafidiwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabla kengele ya pili haijalia; Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa *champion* mkubwa wa kupinga mbolea ya Minjingu. Alisema kabisa kwamba, hii mbolea haifai. Sasa kwa sababu yuko jikoni huko, hebu atuambie leo baada ya kuingia kule na kuchunguza; je, hiyo mbolea ya Minjingu inafaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nakushukuru, naomba nipate maelezo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Silinde, ajiandae Mheshimiwa Hilda Ngoye.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii na mimi nichangie mambo kama matatu kwa haraka haraka kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huwa najiuliza, tunapokuwa tunatengeneza bajeti tunakuwa tunatafsiri nini! Ukipitia bajeti ya Kilimo, nizungumzie tu fungu namba 5, fungu la Miradi ya Maendeleo. Mwaka jana tulitenga kwenye Wizara ya Kilimo shilingi bilioni 81, iliyotoka ilikuwa shilingi bilioni 41. Cha ajabu mwaka huu kwenye fungu namba 5 kuhusu Miradi ya Umwagiliaji huko huko, fedha za Miradi ya Maendeleo, fedha iliyoombwa ni bilioni 29. Ukipitia Miradi ya Umwagiliaji hakuna kitu. Mheshimiwa Waziri unajua, Jimboni kwangu kuna Mradi wa Naming'ong'o wa umwagiliaji, leo ni mwaka wa tano haujakamilika. Hii ninyi ndiyo mnatakiwa mjibu kwa nini mpaka leo ile miradi haikamiliki.

Mwaka jana Mheshimiwa Wasira alisema hii Miradi yote itaisha katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 na tumetengea fedha. Matokeo yake tunakuja tena Bungeni mwaka huu hakuna kinachoendelea. Sasa wale Wananchi tuwasaidieje? Ukiangalia humu, kazi zimetekelezeka lakini hamna kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wizi na niseme ukweli, miongoni mwa Miradi ambayo fedha zinaibiwa sana nchi hii ni Miradi ya Umwagiliaji na Miradi ya Maji ndiko ambako fedha zinapelekwa na ndiko zinakoibiwa sana, miradi haikamiliki kwa wakati na miradi haiendi popote. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili hatuwezi kuvumilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hapa lazima kama ni CAG aunde tume na ninyi muunde tume iende ipitie Miradi yote na mtuambie lini itakamilika ili Wananchi wetu waende katika hicho kilimo kinachotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, mwaka jana ukipitia kwenye Ripoti ya Mkaguzi *(CAG)*, kulikuwa na fedha za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Sasa kuna Halmashauri nyingi kweli kweli hapa zimepata hati mbaya, hati isiyoridhisha na hati zenye mashaka. Mheshimiwa Zambi, ndugu yangu Naibu Waziri, Halmashauri ya Mbozi imepata hati mbaya peke yake, Halmashauri nyingine hazijaridhisha na nini. Sasa wewe ndiye Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Halmashauri ya Jimboni kwetu kule Mbozi hati mbaya, hapo tafsiri yake ni nini? Ni sawa sawa na mtu ananiambia kuna watu wanagombea Urais halafu Jimbo lao ndiyo la pili kwa umaskini. Hatuwezi kwenda katika mfumo huu. Kwa hiyo, kama Waziri lazima uwe mfano, Jimbo, Wilaya, ina hati mbaya, ni Halmashauri moja tu ya Mbozi. Kwa hiyo na hili tupate ufafanuzi tuelezwe, wale watu waliosababisha haya wanachukuliwa hatua gani ambazo zimepelekea hasara hii na hizi fedha zinarudi vipi katika Halmashari yetu ziweze kusaidia Wananchi wa Mbozi pamoja na Momba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, nizungumzie suala la pembejeo za ruzuku. Pembejeo hususan vocha za mbolea, yaani kama kuna mahali Wananchi wanaibiwa ni kwenye pembejeo za kilimo hususan vocha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, Wananchi hawapewi vocha za pembejeo wanapewa fedha. Wakati wa kilimo badala ya kupewa ile vocha asaini anapewa shilingi 5000/=, shilingi 3000/=, shilingi 8000/=, na jimboni hayo kwangu mambo yamekuwa yakitokea na tumekuwa tukiripoti kila mara. Sasa kama hili jambo litaendelea na mimi niahidi hapa hapa Bungeni, mwakani tutawakamata mawakala wote wanaofanya hii biashara, mtasikia mambo mabaya na nisingependa niyatangaze hapa, mtayaona ninyi wenyewe kwa sababu hamchukui hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, hizo hizo pembejeo; moja ni chache, ugawaji sasa hivi unafanyika kwa upendeleo. Wananchi wanalalamika wanasema ili upate pembejeo ni lazima uwe Mwanachama wa CCM. Nini nyote mnajua kwa sababu kule vijijini upendeleo wa namna hii hauwezi kuleta mantiki na hatuwezi kuokoa kilimo. Tuongee ukweli jamani kilimo cha kumpa mtu mfuko mmoja wa mbolea anawezaje kuinuka kiuchumi katika hali halisi, wakati watu nje tunapokwenda sisi wote kuona mifano, watu wanalima heka 5/10 ndiye mkulima mkubwa lakini uzalishaji unakuwa mkubwa. Kwanza, ukipitia tu hata hii taarifa yenyewe badala ya hizo pembejeo kuongezeka, zinazidi kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuulizane kwamba je, hii ni mantiki kwa ajili ya kusaidia Watanzania au kwa ajili ya kuleta migogoro zaidi, kwa sababu hii ndiyo imekuwa ikileta migogoro katika maeneo ambayo tunatoka. Ieleweke wazi kabisa na niwaambie kabisa Watanzania, fedha zote zinazotumika kwenye Miradi ya Maendeleo, iwe ni barabara, iwe ni Miradi ya Maji, iwe ni Miradi ya Kilimo, ni fedha za Wananchi ambazo zinasimamiwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ni fedha za Wananchi na ndiyo maana Deni la Taifa linapoongezeka, tunagawana wote. Kwa hiyo, msiwe mnasema kuwa Miradi yote ni ya CCM kwani ninyi mnafanya biashara gani kule? Hamna biashara yoyote. Mmepewa mamlaka kusimamia fedha za Wananchi, ndiyo maana tunataka mtoe maelezo katika hatua mlizochukua kwenye ufisadi huu ambao unandelea kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hilda Ngoye, ajiandae Mheshimiwa Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia machache kuhusiana na Wizara hii ya Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la upungufu wa chakula. Nchi yetu isingepata upungufu wa chakula hata kidogo, kama mikakati thabiti ingeweza kuwekwa. Tumeelezwa hapa katika Hotuba ya Waziri kwamba, upungufu wa chakula mara nyingi unatokana na ukame na mafuriko na hii ni kweli. Ukame huu unatokea kwa sababu gani au mafuriko yanatokea kwa sababu gani; ni kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi. Sasa mipango au njia za kuondokana na tatizo hili la upungufu wa chakula inaelezwa kwamba hao wakulima walime au wafanye hivi. Suala la ku-*adress* mabadiliko ya tabianchi halioneshwi hapa hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hapa Wizara haifanyi kazi kwa ushirikiano na Wizara nyingine kama Ofisi ya Rais (Mazingira), kuweka na kubaini mikakati na mipango thabiti ya namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili tuweze kupata hali ya hewa iliyo sahihi, siyo mara mafuriko, mara jua kali, mara hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda hivi bila mipango hii, ndugu zangu hatuendi popote. Tunasahau hili jambo lakini ni jambo muhimu sana. Programu za kuhakikisha tunaweka mipango ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, nchi hii hatujaliwekea suala hili kwa uzito unaotakiwa.

Mheshimikwa Mwenyekiti, nashauri vilevile kwamba, Wizara hii ifanye kazi kwa karibu sana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tumekuwa tukizungumza sana hapa kuhusu uundwaji wa Bodi ya Mazao ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Naipongeza Serikali kwa kuanzisha hiyo Bodi, lakini hivi sasa naambiwa haifanyi kazi, muda wake ulikwisha siku nyingi, wanaofanya kazi ni watendaji tu. Kama tuko *serious* na kuhakikisha mazao mchanganyiko ambayo yanalimwa sana na wanawake vijijini yananunuliwa na wanawake na vijana wapate kuondokana na umaskini, mbona mazao yao hayana chombo kinachofanya kazi kila siku ili mazao hayo yaweze kununuliwa? Mimi hapa nina wasiwasi; ninamwomba Waziri ateue Bodi hii ifanye kazi na atakapoteua azingatie pia kuwaweka wanawake wengi ndani ya hiyo Bodi kwa sababu wanawawakilisha wanawake ambao ndiyo wanaolima mazao mchanganyiko kwa wingi vijijini. Kwa hiyo, naomba hili lichukuliwe *serious*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Bodi imepanga kununua au kusindika mazao ya nafaka katika kinu cha Iringa tani 30,000. Hizi hazitoshi, ni tani chache sana. Kama Bodi hii ingewezeshwa, ingeweza kupewa mikopo na kisheria wanaruhusiwa kukopa, wangeweza kukopa, lakini Serikali iwadhamini maana bado ni chombo kidogo hiki kinaji-*mobilize* mpaka sasa. Serikali iwadhamini, iwakopeshe fedha waweze kujenga *silos* nyingine katika maeneo mengine.

Kwa mfano, katika maeneo ambayo ni ya mipakani wangeweza kujenga kule ma-*silo* ambayo baadaye yangeweza kuruhusu kuweka mitandao ambayo itawezesha mazao kununuliwa kwa njia ya mitandao; mtu kutoka Malawi, mtu kutoka Zambia, kutoka South Africa au Zimbabwe, hana haja ya kuja Mbeya. Nafikiri panaweza pakawekwa ghala Songea, lakini anaweza kutumia mtandao. Wao hawana uwezo wa kufanya mambo hayo kwa sababu hawana fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwanza, aiimarishe hii Bodi sasa hivi ianze kufanya kazi. Ilifanya kazi kidogo tu imesimama haiendi maana yake nini!

Mheshimiwa Mweyekiti, vilevile hii Bodi kama ingeweza kusaidiwa ingeweza kujenga *facilities* katika bandari zetu. Huko kwenye *facilities* hizo wangeweza kuweka vitu vya baridi au ma-*freezer* ya baridi ili mazao mabichi nayo yaweze kusafirishwa kwa meli yaende nje. Vitu kama maparachichi, Mkoa wa Mbeya Wilaya ya Rungwe, kwa mfano, wanalima sana maparachichi, hawana soko, wanauza kwa mtu mmoja tu kwa bei ya chini kabisa. Wangeweza kusafirisha haya mazao kwa meli kwenda nje wakitumia hizi *facilities* ambazo ziko katika badari lakini hawana uwezo huo. Hebu tuisaidie hii Bodi, wakulima wanalima sana lakini *return* zake ni ndogo sana, tuwasaidie na njia za kuwasaidia ni kuimarisha vyombo kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Mwatuka, ajiandae Mheshimiwa Athuman Mfutakamba.

**MHE. CLARA DIANA MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kidogo katika bajeti hii.

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kusimama. Hali yangu leo siyo yenyewe, lakini nimekubali kusimama hapa kuvumilia ili nifikishe kilio changu ambacho siku zote huwa nalia, nakipeleka hapa juu ya kilimo lakini hakisikilizwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua utaelewa tu ninaposema hivyo, kazi yangu siku zote nalia na stakabadhi ghalani, lakini sasa niujulishe Ukumbi huu kwamba, Wilaya ya Masasi mwaka huu imekumbwa na njaa kutokana na mafuriko haya ambayo yamezagaa nchi nzima. Mimi mwenyewe ni mwathirika mmojawapo, sina kitu, mashamba yamezolewa na mengine yamefunikwa. Kwa hiyo, ni jukumu la Serikali kuangalia watu wale watainuliwa kivipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya wakazi wa Masasi ni wakulima na wanategemea kilimo kiwakomboe hasa kwa chakula na hata kwa biashara. Mazao yale ya biashara ikiwemo korosho, mbaazi, choroko, hizo ndiyo ambazo zinakwenda sokoni. Cha kusikitisha, mazao haya hayawanufaishi wakulima wale kama walivyokusudia au walivyokuwa wanategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka miaka ya nyuma mazao yalikuwa yananunuliwa na wafanyabiashara ambao walikuwa wanaomba kibali Halmashauri, walikuwa wanatozwa wanalipia ushuru moja kwa moja. Kwa hiyo, Halmashauri haikuwa inakosa ushuru wake na mkulima anapopeleka mazao yake kule ana uhakika kuwa senti anayokwenda kuipata ni yake. Ajabu hivi sasa kumezuka mtindo huu wa Stakabadhi Ghalani, Mfumo ambao Serikali inasema unamnufaisha mkulima; jamani tusidanganyane mkulima hanufaiki na kusema wananufaika na ule Mfumo ni kulazimishwa tu. *(Makofi)*

Hivi inakuwaje mkulima anachangia sana katika Pato la Taifa lakini hajaliwi katika nchi hii? Hakuna cha kukopeshwa na hakuna misaada yoyote; mkulima anahitaji pembejeo, anahitaji trekta akalimie ili kuinua kilimo, lakini hakuna pembejeo. Wakihitaji pembejeo wanachangishwa kwanza kwa kukatwa kwenye mazao matokeo wanakuja kuuziwa tena kwa bei ya juu; sasa ananufaika na nini?

Shamba anatafuta mwenyewe mkulima hasaidiwi na Serikali, kila kitu ni yeye mwenyewe. Akishalifanyia kazi akapata mazao hasa ya biashara, Serikali ndipo inapojiinua na kufanya shamba lile la kwake na siyo la mkulima tena. Bei za mazao yale, zinapangwa na Serikali na wengine wanaopata pesa zile hawahusiki na chochote, hawatoi msaada wa pembejeo zenyewe, zana za kilimo hakuna. Sasa hizi anazonyang'anywa mkulima zinasaidia nini?

Twende kwenye korosho; eti kuna unyaufu unakatwa humo, kuna kusafirisha pesa sijui zinakuwa tani ngapi pesa hizo zinasafirishwa kwa pesa za mkulima! Mnunuzi anapokwenda kununua mazao yake ya biashara, magunia anatafuta mwenyewe na wapi atatunza anajua yeye na wapi atauzia anatafuta mwenyewe; sasa iweje kwa mkulima huyu vyote magunia alipie, unyaufu alipie, kusafirisha pesa alipie na mambo kadha wa kadha?

Jamani mkulima tunamwonea. Kwa nini kusiwe na uhuru, watu waende wakifika kule wakute kuna ushindani, pale unakuta bei ya juu, hapo ya wastani, mtu ambaye ana uchungu na mazao atamtafuta mnunuzi ambaye ananunua kwa bei nzuri, lakini sasa unalazimishwa tu kwamba bei itakayopangwa ni hiyohiyo! Nguvu tunakopa, kama ni kwenye korosho mtu hawezi kulima heka kumi, ishirini na kupalilia mwenyewe, tunakopa nguvu kwa Wananchi wenzetu wenye shida, tunapopata fedha za kwanza tunawalipa na zinazosalia utaona

kuwa ni kidogo. Hivi ni nani kati yetu atakubali mshahara wake alipwe nusu; hakuna hapa tusidanganyane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini mkulima hela yake apate nusu nusu ambayo haimfikishi popote? Nusu ya kwanza inaishia kwenye madeni, nusu ya pili anasema ni majaliwa; kwa nini kama siyo kumdhulumu mkulima? Serikali iangalie sana, badilisheni huo mfumo unamwumiza mkulima; kwa nini mnang'ang'ania mazao ambayo ni yake? Tusimdhulumu, mnamsaidia nini huyu? *(Makofi)*

Ninaomba lieleweke hilo, kilio changu ni hicho, tafuteni masoko ya mbaazi na choroko. Mazao kama mbaazi, choroko na karanga yanalimwa kwa wingi, tafuteni masoko wapate kunufaika siyo kukalia tu kila siku mkulima tutamnyonya kiasi gani haipendezi, mwoneeni huruma. Jamani huku ni kushindwa kazi, kwa sababu kama unajua kuwa mkulima hiyo ndiyo ofisi yake, ofisi yako wewe ni nani anaingilia? Ninaomba liangaliwe sana hili, kwa kweli sikupenda kusema, afya yangu ni mtihani kwa leo, lakini kwa ajili ya hali hiyo na kilio changu juu ya wakulima. Mimi mwenyewe ni mkulima, inaniuma, tutumie mtindo wa zamani watu waende kuuza mazao yao kwenye ushindani, tumechoka kudhulumiwa. Ninashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Ninatumaini Wizara mmesikia kilio hicho. Ninamwita Mheshimiwa Athuman Mfutakamba, ajiandae Mheshimiwa Charles Mwijage.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Kwanza, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa Hotuba nzuri.

Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, alikuja Chabutwa na akazungumza na Wananchi walipokuwa na malalamiko ya malipo yao kuhusu tumbaku msimu uliopita. Vijiji vya Chabutwa, Kigwa, Igalula, Kawekapina, Imalakaseko na Vumilia, bado wanahitaji walipwe malipo yao ya msimu uliopita kwenye Jimbo la Igalula kuhusu suala la la tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nnaipongeza Serikali kufuta *APEX* na pia kuwatoa Viongozi wa Kisiasa katika Uongozi wa Ushirika. Huo ulikuwa ni uamuzi wa busara, uamuzi wa uhakika, utakaomsaidia mkulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya *CAG* kufanya uchunguzi wa zile bilioni kumi na mbili zilizopotea, wahusika wote waliotafuna zile pesa za wakulima, wafikishwe katika vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Goweko Nsololo ninaamini kabisa umefanyika upembuzi yakinifu, usanifu na utafiti kwenye mazingira

*(Environmental Impact Assessment)*. Wananchi wa Goweko na Nsololo wanataka kujua ujenzi unaanza lini? Bwawa hili ni muhimu kwa umwagiliaji, kwa kunywesha mifugo na pia kwa maji ya kunywa na matumizi mengineyo.

Miswaki na Loya; hii ni sehemu katika Mbuga ya Iwembele, ni sehemu ambayo umwagiliaji ni suala muhimu, lakini miundombinu bado iko katika hali ngumu. Mheshimiwa Waziri, hakutaja kama moja ya maeneo muhimu sana, kuna zaidi ya heka elfu mbili pale ambazo zinafaa sana kwa umwagilliaji wa kilimo cha mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu ya *Sero Five,* Benki ya Maendeleo ya Afrika imesaidia nchi za Magharibi mwa Afrika, Uganda na Kenya, basi ninaomba ile *pilot scheme* ya majaribio iletwe Igalula hasa Miswaki na Loya ili tuweze kuboresha uzalishaji wa mpunga. Suala muhimu pia ni ongezeko la thamani, tungeomba ule mpunga ukobolewe palepale Miswaki pamoja na Loya ili tuwe na *Igalula Super Rice,* mchele mzuri kutoka Igalula. Hilo linawezekana, wasije walanguzi tu wananunua mpunga pale na kuondoa fursa na nafasi nzuri ya ajira kwa Wananchi wetu.

Niombe tu suala la uongezaji wa pembejeo, pembejeo tunapata lakini bado kiasi hakitoshi, mahitaji ni makubwa na tunajua umuhimu wa mbegu bora, tunajua umuhimu wa madawa pamoja na mbolea. Pembejeo hizi zitasaidia sana kuongeza uzalishaji. *Sero Five* ni mbegu ya mpunga ambayo inaota kwenye sehemu za juu na inahimili mazingira tofauti. Mbegu hii inatumia maji kidogo, viatilifu na wadudu hawaathiri na pia heka moja utapata maradufu ukilinganisha na mbegu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii, asante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru kwa kuokoa muda. Mheshimiwa Mwijage, ajiandae Mheshimwa Bulaya.

**MHE. CHARLES P. J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Wizara hii muhimu. Awali ya yote, kupitia Wizara ya Kilimo, naishukuru Serikali kwa jinsi mlivyowajali Wananchi wa Muleba Kaskazini katika Kijiji cha Bulembo na Mafumbo pale tulipopata kimbunga. Ninawashukuru sana na nimefaidi hayo mafanikio ya kilimo kwa sababu tumepata chakula cha kutosha. Ombi langu la pili, ninaiomba Serikali pamoja na jitihada zenu sasa elekezeni jitihada za *shift* kubwa ya kuwahamasisha watu wa Mkoa wa Kagera kulima mashamba makubwa na kutumia matrekta. Tunafurahia sehemu nyingine kwa mfano, Kusini wanavyofaidi, sasa umefika wakati wa kuja kwetu.

Niieleze Serikali kwamba, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maliasili na Ardhi, kuna matatizo ya migogoro yanayotokana na ongezeko la Wananchi. Wananchi wakigombania ardhi ya kulima ni wajibu wako Waziri wa Kilimo uwahimize waanze kufanya kazi kwa tija, sehemu ndogo izalishe sana, twende kwenye *high productivity* badala ya kuhamahama tukitafuta mahali pa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo uiambie Serikali na nitakusaidia, hatuwezi kukubali Serikali kuajiri watoto sijui mia nne, sijui elfu moja na mia nne, wakati kuna wanafunzi wamemaliza Vyuo Vya Kilimo na Mifugo tangu mwaka 2012 wako nyumbani. Tuliwapeleka shule wasome na tunawahitaji kwenye maeneo yetu. Wataalamu wote waliosomeshwa tunawahitaji, bado kuna watu wanahitaji. Mnapogawa wataalamu wa ugani katika sehemu zingine za nchi na sehemu zingine mnaacha ziwe nyuma kwa nini? Tunataka wataalamu waajiriwe, kakope muwaajiri vijana tunawahitaji.

Nieleze Serikali, sina shida na Wizara hii, tutagombana sana kwenye Wizara ya Fedha kama Serikali hamtabadilika na kuamuru kuwaajiri vijana wote. Kwanza, wazazi wao wamewasomesha kwa shida, lakini vijana hao wako tayari kwa ari kwenda kuzalisha. Mafaniko ya Wizara ya Kilimo yametokana kwa kuwa na Wagani. Sina zaidi kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Ushirika na Kahawa. Historia ya Ushirika nchi hii unajulikana haukuanzishwa na Serikali, iwe ya Mkoloni, iwe hii ya kwetu. Serikali imeukwamisha Ushirika huu, halina mjadala, ni wajibu sasa ninyi Serikali kuuingilia Ushirika huu muujenge upya na hamuwezi kuepuka, hamuwezi kuwapa uhuru watu ambao mnawapa dhamana. Wanapokwama na kuharibu pesa mmekuwa mkiingilia, muingilie sasa; haitoshi kuja hapa na kusema *COASCO* haifanyi vizuri; kama haifanyi vizuri mbona haujaindoa? Kwa hiyo, muingie kwa nguvu, Ushirika ndiyo nguvu yetu, ndiyo nguvu ya wanyonge hata wakubwa wanahitaji ushirika.

Niende kwenye suala la migomba. Migomba hutoa chakula na migomba ni pesa. Mkoa wa Kagera tuna tatizo la chakula. Mkoa unajitahidi, Mamlaka ya Mkoa na Wilaya wanajitahidi, lakini Mheshimiwa Waziri unajua, nimekuja ofisini kwako, bahati mbaya sikuelewana na wataalamu wako. Kagera hatutaweza kuondoa mnyauko na ninasikia sasa unashuka kuja Kigoma, kwa sababu Kigoma na Kagera ni walewale hawa ni Waha na hawa ni Wahaya, ni herufi ya tu. Ninyi pia ugonjwa wa mnyauko utawaangamiza na migomba yenu ile kinachotakiwa na nimekuwa nikiwaambia; *The Central Government should take the lead role*. Mnapaswa kuwa mstari wa mbele, muwe viongozi, mifano yote, taratibu zote nilizowaekeleza mje msaidie Mamalaka za Wilaya na Mkoa, muwaletee chakula wale watu walioathirika, mfyeke migomba yote, mfanye operesheni kwa miezi mitatu, waghani wenu

washuke chini wawaelekeze Wananchi kupanda mazao ya muda. Operesheni hii ikifanyika, tutaweza kufanikiwa. Zipo nchi sitaki kuzitolea mfano nitachekwa, zimejifunza kwetu, zimekwenda kwao zimetekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muwaambie Mawaziri hawa, wawaambie wataalamu wao watekeleze hayo. Kama hawataki turudi Bungeni tutengeneze mfumo mpya wa hawa wataalamu kufanya kazi. Lazima mtu unayekuja kufyeka migomba yake umwambie atakula nini, *otherwise,* atatetemeka na migomba yake ambayo haiwezi kuleta tija. Sisi kwetu tunategemea ndizi, lakini tukipata ndizi tukauza ndizi tutaongeza pato. Lengo la Serikali, lengo la Ilani ya Chama changu, litatimizwa kwa sababu tutaweza kuleta kipato na kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Nizungumzie suala la wataalamu. Tunahitaji wataalamu zaidi, lakini kitendo cha kutowapatia ajira watoto waliosomeshwa kwa shida kwa miaka miwili, mitatu, mine, kinawafanya wazazi wakate tama. Suala hilo ninaomba mlifuatilie sana na baada ya hapo tutaweza kwenda kwa kasi inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilidokeza mwanzoni, sisi tumekuwa ni watazamaji, kwetu tuna mabonde mazuri lakini hatuwezi kuyalima mpaka tupate msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana ninakushukuru. Mheshimiwa Esther Bulaya, ajiandae Mheshimiwa Shibuda na Mheshimiwa Lugola.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Kilimo. Ninaamini vijana sasa hivi wameamka wanasema Kilimo na Vijana, Kilimo ni Ajira. Nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kushughulikia matatizo ambayo yalijitokeza katika Mkoa wa Morogoro hasa Wilaya ya Kilombero, baada ya mafuriko na kwenda kutembelea na kuwapa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kwamba. Sera ya Chama Changu siyo kufumbia macho ubadhirifu wowote katika Sekta ya Kilimo. Sera ya Chama changu siyo kufumbia macho ufisadi wa watendaji ambao wanafanya makusudi katika kukwamisha jitihada za Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Azza amezungumzia ubadhirifu wa shilingi milioni mia mbili, lakini katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia tani ishirini na saba za mbolea feki. Sera ya Chama changu cha Mapinduzi ni kuhakikisha wakulima wanapata mbolea. Suala la mbolea feki hatuwezi kuwa tunalizungumzia kila mwaka katika Bunge letu Tukufu. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri, simamia

vyema Ilani ya Chama cha Mapinduzi, simamia vyema watendaji wanaohujumu utekelezaji huu. Haiwezekani, tani ishirini na saba ni nyingi; ni wakulima wangapi wamedhulika waliotumia mbolea hizo feki? Kwa hiyo, ninakuomba sana Mheshimiwa Chiza, ninakuheshimu sana, hawa watu waliohusika na huu usambazaji wa mbolea feki wachukuliwe hatua. *(Makofi)*

Tunajua Umoja wa Nchi za *SADC* zimeazimia kuhakikisha asilimia kumi ya bajeti ya nchi inakwenda katika Wizara ya Kilimo. Asilimia kumi katika bajeti yetu ya mwaka huu ambayo ni trilioni kumi na tisa, ni trilioni 1.9. Leo hii Wizara ya Kilimo inaomba bilioni mia tatu, hata robo haijafika. Nimemsikiliza Mwenyekiti wa Kamati, amezungumzia kushuka kwa kilimo, lakini katika makubaliano hayo kwamba, kilimo kila mwaka kipande kwa asilimia sita. Sasa ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atupe mikakati madhubuti ya Serikali kuhakikisha tunatimiza malengo haya ambayo na sisi ni miongoni mwa nchi za *SADC,* lakini maazimio haya nchi zote zinajua umuhimu wa Sekta ya Kilimo katika kuchangia Pato la Taifa na katika kuogeza ajira.

Mimi hapa ndipo nina shida napo, tunajua asilimia 61 ya Watanzania ni vijana na kati ya watu ambao wanapata matatizo makubwa na wanaathirika na suala la ajira ni vijana. Vijana *graduates* ambao wamemaliza elimu ya juu, wamechoka kutembea na vyeti kutafuata kazi, wameamua ku-*invest* katika Sekta ya Kilimo. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali yangu sikivu, mtenge bajeti ya kutosha kuhakikisha dhamira hii inatekelezwa.

Nimeona mwaka jana mlitenga biloni tatu katika kutoa mikopo ya pembejeo na kilimo cha umwagiliaji. Mwaka huu mmetenga shilingi bilioni sita, lakini kama mngetimiza azimio lile kungekuwa na fedha zaidi kuliko hizi zilizokuwepo. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali, vijana wameamua ku-*invest* kwenye Sekta ya Kilimo, ninaomba fedha za kutosha zitengwe.

Leo hii tunasema tatizo kubwa la ajira liko mijini, vijijini ni asilimia tano; ni asilimia tano kwa sababu walioko kule vijijini wanakimbilia mijini. Walioko kule vijijini wengi wanalima kilimo cha kubangaiza na kupewa mashamba ya baba, mama, mjomba, shangazi, hawana maeneo. Pia ningependa unijibu Mheshimiwa Waziri utekelezaji wa azimio ambalo tulilipitisha katika Bunge hili Tukufu, limefikia wapi kuhakikisha vijana wanatengewa maeneo ya kilimo na kupewa fedha za kutosha ili waweze kujikwamua na tatizo la ajira nchini.

Pili, uliniahidi kwenda kuwatembelea vijana wa Kalukekere kule Wilaya ya Bunda kwenye Jimbo la Mheshimiwa Kangi, kwenda kuwatembelea vijana kule Mgeta ambao wanalima mpunga. Vilevile kwenda kuhakikisha vijana wa Mkoa wa Mara wananufaika na mpango huu na wa Tanzania nzima. Ninaomba unijibu ombi hilo limefikia wapi? Uliniahidi bajeti ya mwaka jana, lakini kimya

hujafika Bunda wala sijakuona ukienda katika Mkoa wa Mara kuhakikisha vijana wanahamasika. *(Makofi)*

Wilaya ya Igunga wamehamasika na baadhi ya maeneo mengine. Tengeni fedha za kutosha, vijana wajiajiri kupitia Sekta ya Kilimo, kwa sababu ajira ni Kilimo, Kilimo na Vijana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba sana hilo. Sitaki kuongelea hapa matatizo mengine. Mimi natoka Kanda ya Ziwa, kilio cha Wakulima wa Pamba mnakijua, kila siku tunaimba, Mheshimiwa Ndassa ametoka kulizungumzia suala hili. Naomba Mheshimiwa Waziri pia suala hili ulishughulikie, Wakulima wa Pamba wamechoka kutoa malalamiko yale yale, kupata majibu yale yale na mwisho wa siku hawanufaiki na kilimo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Shibuda, ajiandae Mheshimiwa Lugola na Mheshimiwa Machali.

**MHE. JOHN P. M. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii. Awali ya yote, naomba kusema ya kwamba, Sekta ya Pamba katika nchi yetu imejaa ushupavu wa kusengenyana kati ya Watumishi wa Serikali dhidi ya Wanasiasa na Wabunge ambao ndiyo wasikivu kwa masilahi ya Wakulima ambao wanadhulumika, hawama masikio sikivu ya Wakuu wa Mikoa.

Naomba ieleweke ya kwamba, Sekta ya Pamba ina fikra mgogoro. Kwa hiyo, namwomba Waziri wa Kilimo, ashauriane na Waziri Mkuu, ni lini watakuja katika Sekta ya Pamba waweze kukutana na Wakulima, wasikie vilio vya Wakulima wa Pamba peke yao, waweze kuelewa kwamba Wakulima wa Pamba wanataka kujitegemea siyo kuwa manamba na vilevile waelewe athari ya kilimo cha Maktaba.

Vilevile namwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe safari hii msimu wa Pamba unafunguliwa mapema na bei ya Pamba itambulike mapema. Sasa hivi Wakulima muelewe kwamba, wana chuki za kuzuiwa na wanunuzi wa Pamba ambao kazi yao kila siku ni kuwadhulumu Wakulima wa Pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri Mkuu atahadhari kuamini vyeo vya Wakuu wa Mikoa kwamba ni utakaso na uaminifu. Wakuu wa Mikoa hao hao ndiyo waliompeleka kwenye Kampuni ya *Quton* wakamdanganya, zimeoteshwa mbegu mbovu wakaamini ya kwamba, mbegu za manyoya hazioti. Napenda kuthibitisha kwamba mbegu za manyoya zinaota na kwa taarifa ya bodi ya Pamba mavuno kwa *kilogram* kwa hekari moja 1,425 yalitokea, Geita, Meatu, 1200. Kwa hiyo, kwa Wakulima wanaofuata *study* za Kilimo wanapata zaidi ya kilogram 1000 katika hekari moja.

Sasa mbegu ya *quton* manyoya yake ni dhuluma na udhalimu mkubwa na ninashangaa kwa nini zinapigiwa debe na Wakuu wa Mikoa! Hivi Wakuu wa Mikoa waliajiriwa na nani? Kwa nini Waziri Mkuu amekaa kimya mpaka Wananchi wanaanza kuhisi labda kuna *percent,* kuna shurti za dhuluma, za rushwa, ambazo zinapenyezwa hadi Wakuu Mikoa na *DCs* wamekuwa Maafisa masoko katika Kampuni ya *Quton.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Pamba imejaa hivi sasa Mpango ambao hauna dira hata kidogo. Naomba Mheshimiwa Waziri utuambie leo, hivi Sera ya Pamba pamoja na kuwa na Sheria, ina sera gani ya kuendeleza ustawi na maendeleo ya Pamba? Vilevile napenda kuelewa Mheshimiwa Waziri utuambie mfadhili wa *TGT* amesaidia nini kutiririsha pesa zake bilioni 20 kwenda kwa Wakulima? Amesaidia nini na zinafanya nini na kwa nini yeye anahangaika na Wakuu wa Mikoa hataki kukutana na Wakulima?

Ninaomba Balozi wa Uingereza atuambie misaada iliyoletwa kutitririsha kupambana na umaskini wa Wakulima wa Pamba, inasaidia vipi na imetumika wapi kuliko kila siku panafanyika semina. Je, kuna siri gani ya kubaguliwa Zao la Pamba katika masuala ya Ruzuku?

Mheshiwa Waziri, tuambie kwa nini Rais alipokuja kwenye ziara alisema anashangaa pesa ya ruzuku haijatolewa? Kwa nini Zao la Pamba halipewi ruzuku wakati mazao mengine yanapewa? Naomba maelezo na utoe huku. Vilevile Mheshimiwa Waziri, kwa nini Bodi ya Pamba na Wizara mmekaa kimya Wakulima wanataka *passbook* ili wapate mfumo wa kujitegemea lakini leo miaka mitatu Bodi ya Pamba hawataki? Naomba Mheshimiwa Waziri utueleze.

Bodi ya Pamba ni laana, ni nuksi na ni giza kwa ustawi na maendeleo ya Pamba. Mheshimiwa Waziri, naomba Bodi ya Pamba ambayo ni laana uhakikishe inarejeshewa uwezo wake. Naomba vilevile Bodi ya Pamba itambue kwamba, mbegu ya manyoya ambayo walikuwa hawataki itumike wewe ukairuhusu ikazuiwa na Wakuu wa Mikoa, imeleta hasara kwa Wakulima wa Pamba. Sasa Wakuu wa Mikoa waliokuwa pingamizi na mimi ni shahidi; ulimkuta Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, alikuwa jeuri na Mkuu wa Mkoa wa Geita na Wakuu wa Wilaya; je, hasara hiyo ni nani atatoa fidia?

Leo ninapenda kukwambia Mwenyekiti, ambaye pia ni Mjumbe wa *NEC* na Waziri Mjumbe wa *NEC,* hiyo, mmeshazalisha hasira na adhabu yake, kama hamtoa fidia, CCM itanyimwa kura na Wakulima wa Pamba. Tambua ya kwamba, Mkulima amekatwa pesa nyingi sana ambazo zinaitwa eti ni Mradi wa *Contract Farming*.

Mheshimiwa Waziri, hebu taja hapa *Contract Farming* mtaji wake ni nini na ni shilingi ngapi? Wanalazimisha wakulima fedha walizokatwa katika bei yao ya pamba waambiwe ndiyo Mradi wa *Contract Farming;* kwa nini unakaa

kimya dhidi ya udhalimu huu ambao unasukumwa na Wakuu wa Mikoa; maana yake ni nini?

Jina la Rais Kikwete linatumika hovyo hovyo; kwamba, eti yeye ndiye kamleta Mfadhili huyo, kwa hiyo, awe ni mtaji wa umanamba kwa Wakulima wa Pamba, hapana! TANU iliwakomboa na hawataki.

*Victoria Federation* ilivunjwa kwa sababu ya dhuluma na leo mnataka Wakulima wa Pamba wawe tena manamba, haiwezekani! Kama mnataka *Contract Farming,* tunaomba walipwe nguvu kazi wanazotumia kulima, kupalilia, kuvuna, wasiambiwe kwamba, hiyo ni sadaka kwa wanunuzi. Wakulima wa Pamba siyo utajirisho kwa wafanyabiashara. Ninaomba fedha ambazo zimetolewa na Uingereza pamoja na huyu Mfadhili zitambulike, msiwe watu wa kuwanyima haki ambazo zimetolewa na wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika sana kuona uzalishaji wa *Contract Farming* unadidimiza Zao la Pamba, ninaomba *passbook* irejeshwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninashukuru sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Lugola, ajiandae Mheshimiwa Machali.

**MHE. ALIPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwanza, ninaomba niwape pole Wakulima wa Pamba 100 ambao nilikuwa ninawasafirisha kutoka Mwibara kuja hapa Bungeni, ambao ni waathirika wa mbegu aina ya *Quton* ambayo haikuota. Walikuwa wanakuja kushirikiana na Mbunge wao kumzomea Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, endapo katika Hotuba yake asingeonesha namna Wakulima hawa watakavyofidiwa na kwa kweli hakuonesha katika Hotuba yake kwamba watafidiwa na hivyo angeweza kuzomewa na wahanga hawa 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje Wakulima wanapelekewa pembejeo feki Waziri bado ni Waziri? Wakulima wanapelekewa madawa feki bado ni Waziri? Skimu za Umwagiliaji zinachakachuliwa bado ni Waziri? Waziri huyu huyu ndiye aliyezindua mbegu za *Quton* ambayo haioti bado ni Waziri! Waziri huyuhuyu analipa ruzuku mbegu ya Pamba isiyoota bado ni Waziri! Hainiingii akilini, kama Mchina tu Kilombero anajenga daraja lisilo na viwango kwa kuhofia kwenda China angeweza kupigwa risasi akaamua kujiua! Simshauri Waziri huyu ajiue, lakini kwa vitendo vyote hivi Waziri huyu angekuwa ameacha Wizara hii na kupumzika na kufanya kazi nyingine mbadala. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema hivi? Wizara ya Kilimo ndiyo yenye ajira kwa Watanzania kuliko Wizara nyingine yoyote. Waziri huyu pamoja na kwamba, alikuwa akiitwa Waziri mzigo kwa Wakulima, pamoja na kwamba

jina hili aliliona lina ukakasi, mimi ninakishauri Chama cha Mapinduzi, ambacho kinasimamia Ilani ya CCM na amesema Mheshimiwa Shibuda hapa, Wizara hii itakigharimu Chama cha Mapinduzi, endapo hali hii itaachwa bila kudhibitiwa. Ukiangalia Hotuba ya mwaka jana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, alisema kabisa ukurasa wa 45 kwamba, Serikali ipo kwenye mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Kinga ya Bei ya Pamba ili kuwasaidia Wakulima.

Kwenye Hotuba iliyopita ya Waziri Mkuu, hakuna mahali ambapo amezungumzia Mfuko huu na nilitarajia pengine nitaikuta kwenye Hotuba ya Waziri wa Kilimo nako hakuna. Hivi nchi tutaiendesha kwa usanii mpaka lini? Usanii juu ya usanii, hatuwezi kuwadanganya Wananchi kwa kiwango hiki. Sasa leo humu hakuna huo Mfuko wa Kinga ya Bei ya Wakulima. Itakuwaje mimi Mbunge wa Mwibara nikuunge mkono kwenye bajeti ya kisanii namna hii? Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwibara tumekuwa na njaa ya kila mwaka, kila mwaka Mwibara ni njaa ya chakula.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mwache amalize muda wa dakika saba ni mdogo sana.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, thamini kazi Mheshimiwa!

**MHE. ALIPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni njaa kila mwaka, matokeo yake tunaletewa chakula, Kaya moja inapewa kilo nne. Hivi hata huyu Waziri nyumbani kwake kilo nne anaweza kula yeye na familia yake kwa siku ngapi?

Tuna mabonde kule Kalukekere, Kata ya Namhura, Iramba kule Mwiruruma, Igundu na Nsimo, lakini mpaka leo tunasema tupewe skimu za umwagiliaji tuondekane na balaa la njaa ya chakula, Serikali ya Chama cha Mapinduzi haitaki kutusikia.

Juzi juzi hapa ile Skimu na Nansimo, nilisema hapa Bungeni kuwa imechakachuliwa haipo. Nikasema kwamba, Serikali imesema uongo, nilisulubiwa hapa kuwa neno uongo niliondoe!

Sasa katika mazingira haya ya kudanganyana, kwa nini tusiseme kwamba tunadanganywa? Wananchi kule Mwibara, Mbunge wao mimi nitakuwa mgeni wa nani; wanapelekewa vibaba vya mahindi!

Mheshimiwa Zambi, nilikwambia utakapokuja na bajeti yako uniambie 20% ya malipo ya Wakulima ambao waliahidiwa kwamba wakitumia mbegu ya *Quton* walipwe 20% kama sehemu ya malipo, lakini humu ndani kwenye bajeti yako hakuna lolote ni blabla tu!

Mheshimiwa Zambi wewe ulikuwa *backbencher* hapa kama mimi, ulikuwa unapiga muziki kama kasuku juu ya Wizara hii, leo unashirikiana na Waziri wako, unakuja na vitu ambavyo havina majibu juu ya matatizo ya Wakulima maana yake ni nini? *(Kicheko)*

Siwezi kukubaliana na Hotuba za kila wakati ni maneno yale yale, lugha zilezile, tutawaambia nini wakulima hawa? Wakulima wa Pamba wamekuwa wa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lugola kengele ya pili hiyo, ninakushukuru sana. Mheshimiwa Joseph Machali, ajiandae Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa fursa na mimi nichangie Hotuba ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kuwapongeza Wabunge wanaotokana na Chama cha Mapinduzi, ambao wanasema Serikali inaendesha mambo yake kwa usanii mkubwa. Ninaposema usanii, wasanii huwa wanaigiza, haina maana kwamba usanii siyo kazi, ninaomba nieleweke hivyo na iwe kwenye rekodi, ninaheshimu sana kazi za wasanii.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Kangi amerejea kuwa Serikali huwa inawadanganya watu katika kutatua matatizo, ndiyo maana tunaona kama ni Serikali ya maigizo katika baadhi ya mambo ambayo wanapaswa kuwa *serious.* Mambo haya hayakubaliki.

Ukisoma Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ukurasa wa 72, anasema kwamba, Tanzania ina eneo la hekta 144,000,000 zinazofaa kwa kilimo.

Ninaomba niseme kwamba, ardhi tunayo, hakuna asiyejua kuwa Tanzania ina ardhi kwa ajili ya kilimo. Maajabu ya Serikali ya Tanzania ni kwamba, ndiyo ambayo imekuwa kwa sehemu kubwa inawa-*discourage* na kuwa *disappoint* Wakulima wa nchi yetu, ambao wameamua kutumia nguvu

zao kuingia kwenye mapori mbalimbali kwa lengo la kuendesha shughuli za kilimo kisha inaenda kuwaondoa na kuwanyanyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kigoma, naye leo hii ametambua kuwa eneo lile la Kagerankanda ambalo Serikali imekuwa ikisema kuwa ni eneo la Hifadhi, kwamba, sasa Serikali ichukue hatua za makusudi kwa kuhakikisha Wakulima wale wanaendelea kulima katika maeneo yale. Mwanzoni walikuwa wanapinga, ninawapongeza kwa sababu imefika mahali wanauelewa ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la ajabu sana kuendelea kusema kwamba, eneo ambalo lilitambuliwa na Serikali ya Kikoloni mwaka 1955 ni Hifadhi. Wakati huo idadi ya watu ilikuwa ni takribani kwenye laki moja na kidogo, leo ukizungumzia *population* ya iliyokuwa Wilaya ya Kasulu pamoja na Wilaya nyingine ni takribani watu milioni moja.

Haiwezekani maeneo ambayo yalikuwa ni Hifadhi toka mwaka 1955 kabla ya Uhuru wa Tanganyika, bado Serikali imeendelea kuyatambua kuwa ni Hifadhi, wakati Wananchi hawa kwa zaidi ya miaka hamsini sasa wameingia kule wakawa wanaendesha shughuli za kilimo. Tunajiuliza swali moja na nimekuwa nikiiuliza Serikali siku zote; Maafisa wa Maliasili na Maafisa wa Kilimo ambao wapo tangu Serikali hii imekuwepo kwenye Halmashauri zetu walikuwa wapi kuwazuia watu wale wasiingie kwenye eneo hilo linaloitwa Kagerankanda? Kwa nini hawakuwazuia kwa zaidi ya miaka hamsini watu wamekuwa wakilima kule?

Ninaomba niendelee kupata ufafanuzi; tatizo ambalo liliwakuta Wakulima wa Wilaya ya Kasulu ambao mwaka jana walifyekewa mazao yao Serikali itawa-*compensate* kitu gani?

Maamuzi hayo yamekuwa yanafanywa na Viongozi na watu ambao wamepewa Uongozi, lakini hawakustahili kuwa Viongozi. Ninaomba niseme kuwa, tuna Mkuu mmoja wa Wilaya wa ajabu ambaye nimekuwa nikipiga kelele siku zote, Bwana Dani Makanga, aliyeongoza operesheni ya kwenda kufyeka mazao ya wakulima, wakati huo huo mnasema KILIMO KWANZA. Watu wametumia nguvu zao kwa ajili ya kwenda kulima halafu mnakwenda kuwafyekea mazao, mnakwenda kuwapiga na mgambo pamoja na askari polisi, mnawakamata mnawafunga; sasa mnataka waache kulima waingie mtaani waanze kupiga roba?

Ndicho mnachokitaka CCM? Matatizo gani haya? Serikali gani? Tunaposema Serikali ina Viongozi baadhi wamechoka mnasema tunawatukana; kama Mkuu wa Wilaya huyu hajachoka? Nini maana yake?

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana. Mheshimiwa Subira Mgalu, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye Bajeti hii ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Kipekee, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa namna ambavyo amenijalia leo kusimama ndani ya Bunge hili. Nichukue fursa hii kutoa pole kwa Wananchi waliokumbwa na mafuriko katika maeneo mbalimbali ya nchi hususan maeneo ya Mkoa wa Pwani, Bagamoyo, Rufiji, Kibaha pamoja na maeneo ya Wilaya ya Mafia.

Nianze kwa kusema ninaunga mkono hoja na kupongeza kazi mbalimbali zilizotekelezwa katika Wizara hii, licha ya ufinyu wa bajeti na mtiririko wa fedha kutoka Hazina. Ninayo faraja ninapochangia katika Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo, nikitambua mchango wa Sekta ya Kilimo katika kutoa ajira asilimia 74, katika kuchangia upatikanaji wa chakula asilimia 100 na pia kuwa kuwa ni sekta ya pili katika kuchangia Pato la Taifa kwa kiwango cha asilimia 24.8, pamoja na kwamba kiwango hiki kinashuka.

Pamoja na faraja hiyo, nieleze masikitiko yangu kwa namna ambavyo bajeti inavyotengwa kwa ajili ya sekta hii na kupungua mara kwa mara na hatimaye mwaka wa fedha huu tunaoujadili kuwa asilimia tano ya bajeti yote. Licha ya hilo, mtiririko wa fedha katika Wizara hii mpaka tarehe 31 Machi ni asilimia 63 tu, lakini kwenye fedha za maendeleo ambako tunatekeleza Mpango huu wa *BRN* ni kiasi cha asilimia 50 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Bunge lako Tukufu kwa namna ambavyo Kamati yetu iliwasilisha maoni kupitia Mwenyekiti wetu, kutukubalia maombi ya nyongeza ya bilioni thelathini. Fedha hizi zitaweza kuisaidia Wizara hii itekeleze Miradi mbalimbali iliyokuwa chini ya Mpango wa *Big Results Now,* ambao kwa kweli una lengo la kusaidia upatikanaji wa mapato kupitia mazao ambayo yatazalishwa ya sukari, mahindi na mchele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Mpango huu wa *Big Results Now,* matokeo tunatarajia kuyapima 2015/2016. Huu ni mwaka wa kwanza ambao tumeanza kutekeleza, lakini nieleze masikitiko kwamba, mpaka mwaka huu unakaribia kumalizika, ni kiasi cha shilingi bilioni kumi tu ambazo ziliwasilishwa katika Wizara hii kutekeleza Miradi hiyo ukilinganisha na Wizara nyingine; kwa mfano, Uchukuzi, zaidi ya shilingi bilioni mia moja na hamsini, Wizara ya Nishati zaidi ya bilioni mia mbili na hamsini, Wizara ya Miundombinu zaidi ya bilioni mia tatu na hamsini na saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali za kutengeneza miundombinu, lakini ni wazi miundombinu hiyo inategemewa kutumika na

wakulima. Hatuwezi kuendelea kujenga zaidi barabara, uchukuzi na kadhalika, lakini kama kilimo kitatengewa bajeti ndogo kama ilivyo sasa, ninaamini hata tija ya uwekezaji mkubwa katika mazingira hayo inaweza isipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalisema hilo kwa sababu mipango yote ambayo ilipangwa katika *Big Results Now*, ukarabati wa maghala 275 hakuna ghala ambalo mpaka sasa hivi limekarabatiwa, uendelezaji wa mashamba 25 yanayotarajiwa kuzalisha mahindi na mpunga, kwa kweli bado hamna hata moja ambalo limeshaanza kazi. Kwa hiyo, nina wasiwasi itakapofika mwaka 2015/2016 inawezekana tukashindwa kupima mafanikio katika Mpango huu ambao tunaendelea kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee pia katika utaratibu wa utoaji wa pembejeo, ulikuwepo utaratibu wa vocha lakini Serikali sasa inajipanga kupitia kukopesha kwenye Vyama vya Msingi, *SACCOS* na kadhalika. Ninaiomba Serikali katika hili ambalo mwaka huu wa fedha wametenga shilingi bilioni 96, kama kweli nia ni hiyo ya kubadilisha mfumo ili kuboresha upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima, pesa hizi zitoke mapema zipelekwe kwenye mabenki ili waweze kukopesha kwa haraka kabla msimu haujaanza. Hii ni kwa sababu taratibu za mkopo zinachukua muda, ni wazi hizi pesa kama hazitapelekwa mapema mwaka wa fedha unapoanza, inawezekana kabisa tusiweze kutimiza lengo ambalo limekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nijielekeze kwenye mashamba ambayo yalibinafsishwa, mashamba ambayo yalipewa wawekezaji mbalimbali hususan katika Wilaya ya Muheza, yaliyokuwa mashamba ya Mkonge. Ninaiomba Serikali mashamba yale ambayo zaidi ya miaka kumi hayajafanya kazi yoyote na sheria ipo ya kwamba kama hujatumia shamba zaidi ya miaka mitatu mfululizo, Sheria ya Ardhi inaruhusu uhalalishaji wa ile ardhi kwa matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itafakari maombi haya hasa Mashamba ya Bwembwera, Songa, Kumburu, maeneo ya Kitisa na Lewa. Kwa kuwa Halmashauri yetu ya Muheza imepata Hati Safi kwenye Miradi hii ya Kilimo, uwezo tunao na nguvu tunayo ya kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninashukuru Mradi wa Bwawa na Misozo uliokamilika. Ninaiomba Serikali imalizie pesa za mfereji uliobaki ili tuweze kulitumia. Naliomba pia Bunge lako Tukufu likubali nyongeza tuliyoomba kwa Miradi ya Umwagiliaji ambayo ilitengenezwa haijakamilika kutokana na Mradi wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo kuisha muda wake. Kiasi kinachotakiwa ni shilingi bilioni 49. Kwa kuwa Miradi ile ilianza kutengenezwa na haijakamilika, haijaanza kufanya kazi, ni wazi tija yake au *value for money* ya pesa ambazo zimetumika kwenye uwekezaji huo inaweza isionekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nashukuru kwa Mradi wa Kambi ya Vijana Mkongo. Lazima niseme vijana wale walikaa wiki mbili tu chakula kikaisha mpaka sasa hivi hawapo. Wizara waangalie na Rais ndiye aliyeizindua ile Kambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo pia naomba nijielekeze kuomba ongezeko la pesa katika Mfuko wa Taifa wa Pembejeo na ikizingatia utaratibu wa awali wa kukopesha pembejeo hizi kupitia SUMA JKT. Sasa hivi inakuja awamu nyingine ambayo haijakamilika, kwa hiyo, nina imani pesa zikiongezeka kwenye Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, ni wazi wakulima wengi watanufaika.

Mwisho kabisa, kwenye Bodi za Mazao, naiomba Serikali katika ongezeko tunaloomba Kamati yetu, tuitazame kwa makini Bodi ya Tumbaku kwa kuwa Zao la Tumbaku linachangia kwa kiwango kikubwa pesa kwa ajili ya Pato letu la Taifa. Naomba nyongeza tuliyoomba ikubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Dkt. Nkya na Mheshimiwa Sakaya ajiandae.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwepo hapa nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kutoa pole kwa Watanzania wote waliokumbwa na mafuriko katika kipindi cha mvua cha mwaka huu, wakiwemo Wananchi wangu wa Kijiji cha Kidunda, Kata ya Selembala na Kata ya Magogoni kule Morogoro Vijijini. Maeneo haya ya Morogoro Vijijini yamefunikwa na mafuriko yaliyotokea Kilosa. Kwa hiyo, hawa Wananchi mpaka sasa hivi hawana chakula na hatuwezi kuwafikia. Kwa hiyo, naomba Taifa lijue kwamba, tunahitaji kuangalia kwa jicho la pekee Morogoro Vijijini katika Bonde ambalo patajengwa Bwawa la Kidunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake, kwa Hotuba nzuri. Niwape pole sana kwa kupewa nyenzo chache sana za kufanyia kazi, yaani fedha kwa ajili ya Miradi ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu tunaposema kilimo ni Sekta Kiongozi, lakini inapokuja kwenye kupewa *resource* za kufanya kazi inakuwa ya tano

mpaka ya kumi. Nilitarajia kwenye Mpango wa *BRN* kilimo ingekuwa ndiyo sekta ya kwanza kupewa pesa nyingi, lakini imekuwa kinyume chake. Sasa huyu Waziri atafanyeje kazi mpaka analaumiwa na watu kwamba hafanyi kazi? Hawezi kwenda kutafuta hela za mke wake na watoto kuja kufanya kazi. Kamati yetu imeiomba Serikali iongeze pesa kwenye Wizara hii, naomba hilo lionekane na waongezewe pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hilo ongezeko la pesa lisiwe ni la kisiasa hapa ndani ya Bunge kama ilivyofanyika mwaka jana. Waongezewe pesa kweli na hizo pesa wapewe wafanyie kazi ambazo watakuwa wamepanga kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, naomba nizungumzie juu ya Shamba Na. 217, ambalo lipo Kata ya Mkulazi. Ninaliona lipo kwenye mpango wa *BRN* kwenye kubinafsishwa kupewa mwekezaji atakayelima miwa na watakaolima mpunga. Lile Shamba lilikuwa na mwekezaji, kulikuwa na Watanzania walikuwa wanafanya kazi wakati wa ukoloni, kwa bahati mbaya walikuwa wanawaita manamba, watu ambao walikuwa nyumbani kwao. Baada ya yule mwekezaji kuondoka, Wananchi wlaiokuwa pembezoni pamoja na wale wafanyakazi, wame-*settle* ndani ya lile Shamba kwa sababu hawakuwa na mahali pa kwenda, wameanzisha vijiji. Kijiji kimojawapo kinaitwa Usungura.

Serikali ilipoona wanahitaji kutumia hilo Shamba kwenye Mpango wa *BRN*, lingekuwa ni jambo la busara kushirikisha Wananchi kwenye Kata, kwenye Vijiji pamoja na Viongozi wao ili tukubaliane kwamba, tunaachia shamba kiasi gani liende kwa mwekezaji kwa sababu na vijana wetu wanataka vibarua pia, lakini basi na Wananchi wapate mahali pa kulima wapate chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahamisha Wananchi kutoka kwenye Kijiji cha Kidunda wapishe ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Wale Wananchi watalipwa, lakini watakapolipwa sasa wanakwenda wapi? Wataanza kudhalilika tena kuzunguka kama wafugaji kutafuta eneo. Ninaomba Serikali ikubaliane na mimi kwamba, barua niliyoiandika Wizara ya Ardhi, kuomba ekari zisizopungua mia nne kwa ajili ya Wananchi hawa ambao wanapisha eneo la kuweka bwawa, ili Wananchi wa Dar es Salaam na Pwani wapate maji, tuliangalie hilo, ni uzalendo wa hali ya juu, waweze kupata mashamba walime, kwa sababu wanahitaji kula na wanahitaji kuwa na nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu skimu za umwagiliaji. Naishukuru sana Serikali imetujengea skimu za umwagiliaji Morogoro Vijijini; kuna Skimu ya Mbarangwe inafanya kazi tu wakati mto una maji. Niliomba wajengewe bwawa ambalo litahifadhi maji ili ile Skimu iweze kutumika mwaka mzima. Nashukuru wamesema watafanya hilo na kweli

ifanyike. Pia kuna Skimu ya Kiroka, Skimu ya Maturi ambako sasa hivi maji yamefurika, Mto Ngerengere ume...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Nkya. Sasa ninamwita Mheshimiwa Sakaya, atafuata Mheshimiwa Kidawa na Mheshimiwa Soni ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mweyekiti, nakushukuru nami kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo kwenye Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli Serikali iliyopo madarakani haina nia ya dhati kuinua kilimo hapa Tanzania. Ni jambo la ajabu, kuna mipango mizuri sana kwenye vitabu na kila mwaka mnakuja na mipango mizuri, Waziri amekuja na mipango mizuri, lakini utekelezaji hakuna kwa sababu pesa haitolewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo pesa ya kufanya Maadhimisho ya mabilioni ya Muungano kwa ajili ya sherehe watu wafurahi, lakini fedha kwenda kwenye Miradi ya Maendeleo ya Kilimo wakulima wanyanyuke hakuna pesa, hilo ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la ajabu, Sekta ya Kilimo inakua taratibu sana. Sekta inayoajiri zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania inakua kwa asilimia 4.3 mpaka 4.7 kwa miaka yote. Ukiangalia hata kwenye mchango wa Taifa, Sekta ya Kilimo inazidi kushuka; mwaka 2012 kilichangia asilimia 24.8, mwaka 2013 kimechangia asilimia 24.7, badala ya kupanda inashuka wakati Watanzania wanaongezeka, mahitaji yanaongezeka na shughuli zinazidi kuongezeka; hilo ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Serikali iangalie ni namna gani ya kunyanyua Sekta ya Kilimo. Ninaungana na Wabunge wenzangu wa Kamati, pesa tuliyoomba Kamati iongezwe kwenye Sekta ya Kilimo ili miradi ikatekelezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye utaratibu wa pembejeo; mwaka jana Serikali imekuja hapa na utaratibu mzuri kabisa. Baada ya kuona changamoto za utaratibu uliokuwepo wa pembejeo, vocha zinaibiwa, wizi, ubadhirifu na ucheleweshaji wa mbolea, wamekuja na utaratibu mpya wa kuonesha kwamba tunatumia mabenki na Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliwamahasisha Wananchi waunde Vikundi, *SACCOS* zikawepo, Serikali ilitakiwa itoe dhamana ya asilimia hamsini benki ya mahitaji ya pembejeo na wakulima watoe asilimia ishirini benki, mahitaji ya pembejeo ili wakulima wale waweze kukopesheka. Matokeo yake, Serikali haikutoa hata shilingi benki mwaka mzima!

Wakulima utaratibu ule haukutekelezeka mwaka jana kwa sababu Serikali haikutoa pesa wakati wakulima wametoa pesa asilimia ishirini benki. Naiuliza Serikali; ilikuwaje mkaja hapa Bungeni, mkaleta utaratibu mpya, mkaitisha semina pale African Dream, Wakuu wa Mikoa yote, Wakuu wa Wilaya wote Tanzania nzima, Wabunge wa Mikoa ya Kilimo, semina siku mbili mmetoa na posho kwa utaratibu ambao mlikuwa hamjajiandaa? Haya ni matumizi mabaya ya fedha za Watanzania. Haiwezekani ukaja utaratibu mzuri, watu wakaupokea, Serikali inashindwa kutekeleza! Hii ni dhamira ya dhati kwamba, Serikali haipo makini kuinua kilimo hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo upungufu mkubwa, ni Serikali ya CCM ambayo ipo madarakani imepewa dhamana kubwa imeshindwa kuinua kilimo, kwa maana hiyo imeshindwa kuondoa umaskini kwa kupitia Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa wataalam ni mkubwa kweli na hatuwezi kuwa na kilimo chenye tija kama hatuna wataalam, hatuna maafisa ugani. Wizara ya Kilimo imeomba kuajiri angalau kila kijiji kipate afisa ugani mmoja, wameomba kuajiri kupitia Utumishi, mahitaji waliyonayo ni makubwa, wameletewa kuajiri asilimia kumi tu ya mahitaji yao. Hivi kweli Serikali sijui hatuwaelewi wenzetu; *are we serious*? Asilimia kumi ya mahitaji wakati wakulima wapo maeneo mengi, tunahitaji wapatiwe huduma, tunahitaji wapatiwe utaalam, walime kwa tija, kilimo kiwe cha tija, hili ni tatizo! Serikali itoe kibali cha kuajiri wataalam wa kutosha kwenye Sekta ya Kilimo, tupate maafisa ugani wa kutosha, kilimo chetu kiweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la mawakala. Serikali imetoa kibali kwa mawakala 460, wamepewa leseni kwa ajili ya kufanya biashara ya mbolea katika maeneo mbalimbali Tanzania nzima; ni jambo jema. Napenda kujua mawakala wanavyopewa dhamana au wanavyopewa vibali kwa ajili ya kufanya biashara za pembejeo wanapewa taratibu gani, wanapewa maagizo gani, wanapewa miongozo gani?

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Ni kengele ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Ni kengele ya pili Mheshimiwa. Meza imesema ni kengele ya pili, kaa chini. Mheshimiwa Kidawa, ajiandae Mheshimiwa Soni na Mheshimiwa Makani.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja hapa zinatolewa ya kwamba, sisi Wabunge kutoka upande wa pili wa Muungano wa Zanzibar, kuna sababu gani ya sisi kuchangia Wizara ambazo siyo za Muungano. Ninadhani kuna sababu lukuki na moja kati ya Wizara ambazo siyo za Muungano ni Wizara ya Kilimo. Kuna muunganisho mkubwa sana wa Watanzania wanaoishi Zanzibar na wanaoishi Tanzania Bara kuhusu Sekta hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Wizara hii siyo ya Muungano, lakini mazao ya kilimo tunatumia sana kule Zanzibar kutoka Tanzania Bara; tunakula mchele wa Mbeya, tunakula viazi na tunapata nyama salama kutoka Tanzania Bara. Kwa hiyo, tuna kila haki ya kuchangia kilimo ili kiweze kukua na Wananchi wote wa Tanzania waweze kunufaika. Katika kufanya shughuli za maendeleo ni lazima ushibe. Ukienda kwenye mikutano ya hadhara ni lazima uwe umeshiba. Ukifanya maandamano lazima uwe umeshiba. Kwa hiyo, yote hayo ni kwa sababu ya hiki kilimo ambacho kinatupatia lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza jitihada za Serikali ambazo matunda yake yanaonekana. Hivi sasa nchi yetu ina chakula cha kutosha, inajikimu kabisa kwa chakula na imebakia ziada ya kuweza kuuza nje. Mfumuko wa bei hasa unaotokana na chakula sasa umeshuka, kwa maana hiyo, Wananchi wetu hali yao imekuwa kidogo afadhali kutokana na jitihada hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya jitihada hizo, bado kuna changamoto nyingi katika Sekta ya Kilimo, mojawapo ni ile ambayo imezungumziwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa, ukuaji wa uchumi unakua kwa asilimia saba lakini upunguaji wa umaskini wa Watanzana unapungua kwa asilimia ndogo. Hii ina maana kwamba, zile sekta ambazo zina watu wengi, uwekezaji wake bado haujatosheleza. Sekta yenye watu wengi ni hii ya Kilimo, karibu asilimia sabini na zaidi wanaishi vijijini na wanajishughulisha na kilimo. Kwa hiyo, hapa Serikali ni lazima iongeze jitihada ya kuhamasisha watu washiriki katika kilimo hasa vijana na kuendelea kuwekeza katika Sekta hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ule utaratibu wa *BRN,* Sekta mojawapo inayoshughulikiwa mle ni Sekta ya Kilimo; kilimo cha mpunga, kilimo cha mahindi na kilimo cha miwa. Kuwekwa kwenye *BRN* ni kitu kimoja, lakini kupatiwa fedha za kutosha ni kitu kingine. Bajeti inaweza ikapangwa lakini *allocation* ya *resources* kwa kuwapatia fedha za kutumia zinaweza zisitosheleze. Kwa hiyo, naishauri Serikali, kwa Sekta hii, wajitahidi fedha zipatikane za kutosha kabisa kuendeshea Miradi iliyomo kwenye BRN na Miradi mingine ambayo haimo katika *BRN.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Maputo Protocal* imezungumzia na wamekubaliana nchi zetu za *SADC* kwamba, uwekezaji ufikie angalau asilimia kumi ya bajeti yote ya nchi. Kwa Tanzania ipo chini, imeendelea kushuka mwaka hadi mwaka. Mwenyekiti wa Kamati hapa ametueleza kwamba, mwaka huu wa 2013/2014 ni asilimia tano tu. Kwa hiyo, hilo ni jambo la kuweza kuangaliwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maboresho ya kilimo, nchi yetu imejitahidi, Serikali imejitahidi kufanya utafiti na kusambaza mbegu bora kwa asilimia karibu themanini, asilimia 20 tu ndiyo inayoagizwa kutoka nje. Tunaipongeza Serikali, lakini bado tunasisitiza utafiti uendelee kufanywa ili asilimia mia moja, mbegu bora zitoke ndani ya nchi yetu kulingana na mazingira yetu.

Kwa kufanya hivyo tutaepukana na tatizo la mbegu kukataa kuota. Ninasisitiza kwa Serikali, baada ya kuanyika utafiti na kupatikana mbegu bora, utafiti uendelee kufanyika wa udongo kwa sehemu mbalimbali ambazo mbegu zile zinapelekwa ili kuondokana na hasara. Wananchi tunawapa mbegu wanalima, lakini mbegu hazioti, kumbe utafiti ulikuwa hautoshelezi, haukidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kwa wale wafanyabiashara ambao wameingia mkataba na wakulima kuwapatia mbegu, kama zile mbegu hazikuota, kwa hiyo, ni wao ndiyo watakiwe kuwafidia wakulima hawa. Kipengele cha kutoa fidia kiwemo ndani ya mkataba tokea awali wanaposaini mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa jana hapa, mbegu za pamba hazikuota, zimekataa kuota, sasa Waziri anasema labda tutazungumza nao; lakini kama ndani ya mkataba kimewekwa kile kipengele, isingekuwa tena kuzungumza nao ni moja kwa moja wangetakiwa wawalipe fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana na ushiriki wao kwenye kilimo, tunajua kilimo kinaendeshwa na …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Kidawa. Waheshimiwa Wabunge, dakika saba ni ndogo sana! Mheshimiwa Soni, ajiandae Mheshimiwa Makani na muda nafikiri utabakia ajiandaye Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** *Ooh my God!*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kidawa. Waheshimiwa dakika saba ni ndogo sana Mheshimiwa Soni jiandae Mheshimiwa Makani na muda nafikiri utabakia Mheshimiwa Kawawa jiandae.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kwanza niwapongeze Wizara ya Kilimo ikiongozwa na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu mzima ya Wataalam kwa kuleta mipango mizuri kila mwaka ya kuendeleza Sekta ya Kilimo, lakini nasikitika kuwa, mipango yao inabaki kwenye vitabu tu kwa sababu fedha za kutosha za kutekeleza ile mipango hazijawahi kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ile fedha ambayo kila mwaka tunapitisha katika Bajeti zetu ni asilimia 50 au 60 tu ndiyo inatolewa kwenda kutekeleza hiyo miradi. Sasa kama tulivyokubaliana kwamba Serikali itoe bajeti ya kutosha kufikia asilimia 10. Hata mwaka huu ilitoyotolewa asilimia tano ukiangalia asilimia 66 iliyotolewa ni sawa na asilimia 2.6 tu ya fedha ya bajeti yetu ndiyo inayotolewa.

Kwanza kabisa ningependa kushauri Serikali ihakikishe kuwa migogoro ya ardhi iendelee kutolewa yote iishe ili wakulima waweze kufanya kazi yao kwa tija na ardhi yote ile ya kilimo ambayo sasa inageuzwa kuwa ya makazi na viwanda na mambo mengine hiyo Sheria ije mapema, la sivyo itafika mahali hatutakuwa na ardhi ya kilimo. Pia Serikali iangalie kwamba kuna kodi nyingi ambazo tumeshapitisha na iko kwenye *Finance Bill* kwa kuondoa kodi zile katika vipuri, katika pembejeo na zana za kilimo, bado Serikali inaendelea kutoza kodi hiyo kinyume na Sheria ambayo Sheria ya Bunge hili imepitisha hizo kodi iangalie namna ya kuondoa.

Kuna mtiririko wa aina zaidi ya 26 za kodi ambazo ni kandamizi kwa Sekta ya Kilimo, lakini pia Serikali iangalie tunaposema kwamba tuzalishe mbegu nchini, tuzalishe madawa nchini, yale madawa na mbegu inayozalishwa nchini inatozwa kodi ya kila aina, lakini ile ambayo tunaagiza kutoka nje haina kodi yoyote, ina maana tunaendelea kuwahimiza watu kwamba msizalishe nchini, kazalisheni nje ya nchi, wanufaike wakulima na viwanda vya nje ili Tanzania iwe *dumping ground* sehemu ya kuwa kama *market*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu tuangalie vile vitu ambavyo vinazalishwa nchini, viwe pia vinapata msamaha ili viweze kushindana katika soko la ndani, lakini pia vituo vyetu vya Utafiti havipatiwi fedha za kutosha. Ukiangalia hali ya Vituo vyetu ni mbaya kabisa. Serikali iangalie namna ya kuwekeza, kama wanasema, *no research, no right*. Kwa hiyo, kama tunasema Sekta hii ya Kilimo ikue kama hatufanyi utafiti na hizo nanihi zetu za utafiti hazipatiwi fedha, sidhani kama tunavitendea haki, vipatiwe fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya matunda mbalimbali tunaagiza kutoka nje ambayo yangeweza kuzalishwa hapa nchini pamoja na vyakula mbalimbali na kwa mfano, juisi asilimia 95, mvinyo asilimia 95, yote ile ni mali ya kutoka nje ya nchi inanufaisha wakulima wa nje ya nchi wakati vingeweza kuzalishwa hapa nchini na wakulima wetu wakanufaika. *(Makofi)*

Serikali iangalie namna ya kuondokana na hicho kitu ili wakulima wetu waweze kunufaika. Pia tungeendelea kuomba Serikali iwekeze katika umwagiliaji. Leo hii ukiangalia bajeti ile ya umwagiliaji haina kitu, ile pesa haitoshi hata Wilaya moja. Sasa kama tuko *serious* kwenye hii tuangalie namna ya kuwekeza kama Serikali ilivyofanya katika miundombinu, katika nishati, katika Sekta zingine kwa mfano Afya, pia ifanye katika Sekta hii ya Kilimo katika mambo ya umwagiliaji, itafute fedha za kutosha ili tuweze kuzalisha chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya ukame ndiyo ile fedha ambayo tunaitengea *NFRA* nusu ya ile fedha ingekwenda kuboresha ile miundombinu ya umwagiliaji katika ile mikoa tungeweza kuzalisha chakula na tusingekuwa na haja ya kununua chakula kingi na kuweka tu ambapo kile chakula kinakwenda kugawiwa bure na ile fedha kila mwaka inapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwezesha wale wananchi kulima wenyewe tutakuwa na chakula cha kutosha na usalama wa chakula utakuwepo. Pia kuna maeneo mengi ambayo Serikali tunatumia mabilioni ya fedha kwenda kukarabati miundombinu ambayo inaharibiwa na mafuriko na majanga mengine. Tungeweza kujenga mabwawa katika maeneo ambayo yana mafuriko. Mabwawa hayo yangeweza kusaidia, tusingetumia fedha kwenda kukarabati baada ya mafuriko kutokea na yangesaidia katika umwagiliaji, katika uvuvi, maji kwa ajili ya mifugo na pia kwa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tujipange, Wizara inajitahidi sana kuweka mikakati na mipangilio mizuri, lakini fedha ya kutosha haitengwi. Wakulima hawahitaji hisani, wakulima wanahitaji kuwekewa mazingira bora ya kufanya biashara. Kilimo kiangaliwe kama biashara ili wakulima waweze kufanya kazi yao vizuri na ikifika mahali hizi kodi zote ambazo ni kandamizi kwa wakulima sisi tunashauri kwamba tutaendelea kuhamasisha wananchi ili

gharama za uzalishaji zijulikane. Hakuna mtu anafanya kazi ya kusaidia mtu mwingine. Kila mtu anafanya kazi ili apate faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutawahamasisha wakulima ili gharama zao za uzalishaji pamoja na kodi zote kama Serikali imekataa kuondoa katika zile zana zao na mambo mengine. Gharama halisi ijulikane, ili mkulima apatiwe bei halisi ya mazao yake kama mahindi wanatakiwa wauze kwa sh. 800 au sh. 1,000 kwa kilo, basi iwe ndiyo bei halali na watakaoumia ni hao wachache ambao hawalimi. Asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima. Sasa Serikali iwe *serious* kuangalia kwamba yale mahitaji ya wakulima inawapatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kusema kilimo ni uti wa mgongo, lakini Taasisi kwa mfano ya *SUA* ambayo ni Taasisi pekee ya kilimo nchini, ukiangalia hali yake fedha ya maendeleo wanayopata ni ndogo, lakini pia ile ndogo hawafikishiwi kwa wakati na unakuta hakuna kazi ya maana inayoendelea. Tunategemea sehemu kubwa pale inaendeshwa kwa hisani ya watu kutoka nje wakati tuna uwezo kabisa ndani ya nchi hii kuhakikisha Taasisi kama ile inafanyiwa kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine muhimu ni Benki ya Kilimo. Tunashauri hii benki ianzishwe mapema na kama bado ile bilioni 50 tuliyotenga mwaka jana ya hii Benki ya Kilimo zingepelekwa hata bilioni 20 ziende kwenye Mfuko wa Pembejeo wa Taifa ili ule Mfuko uweze kunufaisha wakulima kwa sababu ule Mfuko umekuwa mkombozi na ukiwezeshwa wakulima wataendelea kupata zana za kilimo, kwa mfano matrekta, pia zana za kukamulia nafaka, pia vifaa vingine kwa mfano vya umwagiliaji. Huo Mfuko unatoa katika sekta zote kwa hiyo, uwezo wa ule Mfuko ungeendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu kuliko yote naamini Serikali ni moja, Wizara ya Kilimo inajitahidi, lakini Wizara ya Fedha bado...

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Makani, ajiandae Mheshimiwa Kawawa!

**MHE. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya afya na uzima na kwa fursa hii ya kusimama wakati huu ili nami niweze kuwa mmojawapo kati ya watu watakaochangia katika hoja iliyoko Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja ningependa kwenda ukurasa wa 30 wa kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, halafu kwa haraka tu miongoni mwa mazao yaliyoorodheshwa pale kuwa ndiyo mazao makuu nchini, zao la korosho linaonekana kushuka uzalishaji wake kwa maana ya matarajio kama Wizara ilivyoainisha pale kwamba mwaka 2014/2015 uzalishaji utashuka kutoka tani laki moja elfu ishirini na saba mia tisa sitini na tisa kwenda laki moja na elfu ishirini. Ningependa kujua utabiri huu unatokana na sababu zipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kusema tu ukurasa huo huo wakati tunazungumza kwamba, katika kukabiliana na changamoto za soko la kahawa, Serikali imeunda Kikosi Kazi ili kutathmini mwenendo wa soko la kahawa ya Tanzania. Napenda kuishauri Serikali kama ambavyo nitaainisha muda mchache ujao changamoto za soko ziko kwenye mazao karibu yote yale makuu yaliyoainishwa kwenye jedwali lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa namna ya pekee nataka kuzungumzia juu ya changamoto za soko la korosho. Muda hautoshi kuzungumzia umuhimu wa zao la korosho hapa nchini kwa ngazi ya Taifa, lakini pia katika ngazi ya Halmashauri ningeweza kusema tu kwa haraka haraka kwamba zao la korosho, pato lake linachangia asilimia 28.5 ya pato zima la Halmashauri ya Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake nini? Ni kwamba zao hili ndiyo tegemeo kwenye Halmashauri yetu na kwa hiyo, changamoto zinazolizunguka zao hili, zinaathiri moja kwa moja maendeleo ya Wilaya ya Tunduru, maendeleo ya nchi, lakini pia umaskini na hali ya kipato cha wananchi wa Tunduru kwa ujumla. Sasa liko jambo moja linatajwa hapa kuwa ni mojawapo ya jambo linalochangia ugumu wa biashara ya korosho. Nalo ni juu ya suala stakabadhi ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi kabisa niseme kwamba, kikiundwa kile chombo nilichokitaja hapa sasa hivi basi kiangalie upya juu ya suala la changamoto zinazozunguka mfumo wa stakabadhi ghalani na kwa namna ya pekee niipongeze Kamati ya Sekta inayohusika kwamba na wao pia wameeleza kwa umahiri mkubwa kabisa kwamba suala hili tumezungumza kwa muda mrefu na linaonekana kuwa bado halijapata suluhisho na kwa hiyo, sasa ufike wakati tuone matokeo yake kwamba, ni namna gani tunaweza tukaboresha au tukaachana nao kabisa mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Tunduru sisi tuna mfano hai kwamba, misimu miwili iliyopita kwa kuachana na kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani kwa sababu ya mazingira yaliyokuwepo na hapa niishukuru Serikali ya Mkoa, Serikali ya Wilaya na hata pia Serikali kwa upande mwingine kwa kukubaliana

na Serikali za Mkoa na Wilaya hatukutumia mfumo huu na kwa hiyo takwimu zinaonesha kwamba uzalishaji ulipanda, lakini pia pato lilipanda kwa maana ngazi ya Halmashauri na msimu uliopita tuliweza kufikisha asilimia 59.26 kama mchango wa zao la korosho kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwa sababu muda ni mfupi, jambo lingine kuhusiana na suala la korosho. Suala la Viwanda vya Kubangua Korosho tumelisema sana. Naomba Waziri atakaposimama atuambie Viwanda vya Korosho ambavyo vilibinafsishwa na ambavyo mpaka sasa hivi tumeona wazi kabisa havijatoa *impact* yoyote kwenye uchumi wa nchi hii, tumefikia wapi juu ya suala la kurudisha viwanda vile mikononi mwa Serikali au mikononi mwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vidogo vidogo vya ubanguaji, kwanza niishukuru Serikali kwamba kutokana na kuleta umeme katika mpango wa umeme vijijini Wilaya ya Tunduru, uwezekano mkubwa sasa wa kuwa na viwanda vidogo vidogo vipatikane kwa ajili ya wananchi kuweza kubangua korosho na kuongeza tija, kuongeza thamani kwenye zao la korosho badala ya kuuza korosho ghafi sasa hili litawezekana kutokana na jitihada za Serikali za kupeleka umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la masoko litaboreka kwa sababu ya kuboreshwa kwa miundombinu, kwa sababu muda hautoshi, lakini ningeweza kutaja barabara nyingi ambazo sasa hivi zinaweza kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuwezesha sasa mazao haya yaweze kufika kwa haraka zaidi kwenye masoko na kwa hiyo kuweza kuhamasisha uzalishaji zaidi kwa ajili ya maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka kuhusu *research,* kama muda utatosha, utafiti ndiyo utakaotuwezesha kupiga hatua katika jambo lolote lile ikiwemo uzalishaji wa mazao. Lakini asilimia 100 tunayoitaja kama *figure global,* imefika wakati sasa tui-*cascade* twende kwenye maeneo ya kila sekta. Kwa mfano, kwenye kilimo ni kiasi gani cha fedha hata kama ni kwa utaratibu wa kuangalia asilimia itakwenda kwenye Sekta ya Kilimo na kwa sababu ya umuhimu wake ambavyo tunaimba kila siku juu ya umuhimu wa kilimo natarajia kwamba fedha za *research* nyingi zitakwenda upande wa Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wataalam ni vile vile, sasa tufike wakati tutengeneze *kanzidata* ya Taifa ya kila sekta, wataalam tunaoimba kila wakati wanahitajika ni wangapi? Wataalam wa maeneo yapi ni wangapi na kwa hiyo watapatikana...

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Namwita Mheshimiwa Kawawa na ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho mchana huu.

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Watu wote waliohutubia hapa leo wamelalamika sana kuhusiana na masuala ya mbegu na mbolea feki. Serikali lazima ifahamu kwamba mkulima malighafi yake ni tatu; maji, mbegu na mbolea na mkulima anazalisha kama kiwanda kingine chochote kile ambacho kinategemea malighafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tutaendelea kuruhusu au kuachia tu bila kuchukua hatua stahiki kwa wazalishaji au kwa wazalishaji wa mbegu na waingizaji wa mbolea feki kwa kuwafungia tu maduka yao au kuwanyang'anya leseni na kuishia pale tutakosea. Lazima tuwapeleke Mahakamani walipe fidia ya hasara ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wakulima ni wadogo na maskini. Sasa wakipata mbegu feki, wakipata mbolea feki, wanapata hasara, wasipolipwa fidia na fidia walipe waliosababisha. Wao wameshapata faida kutokana na mbegu na mbolea hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niende katika Halmashauri yetu ya Namtumbo ambako pia tuna tatizo la kutopewa *cess* yetu ya mauzo ya mahindi. Tunadai Serikali milioni 105, Wakala wa mahindi *SGR* wamenunua na tunapaswa yeye kama pia Wakala wa kukusanya mapato yetu katika Halmashauri yetu. Tunaomba Hazina itoe fedha kwa *SGR* ili iweze kulipa fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuna tatizo la ununuzi wa mazao ya mahindi wakulima kutolipwa kwa wakati. Mwaka jana wakulima wa Namtumbo walilipwa mwezi wa Desemba, tena baada ya presha kubwa sana, mpaka Mawaziri wengine wakaitwa mizigo kwa sababu ya Hazina kutotoa fedha mapema. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali itoe fedha hizi hawa wakulima ni maskini. Wao lazima wajue matunda ya jasho lao; wanalima, wanapalilia, wanavuna, wanapiga mahindi, wanapeleka sokoni, halafu hawalipwi fedha zao kwa wakati unaotakiwa. Naomba wenzetu watendaji wa Serikalini wanaohusiana na masuala haya ya fedha wafahamu kwamba, wakulima Ofisi yao ni mashambani. Wao wanatoka nyumbani wanaingia kwenye kiyoyozi, wao wenzetu wanafanya kazini porini, walipwe mapema fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumbaku; naungana na Kamati ya Kilimo, kwamba Bodi ya Tumbaku iongezewe bilioni 1.2. Uzalishaji wa tumbaku umeongezeka. Bodi ya Tumbaku ilikuwa inazalisha au tumbaku ilikuwa inazalishwa tani elfu arobaini, lakini Bodi ya Tumbaku imesaidia ilitengeneza mpango mkakati imefikia sasa inazalisha tani laki moja na elfu ishirini na tisa ya tumbaku. Ilikuwa inatoa kodi ya Serikali bilioni 60, lakini kodi inayotokana na mazao ya tumbaku imefikia bilioni 149. Leo wanaomba bilioni 1.2 ili kufanya kazi yao, waajiri *classifiers* kwa sababu uzalishaji umeongezeka, kazi zimeongezeka inakuwa shida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti tunaomba Kamati ya Bajeti inakaa, inataka kuwaongezea Wizara ya Kilimo fedha. Tunaomba Wizara ya Kilimo fedha mkiongezewa wapelekeeni Bodi ya Tumbaku bilioni 1.2, waongeze *classifiers,* wafanye kazi yao vizuri ili waweze kuzalisha vizuri tumbaku na ili Serikali iweze kupata fedha yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya tumbaku yalikuwa dola milioni 60, sasa hivi yalifikia mpaka dola milioni 300, mauzo ya nje. Sasa kwa nini hii isipewe fedha ili kusaidia uzalishaji huu unaoingizia Serikali na nchi hii mapato. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali ilifikirie hili kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema hayo tu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge orodha ya wachangiaji wetu mchana imemalizwa na Mheshimiwa Kawawa. Jioni tutaanza na Mheshimiwa Mashishanga, Mheshimiwa Mchuchuli na Mheshimiwa Mushashu.

Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Kamati ya Ulinzi na Usalama na Wabunge wengine wote watakaopenda kupata maelezo ya huduma ya bima ya afya wanakaribishwa saa saba mchana kwenye Ukumbi wa *Msekwa Hall,* Watalaam wa *Jubilee Insurance* watawapatia maelezo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji anawatangazia Wajumbe wake wote kuwa kesho saa nne asubuhi kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi wa Msekwa B.

Mwenyekiti wa Bunge *Sports* Mheshimiwa Idd Azzan anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge na wanamichezo wa mpira wa miguu, mpira wa pete na mazoezi ya viungo kuwa, mazoezi rasmi ya kujiandaa na michezo ya kirafiki yataanza siku ya Jumatatu tarehe 12 saa 11 asubuhi kwenye Uwanja wa Jamhuri wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi kamili jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge liliahirishwa hadi saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mchana nilimtaja Mheshimiwa Mashishanga; sasa nakuita Mheshimiwa Mashishanga, jiandae Mheshimiwa Mchuchuli!

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kabla sijaanza kuchangia naomba kuunga mkono Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara hii, lakini kabla sijaendelea nataka nijikite kwenye Ukurasa wa 22 mpaka 25 katika Hotuba ya Waziri wa Chakula, Kilimo na Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma, lakini nimepitia kimafungumafungu nikagundua kwamba, nasikitika na nachelea kusema kwamba, Serikali imekumbuka shuka wakati kumekucha. Nazungumza hivyo kwa nini; wakulima wa pamba, huu ni mwaka wa pili sasa hivi wamekuwa wakilalamika kuhusu suala la kuuziwa pamba ambayo haikuota, lakini kumekuwa na mbolea feki, kumekuwa na dawa feki, mbegu feki, lakini leo Serikali ndio inagutuka kutafuta udhibiti wa vitu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa kama mimi natoka Shinyanga natoka Simiyu naunga hii hoja kwa nini? Nafikiri hata wana Shinyanga na Simiyu watanishangaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kwa kweli, lakini bado Waziri amekuja hajazungumza atawafidia vipi hawa wakulima. Ni kwamba, amefurahishwa na kitendo cha wauzaji wa mbegu za pamba kuwauzia wakulima mbegu ambazo hazioti? Sijaelewa kwa kweli mpaka saa hizi, sioni haja ya kuunga mkono Hotuba hii ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Kilimo cha Mkataba. Hili ni janga, hawa wakulima wa pamba watanyanyasika mpaka lini? Kwa nini wanalazimishwa kuingia katika kilimo cha mkataba? Sidhani kama Wizara inajua kuna tatizo sana kwenye hiki Kilimo cha Mkataba kwa sababu, humu ndani kumejaa ufisadi. Sidhani kama wanajua hili suala na sidhani kama wamewatembelea wakulima wa pamba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi nimetembelea Mkoa wa Shinyanga na Simiyu kila Wilaya na ulikuwa ni msimu wa kuuza pamba. Kwa kweli,

inasikitisha sana; kwanza bei ya pamba iko chini, wakulima wanalalamika, matokeo yake sasa hivi pamba iliyokuwa inasifika kwa ubora, ya Tanzania, sasa hivi imekuwa haisifiki kwa ubora kwa sababu, wakulima kwanza wanapunjwa, matokeo yake wanaweka maji kwenye pamba, matokeo yake pamba inakuwa haina ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Pamba ipo, sijui Bodi ya Pamba inamsaidia mkulima wa wapi? Inamsaidia mkulima gani? Inawezekana sio mkulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, inasikitisha sana. Siwezi kuunga hii Hotuba, yaani siwezi kuunga mkono hoja kabisa hata siku moja, mpaka nijue wakulima kwa sababu, kila siku tunasimama hapa tunazungumzia masuala ya pamba. Tunazungumzia wakulima wa pamba, hivi hawa wakulima wa pamba walime nini na ndio walikuwa wamezoea kulima pamba? Nawaambia Wasukuma wenzangu, "*Jagimtwe 2015,*" mtajibeba! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la uchelewashaji wa pembejeo za kilimo. Serikali imekuwa haifikishi kwa wakati pembejeo za kilimo pamoja na kuwa ni *fake,* hazisaidii wakulima, lakini bado wanazichelewesha, tunafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake kuna wafanyabiashara ambao wanawahi kuzipeleka kule kwa wakulima, wanajikuta wananunua kwa bei ya juu halafu pembejeo za Serikali zinachelewa kuja, wanajikuta wameingia hasara mara mbili. Kwa kweli, sioni kama kuna umakini kwenye hili suala. Kuna haja ya Serikali kuangalia upya zao la pamba vinginevyo, muwaambie walime nini wakulima wa pamba kwa sababu, ndio zao ambalo wamezowea kulilima. Labda kama mna zao mbadala ambalo mnategemea labda Serikali mtalileta baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nizungumzie tena kuhusu Vyama vya Ushirika. Vifufuliwe, hata kama vilikuwa vinawanyonga wakulima, lakini ilikuwa ni afadhali kuliko wanunuzi sasa hivi wanavyowafanya wakulima. Vifufuliwe tuone basi utendaji wake, visukwe upya kwa sababu, naona kama ndio vilikuwa vinasadia kuliko hata wakulima ambao wako sasa hivi. Rai yangu kwa Serikali, naomba hivi Vyama vya Ushirika vifufuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuzungumzia kuhusu Manispaa ya Shinyanga; kuna *schemes* za umwagiliaji, Mwamashele, Iweleyangula na Mwamalili, lakini hizi *schemes,* kama tunavyojua Shinyanga, Shinyanga ni Mkoa ambao una ukame sana. Hizi *schemes* zimekwisha, lakini ziko chini ya kiwango; nyingine hazijajengwa mifereji, hakuna mabwawa, unapotengeneza *scheme*

bila mabwawa unategemea nini kwa Mkoa kama wa Shinyanga wenye ukame? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niishauri Serikali; tuna maji ya *Lake Victoria,* yale maji ni mengi sana na Serikali imepoteza pesa nyingi sana kwa ajili ya ule mradi. Kwa nini, sasa Serikali isitumie yale maji kwa ajili ya kuendeleza hizo *schemes* za umwagiliaji? Nafikiri lingekuwa suala la muhimu sana, ili watu wa Shinyanga na wenyewe waweze kujikomboa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, ardhi nyingi imechukuliwa na watu binafsi, imechukuliwa na mashirika, haijaendelezwa mpaka sasa hivi na wakulima wanabaki wanahangaika. Naomba sana Serikali irudishe ardhi iliyowanyang'anya watu ambao hawajaiendeleza ardhi hiyo, ili waweze kutumia wakulima kwa sababu, sasa hivi tuna mgogoro na wakulima na wafugaji kuhusu ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo ambalo lingekuwa la busara sana Serikali ikaangalia upya ile Sheria kwa sababu, inajua ilitengeneza Sheria yenyewe, lakini sasa sioni kama inatilia mkazo. Kuna watu wana mashamba makubwa, lakini hawayaendelezi na wakulima wanabaki wanahangaika na maeneo machache. Naomba Serikali iliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu yalikuwa hayo tu. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa nikiwa salama. Kipekee pia napenda nitoe pole zangu kwa wananchi wa Wilaya ya Rufiji, kwa kuwa, mafuriko yametuathiri sana mwaka huu. Mazao yetu yote yamekwenda na maji, hasa watu ambao wapo kwenye Tarafa ya Ikwiriri, Tarafa ya Muhoro, watu wa Kipo, Kipugila, Mkongo na Utete. Nawaambia wananchi wangu tupo pamoja. Poleni sana, Mwenyezi Mungu atatuletea wepesi, *Inshallah*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kwa kina sana Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Mheshimiwa Waziri namheshimu sana, baba yangu Chiza, ni mtu timamu na namwamini sana, lakini Mheshimiwa Waziri anapata bahati mbaya kufanya kazi na watu ambao sio waadilifu, watu ambao hawaitakii mema Tanzania hii, watu ambao hawawatakii mema wakulima; lakini pia haitoshi, anafanya kazi na watu ambao wanayageuza maisha ya Watanzania kama siasa. Kuna watu ambao wanafanya kazi zao kwa kupata manufaa wao wenyewe. Yaani wanafanya maisha ya watu wengine kama siasa, kitu kibaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Ukurasa wa 62, alikuwa anaongelea kuhusu mashamba ya kilimo cha biashara na pia akaongelea masuala ya Kambi ya Vijana ya Kilimo, Mkongo Rufiji. Nasikitika sana Mheshimiwa Waziri, hii kambi uliyoambiwa hapa ambayo tarehe 5 Oktoba, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alikuja kuizindua; kwanza nikupe Taarifa, Mheshimiwa Rais alivyofika pale wakati *RUBADA* wanamsomea Taarifa kuhusu Kambi hii na akiwa pale *site,* kwanza aliwaambia *RUBADA* sitaki Taarifa yenu ya kinafiki. Kwa sababu, *RUBADA* wamezowea kuwagombanisha wananchi wa Rufiji na wawekezaji ambao hawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Kambi baada ya Mheshimiwa Rais kuondoka tu, ilikuwa kambi ya mwezi mmoja ya vijana 50, lakini cha kusikitisha kambi hii ilidumu kwa wiki moja, wiki ya pili kulianza matatizo, hakukuwa na huduma yoyote, matarajio ya vijana kwenda kujifunza yalikufa. Kambi hii, kwa kuwa mimi ni Mpinzani mtasema Kuruthumu ni Mpinzani, kamuulizeni Mheshimiwa Diwani wa Mkongo Mheshimiwa Mansoor, Kambi hii ilifungwa.

Sasa nasikitika sana Mheshimiwa Waziri, watu wanakupa Taarifa za unafiki na huyu ni Masanja, anayejiita Mkurugenzi wa *RUBADA*. Ni mnafiki, ni msaliti, ni tapeli. Hatuwezi kufanya kazi na matapeli, hatuwezi kufanya kazi na watu ambao wanafanya maslahi yao kwa kutumia migongo ya wenzao, kitu kibaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema wazi, nimeshamsema Masanja kwenye Bunge hili, hii sio mara ya kwanza. Ni mnafiki, mzandiki, tapeli mkubwa; kwa nini anakupa Taarifa za uwongo unaweka kwenye Kitabu? Hii ni Hotuba Mheshimiwa Waziri, anakudhalilisha, hatuwezi kufanya kazi na Viongozi kama hawa ambao wanakudhalilisha wanatoa heshima yako. Mheshimiwa Waziri, umwangalie sana Masanja ni tapeli sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haitoshi huyo Masanja pia amekupa Taarifa za *Agro Forest*. *Agro Forest* imeanza kuzungumziwa kwenye Bunge hili tangu katika Mpango wa 2011/2012 kwenye Mpango wa Mheshimiwa Wassira, nikasema hapa huu ni unafiki. *Agro Forest,* Mheshimiwa Waziri, walikuja; kwanza tuliambiwa wameshapata eneo, leo tunaambiwa mchakato wa kupata eneo unakwenda, lakini walikuja Rufiji wakaleta matrekta yao mwaka jana, takribani matrekta zaidi ya 50, lakini baada ya wiki mbili, tatu, matrekta kila siku yalikuwa yanapungua kwenye ile kambi pale Ikwiriri, ni wanafiki pia nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tusiwe tunaletewa Taarifa hapa, Mheshimiwa Waziri nakushauri ukitaka kufanya mambo ya kilimo Rufiji niulize, mimi mwana Rufiji, nakaa Rufiji, nimezaliwa Rufiji. Kwa hiyo, sitakuwa tayari kupokea taarifa kwenye vitabu vizuri kama hivi ambazo hazina ukweli, sio kweli kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Agro-Forest* wamekwambia hapa wao kilimo cha tawi, Muhoro, miwa, tuliambiwa kwenye Mpango tangu 2011, mpaka sasa hakuna walichofanya. Walisema Disemba wangekuwa wameweka japo vitalu kwa ajili ya miwa, hakuna kitu Mheshimiwa Waziri. Hatuwezi kufanya kazi na wawekezaji wababaishaji ambao wanakuja kupata mikopo kwetu halafu mikopo hiyo wanaweka kwenye mifuko yao. Hatuwezi kufanya kazi na watu kama hawa halafu tunawaita wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikuja wakasema wanataka kulima muhogo, Mheshimiwa Wassira aliandika kwenye Mpango, Rufiji aliitaja, kiko wapi? Hakuna hata kitu kimoja kilichotekelezeka; hatuwezi kufanya kazi na watu ambao sio wakweli, wanakopa, wanachukua pesa kwenye nchi yetu kwa ajili ya kuweka kwenye mifuko yao, hili hatulikubali kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; kuna suala hili la kilimo kwa kusimamiwa na Ngazi ya Kanda. Mheshimiwa Waziri naomba unieleze leo, takribani miradi yote ambayo ni ya kilimo ya umwagiliaji iliyosimamiwa na Ngazi ya Kanda imeshindwa kabisa kutoa matokeo tuliyoyatarajia. Mmojawapo ni Mradi wa Nyamwike Rufiji, tangu 2007/2008 mpaka leo ukienda Nyamweke bilioni moja na *point* imeingia pale; sasa hivi miundombinu, mifereji ile inakufa, manyasi, hakuna kinachoendelea. Sasa tunaposema Kilimo Kwanza tunapeleka hela bilioni moja na hakuna tija, tunategemea nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mradi wa Ngongowele, nilikwenda Liwale, aibu; takribani *1.5 billion,* hakuna kitu kinachoendelea kwenye ule mradi. Nilikwenda Lindi, Mradi wa Ngongo, kwa macho yangu, sasa tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hawa watu wa Kanda ambao wanakuja kutunyanyasa kwenye Halmashauri zetu, wanasema wao kazi wafanye watu wa Halmashauri. Wanakuja na pesa, hela zikiingia wanakuja kuzichukua, wanalipana *per diem,* miradi haiendi, ni nini hii? Tunavyozungumzia kumkomboa mwananchi wa chini kwa kilimo cha umwagiliaji ndio kwenda kuweka hela milioni moja na laki tano halafu inapotea tu, haina tija yoyote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aniambie, hawa watu wa Kanda, wao katika nchi hii kama nani ambao wamezowea kutuangamiza katika miradi ya kilimo cha umwagiliaji? Hili hatukubaliani nalo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini narudi kwenye Wizara, tunasema tunataka Kilimo Kwanza, inakuwa kama hadithi. Katika Mwaka wa Fedha 2012/2013, *CAG* anatuelezea takribani bilioni 22 ambazo zingekwenda kukwamua sekta ya kilimo, zingekwenda kuendeleza miradi ya kilimo hazikupelekwa; sasa tunakuja

tunaongea hapa Kilimo, Kilimo Kwanza, *BRN* kwenye kilimo, haa, bila ya pesa kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa tunapiga hadithi. Haiwezekani bilioni 22 ambazo zingeenda kwenye kilimo hazikupelekwa, halafu tunategemea watu wetu zaidi ya 80% watakwamuka kutokana na kilimo…

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Mshashu, ajiandae Mheshimiwa Kandege!

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nitangulie kwanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuondoa umaskini kama tutaendelea kutegemea kilimo cha jembe la mkono na kilimo hiki hakina tija. Napenda kuipongeza Serikali kwa kuagiza na kuingiza matrekta mengi nchini kiasi ambacho mmeona matokeo yake na sasa hivi tumepata chakula cha kutosha na hata ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini matrekta hayo hayakuenea sehemu zote za Tanzania na hata utaratibu wa namna ya kuyapata haukuweza kueleweka kwa kila mtu. Napenda kuishauri Serikali kwamba, iendelee kuagiza hayo matrekta, lakini ningependa Serikali iniambie ni lini matrekta mengine ya bei nafuu yataletwa hapa nchini na ni utaratibu gani utatumika ili watu waweze kuyapata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoani Kagera zao la kahawa ni zao la biashara. Mwaka huu wametangaza bei ya kuuzia hilo zao, lakini bei iko chini sana kiasi ambacho mkulima ambaye anatoka pale Manispaa ya Bukoba, Bukoba Vijijini, Misenyi, kule Muleba, watapata hasara kwa sababu ile gharama haiwezi kurudisha hata gharama ya kuutunza ule mbuni kwa mwaka mzima. Serikali mnawasaidiaje hawa wakulima wa kahawa wa Mkoa wa Kagera, angalau bei iweze kupanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera umekumbwa na huu ugonjwa hatari wa migomba unaoitwa Manjano. Mara kadhaa mmewasikia Wabunge wa Mkoa huo, kila wakiinuka wanazungumzia juu ya huu ugonjwa wa mnyauko. Wakazi wa Mkoa wa Kagera wanategemea ndizi kama chakula, ndizi kama zao la biashara. Ugonjwa huu wa manjano umeendelea kurudisha maendeleo ya Mkoa nyuma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa huu ulianza kwenye Wilaya moja, sasa hivi umesambaa katika Wilaya zote nane za Mkoa wa Kagera na gonjwa hili ndugu zangu halitibiki. Mgomba ukishaathirika Wataalam wanakwambia kwamba, wewe ng'oa, wewe kata; watu wameng'oa wamebaki na nusu shamba, wengine wamebaki hata na robo shamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia uchungu sana, mkulima kila siku wanamwambia ng'oa, ng'oa, lakini tatizo haliishi. Watu wamepoteza chakula, wamepoteza mapato na wanaendelea kuwa maskini. Hili ni janga kama janga lingine la Kitaifa. Watu wakipata ukame wanapelekewa hela ya chakula au wanapelekewa chakula, naomba Serikali ipeleke chakula Mkoa wa Kagera, ili kusudi hawa wakulima waweze kuendelea kung'oa hiyo migomba wakati wanapata chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza vilevile kile Chuo cha Maruku cha Utafiti kiweze kuwezeshwa kipewe hela kiendelee kufanya utafiti. Kiweze kugundua ni namna gani ya kuweza kutokomeza huu ugonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali iwaonee huruma wakazi wa Mkoa wa Kagera kwa sababu, watu wanaendelea kuwa maskini. Serikali ya Mkoa imejipanga vizuri na Wilaya zake wanataka kuwa na *operation* ya Tokomeza Mnyauko, lakini hii *operation* itahitaji hela. Hata kwa mtu mmoja mmoja anahitaji kununua vifaa, anahitaji hizo *chemicals* kwa hiyo, hawawezi ku-*afford.* Napenda Serikali iniambie, iko tayari kutenga pesa za kutosha kama kweli wanawajali watu wanaokaa Mkoa wa Kagera kusudi hizo ziweze kwenda kuendesha hiyo *operation* ya Tokomeza Mnyauko na watu waondokane na hili gonjwa na waendelee kushamiri na uchumi uendelee kukua kama ulivyokuwa zamani Mkoani Kagera?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika. Ushirika ni mkombozi wa watu, hasa watu ambao wana kipato kidogo. Tumeanzisha vyama vingi vya ushirika kwa sababu, hapo zamani ushirika ulikuwa umekufa, lakini vilevile tumeanzisha na *SACCOS* nyingi. Leo nimesikitishwa na Mheshimiwa Waziri kwenye Hotuba yake alipoanza kuvitaja na kutaja namba ya vyama vilivyokufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirika, Ushirika ni mkombozi wa watu hasa watu wenye kipato kidogo. Tumeanzisha Vyama vingi vya Ushirika kwa sababu hapo zamani Ushirika ulikuwa umekufa, lakini vile vile tumeanzisha na *SACCOS* nyingi. Leo nimesikitishwa na Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake alivyoanza kuvitaja na kutaja namba ya Vyama vilivyokufa, hivi Vyama vimekufa kwa sababu, vimekosa kwanza, ulezi wa Serikali, maelekezo kutoka kwa Serikali na Elimu kutoka kwa Serikali. Vilevile kwa sababu, wamekosa mitaji na mikopo ya masharti nafuu havisimamiwi na vilevile havikaguliwi.

Kila mwaka Wizara mnatwambia kwamba, mnawezesha hizi *SACCOS,* mnatoa elimu, hiyo elimu mnaitoa wapi mbona sisi hatuioni ambao tuko kule chini? Au mkichukua watu wawili kwenye *SACCOS* moja wakaenda kwenye semina ya siku moja, hiyo ndio elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri, pale Wizarani mnao Wataalam. Walipaswa baada ya kuwa tumehamasishwa tukaanzisha Vyama vya Ushirika walipaswa waje na li-programu likubwa ambalo watatambua Vyama vyote vya Ushirika, watatambua *SACCOS* zote, baada ya kuzitambua waandae mafunzo ambayo yako *structured,* ambayo matokeo yake yanaweza kupimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anajua amesoma mpaka hapa, waelimisha wananchi ambao ni wajumbe wa hizi *SACCOS*, waelimishe Wajumbe wa Bodi, waelimishe watendaji kusudi hizi *SACCOS* ziweze kufanya vizuri. Ndugu zangu tafadhali msiue Ushirika, huu ushirika unatoa masoko kwa watu wetu wale wa kawaida walio kule vijijini, ushirika umetoa mitaji kwa mtu ambaye hana dhamana ya kukopesha benki, lakini kwa kupitia *SACCOS* ameweza kupata mtaji. Kwa hiyo, naomba tafadhali Wizara mjitahidi muweke mipango kusudi muweze kuzilinda hizo *SACCOS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile ningependa mnieleze kuna *SACCOS* za akinamama Mkoani Kagera, wako wanahangaika, wangependa kujua kama wanahitaji mikopo ya muda mrefu kama miaka miwili, miaka mitatu ambayo ina riba nafuu kama ya asilimia nne mpaka tisa, wataipata wapi? Tunaomba Wizara mtueleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania iliridhia Azimio la Maputo la mwaka 2003, lakini vile vile imeingia mkataba na *Comprehensive African Agricultural Development Program (CADP)* kwamba kila nchi mwanachama watahakikisha kwamba anatenga asilimia kumi ya bajeti yake iingie kwenye kilimo na sekta ya kilimo itakuwa angalau kwa asilimia sita Tanzania tumefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Burkina Faso, Ethiopia, Ghana, Malawi, Senegal wamefikia asilimia kumi na zaidi sisi ni lini tutaweza kutenga asilimia kumi ikaweza kuingia kwenye kilimo? Mnajua kama tukiweza kuweka angalau asilimia kumi ikaingia kwenye kilimo tutakuwa tumemgusa mtu mmoja mmoja katika Tanzania na hiyo ndiyo itatusaidia tuweze kupunguza umaskini katika Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naunga mkono hoja na nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi jioni ya leo ili nami niweze kuchangia. Awali ya yote nina kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kila Mtanzania ambaye anataka kufuatilia na kujua uhalisia anajua kwamba takribani asilimia themanini ya Watanzania wako vijijini na wengi wanajishughulisha na shughuli za kilimo na ili uchumi wa Taifa hili uweze kukua na kupunguza umaskini nguvu kubwa lazima ielekezwe kwa wakulima ambao ndiyo walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, upunguzaji wa umaskini unatafsiriwa kwa namna ambavyo bajeti inatengwa kuelekezwa kwa hao Watanzania walio wengi, maskini ambao wako vijijini, nini cha kufanya? Serikali inawajibu wa kuhakikisha kwamba wananchi walio wengi wanapunguziwa adha ya ukali wa maisha kwa kuhakikisha kwamba pembejeo za kilimo zinapelekwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuja na utaratibu mpya, maana ule utaratibu wa mwanzo wa kupitia kwa Mawakala ulikuwa ni utaratibu mbovu ulikuwa unaudhi sana. Ukisoma katika taarifa yake, Serikali imelitambua hilo na kwamba kuanzia sasa hivi, utaratibu utakuwa ni kuwalenga wakulima moja kwa moja wakopeshwe kwa kutumia taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukisoma maelezo anasema utaratibu huu kwa mwaka jana haukuweza kufanikiwa kwa sababu taasisi za fedha zilitaka Serikali iweke fedha ili mkulima aweze kukopeshwa mara mbili yake, kama mlichelewa wakati ule naomba kisingizio hicho kisitokee kwa safari hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi sana tumekuwa tukijitahidi kuongelea juu ya kuhakikisha kwamba kilimo kinapata tija ya kutosha, lakini kwa mkulima wa kawaida na hasa katika ile mikoa ambayo inazalisha chakula. Unachopaswa kufanya kwa mkulima ni kumhakikishia kwamba pembejeo zinafika kwa wakati, lakini pia unampa soko la uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haingii akilini, juzi nimesikia Serikali inaruhusu kwamba sasa wakulima wanaruhusiwa kwenda kutafuta masoko nje. Hivyo huyo mkulima ambaye mnataka akatafute soko nje mna uhakika na hilo mnalolisema. Mkulima mwananchi wa kijijini kwangu kule Kalambo leo unataka apeleke mazao nje, wapi huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Naibu Waziri sina uhakika kama wananchi wake wa Mbozi yule mwananchi ambaye anategemea kilimo cha mahindi eti atakwenda kutafuta soko nje. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba,

wanatafuta soko ili mwananchi alime na asiwe na kazi ya kuhangaika kutafuta masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ambao natoa, *NRFA* ipo lakini uwepo wake umekuwa wa kizamani sana. Huu utaratibu wa kwamba wananunua na wanatunza chakula eti wanasubiri litokee janga, itokee balaa ya njaa ndiyo wafanye kazi, ni utendaji wa kizamani sana. Ni wajibu wa *NRFA* ikajitanua kuhakikisha kwamba kipindi ambacho chakula kipo cha kutosha watafute masoko, wao *capacity* hiyo wanayo na Serikali ikiweka mkono wake ni rahisi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kushangaza sana eti unasikia Tanzania tuna chakula kingi, Sudan kuna njaa na *NRFA* ipo *stocks* zimejaa lazima tubadilike tufanye kisasa hii habari ya kwamba unasema una-*target* ya metriki tani laki mbili ukakaa unajivuna, unajivuna kwa sababu unadhani kwamba Tanzania inaishia kwenye mipaka, Tanzania sasa hivi dunia ndogo tutafute masoko nje ya nchi ili mwananchi awe na uhakika kwamba anachokilima chote ambacho hakihitaji kinaingia sokoni na si wajibu wake yeye kutafuta soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusiana na deni la *NRFA*. Sisi wananchi wa Kalambo tumekuwa tunaidai *NRFA* takribani shilingi milioni mia tatu tisini na tatu na deni hili milioni mia moja na tatu tuliirithi wakati tunagawana na Halmashauri ya Sumbawanga na milioni mia mbili tisini na tatu ni deni ambalo msimu uliopita *NRFA* tunawadai jumla inakuwa ni milioni mia tatu tisini na tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Kalambo kwa kujua kupanga vizuri, fedha hii tulipangia milioni arobaini na nne iende kufanya kazi ya ujenzi wa zahanati ya Kipwa, zahanati ambayo mwaka jana yalitokea majanga makubwa, watu kumi na tatu walifariki wakiwa wanafuata huduma ya tiba. Tukipata hii milioni arobaini na nne tunakwenda kuhakikisha kwamba zahanati ile inakamilika lakini pia tulitenga milioni arobaini na moja iende kujenga kumalizia ujenzi wa zahanati ya Safu. Asilimia tano tulisema iende kutunisha Mfuko wa Vijana, asilimia tano kutunisha Mfuko wa Wanawake na zingine zimepangiwa matumizi yake kwa usahihi. Kwa hiyo tusipolipwa deni hilo tafsiri yake ni nini? Kwamba hata vifo ambavyo vitatokea maana yake itakuwa imesababishwa na Serikali kwa *NRFA* kutokutulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba waruhusu nimesikia juzi wanasema kwamba wanaruhusu *NRFA* iuze

tani 150 katika deni la kwanza kuanza kulipwa hiyo pamoja na Halmashauri ya Kalambo ili fedha hii tukafanyie shughuli ambayo tayari tumeshaipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kuhusiana na Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Juzi nilisikia mama yangu Mhita akiuliza swali hapa na Mheshimiwa Naibu Waziri mwenye dhamana akajibu hapa kwamba, kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kwenda kukarabati kinu cha Iringa, nilishangaa kweli. Kwamba hivi katika mipango yote ambayo ipo pamoja na barua na idhini kutoka Baraza la Mawaziri kwamba, Bodi ya Mazao Mchanganyiko ikabidhiwe vinu viwili, nilishangaa Mheshimiwa Naibu Waziri hakulitaja kabisa na cha kushangaza zaidi hata Kamati ya PAC...

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nakushukuru sana. Mheshimiwa Suzan Lyimo, ajiandae Mheshimiwa Mangungu!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ambayo nimeisubiri kwa muda mrefu. Nianze kwa kuwapongeza sana hotuba ya upinzani, lakini pamoja na ile ya Kamati inayohusika na Wizara hii. Ni wazi kwamba kilimo chetu kinahitaji msukumo wa hali ya juu sana, kinahitaji utashi wa kisiasa, lakini kwa muda mrefu sana Wabunge na wadau mbalimbali wa kilimo wamekuwa wakizungumzia tatizo kubwa la Serikali kutoipa kipaumbele Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Wizara hii au sekta hii imekuwa moja kati ya sekta sita za vipaumbele lakini ukiangalia kiuhalisia bado kwa kweli bajeti ya Wizara haiendani kabisa na kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ambapo tunaona katika vitabu kwamba Wizara hii imetengewa asilimia tano tu ya bajeti yote, halafu tunasema kilimo kwanza wakati Watanzania zaidi ya asilimia sabini kati ya asilimia sabini na themanini wanategemea kilimo na ni wazi kwamba kilimo chetu cha sasa ni lazima kiwe cha kisasa, lakini vile vile tunajua kwamba tuna tatizo kubwa sana la matatizo ya tabia nchi na kwa vyovyote vile hatuwezi kutegemea kilimo cha mvua tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni wazi kwamba Mwenyezi Mungu ametugawia rasilimali kubwa sana ya ardhi, wakati ambapo tuna takribani hekta milioni arobaini na tatu ambazo zinafaa kwa kilimo, lakini ni hekari miliomi kumi na moja tu kama ambavyo ipo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambazo zinalimwa, lakini hekari milioni thelathini zinawezekana kabisa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba bila kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji hatuwezi kusema kilimo chetu kitasonga mbele. Ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri na hasa jedwali lake kuhusiana na kilimo cha umwagiliaji kwa mwaka huu 2013/2014, tunaoumaliza, anasema kwamba, kilimo cha umwagiliaji maeneo ambayo yametekelezwa ni hekari kumi na tisa elfu mia nane tisini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake kama tunaenda kwa kasi hii, kama tuna hekari milioni thelathini na moja ambazo zinafaa kwa kilimo hiki, ina maana tunahitaji miaka 1,502 ili tuweze kumaliza eneo hili na nina hakika kwa kasi hii ya kinyonga hakuna jinsi tutaweza kupata kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Wizara na kwa Serikali kama kweli wameona kilimo ni muhimu sana, ambacho mimi naona na Watanzania wote wanaamini kwa sababu wananchi wa Kitanzania *majority* kama nilivyosema asilimia sabini mpaka themanini wako kwenye kilimo, basi naamini kabisa ni lazima kasi ya uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji maji iongezwe ili wakulima waweze kuwa na uhakika wa mazao, lakini vile vile Watanzania wote wawe na uhakika wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu, ni wazi kwamba, kama tunakuwa na *insecurity* kwenye chakula maana yake ni kwamba tunauza uhuru wetu, lakini kama tuna maeneo ambayo yana kilimo bora katika zile *G4* halafu kuna maeneo yenye ukame mkubwa, lakini hawapati kilimo ni wazi kwamba kunahitaji mikakati ya haraka sana katika Wizara hii ili wananchi wawe na uhakika wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hilo, niende sasa kwenye tatizo kubwa sana la Maafisa Ugani. Hata tungewekeza kiasi gani kwenye kilimo kama hatuna Maafisa Ugani ambao wangeweza kwenda kuwasaidia wakulima wetu ili wawe na kilimo bora na kilimo cha kisasa ni wazi kwamba hatufanyi lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali imejitahidi kuongeza udahili katika Vyuo vyetu vya kilimo hasa Chuo Kikuu cha Sokoine, bado tatizo ni kubwa sana kwenye ajira na naona jinsi ambavyo Kamati imeliongelea na mimi naliongelea na wadau wengine wanaliongelea, Wagani hawa wako mijini wakati wakulima wako vijijini, wako kwenye mashamba. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni wazi kwamba hata wakipelekwa vijijini wanakwenda wanarudi kwa sababu hakuna mazingira bora ambayo yameandaliwa kwa ajili ya Maafisa Ugani hao kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wetu, hivyo wakulima

wetu bado wameendelea kutokuwa na kilimo cha kisasa na hivyo kilimo chetu kimekuwa hakina tija hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuongelea suala zima la hizi *irrigation schemes* na naomba sana kule Kilimanjaro eneo la Moshi vijijini, *lower* Moshi *irrigation* kwa miaka mingi Wajapani walikuwa wamewekeza kule, kulikuwa na mashamba makubwa ya mpunga na mchele baadaye, lakini mpaka sasa hivi *lower irrigation* Moshi imekufa sasa hivi wakulima wadogo wadogo hawana nyenzo za kisasa na kwa maana hiyo mashamba yale yamekufa kabisa. Kwa hiyo, ni wazi kwamba tunaomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba wanatoa fedha kwa ajili ya *lower irrigation* kule Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuongelea suala la Ushirika kwamba Ushirika ni jambo la muhimu sana. Wengi tuliomo humu ndani tumesomeshwa na fedha zilizokuwa zinapatikana katika Vyama vyetu vya Ushirika, lakini Vyama hivyo vimekufa kwa sababu tunazozijua za kifisadi, fedha zinaibiwa, mahesabu hayakaguliwi kwa hiyo tunaomba sana Vyama hivi vya Ushirika virejeshwe na wahakikishe kwamba wakaguzi wanakwenda kukagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni zao la mnazi. Watanzania wengi hasa wa ukanda wa pwani wanategemea sana zao hili, lakini kwa muda mrefu sasa zao hili limekumbwa na ugonjwa ambao sina hakika kama Wizara inajua ni ugonjwa gani kwa sababu hakuna watafiti ambao wameshalifanyia kazi lakini wote tunajua kwamba nazi ni zao ambalo linatoa chakula kizuri, lakini vile vile pia ni mafuta na vile vile linatoa mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri naomba kujua ni ugonjwa gani kwa sababu umepelekea sasa hivi nazi moja kufikia mpaka shilingi elfu moja mia tano na hivyo kufanya wale waliokuwa wamezoea kiungo hicho kupata matatizo makubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ihakikishe kwamba watafiti wa nazi wanatuambia ni ugonjwa gani na ikiwezekana uweze kupatiwa dawa kwa sababu kwa kweli kuna wengi pia wamesomeshwa kwa zao hilo mmojawapo akiwa ni Mheshimiwa Zaynab Vullu. Kwa hiyo, naomba sana muangalie ni jinsi gani mtaweza kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Mangungu, ajiandae Mheshimiwa Barwany!

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmechangia na wale ambao

hawajachangia kwa kipindi cha zaidi ya miaka sita au saba Serikali imekuwa ikitoa mwongozo kwamba sasa tuna Kilimo Kwanza. Naomba tukubaliane kama ikiwa tumejiandaa kupitisha kasma ya bajeti kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Kilimo bila kufikiria namna ya kuongeza fedha kwa ajili ya kusaidia kilimo hiki, tukubali hatuna Kilimo Kwanza na dhana ambayo tutakwenda nayo iwe ni Kilio Kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mantiki hata kidogo ikiwa tunazungumzia Watanzania ambao wameajiliwa zaidi ya asilimia themanini katika kilimo na hatuweki fedha za kutosha kwenye kusaidia kilimo. Tutalaumu hapa, tutasema, tutakuja kudai na inavyoonekana Wabunge wote hapa wameondoka katika majimbo yao wamejiandaa kuja kulalamika. Uamuzi wa kutenga mafungu tunao sisi kwa hiyo sasa tuhakikishe katika kasma za bajeti ya Wizara zote tunakata, tunapeleka katika kilimo ili tuweze kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu Susan hapa amezungumza, Wizara ya Kilimo kuna mambo ambayo wakati mwingine mnafanya mnatustaajabisha. Mpaka kufikia mwaka 1985 kulikuwa na utafiti wa minazi ambao ulikuwa ukifanyika kwa msaada wa Wajerumani. Kipindi kile hakukuwa na matatizo makubwa kama yaliyopo sasa. Leo hii kipindi ambacho matatizo makubwa minazi inanyongwa, inakufa, ndiyo ule utafiti unaondoka sasa mnatueleza kitu gani? Kipindi ambacho tuna matatizo hamtusaidii, wakati ambapo kulikuwa hakuna matatizo mlitenga fedha nyingi kwa ajili ya kusaidia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna matatizo ya michungwa, machungwa yanaoza kabla ya kuiva na kabla ya kufika kwenye soko. Embe vile vile sasa zimeingia kwenye matatizo haya. Sasa huu utafiti ambao mnauzungumzia, sijui mnasubiri yaani mpaka miembe yote iwe imekufa na michungwa yote ndiyo mje kuleta tena watafiti ambao watakuja kurejesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao haya ya asili ambayo nimeyataja embe, nazi, michungwa, mikorosho kwa kipindi chote wakulima wanahangaika nayo wao wenyewe, lakini tozo kubwa zinazotozwa katika kufidia tozo za Halmashauri pamoja na Serikali Kuu, hebu tuangalie namna ya kuweza kuwasaidia wananchi kwa hizi fedha ambazo wamekuwa wakitozwa kila mwaka zichangie kufanya utafiti wa kuboresha mazao na kilimo cha mazao haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri, leo amezungumzia Serikali inataka kuweka mfumo mzuri wa uagizwaji wa sukari nje. Nasema hakuna mfumo wowote ruhusuni sukari itoke nje bei ishuke, viwanda vya ndani vimeshindwa kukidhi mahitaji ya soko, mahitaji yetu ni zaidi ya tani milioni moja na nusu, tunaweza kuzalisha chini ya tani laki tatu na hili mjiulize, bei ya sukari katika maeneo yenye viwanda vya sukari Moshi, Mtibwa,

Kilombero inashindana na bei katika maeneo mengine ya mji kama Dar es Salaam na maeneo mengine kama Dodoma. Hii nyie hamjiulizi hapa pana mchezo ambao unachezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hakuna haja ya kulinda viwanda ambavyo havina faida kwa wananchi, sisi tunataka wananchi wapate bei ya sukari iwe chini. Agizeni sukari iwe nyingi, wenye viwanda kama wanaweza waingize ushindani wa soko, wataweza kushiriki, tunataka bei ya sukari ishuke. Huyu Rais wa Simba hapa analalamikia anasema bei ya sukari Tabora ni kubwa mno, shusheni bei kwa kuingiza sukari nyingi kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kwenye kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 16 kwenye *roman two* imesema hivi: "Kuwezesha upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kilimo". Lakini hili mnaliangalia kwa umakini kiasi gani, leo hii viwanda vyote vinavyosindika matunda havinunui matunda ambayo yanazalishwa hapa nchini, wanaagiza *concentrate* kutoka nje na inafungwa na inauza, mazao ambayo wakulima wetu wanayazalisha kule vijijini, kama maeneo ya Kipatimu, Chumo, Kinjumbi, Njinjo na kadhalika yanaharibika, matunda yamekaa kule yanaoza nyinyi mnaruhusu watu wanaagiza *concentrate* kutoka nje kiasi ambacho viwanda vyetu vinashindwa kuyatumia mazao hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa kwamba tunapozungumzia kuboresha kilimo, pia tunahitaji tuwe na miundombinu inayofaa. Leo hii ikiwa mwananchi ameweza kukaa njiani kwa muda wa siku zaidi ya nne au tano akiwa anasafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Kilwa au kutoka Kilwa kwenda Dar es Salaam, halafu unaniambia kwamba tuwezeshe uboreshaji wa masoko, hizo bidhaa zitafika vipi? Mapapai au embe au ndizi vitaozea njiani na hata hiyo nazi ambayo unazungumzia, utatoka na nazi nzima Kilwa inafika Dar es Salaam imeshakuwa makasamala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe kwamba utafutaji wa masoko uwiane pia na uboreshaji wa miundombini ili mazao yaweze kufika katika soko kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba hii hoja ili tuweze kuiunga mkono vizuri, lazima tuhakikishe mafungu yanaongezwa kwa Wizara ya Kilimo, tuweze kuwasaidia na kuweza kukamilisha miradi ambayo imekusudiwa. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Barwany, jiandae Mheshimiwa Cheyo.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nitumie nafasi hii kuunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani, lakini pia nimpongeze Mwenyekiti wa UKAWA Bungeni kwa kutangaza rasmi Baraza la Mawaziri ambavyo limeunganisha Vyama vitatu vya Siasa, Vyama vikuu vya Upinzani katika nchi yetu CHADEMA, *CUF* na *NCCR* – Mageuzi. Tunawaahidi Watanzania sasa wakati umefika tutafanya kazi ile ambayo mlikuwa mnaitarajia kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maneno ya kebehi kwamba eti mnakumbuka kucha kumekucha, lakini mnashindwa kuelewa kwamba ninyi pamoja na sisi kukumbuka mapema, ninyi bado mnaendelea kujifunika shuka hiyo zaidi ya miaka hamsini mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, kwa mujibu wa taratibu ambazo ninazo katika kuboresha kilimo chetu katika Taifa letu, tumeshindwa kufikia malengo ambayo sasa ilikuwa baada ya miaka hamsini tuone tunanufaika na matunda ya kilimo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tukiendelea kutegemea kilimo cha mvua ambacho katika nchi nyingi kimefeli na wenzetu sasa wameamua kutumia kilimo cha umwagiliaji ili kuboresha kilimo chao. Tuna hakika kabisa kwamba kama tutakuwa tumedhamiria kwa kweli kuboresha kilimo chetu, kwa kutugemea kilimo cha umwagiliaji, tunaweza tukafikia malengo ambayo tulikuwa tunayatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mito ya kutosha katika Taifa letu, tuna maziwa, tuna maji ya kutosha kabisa ambayo kama tungekuwa tumepanga vizuri tungekuwa sasa hatuna sababu tena ya kutangaza Taifa hili kwamba ni Taifa la watu wenye njaa. Hivyo naishauri Serikali pamoja na program zake zote ambazo zimefeli, sisi tunawaita hawa kwamba ni mabingwa wa mikakati iliyoshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani tunaweza tukafanya jambo gani katika Taifa letu likatuletea maendeleo zaidi ya kilimo, kwanza kilimo ni ajira hata kama ni pamoja na chakula, asilimia 80 ya Watanzania wamejiajiri kupitia kilimo, lakini wamekosa msaada kupitia Serikali yao. Hili tukae tufikirie na tutafute namna gani sasa Watanzania hawa ambao sasa wamepata uwezo wa kupata uelewa wa kujua nini maana ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu hapa wamezungumzia suala zima la zao la minazi, lakini sisemi tu kwamba minazi ni zao la chakula, minazi ni zao la biashara. Tulikuwa Malaysia miezi mitatu au minne iliyopita, tumeona jinsi gani Malaysia ilivyoboresha kilimo cha minazi mpaka inapata pesa za kigeni kupitia

zao lile. Tuna ukanda wa Pwani, kutoka Mtwara mpaka Tanga ni eneo nzuri kabisa la minazi, lakini leo ukienda Kilwa, ukienda maeneo ya Mchinga, ukienda maeneo ya Ng'apa na maeneo mbalimbali, minazi imeanza kukauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mdudu ambaye tayari anaitwa *chonga*, tulitegemea Serikali ianze sasa na utafiti wake namna gani tunaweza tukatokomeza ugonjwa huu, lakini mpaka leo bado Serikali imekuwa kiziwi juu ya kilio cha wakulima wa minazi katika maeneo yetu. Wengi tunajua tumesomeshwa kupitia minazi, tulikuwa na viwanda vikubwa vya mbata kule kwetu kama vile Kilwa, kule Lindi Mingoyo, lakini viwanda vile vimefungwa, leo tunaagiza nazi, mafuta ya nazi kutoka nje kwa ajili ya sabuni katika nchi yetu. Kama tungekuwa tumesimamia vizuri zao la minazi tusingepoteza pesa za kigeni kuagiza mafuta ya nazi kutoka nchi mbalimbali huko nje. Ni vyema sasa Serikali ikaona umuhimu wa kuboresha na kusimamia zao hili la minazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo juu ya stakabadhi ghalani ambayo mama Clara hapa amezungumza asubuhi. Tangu tumeingia katika Bunge hili, nyimbo yetu ni hiyo, stakabadhi ghalani inawaumiza wakulima, wakulima wamepoteza matumaini hasa wakulima wa zao la korosho, wamepoteza uhuru wao wa kujiamulia ni bei gani ya korosho wanahitaji. Sasa hivi zaidi ya miaka mitano sita, Stakabadhi Ghalani ni Sheria ya Bunge ambayo imepitishwa katika Bunge hili. Waziri wa Kilimo tumekaa naye mara kadhaa, tumezungumza juu ya hoja nzima ya stakabadhi ghalani, tumeahidiwa hapa kwamba Serikali sasa itakaa na kutafuta namna gani itaboresha mfumo huu wa stakabadhi ghalani ili iweze kuleta tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeangalia katika taarifa hii, hakuna matumaini hata kidogo ya kuwafanya wakulima wa korosho waweze kupata nafuu. Pia suala zima la stakabadhi ghalani, limekwenda kinyume na utaratibu ambao zao hili linatakiwa lifanyike, tuna viwanda kule vya korosho, bado vingi vimefungwa, wananchi hawana soko la uhakika, korosho zao watapeleka wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizungumzie suala zima ambalo linahusiana na mashamba ya mkonge. Mashamba ya mkonge wale wenzetu Wazungu wakoloni walipokuja, walitafuta maeneo yenye rutuba, yote waliyachukua, wakayamiliki wao. Leo yanatumika maeneo yale kwa kukopea fedha katika taasisi za fedha na wananchi wanahitaji maeneo kwa ajili ya kilimo, hicho kilimo kwanza mnachozungumza wananchi watalima katika maeneo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeahidiwa hapa yale maeneo ya Ngongo kule Lindi, Mkwaya, Kitunda na maeneo mengine ni maeneo ambayo yana rutuba, lakini wananchi wanazuiwa wasitumie maeneo yale, eti maeneo haya

yako kisheria na yana wawekezaji. Wawekezaji hao pale zamani ninyi mlikuwa mnawaita mabepari, leo mmebadilisha jina mnawaita wawekezaji.

Mlishazungumza hilo, kwamba utaratibu utafanywa Rais afute hati katika maeneo yale ili wananchi wapate fursa ya kuyatumia maeneo yale kwa ajili ya kilimo chao. Mpaka leo bado kauli zile ziko juu ya meza na karatasi yenu hamjazifanyia kazi, wananchi wanahitaji sasa ardhi yao kwa ajili ya maendeleo yao. Ardhi ndiyo uchumi katika nchi yetu, watu wanapigana huko nje, wanagombana katika Mataifa mbalimbali kwa sababu ya ardhi tu, ardhi yetu bado haina thamani kwa mwananchi wa kawaida, kama huna uwezo bado ardhi si mali yako hata kama ni mwananchi wa Taifa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie kwa makini, irejeshe ardhi kwa wananchi, kuwe na sera madhubuti ambayo itaeleza kwamba ardhi hii ni mali ya nani? Ardhi ni mali ya Serikali kwa mujibu wa sera, inawanyang'anya uhuru wananchi, tunataka wananchi wamiliki ardhi yao sasa kwa mujibu wa Katiba mpya ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Cheyo, jiandaeni Mheshimiwa Dkt Ishengoma na Mheshimiwa Kilufi.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nianze palepale pamba; msimu umekaribia lakini mpaka hivi sasa pameanza kuonekana walanguzi kibao, wanakwenda kwa wakulima, wananunua pamba kwa sh. 400/= na Serikali inaangalia na baadhi ya watu wanajulikana, sijui kwa sababu wako karibu zaidi na Chama ndiyo maana wanaachiwa. Kwa hiyo, naomba mara moja Serikali ifanye kazi yake, watu ambao wanaonunua pamba kwa sh. 400/= mara moja wakamatwe na tuache liendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Waziri kwenye *paragraph* 57 amesema kilimo cha mkataba kimekuwa na changamoto na bado anahitaji kuelimisha watu, lakini hivi sasa anapozungumza watu wenye *ginneries* ambao wameomba nafasi ya kuweza kununua pamba, ma-*DC* wanawakatalia, mpaka kwanza wawe na mikataba. Sasa kilimo kimekwisha, utaipata wapi hiyo mikataba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni njia nyingine ya kuhakikisha kwamba tuna soko ambalo halina ushindani, watu watachaguliwa kwa mambo mbalimbali, sisi tunataka soko lenye ushindani. Kama mtu una kiwanda chako, una kiwanda cha kuweza kuchambulia pamba, uruhusiwe ili ulete ushindani na wewe Mheshimiwa Waziri…

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa dakika saba ni ndogo sana kumkatisha mtu, niwie radhi kaa chini Mheshimiwa endelea.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri unafahamu kabisa kwamba, katika miaka ya karibuni kwa sababu ya ushindani tumeanza na bei ndogo ya pamba, lakini karibu na mwisho wa msimu, bei zimeweza kuongezeka. Kwa hiyo, natoa wito, ma-*DC* waachane na hii biashara ya pamba, watoe leseni kwa watu ambao walio na viwanda, watoe leseni kwa watu ambao wanamajineri ili ushindani uweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, nimefurahi umesema bwana Quton hatapata bilioni 1.7, lakini bado ningependa ufanye utafiti zaidi je, zile zingine ambazo amelipwa, ni kweli zina thamani na ubora wa mbegu ambayo imetolewa. Kama thamani na ubora wa mbegu uliotolewa haupo, basi nakuomba hata zile zingine ambazo zimebaki na zenyewe zipunguzwe ili tusitumie pesa ya wananchi kwa ajili ya kumnufaisha mtu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haitoshi, haya mambo ya Serikali kujingiza katika biashara ya mbegu hayafai. Nilisema kwamba ni kwa nini Serikali na Bodi inaibeba *Quton*, jambo la ku-*de-lint* yaani kunyoa mbegu, siyo teknolojia ambayo ni kali sana. Watu wengi wanaweza wakafanya, lakini Bodi ya Pamba imeingia mkataba sijui ya miaka mingapi na mtu mmoja, hakuna ushindani. Kwa hiyo, hiyo ni njia, ni mkondo wa ufisadi, ni mkondo wa kula pesa ya Serikali bila sababu hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lingeangaliwa upya ili pawepo na ushindani wa watu mbalimbali, watupe mbegu nzuri, waweze kutueleza hata namna ya kuweza kupanda hizo mbegu kuliko kumbeba mtu mmoja. Serikali haiko pale kubeba mtu atajirike kwa hela za watu wanyonge. Hili jambo naomba Mheshimiwa Waziri uliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, kweli sisi sehemu ya Sukuma *land* tunategemea sana pamba, lakini tumeanza kuonekana sasa uwezekano wa alizeti katika sehemu mbalimbali tunataka mbegu ya alizeti na siku hizi vijijini tumeanza kupeleka umeme; pale kwangu umeme unakwenda, nawaona kuna vijana mbalimbali hata pale Gambasingu, wanakamua mafuta ya alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri wa kufanya hii biashara ya kukamua alizeti, yale makapi yanayobaki yanatumika pia katika kunenepesha ng'ombe, yanatumika pia katika kutoa chakula kizuri, mafuta mazuri ambayo hayana *chemical*, kwa ajili ya watu. Kwa hiyo, hii ni sehemu nyingine ambayo wagani wanaweza kuwasaidia wakulima kuhakikisha kwamba tumepata pia zao mbadala. Badala ya kutegemea mwaka hadi mwaka zao moja tu ambalo ni zao la pamba, ambalo lina matatizo kibao, lina sheria chungu mbovu na mara nyingi watu tunapunjwa mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, Mheshimiwa Waziri kila wakati nataka hela yako iongezeke na itumike vizuri na zaidi ningependa upande wa umwagiliaji tuanze kuona hekari nyingi za kumwagilia ili tuwe na uhakika wa kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. ROSE K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa kunipa fursa nitoe taarifa kwa mzungumzaji aliyepita. Mzungumzaji aliyepita jana aliliarifu Bunge kwamba Mkoa wa Simiyu hauna pamba na leo anarudia tena kusema watu wameanza kununua pamba. Sasa anazidi kuwachanganya wananchi na mimi niliyesimama hapa ni Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba pamba mbegu zile za *Quiton* hazikuota, lakini kwenye Wilaya zetu tuli-*shift* kwenda kwenye mbegu zetu za siku zote na pamba imeota vizuri kwenye maeneo mengi ikiwemo Wilaya yangu ya Meatu. Kwa hiyo, namwomba mzungumzaji, asizungumze kwa ku-*generalize,* awe *specific,* kama anaongelea Wilaya yake ya Itilima, basi aseme Wilaya ya Itilima, lakini vile vile...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hiyo ni taarifa usianze mjadala. Mheshimiwa Cheyo!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampenda sana Mheshimiwa *DC* ameniwekea maneno ambao sijaweka mimi, mimi nimesema zao linaweza likapungua kwa sababu Quiton *seeds* hizi hazikuota.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo, *whether* unaikubali taarifa au unaikataa. Basi yamekwisha pumzika. Dkt. Ishengoma!

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia hii nafasi. Kwanza naanza kwa kuwapatia pole wananchi

wa Morogoro kwa kupata mafuriko. Pili, naomba niwapatie hongera wananchi wa Iringa kwa kazi nzuri wanayoifanya kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na bajeti, tukitaka mambo ya kilimo yaende vizuri lazima tujali bajeti. Bajeti ya kilimo mara kwa mara imekuwa ndogo, imekuwa haina msimamo, tukisema kuwa kilimo, ni lini kilimo kitapewa kipaumbele namba moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wote wanategemea kilimo, bila ya kujali kilimo kuwa kipaumbele namba moja hatutafika mbali. Kila mmoja ili tuweze kupunguza umaskini hapa nchini lazima tujali kilimo. Ili vijana waweze kujiajiri na akinamama lazima tujali kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inafanya mambo mazuri sana, lakini nashauri kuwa bajeti ya kilimo iweze kuongezeka angalau kwa asilimia kumi kama nchi zilivyokubaliana. Kwa mfano, Ethiopia, hawana matatizo kwa upande wa kilimo, tulikwenda Ethiopia, asilimia 12 wanazitenga kwa kilimo. Kwa hiyo, naomba tuige kwa wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea utafiti, bila ya utafiti hakuna kilimo, kwa hiyo, lazima tutenge hela ya kutosha kwenye utafiti kusudi utafiti ufanyike wa mazao, wa mbegu, wa udongo, kusudi tuweze kupata mazao ya kutosha na kuweza kuwakomboa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afisa Ugani. Sera yetu ni kuwa kila kijiji lazima kiwe na Afisa Ugani, ili wananchi waweze kupata elimu ya kilimo, waweze kujikomboa na kilimo cha kisasa, kilimo cha biashara, kilimo chenye tija, lazima wawe na Maafisa Ugani. Vijiji vingine mpaka sasa vina Afisa Ugani mmoja vijiji vitatu au vinne, Maafisa Ugani hawana usafiri, watasafirije mpaka kwenye vijiji ili wafanye mambo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba wahitimu wote kutoka Vyuo vyote vya Kilimo, nikianza na Chuo cha *SUA* na vyuo vingine vya kilimo vidogo vidogo wahitimu wote wapewe kipaumbele cha kuajiriwa mara moja kama Wizara ya Elimu pamoja na Afya, ndiyo tutaweza kutosheleza na kuwakomboa wananchi katika umaskini kusudi waweze kujikomboa na mambo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo cha Umwagiliaji. Ni kweli na naunga mkono kilimo cha umwagiliaji ndiyo ukombozi. Mpaka sasa hivi ni asilimia 1.6 ndiyo inayotumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Naomba sana tuweze kukazania kwenye uvunaji maji, mnaona kuwa tunapata mafuriko, maji yote yanaharibika bure, lakini tungeweza kuyavuna haya maji na tuweze kumwagilia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye kilimo cha umwagiliaji pia kinahitaji wataalam, tuna shida ya wataalam ambao ni *engineers* na

*technicians*. Kwa hiyo, nashauri kuwa, tuweze kuwasomesha kwa wingi hawa *technicians* pamoja na *engineers* kusudi waweze kujikita kwenye kilimo cha umwagiliaji hasa nikisema kwenye kutengeneza *scheme* mbalimbali za kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa pembejeo. Nikisema mfumo wa pembejeo nashukuru Serikali, huu mfumo wa pembejeo mnaokuja nao ambao ni wa kukopesha hasa vikundi ni mfumo mzuri sana kwa sababu huu mfumo wa vocha uliopita ulikuwa ni mfumo ambao kwa kweli siyo mzuri sana ambao ulijawa na mambo ya rushwa. Kwa hiyo, huu mfumo utakuwa mzuri sana na utaweza kuwakomboa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ilikuwa ni Mfuko wa Pembejeo. Mfuko wa Pembejeo mpaka sasa hivi bado hatujaanzisha sawasawa na Benki ya Wananchi na huo Mfuko wa Pembejeo, naomba uongezewe hela kama tulivyoomba. Tukipata hela za kutosha wananchi wataweza kujikomboa na kuweza kukopa kwenye Mfuko huo wa Pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kilimo cha jembe la mkono; kwa kweli kinaumiza sana na kwa hiyo naomba tuweze kujikita sana kwa wananchi kujiunga kwenye vikundi vikundi. Wakijiunga kwenye vikundi watapata nguvu ya kukopa matrekta. Kwa hiyo, nawashauri wananchi tujiunge kwenye vikundi vikundi tuweze kukopa matrekta. Hata hivyo, naomba Serikali na yenyewe iangalie jambo hili kwa macho mawili, jinsi ya kuagiza hayo matrekta ili tuweze kupata matrekta nafuu kusudi wananchi waweze kupata matrekta na waweze kuzidisha hekari nyingi za kilimo na tuweze kuvuna kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamalizia, nashukuru sana kusikia kinu cha Iringa cha mazao mchanganyiko kitaanza mwaka huu. Kinu cha mazao mchanganyiko Iringa kitakuwa mkombozi kwa wananchi wa Iringa. Kwa hiyo, nawambia wananchi wa Iringa ambao wamezoea kulima mahindi, kuwa sasa hivi itakuwa mkombozi, hamtapata shida ya soko na itakuwa ni mkombozi wa kinu hiki. Naomba sana hela zilizotengwa ziweze kwenda kwa makini.

Mheshimwia Mwenyekiti, jambo lingine kilimo cha Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)*. Serikali tunashukuru tunafanya mambo vizuri, mipango ni mizuri, tukikaa tunapanga vizuri, lakini naomba hela zote tunazozitenga ziweze kutiririka na…

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana. Mheshimiwa Abdusalam na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mariam Kasembe.

**MHE. ABDULSALAAM S. AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niongee kuhusu Wizara ya Kilimo. Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kuwapa pole wale wote walioathirika na mafuriko katika nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naunga mkono Wajumbe wa Kamati waliotangulia kuhusu Wizara ya Kilimo kuongezewa pesa na wapate pesa kwa wakati muafaka, kwani kuchelewa kwa pesa inaathiri sana Wizara kufanya mambo yake ambayo imejipangia kwa bajeti inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua fursa hii kumpa pole Naibu Waziri kwa vijembe alivyopata kwa baadhi ya Wabunge, kwa kweli naona kama wanamwonea ni mara ya kwanza hata miezi mitatu haijafika kwenye kazi hii. Naamini atashirikiana na wenzake ili tupate maendeleo katika Wizara ya Kilimo. Nampa pole sana Mheshimiwa ila kaza buti.

Mheshimwia Mwenyekiti, pia naipongeza Wizara kwa kuunda Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, suala la umwagiliaji hasa katika Halmashauri zetu ni sehemu nzuri kwa viongozi wa Halmashauri kula pesa za Serikali za Walipa kodi. Miradi mingi inakufa na haifanyiki inavyopaswa, kwa hiyo, kwa muda mfupi miradi inatengenezwa na pesa zinaliwa na miradi ya maji ya umwagiliaji inakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda moja kwa moja kwenye suala la wakulima wa miwa. Ndugu yangu Mangungu amesema sukari iagizwe kutoka nje kwa wingi ili ikidhi mahitaji ya wananchi kwa suala la sukari. Mimi kidogo napinga wakati kwa upande wa pili Serikali izuie *juice* kutoka nje ili wananchi wake wavune mazao yao ya matunda wafanye *juice*, namshangaa Mheshimiwa Mangungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 5 Juni, Kampuni ya Illovo ambao wanaendesha Kiwanda cha Sukari, Wilaya ya Kilombero na Kilosa waliwaandikia barua Wenyeviti wa Vyama vya Wakulima Wadogo wa Miwa Bonde la Luhembe na Bonde la Kilombero. Katika misimu ya miwa wakulima wa miwa huwa wanaachiwa asilimia kumi ya pesa yao ambayo hawalipwi na wanalipwa baada ya msimu ule kwisha, lakini zile asilimia kumi wameambiwa hawatalipwa kwa sababu sukari imejaa kwenye *godown* lao soko hakuna. Kwa hiyo, itawaathiri wakulima wadogo wa miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine wameambiwa kwamba mgao wa miwa kule kiwandani utapunguzwa, wata-*base* kwenye kuvuna miwa yao, ambayo pia itakuwa athari kubwa kwa wakulima wadogo wa miwa wa bonde

la Wilaya ya Kilosa na Kilombero pia kwa ujumla. Pia wamesema bei ya ununuzi wa miwa itapungua tena msimu huu, *either* wapunguze au hawataongeza tena wakati gharama za uzalishaji wa miwa zimeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine wamesema mgao wa kupeleka miwa kiwandani utapunguzwa kutokana na wingi wa miwa yao wenyewe, kwa hiyo wanasema watavuna miwa yao kwanza *and then* watawafikiria wakulima wadogo ambao wamepata gharama kubwa ya kulima miwa. Kwa hiyo, Serikali inawahamasisha wananchi kulima miwa ili kujikwamua katika uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo ni la kujiuliza ni kwamba, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuunda kikosi kazi, sasa wakulima wa miwa kuanzia sasa hivi watakaa katika msimamo gani? Hali ya maisha imekuwa ngumu, wamekopa hela benki na wana madai ya wanafunzi wao waliopo sekondari na shule tofauti tofauti, kwa hiyo naona wamekwama kwa hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nashangaa kupitia Bodi ya Sukari, kuna sheria ambayo imesema kwamba hutaweza kufunga Kiwanda cha Sukari katika eneo lenye mzunguko wa kilometa 50. Kuna baadhi wa wakulima wana uwezo wa kununua viwanda vidogo na hata baadhi ya vikundi wako tayari kununua viwanda vidogo ili kufunga na kuzalisha sukari kwa ajili ya wakulima hao wadogo wanaolima miwa katika sehemu husika. Naomba Wizara ifikirie suala hili ili iweze kuwasaidia wakulima wadogo kuwawezesha kufunga Viwanda vya Sukari ili waweze kukamua sukari wenyewe na kukidhi mahitaji ya sukari katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini sukari ya nje *either* inaingia kihalali au kiharamu ina athiri lakini pia bei ya sukari nayo iko juu kutokana na kodi kuwa nyingi kwa upande wa uzalishaji wa sukari. Naamini Serikali ikijipanga vizuri kuweza kuzuia mianya ya sukari inayoingia kiholela inaweza kujitahidi sukari ikapatikana kwa wingi na naamini wazalishaji wa Viwanda vya Sukari nchini wanaweza kukidhi mahitaji sukari ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nashukuru sana kwa nafasi hii na Mungu akujalie sana. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya mwisho ya kuchangia jioni katika Wizara hii ya Kilimo. Naomba nianze kwanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa jinsi walivyoshughulikia tatizo la wafanyabiashara wanunuzi wa zao la korosho katika Wilaya yangu ya Masasi na Nanyumbu. Kwa kweli wametoa ushirikiano wa karibu sana kwa sababu wafanyabiashara hawa hawakupata fursa ya kununua mazao mchanganyiko katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema ahsanteni sana na naomba jinsi mlivyoshughulikia suala la wafanyabiashara hawa, wakapata fursa ya kuweza kununua korosho katika msimu huu, naomba mjipange vizuri mtusaidie ununuzi wa zao la korosho msimu utakapofika, watu wapate haki, wakulima wetu wauze zao la korosho, wapate haki yao bila matatizo ya aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kwa kuwashukuru kwa sababu gani? Halmashauri zetu za Wilaya ya Masasi na Mji Masasi tegemeo letu kubwa ni kupata ushuru katika mazao. Hasa ukiangalia kwamba, bajeti tunazopitisha hapa za maendeleo kama wengi walivyozungumza hapa kwamba haziendi kwa wakati au haziendi kabisa au zinaenda kiasi kidogo. Sasa sisi ili Halmashauri zetu ziende tunapata ushuru katika mazao mbalimbali na zinasaidia sana katika kuendesha shughuli zetu katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nataka nizungumzie kwamba mvua zinazoendelea katika nchi yetu Wilaya ya Masasi ni mojawapo ambayo tumepata athari kubwa sana; nyumba za watu zimeanguka, mashamba yamefunikwa na maji, barabara hazipitiki. Hivi ninavyozungumza vyakula vimepanda bei kwa sababu ya miundombinu mibovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachowaomba, kwa sababu athari hii imetokea karibu Wilaya nzima, watu wengine hawana tegemeo kabisa la kuweza kuvuna, naomba mpeleke wataalam mapema ili waweze wakafanya tathimini kutakuwa na upungufu wa chakula kiasi gani, ili wale watakaobainika kwamba wana upungufu mkubwa wa chakula, basi chakula kiende kwa wakati kuwasaidia watu hawa ambao sasa hivi hawana makazi na mashamba yao yamejaa maji hawataraji kuvuna kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni malipo ya korosho kipindi cha msimu kwa wakulima. Wakulima wetu wamekuwa wakiuza zao la korosho kupitia stakabadhi ghalani. Kama mnavyofahamu, stakabadhi ghalani mkulima akienda kuuza korosho yake hapati hela yake yote, hela nyingine inategemea alipwe baada ya korosho zitakaouzwa kule bandarini. Hata hivyo, kinachotokea ni kwamba, Vyama vyetu wakipeleka korosho zikishauzwa, wanachelewa sana kurudi kuwalipa wakulima wetu yale malipo yao ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza kama umeshafanya biashara, kinachokufunga kurudi mara moja ukampatia mkulima haki yake ni kitu gani? Ndiyo maana unakuta watu wengi Wabunge wenzangu wamelalamikia mfumo huu wa stakabadhi ghalani, lakini nafikiri kama haya makosa ninayoyasema yatafanyiwa marekebisho, mkulima akakopesha korosho zake, akalipwa kwa wakati, nafikiri malalamiko yatapungua.

Nakuamini sana Mheshimiwa Waziri, nakuamini Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaomba mtusaidie, kila bajeti mnatusikia tunavyopiga kelele kuhusu zao la korosho. Ifike wakati bajeti itakayokuja mwaka kesho, tuwe tunawapongeza kwamba wakulima wetu msimu uliopita wameuza zao lao la korosho bila tatizo la aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile niwaombe wakulima wenzangu wa Mkoa wa Mtwara, Mkoa wa Lindi na maeneo yote ambayo kwa kweli ndiyo yalikuwa yanaeleweka kwamba tunalima zao la korosho. Nataka niwajulishe wapiga kura wangu kwamba, sasa hivi kuna kasi kubwa sana ya mikoa mingine kuanza kulima zao hili la korosho.

Rai yangu nawaomba kwamba mikorosho yetu imeshakuwa sasa ya karne, tuanze na sisi kuandaa maeneo ili tuanze kupanda mikorosho mipya kwa sababu baada ya muda inawezekana, hiki tunachovunia kwamba Mtwara na Lindi tunalima korosho kwa wingi nafasi hii inaweza ikachukuliwa na mikoa mingine ambayo sasa hivi wameanza kulima korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wanakuwa na utaratibu katika Vyama vyetu. Kuna wakulima wengine wanakuwa na imani na Vyama vyetu na Serikali yetu. Wanakwenda kukopesha korosho hawachukui hata senti tano. Ninachoomba ni kwamba, korosho zikishauzwa basi wakirudi wale ambao wamejitolea kabisa kwamba, mimi korosho yangu naipeleka sitaki kuchukua hata senti tano, korosho zikishauzwa waje walipwe pesa zao zote, haina sababu tena ya kuwalipa nusunusu kwa sababu wao Vyama walikuwa wameshaviamini na wao tunawategemea kwamba wakiuza, basi mwananchi atapata hela yake yote ili aweze kutatua matatizo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la korosho linaendana na suala la pembejeo. Ninaviomba Vyama Vikuu vya Ushirika vifuatilie kwa karibu upatikanaji wa pembejeo kutoka kwenye Mfuko wa Wakulima, kwa sababu korosho bila pembejeo kwa kweli tunajidanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kuna wageni wa Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kutoka Wilaya ya Bunda ambao ni ndugu Samson Kisonginda na ndugu Kitabunda Bomboi. Karibuni sana Bungeni na Ester Bulaya anawasalimia vile vile. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu humu ndani wamekwisha.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia maandishi nichangie hotuba ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Wizara hii ni muhimu kwa ustawi wa Taifa kutokana na ukweli kwamba mbali na kuzalisha chakula ni mwajiri wa karibu ya Watanzania zaidi ya asilimia 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoshauri mwaka jana niendelee kusisitiza kuwa ipo haja ya Serikali kupanua miundombinu ya kuhifadhi mazao (chakula) kwa kuwa na chakula cha kutosha miaka mingi zaidi. Pili, ni muhimu miundombinu hiyo ikajengwa kimkakati ikilenga maeneo ya kuuza nje na mahitaji ya ndani sambamba na hifadhi.

Nakumbushia haja ya kuwa na miradi mikubwa ya kuzalisha chakula sehemu zote za chakula pamoja na mradi wa *SAGCOT* eneo la Magharibi na kanda ya Ziwa lazima kuwepo mradi wa kimkakati ili pamoja na kutengeneza ajira tupunguze gharama ya kusafirisha chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na dalili nzuri za hifadhi ya chakula na mavuno yajayo, nashauri Serikali kuhami wakulima. Serikali kwa muda izuie kwa kutumia ushuru kwa waagizaji wa chakula (mchele & mahindi) ambacho kipo nchini kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kujitoa katika biashara, ni wajibu wake kubeba jukumu la kuwaongoza wakulima kutafuta masoko. Masoko nje ya nchi yanahitaji weledi na nguvu hali ambayo wafanyabiashara wetu hawana. Na wale wenye uwezo huo pindi wakijasiria fursa hii faida wapatayo hawatapeleka kwa wazalishaji (wakulima wadogo) Serikali izungumze na *WFP*, Shirika la Wakimbizi na nchi jirani ili kupanga bei nzuri na masoko ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia mavuno makubwa mwaka huu muhimu kurejea chanzo cha mafanikio pamoja na hali ya hewa nzuri, uwepo wa zana za kilimo na pembejeo zimechangia mafanikio haya. Ili tuendelee kuzalisha kwa tija ipo haja ya kuwekeza katika kuwa na wataalamu na kuwatumia. Naishauri Serikali kuhakikisha kila kijiji na kila kata inao wataalamu wa kilimo, mifugo na uvuvi pale inapobidi. Serikali itumie nafuu iliyotokana na mafanikio katika kilimo kuhakikisha vijana wote wenye fani nilizotaja awali wameajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja kuhakikisha kuwa wataalamu wa kilimo, mifugo na uvuvi wanashirikiana na wananchi katika kilimo na uzalishaji wa kisasa. Ukipitia mahitaji na manunuzi ya vyakula vinavyohitajika katika sekta za madini na gesi nchini ni dhahiri kuwa utaalamu unahitajika katika uzalishaji wa mboga mboga, matunda, nyama, mayai na maziwa. Yote haya yanawezekana iwapo wataalamu wataajiriwa na kufanya kazi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama Taifa maendeleo ya wananchi wake yanategemea ushirika kwa kuzingatia historia ya ushirika nchini. Hatua tuliyofikia ni lazima Serikali ibuni mipango ya kuingilia uendeshaji wa ushirika huu. Haitoshi Serikali kukaa kando ikiangalia ubadhirifu ukifanyika katika chama cha Ushirika. Ikumbukwe kuwa kwa vipindi tofauti Serikali imedhamini au kuokoa baadhi ya vyama vya ushirika visife. Lakini pia ufanisi wa vyama vya ushirika ni nafuu na mafanikio kwa Serikali kwani hiyo maana yake ni kuondolea kwa umaskini katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ichukue jukumu la kushinikiza vyama vya ushirika kurekebisha katiba zake ili wanachama/watendaji wanaopewa dhamana ya uongozi wawe watu wenye weledi na uadilifu unaokidhi matakwa ya wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vipindi tofauti nimewasiliana na Serikali juu ya njia za kupambana na ugonjwa wa unyanjano/mnyauko wa migomba. Ugonjwa huu umepunguza uzalishaji wa ndizi Mkoani Kagera hali ambayo imechochea uwepo wa njaa lakini pia kupunguza kipato kwani ndizi ni zao la biashara sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kuishauri Serikali juu ya mbinu rahisi ya kupambana na ugonjwa huu moja, inahitajika timu ya Kitaifa kusimamia vikosi vya Wilaya, tarafa, kata mpaka vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, moja ya majukumu ya timu hii ni kuhakikisha wananchi wanahimizwa kupanda mazao ya kukomaa kwa muda mfupi. Katika kipindi cha kukomaa operasheni ya kufyeka na kuharibu migomba iliyodhurika ifanyike. Serikali kwa kutumia hifadhi za mazao iwauzie wananchi hao nafaka kwa bei pungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu timu ya Taifa ifuatilie utekelezaji wa mikakati ya udhibiti wa ugonjwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Kilimo hapa nchini hakiwezi kuwa cha tija wala kilimo cha kibiashara kama bado wakulima wengi watategemea kilimo cha mvua, wakulima zaidi ya 70 % wanategemea kulima na jembe la mkono na baadhi kutegemea kilimo cha kukokotwa na ng'ombe. Ni jukumu la Serikali kutenga fedha kwa ajili ya

kuchimba visima vya maji na kunakuwepo na mafuniko ya maji ya mvua. Iangaliwe ni kwa jinsi gani wanaweza kukinga/kuhifadhi maji hayo kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya kilimo pia iweze kupima udongo sehemu za wakulima na kuona ni aina gani ya mazao yanayokubalika katika ardhi husika na wakulima hao wapewe elimu na wapate mbegu bora na za muda mfupi ili waweze kulima kibiashara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwa sasa hivi soko kubwa duniani na vyakula vinavyouzwa kwa bei ya juu sana ni zile *organic,* hili linabidi liangaliwe huko tuendako watu wengi watakuwa hawatumii tena *GM* tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kuwasaidia wakulima waweze kulima kilimo cha kisasa ni lazima wawepo maafisa ugani wa kutosha katika kila Wilaya zote za wakulima. Je, Serikali kwa kipindi hiki ni kwa kiasi gani wameweza kuzalisha maafisa hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, panakuwepo na tatizo la upatikanaji wa mbegu safi na watu wadanganyifu wanakuwa wakisambaza mbegu bandia za mahindi huko Moshi na kupelekea mbegu hizo kutokuota na kuwapatia wakulima hasara. Je, mpaka sasa hivi Serikali ina mikakati gani ya kuzalisha mbegu za kutosha ili tuepukane na kuagiza mbegu kutoka nje ya Nchi? Jeshi letu (JKT) wanakuwa wakizalisha mbegu kwanini wasiwezeshwe ili wazalishe mbegu hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Moshi kuna baadhi ya wakulima ilibidi mahindi yao yang'olewe yale yote yaliyogeuza majani na kuwa rangi ya njano walielezwa mahindi yale yakikua na kuvunwa na kumfikia mlaji ni sumu na yanaleta kansa? Serikali imewachukulia hatua gani wasambazaji wa mbegu hizo hatari au Serikali imechukua hatua gani kupitia maduka yote ya pembejeo na kuhakikisha mbegu hizo hazipo kwenye soko?

**MHE. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Kilimo wakiongozwa na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo ikumbuke kuwa maombi ya Halmashauri na Jimbo la Hanang kupitia kwa Mbunge wao yamedumu kwa miaka saba bila ahadi ya Wizara kutekeleza ujenzi wa Bwawa la Gidahababieg.

Ninaomba Mheshimiwa Waziri awahakikishie wananchi wa Hanang waliosubiri kwa muda wote utekelezaji wa Bwawa hili kwa ajili ya umwagiliaji kutokana na maji yanayopotea kila mwaka kutoka Mlima Hanang.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru kama Waziri atatoa tamko wakati wa majumuisho ya hoja yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kina fursa ya kuwa sekta kiongozi katika kazi ya kuinua uchumi wa nchi na kuboresha maisha ya wananchi. Ili kufikia azma hiyo, mkazo unapaswa kuwekwa katika kushughulikia mnyororo mzima kuanzisha upangaji, upandaji, uvunaji, uhifadhi, usindikaji, usafirishaji, usambazaji, uuzaji, utumiaji, na uthamini katika maeneo yote Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mwelekeo mbovu wa kisera kwa upande wa Serikali na mtazamo finyu hususan kwa vijana juu ya suala la kilimo katika Jiji la Dar es Salaam. Upande wa Serikali kupitia maafisa wa kilimo na miradi ya Halmashauri wana mwelekeo wa kilimo kuwa shughuli ya maeneo ya pembezoni ya Dar es Salaam ambayo hayajapimwa bado na yana mashamba.

Kilimo, ukiondoa cha bustani au cha maghorofani kwa ujumla kinaonekana kuwa si kazi inayopaswa kufanywa na walio katika maeneo yaliyopimwa. Mwelekeo na mtizamo huo unapaswa kubadilika kuwezesha kilimo kuchangia katika ajira kwenye Jiji la Dar es Salaam ambalo linaongoza kwa tatizo la ukosefu na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, izingatiwe kwamba Dar es Salaam yenye wakazi millioni 4.3 ambao ni asilimia zaidi ya kumi (10%) ya wananchi wote wa Tanganyika (Tanzania Bara). Hivyo kuachwa nyuma na pembezoni kwenye sekta ya kilimo ni kuacha pembeni mtaji wa watu wengi hasa vijana waliokimbia toka vijijini na kukutana na uhaba wa ajira Jijini Dar es Salaam. Vijana hao ndiyo ambao kwa sehemu kubwa badala ya kuwa katika uzalishaji wako katika uchuuzi wakijulikana kuwa wamachinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwaacha ni kukosa mtaji wa kada yenye elimu iwe ya msingi, sekondari, vyuo na vyuo vikuu ambao wameondoka mjini. Ni kukosa fursa pia ya nguvu kazi yenye uzoefu wa kilimo wakati wahusika walipokuwa vijijini, lakini pia wenye uzoefu wa mazingira ya mjini. Hivyo kunapaswa kuwe na mkakati maalum wenye kuhusisha, kuhamasisha vijana na

kuwawezesha kureja kijijni ama kuwa na mfumo wa mashamba ya eneo jirani ya Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ifahamike sio lazima kila mtu alime; wapo ambao wanaweza kutoa huduma na kufanya kazi nyingine katika mnyororo wa kilimo. Mfano kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuwa na viwanda vidogovidogo vya usindikaji, kushirikiana na Wizara ya fedha ili kuendesha huduma za kifedha, kushirikiana na Wizara ya Sayansi ili kuwe na msukumo juu ya kilimo mtandao na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari kushirikiana na Wizara ya Kilimo miradi yake, taasisi zake, vyuo vyake na wadau wengine kuandaa na kutekeleza mpango huo wa "Kilimo Kwanza kwa Vijana wa Dar Es Salaam" PDB/*BRN, ASDP, EEAAPP, PHRD, DASIP, AFSP, SAGCPT, CRMP, ASA, FACF, PIOF*, zichukue pendekezo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kuhusu ufisadi katika miradi ya kilimo hasa kwenye pembejeo yanadhihirisha alichowahi kusema Mwalimu Nyerere kwamba rushwa ni adui mkubwa wakati wa amani kuliko vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo pamoja na hali hiyo Serikali haionyeshi mwelekeo wa kudhibiti ufisadi kwenye sekta ya kilimo. Wizara ya kilimo iwasilishe Bungeni orodha ya Makampuni yote yaliyonufaika na ieleze hatua ambazo *CAG* amechukua juu ya ukaguzi alioufanya. Maelezo yatolewe Bungeni juu ya sababu za baadhi ya Makampuni kutokuwasilisha kwa *CAG* nyaraka kwa ajili ya ukaguzi?

Pia kasi ya ushughulikiaji wa ufisadi kwenye pembejeo na katika utekelezaji utaratibu wa stakabadhi ghalani, utaratibu mpya wa kuweka dhamana na mikopo kutolewa na taarifa za fedha nao umekwama. Je, Serikali inamhakikishia vipi mwananchi aliyeweka asilimia 20 na hajapata mkopo kwamba fedha zote zitakuwa salama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika umeporomoka kutokana na udhaifu na ufisadi. Hivyo pamoja na kutaka Wizara ya kilimo kueleza kwa majina wahusika wa kukiuka sheria waliorejewa kwenye hali ya ushirika kipengele 2.3. Aidha katika kupanua kiwango cha huduma za kifedha jumuishi nchini (*Financial inclusion*) ikiwa ni sehemu ya kuziimarisha *SACCOS* katika kufanya hivyo, ufuatiliaji ufanyike kwenye *SACCOS* za Jimbo la Ubungo na nipewe taarifa ya matokeo ya utafiti huo kwa ajili ya ufuatiliaji wa kuwezesha *SACCOS* hizo ziweze kuendeshwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri imeeleza kwamba Serikali imeanzisha kambi ya mafunzo ya kilimo kwa vijana. Hata hivyo ni jambo lenye kuacha maswali kwamba kambi hiyo imezinduliwa na Rais lakini imetoa mafunzo kwa vijana 50 tu. Wizara inapaswa kuwa na mpango wa mafunzo kwa makundi ya vijana wengi zaidi katika maeneo mbalimbali. Aidha mkakati huo uhusishe kutumia majengo ya shule wakati wa likizo za wanafunzi wa msingi na sekondari. Wizara itoe taarifa juu ya utekelezaji wa Azimio la Bunge kupitia hoja ya Dkt. Kigwangala, marekebisho ya Esther Bulaya na mapendekezo yangu juu ya mifuko ya vijana, uwezeshaji na utekelezaji wa sheria ya kuhamasisha ajira. Kipaumbele kiwe kuwezesha vijana kupata ardhi iwe dhamana.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa pole Mheshimiwa Waziri kwa majukumu.

Nimesikiliza kwa makini hotuba yako lakini nimeshitushwa sana na dhamira ya Serikali juu ya kuiwezesha Mikoa mikame kama Dodoma ambayo tumekuwa tukiomba chakula kila mwaka lakini tunazo fursa kadhaa za kuwezesha umwagiliaji kama Wilaya ya Bahi. Kwa bahati nzuri wewe binafsi na Naibu Waziri wako wakati huo Mheshimiwa Malima mlifika Bahi na mkajionea hali halisi ya kilimo cha umwagiliaji na fursa zilizopo Bahi, lakini hazijaendelezwa. Nilidhani kwa kujionea ninyi mngeweza kuikumbuka Wilaya ya Bahi japo hata kwa mradi mmoja tu wa Matokeo Makubwa Sasa na siyo Mbarali, Mbarali, Mbarali mara 15 na Wilaya zingine kadhaa mlizozipendelea kwa kuzipa miradi zaidi ya 4 hadi 5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani hii hali ya Dodoma kuisaidia kama Mikoa mingine kuna dhambi gani? Au Serikali imeona sisi Dodoma na hususan Bahi ni stahili yetu kwa huu ukame na tuendelee kuomba chakula? Kimsingi nimesikitishwa na kushangazwa sana lakini najua kwa barua hii angalau utafikiria Bahi japo mradi mmoja ambayo uliiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini utasikiliza hiki kilio change.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechoshwa na hotuba nzuri na takwimu nyingi ambazo hazisaidii kubadili hali ya maisha ya Watanzania ambao wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, skimu za umwagiliaji Mkoa wa Katavi zimekuwepo katika hotuba zote katika awamu hii ya nne lakini skimu ambazo hazikamiliki, tatizo ni nini? Hivi Wizara yako haifahamu kama Mkoa wa Katavi unazalisha Mpunga kuliko Dodoma lakini Skimu za umwagiliaji

zitakazowezeshwa kuongeza thamani zao la mpunga kupitia *Program* ya *PHRD* hakuna hata Skimu moja Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vigezo gani vinatumika kuifikiria Bahi ukaacha Mwamkulu Mpanda au Skimu ya Mwamapuli (Mlele)? Naomba kujua ni kwa nini imekuwa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kujua ni kwa nini hakuna kituo cha utafiti wa michikichi au *program* ya kuendeleza zao hili hususan Mkoa wa Kigoma ambapo zao hili hustawi sana lakini hakuna mkakati wowote wa muda mfupi au mrefu wa kuendeleza zao hili ambalo linaendelea kupoteza umaarufu wake nchini hata katika uzalishaji wa kimataifa wakati Malyasia inazalisha zaidi ya tani milioni 40 Tanzania milioni 2 hivi. Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha zaidi zao hili ni lazima kuwepo na chuo cha utafiti kwa zao hili na kuleta mbegu bora ili kuongeza uzalishaji ni lazima Wizara itoe kipaumbele cha makusudi kwa zao hili la michikichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana kwa utendaji wa Wizara hii hususan kuwakopa wakulima *(NFRA)* na kushindwa kuwalipa kwa wakati huku mkijua wakulima hawa wanategemea mauzo ya mazo yao ili kukidhi mahitaji ya maisha kwa familia zao na kuendeleza kilimo. Tabia hii ikome, kama *NFRA* haina pesa isichukue mazao ya wananchi na waruhusiwe kuuza katika soko ndani au nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nadhani kauli ya *BRN* ni tunu katika masikio isiyotekelezeka kwa sababu hakuna fedha. Unapotaja matokeo makubwa wakati hauna mtaji (fedha), poleni sana.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ushauri wangu kuhusu malalamiko ya wakulima mbalimbali walioonesha kutoridhishwa na utaratibu wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wa Serikali yetu kuona haja ya kufanya marejeo kwa kuwasikiliza wakulima kuhusu haja ya kuendelea na mpango huu au kuacha, kwani nia nzuri ya Serikali kuhusiana na mpango huu inawezekana kuleta tija iliyotarajiwa na baada yake kuzaa malalamiko makubwa. Hivyo ni ushauri wangu kuupitia upya mpango huu, aidha kuufanyia marekebisho makubwa hasa kuangalia eneo la usimamizi wa jambo hili na kuona kasoro zote zilizojitokeza zinaondolewa na kuleta tija kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu benki ya *TIB*; naomba Serikali iongeze mtaji benki hii ili lengo la kuwasaidia wakulima kupitia dirisha la kilimo liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Mheshimiwa Rais juu ya kuipatia benki hii mtaji wa bilioni 500 bado halijafikiwa hata nusu, jambo hili linazorotesha kabisa ufanisi wa kiutendaji wa benki hii hivyo wakulima wetu kukosa mikopo ya kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umwagiliaji maji; ni dhahiri kwamba ili nchi yetu ifikie malengo ya kujitosheleza kwa chakula na ziada ya kuuza nje, ni lazima kilimo cha umwagiliaji kipewe msukumo maalum. Ni dhahiri kilimo cha kutegemea mvua ni cha kubahatisha na katika miaka hii mabadiliko ya hali ya hewa yamekuwa ni kikwazo kwa wakulima wetu, hivyo hatuna budi kujielekeza katika kilimo cha umwagiliaji, naomba Serikali itueleze ni juhudi gani inachukua kuhusu umwagiliaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uingizaji wa sukari ya nje hapa nchini ni jambo linaloeleweka kwamba sukari inayozalishwa hapa nchini haitoshelezi mahitaji halisi, hivyo Serikali hulazimika kutoa vibali kwa wafanyabiashara kuingiza wastani wa tani 100,000 ili kukidhi pengo hilo. Hilo si jambo baya, tatizo ni utaratibu unaotumika. Kuna taarifa kwamba Bodi ya Sukari hutoa vibali hivi ovyo na kuvigawa kwa watu hata wasiokuwa na leseni ya biashara, na wao huviuza kwa bei ya faida kwa wenye uwezo mkubwa na hivyo kuifanya bidhaa hiyo kupanda bei sana.

Nashauri Serikali jukumu hili la utaratibu wa uagizaji sukari lipelekwe Wizara ya Biashara na Viwanda kwani wao ndio wanajua ni nani mfanyabiashara halisi na siyo hao madalali wa vibali vya sukari. Pia uangalizi uwepo, kudhibiti idadi halisi ya sukari inayotakiwa ili isiingizwe zaidi na kuleta shida kwa Viwanda vyetu kushindwa kuuza sukari ya hapa nchini.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa ubora wa mbegu: Ni vema wananchi/wakulima wakapewa elimu ya kutosha kuhusiana na masuala ya mbegu mpya ili wawe na mapokeo mazuri na utayari wa kutumia mbegu hizo. Ni vema utafiti wa kina ukafanywa kwa kuhusisha mbegu mpya na udongo na upatikanaji wa mvua wa eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wafidiwe kutokana na hasara ambazo wamekuwa wakipata kutokana na pembejeo wanazopelekewa

ambazo si sahihi ukilinganisha na maeneo wanayotoka hasa katika suala la mbegu zisizokidhi viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni yanayofanya udanganyifu ni vema yakachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufutiwa leseni na kunyimwa dhamana ya usambazaji wa pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pembejeo za kilimo na mifugo napendekeza kwamba ni vema sasa jukumu la pembejeo za kilimo na mifugo lipewe na lipelekwe moja kwa moja kwa Wakurugenzi na Vijiji, yaani Serikali ya Kijiji, kwa sababu kumekuwa na ubadhilifu wa pembejeo hizo kuanzia Wizarani mpaka kwa mawakala. Kwa mfano, ni hivi karibuni katika Mkoa wa Katavi kumebainika kulikuwa na udanganyifu wa vocha zilizobainika kutoka Mkoa wa Kigoma, hivyo basi nashauri jukumu hilo wapewe vijiji kwani ndio wanaojua watu wao wa kukopeshwa mbolea na mbegu kupitia Mkurugenzi na wakati wa kuuza vijiji vikate fedha hizo na wale wenye vyama ama ushirika/*SACCOS* ndizo zikopeshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu stakabadhi ghalani, Serikali imekuwa ikiwakopa wananchi mazao yao, hii si haki kwani wananchi ndiyo wanatakiwa waikope Serikali na si Serikali kuwakopa wananchi. Hivyo basi ni vema Serikali ikawalipa wananchi kwa wakati ili waweze kujikimu kutokana na ugumu wa maisha yaliyopo hivi sasa.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia suala la miradi ya *SAGCOT* na suala la kupanda na kushuka kwa bei za mazao ya biashara katika soko la dunia, na kuanzisha mfuko maalum wa kufidia bei za mazao ya biashara (*Price Stabilization Fund*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuporomoka kwa bei ya mazao ya biashara katika soko la dunia limekuwa likitokea karibu kila mwaka na hivyo kuathiri juhudi kubwa zinazofanywa na wakulima humu Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuanzishwa kwa mfuko maalum, wa kufidia bei za mazao ya biashara lilizungumziwa kwa mara ya kwanza katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya *budget* yake ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeonyesha nia nzuri na njema, na ni jambo jema sana na likianzishwa litaleta unafuu mkubwa kwa wakulima, na hivyo kuendelea kuwapa moyo katika kazi ngumu hii ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Serikali ni utekelezaji wa haraka tangu suala la mfuko huu lizungumziwe kwa mara ya kwanza sasa leo ni mwaka wa tatu bado Serikali iko kwenye *logistics* tu. *By the time* mpango wenyewe

unakuja kuanza, unaweza kukuta ni zaidi ya miaka 10 kuanzia sasa. Je hii au utaratibu huu ni kweli utaleta *BRN*? Ushauri wangu ni kwamba mpango huu ni mzuri na uchukuliwe kwa umuhimu wake na Serikali ijitahidi kuhakikisha inaanzisha mfuko huu maalum haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi *SAGCOT*: Mara hii nazungumzia suala la *SAGCOT*, ni zaidi ya mara tatu. Ni kwa nini Mkoa wa Lindi na Mtwara imetolewa katika mradi huu na *SAGCOT*? Ni kweli Mikoa hiyo haina maeneo au mabonde mazuri na makubwa ya kilimo? Je Serikali isingeona umuhimu wa kuiingiza Mikoa hii katika miradi hii ya *SAGCOT* hata kama Mikoa hii si miongoni mwa Mikoa hii, katika mradi huu ili iweze kuwa kichocheo cha kilimo kikubwa katika Mikoa hiyo? Lakini ikumbukwe kwamba Mikoa hiyo ni miongoni mwa Mikoa inayozalisha mazao ya biashara ya korosho, na ufuta kwa wingi sana, lakini pia mazao ya chakula kama vile mtama, muhogo, mahindi, mbaazi, mpunga, nakadhalika. Ninaiomba Serikali ifikirie kuingiza Mikoa hiyo katika miradi hiyo ya *SAGCOT* kwa makusudi kabisa ili iweze *ku accelerate* uchumi wa Mikoa hiyo kupitia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninatoa pole zangu kwa wananchi wa Wilaya Rufiji hasa kutokana na mafuriko makubwa yanayoendelea katika bonde la Mto Rufiji. Mafuriko haya yamesababisha si tu kuzama kwa mazao hasa mpunga na mahindi bali pia kuleta maafa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuriko haya ambayo yanaongezeka kila siku hadi leo hii yamesababisha wananchi wengi wanaolima maeneo ya mabondeni, mazao yao kuzama kwenye maji na hivyo kuwafanya wateseke na njaa kutokana na hali hiyo ni vizuri sasa kwa Serikali kwenda kuona hali halisi na kuona ni kwa namna gani inaweza kuwasaidia wananchi hao katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu Rufiji mafuriko yatokeapo huleta neema kubwa sana mara baada ya kumalizika. Hii inatokana na ardhi hiyo kurutubishwa upya kutokana "*deposition na silt*" iliyosababishwa na mafuriko hayo. Kutokana na hali hiyo basi ninaiomba Wizara kuanzia sasa wawaandalie wahanga hawa wa mafuriko wa Wilaya ya Rufiji mbegu za mahindi, kunde, na aina zingine za mazao ya muda mfupi. Kwa kufanya hivyo kutasababisha wahanga hao kuweza kujitegemea baada ya muda mfupi. Mbegu hizi zipelekwe sasa kwani zikichelewa zitasababisha kutotumika na lengo la kuwasaidia wananchi hao kutofikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa zao la korosho ni miaka mitatu sasa imepita ambayo wakulima wa zao hili kutofanikiwa/kukatishwa tamaa na mwenendo wa ununuzi. Katika kipindi hiki mfumo wa stakabadhi ghalani ambao ni mzuri kwa wakulima hao uliingiliwa na changamoto nyingi. Wakulima wamekuwa hawajui ni nani anayenunua mazao yao na kuwafanya wauze korosho hizo kwa walanguzi na kwa bei ya chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ieleze bayana katika bajeti hii ni njia ipi itakayotumika kununua korosho kwa msimu huu ambao kuna dalili zote za ongezeko la zao hilo katika Jimbo la Kibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli mwaka jana Rais alizindua kambi ya maafa katika kijiji cha Mkonga. Lengo kuu la kuanzishwa kwa kambi hii ni kuwaandaa vijana waliomaliza elimu ya msingi na hata sekondari kwa kuwapatia mafunzo ya kilimo yatakayowezesha kulima kwa kutumia njia ya kisasa ili kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza ni kuwa tangu izinduliwe hadi sasa hakuna matokeo yoyote mazuri yaliyopatikana. Kambi haina uhai na inawezekana ilionekana kisiasa zaidi badala ya kuwasaidia wananchi hawa. Naiomba Serikali iangalie kwa karibu kambi hii ili kuona ni nini kinasababisha kutofanya kazi zake zilizokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuiomba Serikali pindi inapoanzisha miradi basi iwe endelevu na isiwe ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu Wilaya ya Rufiji imekuwa na migogoro baina ya wakulima na wafugaji, migogoro hii kwa kiasi kikubwa imesababishwa kwa kuingizwa ng'ombe wengi katika bonde la Mto Rufiji ambalo tunalitumia kwa kilimo. Kuingizwa huku kiholela na kinyemela kumesababisha wananchi wa Rufiji ambao ni wakulima kuwa na wakati mgumu wa kulinda mazao yao tangu wanapoyapanda hadi kuvuna. Naimba Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo iweze kukaa kwa pamoja ili kutatua tatizo hilo. Naelewa wazi kuwa Wizara yako haihusiani na suala hili lakini ushirikiano baina ya Wizara hizi mbili zitaweza kutoa mwelekeo wa utatuzi wa mgogoro huu.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la masoko, Serikali iunde kikosi kazi kutathmini mwenendo wa soko la korosho za Tanzania kama ilivyofanya kwa kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa korosho Tunduru. Kutokana na changamoto iliyokikumba Chama Kikuu cha Ushirika Tunduru *(TAMCU)* iliyopelekea deni la shilingi 2.6 bilioni mwaka 2012:-

(a) Serikali iendelee kuruhusu korosho za Tunduru kununuliwa kwa soko huru (Korosho za Tunduru pia kuchelewa sokoni).

(b) Serikali ifikirie uwezekano wa kuliona deni la shilingi 2.6 bilioni kama maafa na kulisamehe. Ni mzigo kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimu wa korosho Tunduru huanzia Oktoba. Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo *by* Septemba korosho huwa tayari kununuliwa. Je, Serikali imejipangaje kuhusu ununuzi wa korosho mwaka huu Tunduru? Ucheleweshaji wa ununuzi wa korosho za Tunduru huzifanya korosho hizo zipitwe na msimu wa ununuzi katika soko la dunia kwani tayari zinachelewa kutokana na hali ya hewa ya Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya korosho. Serikali imefikia hatua gani katika mchakato wa kurudisha mikononi mwake viwanda vya korosho vyote vilivyokuwa vimebinafsishwa kwani havifanyi kazi iliyokusudiwa? Azma njema ya Serikali ya kuongeza thamani korosho ghafi kwa tija zaidi itatimia tu kwa kutekeleza hatua hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Vyama vya Ushirika, Serikali isimamie vema utekelezaji wa sheria hii ili kuvirudishia hadhi na uwezo Vyama vya Ushirika kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya kuzuia viongozi na watendaji wa Vyama vya ushirika kutoshiriki siasa moja kwa moja ni nzuri na ikitekelezwa itaboresha sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti *(research)*. Lengo kuu la kufikia asilimia moja ya pato ghafi la Taifa *(GDP)* kama mchango katika tafiti (Kitaifa) liakisiwe katika ngazi ya sekta. Kilimo kama sekta ya kipaumbele ipatiwe kipaumbele pia katika kutenga fedha za utafiti. Tafiti katika kilimo ni ukombozi kwa wakulima na uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wataalam, hivi Wahandisi, Mafundi Sanifu, Wagani na kadhalika wangapi wangetosheleza mahitaji yetu? Wangapi wanakosekana? Ni nini mkakati kuhakikisha wanapatikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pembejeo, mifumo yote miwili (vocha na vikundi kupitia benki) inafaa lakini kila moja una changamoto kadhaa. Hii ni kazi yetu wote; Wabunge, Madiwani Watendaji Kata, Vijiji, Kamati za Pembejeo Mkoa na Wilaya, Kamati za Ulinzi na kadhalika. Hata hivyo, ili kusimamia ni vema zaidi Kamati za Pembejeo zianzishwe katika ngazi za Kata na Vijiji.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono bajeti ya Wizara. Niombe kutoa ushauri kwa Serikali kufanya mazungumzo na wenye viwanda vya mbolea kuona uwezekano wa kuwasaidia wale wakulima wadogo wadogo wa bustani za mboga mboga zifungwe *package* za kilo 5 – 10 – 15 hadi 20 ili kumudu kununua mbolea na kuitumia kutokana na kwamba bei ya mbolea ipo juu lakini wakati huo huo akinunua mfuko wa kilo 50 anaitumia kidogo nyingi inapungua nguvu. Hata mawakala wa mbolea itawaletea unafuu wa kuuza mboleo hiyo badala ya kuifungua mifuko na kuipima jambo ambalo linaharibu mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani waliopo hawatoshi. Niishauri Serikali kuongeza ajira ya Maafisa Ugani angalau wawepo kila kijiji itasaida kuwapatia wakulima elimu ya kilimo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri wakulima walipwe mapema ili waweze kumudu maisha na mipango yao mingine wanayoipanga kama vile kukopa karo za watoto wao na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifuatilie ardhi iliyochukuliwa na watu wachache maeneo makubwa ambayo hayaendelezwi na wakati huohuo yapo kwenye maeneo ambayo yana wafugaji/wakulima ambao wanakosa ardhi na kuishia kugombania maeneo madogo yasiyotosheleza.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa shukrani njema kwa kumshukuru Mungu kwa afya na uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chakula na ushirika ni sekta muhimu sana kwa Taifa letu hivyo ni budi au hapana budi kuwepo mipango madhubuti na endelevu kwa maslahi ya Taifa. Chakula ni muhimu kwa uhai na afya ya binadamu kwa hiyo mipango mizuri ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha kutumia jembe la mkono na kutegemea mvua kutoka mbinguni kimepitwa na wakati, si rahisi kufikia lengo linalokusudiwa. Mabadiliko ya tabia nchi hayaendani na mipango ya kilimo cha kutegemea mvua. Aidha, pale unapotegemea mvua kwa ajili ya mazao unaweza kukosa au ikapatikana mvua nyingi na kusababisha mafuriko. Ushauri wangu tuondokane na kilimo hiki na tuendeleze kilimo cha umwagiliaji, ambapo tunaweza kuendeleza kwa wakati wote wa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu bora ni muhimu sana katika kuendeleza chakula. Wakulima wengi wanakosa mazao mazuri kwa kukosa mbegu bora. Pamoja na juhudi kubwa wanazozifanya lakini hawapati chakula cha kutosha kwa kukosa mbegu bora. Serikali ni lazima isimamie upatikanaji wa mbegu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie pembejeo za kilimo. Pembejeo za kilimo ni muhimu kwa hiyo zipatikane kwa wakati muafaka. Jambo lingine kuhusu pembejeo za kilimo zipatikane kwa bei nafuu ili wakulima wote wamudu kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie elimu elekezi kwa wakulima. Ni muhimu sana wakulima wapewe elimu inayoendana na kilimo chao katika Mikoa yao na inayoendana na jiografia yao.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Mawaziri wa Wizara na Watendaji wa Wizara hii kwa kuwasilisha hotuba hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo ningependa kupata ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa 32, umwagiliaji. Niipongeze Serikali kwa kuendelea na ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye skimu 37 zenye hekta 19,890 za wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kujua ni vigezo gani vinatumika katika kutoa pesa katika miradi hiyo? Kwa kuwa kutoka Kata ya Isakalilo kuna mradi wa *Mkoga Irrigation scheme)* na katika Kata ya Kitwiru kuna mradi wa Kitwiru *Irrigation scheme*. Miradi hii ni ya muda mrefu sana imekuwa haitengewi pesa wakati tayari wananchi na Halmashauri wameshatumia nguvu kubwa sana kwa ajili ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kilimo kiendelee inatakiwa kutoa kipaumbele kukuza sekta ya utafiti. Kutotenga pesa ya kutosha kwa ajili ya kufanya utafiti wa maendeleo ya kilimo kama utafiti wa mbegu bora na mbolea inayofaa ni kosa kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa bajeti, inasikitisha sana kuona bado Serikali haijaona umuhimu wa kutenga pesa ya kutosha katika Wizara hii wakati asilimia kubwa ya Watanzania ni wakulima. Ili kauli mbiu yetu ya Kilimo Kwanza iweze kufanikiwa Serikali inatakiwa kilimo kipatiwe kipaumbele na mbaya zaidi hata pesa ya bajeti wanayotengewa haifiki ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo. Serikali miaka yote inatuletea mpango wa kuwa na Benki ya Wakulima. Je, ni lini benki hii itaanza? Tunaamini uanzishwaji wa benki hii ndio utakuwa ukombozi wa Mtanzania hasa mkulima na ningependa kujua benki hii ikianzishwa itaanzia Mkoa gani sababu siku zote Serikali huwa benki zinaanzishwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kujua mpango wa Serikali katika masoko kwa ajili ya wakulima wetu. Wakulima wetu wamekuwa wanajitahidi kulima mazao lakini hawajui masoko yake hivyo kusababisha walanguzi kuwatumia na kusababisha umaskini mkubwa kwa wakulima na kuwanufaisha walanguzi wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuongelea kuhusu *NFRA*, wakala hawa wanaponunua mazao hufanya hivyo kwa mkopo. Serikali ihakikishe inanunua mazao bila kukopa kwa sababu kwa kukukopa wananchi na kuchelewa kuwalipa, Serikali na wananchi huchukiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko mengi hayajakamilika mfano soko la Isongole Ileje halijakamilika. Hakuna uzio, mifugo kama ng'ombe pamoja na watu wasio waaminifu huharibu miundombinu ya soko na ulinzi kipindi cha msimu wa mavuno na kuuza mahindi hali inakuwa ngumu kulinda mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbolea, kila kinapofikia kipindi cha kilimo, wakulima wanapata shida sana kupata mbolea. Nashauri mbolea ifike mapema maeneo ya Nyanda za Juu Kusini ambako kilimo huanza mwezi wa nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani walio wengi hawafiki kwa wakulima. Nashauri uanzishwe utaratibu wa kuwadhibiti maafisa hawa ili waweze kufanya kazi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa kwa ajili ya ujenzi wa mabonde ya umwagiliaji, makandarasi wengi hawajafanya vizuri kutokana na ubadhirifu wa pesa za miradi ya umwagiliaji. Nashauri kuwe na usimamizi wa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea ya Minjingu. Kwa kuwa yapo malalamiko juu ya ubora wa mbolea hii katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwemo Ileje. Nashauri/kuomba Serikali au Wizara ianzishe shamba darasa Wilaya ya Ileje ili wajionee ubora wa mbolea hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Wizara (Bajeti). Kutokana na umuhimu wa Wizara hii ambayo inagusa Watanzania walio wengi, nashauri fedha iongezwe katika bajeti ya Wizara hii.

**MHE. ABDULSALAAM SELEMANI AMER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na Katibu na Naibu Katibu Mkuu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwapongeza kwa hotuba ya Waziri pamoja na mpango mzuri wa matumizi ya Wizara bado kuna tatizo la kupatiwa pesa kama walivyoomba jambo ambalo linawawia vigumu kutekeleza mipango yao kwa wakati. Naomba Wizara ya Fedha iipe kipaumbele Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuunda Tume ya Umwagiliaji ya Taifa. Ningependa kuomba Wizara yako iwaelekeze kufuatilia miradi hiyo katika Halmashauri za Wilaya ambako miradi itatekelezwa, miradi mingi inakufa au inafanywa katika kiwango duni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na dhamira nzuri ya Wizara kuunda kikosi kazi cha ufuatiliaji wa tatizo la soko la sukari hasa inayotoka nje ya nchi, tatizo hilo ni kero kubwa sana sio kwa wazalishaji tu pia ni kero kwa wakulima wa miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 5 Juni, 2014 Kampuni ya Ilovo ambayo inaendesha viwanda viwili vya kuzalisha sukari katika Wilaya ya Kilosa na Kilombero imewaandikia Wenyeviti wote wa wakulima wadogo wa miwa kama ifuatavyo:-

(1) Kwa asilimia kumi ya mabaki kwa msimu uliopita wa 2013/2014 hawakulipwa kutokana na sukari kulundikana katika ma-*godown* yao.

(2) Mgawo wa miwa kupeleka kiwandani utapungua msimu huu kutoka kwa wakulima wadogo.

(3) Bei ya ununuzi wa miwa msimu huu haitaongezwa huenda ikapungua wakati gharama kila mwaka zinapanda.

(4) Wamepunguza ununuzi wa miwa toka kwa wakulima wadogo ili waweze kununua miwa yao tu jambo litakalowavunja moyo wakulima wa miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ilione jambo hili kwa uzito wa kipekee. Tatizo la kuingiza sukari nchini wakulima hao linawahusu nini? Naamini hao wakulima wadogo hawana *share* kwenye kampuni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya vikundi vya wakulima na baadhi ya wakulima wenye uwezo wako tayari kuwekeza viwanda vidogo katika mashamba yao. Hata hivyo, kuna sheria ambayo inatakiwa kurekebishwa na Bodi ya Sukari kwa kupendekeza marekebisho hayo Serikalini ili kuwaruhusu wakulima hao waweze kuruhusiwa kuleta viwanda vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Naibu Waziri kwa kuteuliwa nafasi hiyo pia nampa pole kwa vijemba alivyopewa na baadhi ya Wabunge. Nasema kaza buti na kwa uwezo wa Mungu utafanikiwa katika kuendeleza gurudumu la maendeleo.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ndio tegemeo kubwa la uchumi wa Taifa na kwa mtu mmoja mmoja. Hivyo Kilimo kinapaswa kutengewa bajeti ya kutosha kutokana na ukweli kwamba robo tatu ya Watanzania ajira yao wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbarali ni Wilaya pekee Tanzania yenye skimu nyingi za umwagiliaji, siyo kwa sababu inapendelewa isipokuwa ni eneo lililo chini ya Bonde la Ufa na eneo lenye rutuba nyingi na mito inayotoka milimani na hivyo kumwagilia mazao hasa kilimo cha mpunga. Natoa shukrani nyingi kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara ya Maji na Kilimo kwa jitihada wanazofanya kutuunga mkono wananchi wa Wilaya ya Mbarali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Serikali zipo changamoto nyingi zinazoikabili sekta hii. Naiomba Serikali kutoa fedha ili kukamilisha miradi ya kilimo ikiwemo mradi wa Mwendamtitu, mradi wa bwawa la Lwanyo ambalo lisipopewa fedha huenda likabomoka na kusababisha hasara kubwa ya mamilioni ambayo yamekwishatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa Bwawa la Madibira ambalo likikamilika litamwagilia zaidi ya hekta 3600. Ipo miradi mingi ya kilimo Wilayani Mbarali naomba ipewe kipaumbele kwa sababu ipo na wananchi wanaendelea kuitumia. Aidha, lipo eneo la Mpunga Mmoja Chimala/Kapunga linalofaa kwa kilimo cha mpunga wananchi wanahangaika linahitaji kuboreshwa miundombinu yake. Pia yapo maeneo ya Yala, Mwashikamule, Luhanga, Munazi, Mwaniungu yanahitaji kuboreshwa miundombinu wananchi wameanza na wanalima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo migogoro Wilayani Mbarali, Wizara inatakiwa kusaidia kupata ufumbuzi. Shamba la Kapunga lililokuwa la *NAFCO* kapewa mwekezaji makazi ya watu na eneo la wakulima wadogo. Tatizo hili

linashughulikiwa bado kurekebisha mipaka, Waziri wa Ardhi anashughulikia wananchi wanataka kujua ni lini litakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushuru wanaotozwa wakulima wanaovuna mazao wanaporudisha nyumbani haukubaliki kisheria, naomba Wizara ikemee. Mimi mwenyewe nimefanya hivyo lakini bado.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii ili nitoe maoni yangu katika bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa nchi hii wananchi wake takribani asilimia 70 wanategamea kilimo, bado sekta hii haijapewa kipaumbele cha kutosha. Kauli mbiu ya Kilimo Kwanza kwa mara nyingine imeshuhudia jinsi Serikali isivyokuwa na nia ya dhati kukuza kilimo kwani inatengewa kiasi kidogo cha fedha ambacho nacho hakitolewi chote. Hakuna jitihada zozote za kuwa na kilimo endelevu hasa katika eneo la umwagiliaji, wakulima wameendelea kutegemea kudra ya Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Kauli mbiu ya Matokeo Makubwa Sasa nayo imekuwa dhihaka kwa wakulima. Wananchi hawana matarajio yoyote ya Matokeo Makubwa Sasa kwa wakati huu au hata siku zijazo kwani Serikali imeshindwa kupeleka fedha zilizoidhinishwa katika miradi ya Matokeo Makubwa Sasa hasa katika kilimo. Mfano kwa mwaka wa fedha unaoisha, kwa ujumla Serikali imetoa takribani asilimia 53 tu kwa miradi yote, hii ni hadi mwezi Machi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la alizeti ikiwa litasimamiwa ipasavyo linaweza kuwakomboa kiuchumi wananchi wa Mkoa wa Singida ambao kwa miaka yote haujawahi kuwa na zao la uhakika la biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba na kuitaka Serikali iwapatie wakulima wa alizeti pembejeo ili waweze kuzalisha kwa wingi na tija. Hata wakulima hawana uhakika na soko wanategemea tu wapita njia ili wanunue mafuta ya alizeti yaliyosindikwa kwa teknolojia hafifu. Wakulima wamekuwa wakipanga madumu ya mafuta barabarani ambako hawana uhakika wa kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia yafuatayo:-

Kwanza, fedha zilizobaki kutoka bajeti ya 2013/2014, asilimia 27% ya bilioni 349.23 itolewe na Serikali ili ifanye kazi zilizokusudiwa.

Pili, ardhi ya kilimo ipangwe, ipimwe na kulindwa ili kuwa na usalama wa ardhi kwa wakulima wadogo na kuondoa mgogoro wa ardhi kati ya wakulima na wafugaji.

Tatu, pembejeo zisimamiwe na uhalifu uliopo hivi sasa kati ya watendaji na Wakala udhibitiwe. Wahalifu wachukuliwe hatua za kisheria.

Nne, rejista za wakulima ziwe *updated* kila mwaka.

Tano, uwezo wa hifadhi ya chakula uongezwe kwa kila kanda, Mkoa na Wilaya.

Sita, ubora wa mbegu zinazouzwa kwa wakulima udhibitiwe na kuwahakikishia wakulima mbegu bora.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielezwe ni kwa nini fedha za maendeleo katika Idara ya Mipango imetengwa tena kuwa matumizi ya kawaida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Wilaya ya Mbulu, Manyara mwaka huu wa kilimo uliopita hawakupewa kabisa pembejeo za kilimo za mbolea huku Mawakala wamelipwa na Mkuu wa Wilaya anawakingia kifua kulikoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu kwenye *program* ya 4486 *ASDP* kwenye maendeleo, fedha zimetengwa za kuandaa mwngozo milioni 25, kujenga uwezo 50 milioni, kuandaa Kanuni milioni 100, kuwezesha sekretarieti milioni 55, kusaidia timu ya uwezeshaji milioni 145, ukurasa 133 wa randama, hivi kwa nini fedha hizo zisitolewe?

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa la Imala halimo kabisa kwenye hotuba ya Waziri. Naomba maelezo bwawa hili la Imala, Kata ya Ndebelwa Manispaa ya Tabora, mkandarasi kasimama kazi alizofanya anadai milioni 400. Athari zake tuta halijakamilika litabebwa na maji na hasara itakuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atakapokuwa anajibu anipe maelezo.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Wizara hii kwa asilimia 100% na nawapongeza kwa hotuba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua kiwanda cha kutengeneza mbolea itokanayo na rasilimali gesi kule Mtwara kimefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha mbolea zisizo na viwango haziingii wala hazisambazwi kwa wakulima hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo ni mkombozi pekee wa wakulima nchini. Serikali imekuwa inaahidi kila siku, ni lini benki hii itaanzishwa na Serikali imefikia wapi katika mchakato huu wa kuanzishwa benki ili wakulima wanufaike na waweze kuongeza uzalishaji wake?

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri na Naibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chakula ni kingi sana na hata mahindi ya mwaka jana bado hayana soko. Mavuno ya mwaka huu ni mara mbili ya mwaka jana, Serikali ione haja ya kununua mahindi yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mvua nyingi na maji mengi kutoka milimani kuelekea Ziwa Nyasa miundombinu yote ya umwagiliaji imebomolewa. Naomba Wizara itembelee maeneo hayo na kuona uharibifu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa miche ya kahawa unazidi kuenea. Naomba sana dawa zije kuimarisha miche ya kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza hotuba na ninaiunga mkono. Naomba kuchangia machache juu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara ya Kilimo kutatua tatizo la muda la wakulima wa Jimbo la Manyovu waliodhulumiwa kahawa zao na vyama vya ushirika/au wanunuzi binafsi kama taarifa zilivyoletwa Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze Wizara kwa taarifa mliyonipa kwamba mnaandaa fidia kwa wakulima wa kahawa. Naomba Mheshimiwa Waziri alizungumzie kwani wakulima wa Mkoa wa Kigoma wanasubiri kusikia, nimepigiwa simu nyingi na wakulima zaidi ya 70 wanaangalia *television* mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma hauombi chakula cha msaada, bali wanajituma, naomba Waziri awaonee huruma. Hotuba iliyosomwa haikuongelea chochote, naomba atakapokuwa anafanya

majumuisho, asisahau kuongelea jambo hilo la fidia kwa wakulima wa kahawa Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nawatakia ufanisi bora.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii pamoja na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri mnayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mpwapwa tunayo skimu ya umwagiliaji hususan zao la mpunga katika eneo la Msagali ambako kazi hii ya ujenzi wa banio la maji ya mvua, uchimbaji wa mifereji na kusakafia mifereji hii, mpaka sasa imeshachukua muda mrefu kuitekeleza. Hali hii imesababisha mategemeo yaliyokuwepo ya kuzalisha mpunga wa kutosha kutokamilika hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie katika mwaka huu wa fedha 2014/2015 skimu hii itekelezwe kwa kumalizia ujenzi wa banio la maji ya mvua, pamoja na mifereji ichimbwe na kusakafia. Skimu zilizotekelezwa kwa mwaka 2013/2014, skimu hii ya eneo la Msagali haikutekelezwa ingawaje kazi hii ilishaanza miaka mingi bila kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kukopesha fedha kwa wakulima kupitia *SACCOs* zilizo tayari kutoka Benki ya Kilimo. Utaratibu huu wa kukopesha wakulima umefikia wapi? Wizara inasemaje kuhusu suala hili?

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ludewa imeuza mahidi mengi sana Serikalini *(NFRA)*. Tunashukuru sana kwa kununua mahindi na bado yapo mengi sana, Serikali ije inunue mahindi Mkoa wa Njombe, amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushuru wa mazao ndio tegemeo la *Council* za Mkoa wa Njombe hususan Ludewa. Wilaya Ludewa inaidai Serikali takribani milioni 400 za ushuru wa mazao. Je, ni lini fedha hizi zitalipwa Ludewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mpango gani wa Wilaya kudhibiti mbegu mbovu na mbolea mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado uhitaji wa matrekta vijijini ni mkubwa sana. Kuna mpango gani wa kukopesha matrekta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ludewa inaomba miradi ya *irrigation,* hivyo tunaomba mtaalam wa *irrigation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NMC* Iringa itaanza kazi lini? Eneo hili litasaidia soko la mazao na ajira.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kusaidia kutengeneza mfereji wa Mchomba uliopo Marangu Vunjo ambao utasaidia umwagiliaji wa maji katika vijiji vya Sembeti na Matala. Wizara ilitoa Shs. 300,000,000/=. Wizara iliniahidi kutengeneza mfereji mwingine. Naomba Wizara inisaidie na wananchi wangu wa Vunjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika wa *KNCU*. Naomba Serikali iingilie kati kuhusu mali za wanaushirika wa *KNCU* zinazouzwa kwa hila na kwa mbinu mbalimbali mfano mzuri ni uuzaji wa nyumba tatu za *TCCCO*. Nashukuru Wizara iliingilia kati ili kuhakikisha wanachama na washika dau wote wanashirikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili ni kuhusu uuzaji wa shamba Gararagua lenye ukubwa wa ekari 3,429 kwa kisingizio cha kulipa deni la billioni nne la *CRDB*. Ikumbukwe kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013, Ibara ya 55(13) inasema:-

"Bila kuathiri vifungu vidogo (1), (2), (3), (4), (7) na (8) bodi itawajibika kwa hasara yoyote itakayopatikana kwenye chama na kila Mjumbe aliyehusika na hasara hiyo atashtakiwa kwa kosa la jinai na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni tano pamoja na kulipa fidia ya shilingi milioni tano ni pamoja na kulipa fidia kwa hasara iliyopatikana".

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwana Menrad Swai, Mwenyekiti wa Bodi ya *KNCU* anadai *KNCU* ilipata hasara ya shilingi bilioni nne na inadaiwa na *CRDB* shilingi bilioni nne. Mwenyekiti huyo akaamua kuitisha haraka haraka mkutano wa *KNCU* ili waridhie kuuzwa kwa shamba la Gararagua kwa shilingi bilioni nne kulipa deni lakini wanachama wa vyama vya msingi hawakutoa ridhaa yao. Naomba Wizara iingilie kati.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani kwa Waziri wa Kilimo kwa kusimamia vizuri Wizara ya Kilimo na Ushirika kwa juhudi na maarifa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mwakilishi wa Jimbo la Kilwa Kusini. Wapigakura wangu wamenituma nikupongeze Waziri wa Kilimo na Ushirika kwa kuwapa fursa ya kuuza zao lao la ufuta kwa soko huria. Hakika wamefaidika wakulima na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya, lakini hakukosi kuwa na changamoto. Changamoto zilizopo, wananchi wa Kilwa wanaomba kwa heshima na taadhima kwako Waziri wa Kilimo na Ushirika ututekelezee mambo muhimu yafuatayo:-

(i) Kusajiliwa kwa Chama cha Msingi *(UNA)* kilichopo Kijiji cha Nanjilinji "A".

(ii) Katika Wilaya ya Kilwa tuna mito mitatu, nayo ni Matandu, Mavuji na Mbwemkuru. Katika hotuba yako aya ya 4.2.7 ukurasa wa 72 inayohusu ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji na udhibiti wa mafuriko, vyombo vya habari na kuhamasisha kilimo, vimetaja Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Kigoma, Mbeya, Arusha na Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima nakuomba pia na Mkoa wa Lindi hususan Kilwa iongezwe katika Mikoa hiyo ukizingatia mito hiyo mitatu; Matundu, Mavuji na Mbwemkuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kijiji cha Makangago kwa miaka mingi kuna mradi wa umwagiliaji wa Makangaga na Mpindilo lakini mpaka hii leo hakuna manufaa kwa wakulima katika mradi huo.
1Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri afike makangaga/Mpindilo ili tusaidiane wapi mradi huu unakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri nipate majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani. Ahsante.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii ya bajeti ya Kilimo kwa kuzingatia uhalisia kwamba Kilimo ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo ya nchi yetu, ikizingatiwa kuwa wananchi zaidi ya asilimia themanini wanaishi Vijjini na kwa tafsiri nyingine wananchi hawa huishi kwa kutegemea Kilimo ili kuendesha maisha yao. Lakini Serikali imeshindwa kubuni mradi/mpango mzuri juu ya kuwawezesha wakulima wadogo/wakubwa na wakati ili waweze kulima kilimo chenye tija ili tufikie malengo ambayo yataendana na kauli mbiu ya Kilimo Kwanza. Ili tuweze kuishi hii kauli mbiu, ni lazima Serikali itimize *principles* zote za kuwezesha kilimo chenye tija na hii ni kwanza.

Katika kuwawezesha wananchi/wakulima mwezesho huu ni kuwatengenezea muundombinu ya barabara ambazo zitawarahisishia ubebaji/usafirishaji wa mazao toka kwa mkulima hadi kwa mlaji bila kuwa na

miundombinu ya barabara kutoka vijijini hadi Mijini/kwenye masoko. Tukiwa na barabara imara, siyo tu mazao yalimwayo hasa *perishable* hayataharibika bali mazao yatapanda thamani maana *supplier/distributor* watakuwa wengi. Hivyo tutakuwa tumesaidia upatikanaji wa masoko ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ili kuongeza thamani ya mazao ni pamoja na kuwepo kwa miundombinu ya umeme ili wakulima wa mazao kama matunda, mboga mboga, nyanya na hata mengine waweze kuchakata katika *level* ya msingi (ku-*process* wenyewe) hili nalo lingesaidia thamani ya mazao yale baada ya kuwa wame-*process* wenyewe. Lakini ilivyo sasa matunda ambayo ni *perishable* yanaharibika sababu hawezi kuyahifadhi bila umeme kwa muda mrefu na wanunuzi wanashindwa kuwafikia sababu ya barabara mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuwezesha Kilimo cha umwagiliaji. Serikali ijitahidi kuhakikisha wananchi wanapata vyanzo vya umwagiliaji hasa kwenye maeneo ya ukame/au misimu isiyotabirika. Lakini lingine ambalo tunabidi tulikemee ni urasimu inapofikia mkulima kuhangaika kulima bila msaada/ruzuku ya Serikali lakini akishavuna tu Serikali inatia mkono wake kwa kuweka masharti kibao. Hii inatia kero sana na inakatisha tama.

Mfano mzuri ni Mkoa wa Mara. Tumeshuhudia jinsi wakulima/wafanyabiashara wa mazao ya nafaka wanavyopata taabu sana na kusema kuwa miradi ya Polisi/*TRA* pamoja na baadhi ya Maafisa/Watendaji Serikalini ikiwemo *DC* wa Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kipindi hiki tunashuhudia *barrier* nyingi sana zinaongezeka, wakulima wanalipa ushuru zaidi ya mara nne na rushwa juu. Vikwazo vya kutopeleka mazao nchi jirani ya Kenya mfano mahindi, wala kutouza mahindi nje ya Mkoa wa Mara kwa maana kwenye Mikoa mingine ya Tanzania Bara, vile vile mchele toka Shinyanga/Mwanza unazuiliwa kuingizwa Mara/Tarime. Sasa hapa tunatarajia hawa Watanzania wataishije? Huu unyanyasaji tunaomba ukomeshwe, mwaache Watanzania walioamua kujiajiri kwa Kilimo/na kwa kufanya biashara ya nafaka wapate tija na kujivunia kuwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni juu ya ukiritimba wa suala zima la ruzuku ya mbolea, pembejeo na vinginevyo. Nashauri kwamba, kwa kuwa njia ambayo inatumika hivi sasa ni mbovu ningependekeza na kwa kuamini ukweli kwamba mkulima yeyote yule akipewa fedha kwa ajili ya ruzuku atazitumia kwa ruzuku na siyo vinginevyo, sababu anajua akiweka mbolea atafaidi mazao, akitumia mbegu za kisasa atafaidi, na kadhalika. Vinginevyo, Serikali iweke ruzuku ambayo itapunguza bei za mbolea, mbegu na hata pembejeo za kilimo

ili iwe nafuu kwa wakulima hata wale familia masikini/wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu na utekelezaji wa yote ambayo nimeainisha hapa.

**MHE. JANET Z. MBENE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ufanisi *SACCOS* ni mdogo ukilinganisha na wanavyojiendesha na matatizo ambayo bado wananchi wengi wanajiunga nazo wanavyoendelea kupata changamoto za kujiendesha na kupata mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko hoja ya kutathmini utendaji wa *SACCOS* katika kila ngazi ili kuanisha matatizo mbalimbali na kuweka mikakati ya kuziandaa changamoto hizi; na

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Usimamizi wa *SACCOS* inahitajika hata kabla ya *SACCOS* kuanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mkakati wa makusudi kuunganisha shughuli za Kilimo na zile za Viwanda katika mfumo mzima wa mnyororo wa thamani *(value Chain)* ya uzalishaji kuhakikisha kuwa mazao yanayozalishwa yanaongezewa thamani *(value addition),* yanapata uhifadhi mzuri wa maghala, unapata masoko yenye uhakika. Hii ikijumuisha taarifa sahihi na kwa wakati za masoko na na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya teknolojia yaimarishwe kwa kuhakiksiha ni mkakati mahsusi unaoingizwa kwenye mipango ya Wizara ya Kilimo, hasa wakati matayarisho ya mashamba, uzalishaji wa mbegu na mnyororo mzima wa uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kitu muhimu katika kilimo kama upatikanaji wa uhakika wa mbegu bora, kwa wakati na kwa kiasi kinachohitajika. Ulimaji/uzalishaji wa mbegu uwekewe kipaumbele kuhakikisha wakulima walio tayari waingie ubia na wawekezaji wa nje kuzalisha mbegu kwa wingi tuachane na kuagiza mbegu zake nje ya nchi.

Vile vile Wizara ihakikishe mbegu zilizothibitishwa zinapandwa kwa wingi kwenye maeneo husika.

Sukai isiagizwe na watu baki, iagizwe na *Sugar Development Board* kwa usimamizi wa karibu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha na Wizara ya Kilimo kwa sababu changamoto kubwa ilijitokeza, sukari na mchele

vilivyoruhusiwa kuingia nchini pasipo kushirikishwa Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvunaji wa maji ya mvua ni lazima uwekewe mkakati wa makusudi katika ngazi ya Kata, Wilaya na Mkoa na Kitaifa na hili ni jambo litakalorahisisha sana umwagiliaji na kuturahisishia Kilimo wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kulia njaa na maji yametuzunguka. Nashauri kwamba tuanze kuingiza elimu ya *green houses* na Kilimo cha matumizi bora ya ardhi kwa kutumia mbinu za *intensive farming* tukitumia wanafunzi mashuleni. Yako mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayoendesha miradi hii. Wizara ishirikiane nao kufanyia mazoezi mashuleni na kwenye Vyuo vya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba wanawake wawekewe mkakati wa makusudi wa kuwawezesha kulima mazao ya mboga, matunda, mazao ya mbegu za mafuta, alizeti, karanga, mchicha, ufuta, viazi, mihogo, migomba na mbogo mboga, nyanya, viungo *(spices)* na kadhalika.

Pia vijana wawekewe mkakati wa kipekee wa kupewa ardhi, elimu ya kilimo cha uvunaji maji, malisho, umwagiliaji na waunganishwe na ufugaji na kadhalika.

Wakulima binafsi Vijijini wanasafirisha mazao, hivyo waruhusiwe kuuza mazao yao bila kudaiwa kodi yoyote.

Kodi itozwe kwa wanunuzi wakubwa kuanzia kwenye Halmashauri zao hadi kwenye masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kodi zipunguzwe kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kuimarisha uongezaji thamani na usindikaji wa mazao ya Kilimo, kuna haja ya Wizara ya Kilimo na Chakula zishirikiane na Wizara ya Viwanda na Biashara na hii ionekane katika chombo kitakachoundwa kuweka mkakati wa pamoja utakaosimamia kuhakikisha hili litafanyika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo iweke mkakati shirikishi wa kuhakikisha sekta binafsi inashiriki kikamilifu katika Kilimo, masoko na kutoa huduma zote kwenye sekta hii pamoja na mitaji. Wizara izingatie changamoto zilizoainishwa na sekta binafsi juu ya ushiriki wao na kuzifanyia kazi.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hotuba yako nzuri kuhusu hali ya kilimo nchini. Kilimo kina changamoto

nyingi kulingana na wakati mwingi kukumbana na hali ambayo haitabiriki ya mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kueleza tatizo ambalo linawakera wafanyabiashara wa Jimbo langu la Longido. Jimbo langu liko mpakani mwa Kenya. Wakati wa kupeleka mazao Kenya wanalazimishwa kwenda kuleta kibali cha Katibu Mkuu wa Kilimo huko Dar es Salaam jambo ambalo ni vigumu kwa wafanyabiashara kufuata kibali hicho. Tunaomba utaratibu huo ubadilishwe wapate vibali hivyo Mkoani. Rushwa kubwa inafanyika nchini; na kwenye Vituo vya Barabara ni kila kimoja kazi ni kudai hongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukumbusha kwamba Wilaya ya Longido haikupata pembejeo mfano matrekta na mabwawa ya umwagiliaji. Naomba kwenye bajeti hii likumbukwe bwawa la Ngereyani ambapo Mto Ngarenaki humwagilia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013 wataalam wa Wizara yako wamekwenda kuangalia sehemu ya kuchimba bwawa hilo lakini hawakurudi tena. Wananchi wa kijiji cha Ngareyani na Tingatinga ni wakulima ambao wanategemea umwagiliaji, wakipata bwawa hilo watajitosheleza kwa chakula. Ikumbukwe kwamba Wilaya ya Longido ni kame na wanategemea kupelekewa chakula kila mwaka. Kutokana na aombi langu jana maeneo hayo yakubalike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ajabu kwenye bajeti ya mwaka 2013 na mwaka huu hakuna sehemu yoyote uliyotaja mradi wowote kwenye Wilaya ya Longido hata kwenye miradi ya *(BRN)* haikutajwa. Wananchi wanajiuliza, kwanini Wizara hii haitambui kwamba nao wanahitaji pembejeo? Serikali ikumbuke kwamba Wilaya hii siyo wafugaji tu, kuna sehemu kubwa ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Longido inapakana na Rombo, Siha na Arumeru. Longido wanaona wametengwa na majirani zao kwa kuwa wanaona wakipata pembejeo na miradi huku wao hawapati. Lawama hizo kwetu ni kwamba Mbunge wao ndio hawatetei. Naomba ombi langu hilo la Bwawa lipangwe kwenye bajeti yako Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja yako.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nAchukua nafasi hii nichangie katika Wizara hii ya hotuba ya Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika. Ni kweli kwamba Kilimo ni moja ya sekta muhimu sana nchini katika uchumi na maendeleo yetu kwa kuwa inatoa ajira kwa asilimia 74 ya watanzania na kilimo kinachangia pato kwa asilimia 24.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kilimo kuwa uti wa mgongo wa Watanzania wengi na kuhimizwa na Serikali kwa kaulimbiu ya majina mengi na mazuri kama vile Siasa ni Kilimo, Kilimo cha Kufa na Kupona, na sasa Kilimo Kwanza, wananchi wanaishia kuwa masikini hasa wakulima wadogo wadogo. Kilimo Kwanza kimezidi kuwadumaza wakulima wadogo wadogo na kuwaangalia wakulima wenyeji zaidi na wawekezaji wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinazowazunguka wananchi ni kama vile mitaji, upatikanaji wa mbegu, upatikanaji wa mbolea umekuwa na ubaguzi na hata zikiletwa zinafika kwa kuchelewa. Naomba Serikali itatute kero hizi ili kila mkulima anufaike na uchumi kupitia Kilimo. Licha ya mazao ya biashara, kila mwananchi atanufaika na chakula bila kutegemea chakula cha msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Scheme* za Umwagiliaji, Serikali ihakikishe fedha zote zilizopangwa kujenga *Scheme* za Umwagiliaji zifanye kazi iliyotengwa ili nguvu kazi isipotee bure na kuambulia taarifa za kwenye vitabu bila utekelezaji. Mfano, Mkoa wa Katavi *Scheme* za Umwagiliaji zilizoahidiwa na Serikali bado hazijakamilika mbuga za Mwamkulu. Sijui Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa ushirika malipo ya wakulima wa zao la biashara, Tumbaku, wamekuwa wakichelewesha malipo yao na hivyo kushindwa kujipanga tena kwa msimu wa ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali isimamie haya kwa dhati kuhakikisha wakulima wanaepukana na matatizo haya ya ucheleweshwaji wa malipo yao nje ya wakati ili wajipange kwa msimu mwingine bila kukwama. Pembejeo zigawiwe bila ubaguzi, watafutiwe masoko, huko ndiyo kumwinua na kumsimamia mkulima, kwani wakulima wengi wanalima kwa kubahatisha. Hili ni muhimu sana. Ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza hotuba ya kina ya Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ushauri au mapendekezo na maombi maalum katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu umwagiliaji. Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji Misozwe, Muheza, umekamilika mwaka 2013 na ujenzi wa mifereji kuendelea mwaka 2013/2014. Baada ya kukamilishwa kwa mifereji, kazi

inayoweza kuanza mara moja, ni kilimo cha mpunga kwa kuwa kipo Chama cha Umwagiliaji Misozwe chenye wanachama wastani 100 na eneo la umwagiliaji wastani wa eka 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi maalumu, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika isaidie Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kupima kuandaa maeneo kujenga mifereji midogo kuwezesha maji kutumika vizuri kwa mgawo katika maeneo ya mkulima mmoja mmoja na kuwezesha wakulima (wanachama) kupata mbegu bora na kuanza Kilimo mara moja mwaka huu 2014 ambapo mvua kubwa zimekuwepo na kuonyesha uwezo mkubwa wa kuongeza chakula Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha uongezaji wa thamani na usindikaji wa mazao ya kilimo, kwa kuwa eneo la umwagiliaji Bwawa la Misozwe ni kubwa, Wizara iandae mpango wa elimu kwa wakulima na wanachama wa mradi wa umwagiliaji Misozwe na maeneo yote nchini juu ya Teknolojia za usindikaji, uhifadhi wa mavuno, ufungashaji na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Muheza imekuwa na kikundi na mashine ya usindikaji wa matunda ambapo sasa kwa kukuza uwezo wa kujiendeleza, kiwanda hicho kimesimama. Basi Wizara ya Kilimo isaidiane na Wizara ya Viwanda na Biashara iliyoahidi Bungeni wakati wa kujibu swali langu Bungeni tarehe 5/05/2014 kutuma wataalamu kuona hali ya kiwanda hicho na kushauri na kutoa msaada wa kukifufua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa umwagiliaji wa Mashewa (Muheza), usimamizi na uendelezaji wa mradi huo hauridhishi na wala haukutajwa popote katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri: Je, Serikali haioni haja ya kuendeleza mradi huo ambao umewahi kutolewa fedha na kupelekwa kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo 2010/2013?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata kauli ya Wizara juu ya uendelezaji wa mradi huu na juu ya uboreshaji na ujenzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya maombi ya fedha kwa bajeti ya Wizara ya Chakula na Ushirika 2014/2015.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nawapongeza wakulima kwa kulima mazao ya chakula hadi kuwa na ziada iliyopelekea maghala ya chakula (hifadhi) kuwa na zaidi ya 100%. Ghala la hifadhi ya chakula ambalo muda mwingi nimekuwa naiomba Serikali kukarabati (siyo kujenga) maghala yaliyopo ya barabara, reli ipo, ni karibu na Mikoa ya Simiyu, Mara na Mwanza yenyewe, bwana Waziri naomba useme leo

kama imeshindikana, kwani ulipokuja Kwimba kwenye Uzinduzi wa Mbegu zisizoota za *Quaton* nilikumbusha ukasema umesikia utalifanyia kazi lakini katika kitabu chako sijaona popote kuhusu ukarabati wa ghala Bukwimba naomba leo useme ukweli inawezekana au haiwezekani nani kwanini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alikuja kuzindua mbegu za *quton* Jimboni kwangu kwa mbwembwe na Mwenyekiti wa Bodi alikuwa ndio *Marketing Manager* wa Kampuni hiyo. Kata ya Mwandu imeathiri kwa kiasi kikubwa wakulima wa zao la Pamba. Katika maelezo yako umesema Kampuni ya *Quton* haitapelekewa pesa zote zaidi ya Shilingi bilioni 10: Je huyu mkulima ambaye alinunua mbegu akapanda hazikuota, akanunua tena hazikuota, tena huyu ambaye ameathirika kutokana na mbegu hizo kutoota yeye anafidiwa nini? Lakini ni nani anayekagua tani (kilo) zilizopelekwa kwa wahitaji natahadharisha eneo hilo lisiwe kichaka cha watumishi wasio waaminifu kwa mfumo wa wakulima na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo awali mbolea ya Minjingu Naibu Waziri wa Kilimo Mhesimiwa Zambi alikuwa anaipinga kwa nguvu kubwa. Nauliza, mbolea hiyo sasa kupitia kwa Naibu Waziri anasemaje kuhusu mbolea hiyo?

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Ushirika cha *KNCU* kinauawa kutokana na uongozi mbovu ambao hawashirikishi washirika na kuwapa elimu juu ya maamuzi na mapendekezo yanayopelekwa kwao kwa ajili ya maamuzi, ubadhilifu wa fedha na mali za ushirika.

Uuzaji holela wa mali zisizohamishika za wanaushirika kama vile magari, nyumba na mashamba kutokana na hali ambayo wanaushirika na wakulima wa Kahawa wamekata tamaa. Wanang'oa Kahawa na kupanda mazao mengine hasa mboga mboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali kuunda Tume ya kuchunguza chama cha *KNCU*.

- Utendaji wa Viongozi wake;
- Mahesabu ya *KNCU;*
- Mali zake zote; na
- Madeni yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Seriklai iwachukulie hatua viongozi wote watakaobainika kuhusika na ubadhirifu wowote ambao utabainika

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pembejeo bado linawasumbua wananchi. Pembejeo zinapatikana baada ya msimu; zinapatikana chache sana na hivyo kuzua manung'uniko kati ya wananchi. Vile vile Mawakala huingia ubia na Viongozi wa Vijiji kuwaibia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali kubuni au kuimarisha mifumo ya ugawaji wa pembejeo ili lengo la Serikali liweze kuwafikia wananchi wote. Soko la nafaka nje ya nchi ni kubwa kupitia mipaka ya Holili na Tarakea. Hata hivyo, wafanyabiashara hasa wa mahindi wanapata usumbufu mkubwa kutoka kwa askari hasa Holili. Tunaiomba Serikali kutoa tamko kuhusu jambo hili ili kuondoa wizi, rushwa na usumbufu ambao wafanyabiashara wanapata kutoka kwa watumishi wa Serikali. Wananchi wapewe uhuru kuuza mazao bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba kutamka kwamba napongeza Uongozi wa Wizara, Waziri na Naibu Waziri na Watendaji wakiongozwa na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAYNABU MATITU VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri Katibu Mkuu na Watendaji wote wa kwa hotuba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, naomba Serikali inipatie taarifa za vipi imejipanga kuhakikisha kwamba zao la asilia la nazi halitoweki kwa maana litaendeleakuwepo kwani linashambuliwa na magonjwa na kuanza kutoweka. Je, ina maana tusahau kama kuwa na zao la nazi ni kukosa kupata mafuta ya kupikia ambayo yana uhakika kiafya, kutoa ajira kwenye viwanda na hata kwa wale wenye mashamba ya nazi ambao mavuno yake yana uhakika wa mara nne kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natarajia kwenye majibu yako ya bajeti hii yataleta maendeleo ya zao hilo la nazi.
Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji kwa maeneo yote ya Kilimo cha umwagiliaji. Hiki ndiyo Kilimo pekee cha uhakika kwa ukombozi wa mkulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuomba Serikali ije na mkakati maalumu wa *Schemes* za umwagiliaji katika Bonde la Eyasi, Karatu kwa Kilimo cha vitunguu na mahindi. *Schemes* hizi zinataka ukarabati mkubwa ili wakulima waweze kufaidi hasa 'Kilimo Kwanza' kipate maana yake.

Mpaka sasa naona kama Serikali imetelekeza bonde la Eyasi, pembejeo za Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iwe na mkakati madhubuti kuhakikisha kuwa pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati muafaka na tathimini ya uhakika wa pembejeo zinazotakiwa kwa maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbolea ya minjingu, naishauri Serikali kuhakikisha kuwa inafanya utafiti wa kutosha kwa udongo katika eneo la Karatu hasa kwa matumizi ya mbolea ya minjingu kuliko kutoa pembejeo hii *(full sett* bila ya utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ipate kuajiri wataalamu wa ugani wa kutosha nchini ili kuimarisha Kilimo hasa Wilayani kwangu Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko kwa mazao ya wakulima wa Vitunguu – Eyasi, naomba Serikali iweze kuwatafutia wakulima wa vitunguu wa bonde la Eyasi kwani wanavamiwa na wafanyabiashara toka Kenya, Sudan Kusini hasa Kenya na kufanya *packing labeled* mada *(Produced in Kenya),*ni vizuri sisi wenyewe tukaongeza thamani ya vitunguu vyetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matatizo ya ardhi ya kilimo kwa mashamba, naishauri Serikali kufuta hati miliki kwa mashamba ya mikataba katika eneo la karatu ambayo hayakuendelezwa kwa muda na kuwapatia wananchi ambao hawana mashamba ili waweze kupata mashamba na makazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Serikali iangalie kwa jicho la upole eneo la Mbulumbulu Karatu kwa umaarufu wa kilimo cha ngano ambacho sasa kimeshuka sana na hata eneo hilo kuwa chanzo cha uharibifu mkubwa wa Ziwa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe mtaalamu wa kutosha kwa wakulima katika eneo hilo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mtikisiko wa uchumi mwaka 2008 kulikoenda sambamba na upungufu mkubwa wa chakula duniani ambapo bei za chakula ziliongezeka kwa 80% katika kipindi cha miezi kumi na nane, nchi zenye upungufu mkubwa wa ardhi (Korea China)

wameamua kuwekeza kwenye kilimo kwa kutafuta ardhi katika nchi mbalimbali za Afrika (Tanzania ikiwa mojawapo) kwa madhumini ya kuzalisha chakula cha kutosha kwa matumizi ya nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu ni kwa kiwango gani Wizara yake imejipanga kukabiliana na changamoto hii hususan katika dhana nzima ya kulinda ardhi ya kilimo inayotakiwa kwa manufaa ya wakulima wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uhaba wa uhitaji wa mafuta duniani, nchi za Magharibi zilikuja na dhana ya uzalishaji wa nishati mbadala hali iliyopelekea kuaminika kwa wanaojiita wawekezaji na kupewa maeneo makubwa, ardhi iliyokuwa ya kilimo cha chakula katika maeneo mbalimbali nchini. Kinyume na matarajio, kilimo husika kilishindwa kuanza kutokana na wawekezaji husika kutokuwa na mtaji wa kutosha licha ya kutoyaendeleza maeneo husika bado miliki za mashamba husika ziko mikononi mwa wawekezaji huku wanakijiji wanaozunguka maeneo husika wana uhaba wa ardhi ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alieleze Bunge hili Tukufu, Serikali ina mpango gani wa kurejesha mashamba hayo yatumike kwa manufaa ya Taifa hasa ukizingatia kwamba nchi yetu inakabiliwa na changamoto kubwa sana ya migogoro ya wakulima na wafugaji kutokana na uhaba wa ardhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013 mwezi wa Tano, nchi nane tajiri duniani wakiwa katika Mkutano uliofanyika Camp David, Marekani waliandaa mkakati uliofahamika kama *The New Alliance For Food Security,* mkakati ambao ulizihusisha/uliwahusisha viongozi wa nchi tano za Afrika (Tanzania, Ghana, Ethiopia, Burkina Faso, na Cote d Ivoir) viongozi hao walihusishwa kwa kuwa nchi zao zilikuwa sehemu ya mkakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huu pamoja na mambo mengine ulikuwa na malengo ya kuwekeza katika kilimo kwa ushirika wa sekta binafsi, Serikali, na nchi wahisani (wafadhili). Lakini pia ulikuwa na malengo ya kupunguza/ondoa umasikini kwa watu milioni 50 katika kipindi cha miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mwaka wa nne toka Mpango wa *SAGCOT* (ambayo ni sehemu/zalio/zao la mkakati husika) uliozinduliwa ni Watanzania wangapi wakulima wadogo wadogo waliofaidika na mpango huu? Ni wakulima wangapi wameondokana na umasikini kwa malengo ya mpango yaliyoainishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya wawekezaji ambao walionyesha nia ya kuwekeza katika mkakati tajwa hapo juu ni *Unilever,* Yara na Monsanto.

Mheshimiwa Waziri atuambie, makampuni tajwa hapo juu, yanakuja kufanya uwekezaji upi na katika maeneo yepi?

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na masoko. Wakulima wa mazao ya mahindi na vitunguu saumu, kwa kukosa viwanda vya kusindika mazao haya, wamepata shida kubwa ya soko la mazao yao. Wakulima wananyonywa vibaya na walanguzi *(middle men)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013/2014, Serikali ilituahidi Wakulima wa Jimbo la Mbulu kwamba, kupitia Mpango wa *Makerting Infrastructure Value Addition and Rural Finance (MIVARF)*, wataweza kuboresha mavuno, viwango vya vitunguu, kuongeza thamani kwenye zao hilo na kupatiwa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huo ulifikia wapi? Wakulima wa Bashay hawajapata umeme na bado wanaibiwa na walanguzi.

Ugonjwa hatari wa mahindi *(Maize Lethal Necrosis Disease - MLND)*. Wilaya ya Mbulu mwaka huu inatarajia kupata mavuno ya mahindi ya kuridhisha lakini Kata nne zilizoko Nyanda za Juu zimeshambuliwa na ugonjwa hatari wa mahindi ambao dawa yake haijapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima hao ambao wanategemea mahindi kama zao la chakula na biashara, wanaomba chakula cha msaada kwa ajili ya janga hili kwamba, kwa hali kama hii Serikali itoe fidia kwa sababu wamepata dhara bila ya makosa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya umwagiliaji ni ndogo sana, Tshs. 28.933 bilioni, ambayo asilimia 18.933 ni fedha za nje.

Bwawa la Dongobesh Mbulu litamalizika lini? Mbona imejengwa chini ya kiwango? Serikali ina habari zaidi ya Tshs. 1.2 bilioni imetumika kwa kazi ambayo haifikii Tshs. 500 milioni? Kadhalika, Bwawa la Mangisa katika Wilaya hiyo hiyo ya Mbulu linategemewa na wakulima wa vitunguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Chiza, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Zambi, naamini sasa upele umepata mkunaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kufahamu kama Wizara imefanya tathmini ya kutosha juu ya Wakulima wa Pamba walioathirika kwa kupanda mbegu za pamba ambazo hazina manyoya. Na kama tathimini ilifanyika je ni

hasara kiasi gani ilipatikana? Je, nani atawajibika kuwalipa au kufidia wakulima hao wa pamba hasara waliyopata mfano wafugaji wakati wa ukame walifidiwa au walipewa kifuta machozi kwa kupewa mifugo ili iwawezeshe kuendesha maisha yao baada ya athari waliyopata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali tena sana kupitia Wizara ya Kilimo, kuliangalia upya swala la Wakulima wa Pamba na kujua nini kifuta machozi chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati gani mmeuandaa kuhusu kuwalinda wakulima na kilimo cha mkataba, kwani mwonekano wa nje ni kuwa wakulima wanaumia na kilimo hiki. Wakati wa kilimo mara nyingi ni vigumu kujua bei iliyopo sokoni; hivyo, wakulima wengi huwa hawajui na kufikia kukubali bei anayopewa na anayempa pembejeo. Kipindi cha mavuno bei unakuta inapanda na kumchanganya mkulima na kuamua kuuza Pamba yake kwa mtu mwingine mwenye bei kubwa, hapo kuanzisha mgogoro baina yao.

Napenda kujua mmewasaidia kiasi gani wakulima hao ili walime kwa faida wajitosheleze na kuachana na umaskini wa kipato kwa kazi yao ya kilimo. Ni wakati sasa kuwalinda wakulima wetu wasikate tamaa, kwani kama unafanya kazi ambayo haina faida hutoona sababu ya kuendelea kuifanya. Tuboreshe, tulinde na tuwasaidie kutafuta masoko yenye tija kwa wakulima wetu kwa ujumla wao. Ahsante.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo ya Taifa letu. Hata hivyo, ingawa Wananchi wengi wa Taifa letu wanaishi vijijini na kujishughulisha na kilimo, lakini bado Wizara ya Kilimo haijapewa kipaumbele kwa kutengewa fungu ya kutosha ili kufanikisha malengo ya shughuli zake kwa Wananchi ambao wengi bado ni maskini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule moto ulioanzisha KILIMO KWANZA sijui umeishia wapi? KILIMO KWANZA kilitegemea kiwanufaishe wakulima wa ngazi zote wanaotumia matrekta na wale wanaotumia jembe la mkono waweze kupanda na kutumia matrekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini KILIMO KWANZA kilitumika kama biashara kwa wakulima wadogowadogo? Wakulima maskini walikopeshwa matrekta yenye thamani ya Tsh. Milioni 37 mwaka 2006 na masharti yalikuwa mkopo ulipwe kabla ya kufikia Februari, 2009. Endapo mkopo haukulipwa kufikia tarehe hiyo basi riba ya 2% kila mwezi inatozwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukame uliopo hapa nchini, katika miaka ya 2006 – 2008 wakulima wengi waliokopa matrekta kutoka Mfuko wa

Pembejeo *(Agriculture Institute Fund - AIF)*, walishindwa kulipa kwa wakati kwani walitegemea mvua, kupata mazao, kuyauza na kupata fedha kulipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana badala ya wakulima wadogowadogo kufaidika na matrekta na hivyo kuondokana na umaskini, sasa hivi wako hatarini kufilisiwa mashamba yao kwa kushindwa kulipa riba ya 2% ambayo ukihesabu imekaribia kuwa zaidi ya shilingi milioni 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la tabianchi lisisababishe wakulima wapate adha na mateso namna hiyo. Wengine wamepelekwa Mahakama ya Biashara Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Wizara isiingilie kati kuwatetea wakulima hao ili ongezeko la riba 2% iondolewe na badala yake walipe thamani ya trekta tu, kwani badiliko la tabia ya nchi kwa vyovyote liko nje ya uwezo wao. Vilevile Waziri wa Kilimo afuatilie Mfuko huu wa pembejeo *(Agriculture Institute Fund)*, kwani biashara ya KILIMO KWANZA kwa kuwakopesha wakulima maskini matrekta ili wajikomboe kutokana na umaskini ingekuwa vizuri endapo tabianchi isingebadilika kuwa ukame na riba ya 2% isingekuwepo baada ya kushindwa kulipa deni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wengi walio vijijini hawana elimu ya kutosha, wengi wameishia darasa la saba na wengine hawajasoma kabisa. Endapo tabianchi au hali ya hewa ilibadilika na kuwa mbaya kiasi kwamba, kilimo kilikuwa kigumu na kusababisha kukosekana kwa mavuno tarajiwa ni kwa nini Wizara isishirikiane na wakulima waliokopa matrekta?

Nashauri Wizara iingie kati ili kuangalia jambo hili kwani wote tunaelewa biashara ya matumizi ya ardhi mwenye mamlaka ya kutoa au kutoa mvua ni Mwenyezi Mungu peke yake; hivyo, wakulima wasilaumiwe pale ambapo hawakukusudia hali ya hewa kuwa mbaya kwani ipo nje ya uwezo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mategemeo yangu kwamba, Dhana ya KILIMO KWANZA itaendelezwa kwa manufaa ya wakulima ili wajikwamue kutokana na umaskini unaowatesa. Sote tunajua kwamba, umaskini ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuilaumu Serikali kutoipa kipaumbele Wizara hii. Msingi wa maneno haya ni bajeti halisi ya Wizara hususani *Development Budget* kwa mwaka wa 2013/2014, ambayo ilikuwa shilingi 349,284,608,000. Kati ya fedha hizo ni shilingi 81,040,288,000 tu ndiyo pesa za maendeleo, nazo kwa asilimia kubwa ni pesa za

nje huku ndani ikichangia *only* 23.913. Hali hii inaonesha nchi hatuko makini. Vilevile kwa mwaka huu Fedha za Maendeleo ni shilingi 47,080,270,000 na katika hizo ni *budget* ya maendeleo ni shilingi 25,000,000,000 tu, hali hii haiashirii neema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Serikali kuwa na vyuo mbalimbali vya kilimo kama SUA, Uyole, Mbeya, Tumbi, Tabora na kadhalika, lakini Maafisa Kilimo ni wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeendelea kupuuza Azimio la Abuja na Azimio la Maputo la kufikia 10% ya Bajeti ya Taifa ielekezwe kwenye Kilimo; hatujui sababu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Wizara ilete mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa Maafisa Ushirika ili waweze kufanya kazi vijijini. Pia kuna haja ya Wizara ya Utumishi kutoa vibali vya ajira ili Maafisa Ugani na Mabwana Shamba waweze kuajiriwa, suala linalopelekea wataalam wengi kujiajiri na hata kwenye Sekta zisizo za Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Wakulima imeendelea kuwa dhaifu ilhali ukosefu wa trekta, mbolea, mbegu, madawa na kadhalika inaendelea kuwa pigo kwa Wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao yenye Bodi yamekuwa yakifanya vizuri licha ya changamoto ya ushindani wa soko la dunia kupanda na kushuka kama Korosho, Pamba, Kahawa, Mihogo, Alizeti na kadhalika. Kianzishwe Kitengo cha Idara ya Masoko kupitia Wizara yako ili kusaidia mazao ambayo hayana Bodi kama Chikichi, Alizeti, Mihogo na Kahawa. Ni vyema Idara hii iwepo kama ilivyo kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Bunge lako lilianzisha Tume ya Ushirika ili kusimamia Vyama vya Ushirika pamoja na Sheria yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Vyama vya Ushirika ni vingi sana hapa nchini hivyo vinahitaji usimamizi wa karibu, ni vyema sasa Serikali itenge bajeti ya kutosha ili kuijengea uwezo Tume na kuwe na Maafisa Ushirika wa kutosha ili kusimamia hivi Vyama vya Ushirika.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ongezeko kubwa la migogoro ya kati ya wakulima na wafugaji hapa nchini, jambo ambalo limegharimu maisha ya watu. Hata hivyo, Wakulima na Wafugaji ni jamii inayotegemeana, mkulima kumtegemea mfugaji, vivyo hivyo mfugaji kumtegemea mkulima. Pamoja na ongezeko la watu na shughuli hizo

bado nchi hii ina ardhi ya kutosha kuwagawia wakulima na wafugaji ardhi bila kuingiliana na kuondoa ama kupunguza migogoro hii. Serikali imekuwa ikitoa vipaumbele kwa wawekezaji wakubwa kuliko hata wakulima na wafugaji hapa nchini, jambo linalotia shaka kama kuna nia njema ya kumaliza migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni haja ya sasa ya kufanya utafiti kupata takwimu halisi ya wakulima na wafugaji?

Pili, ni kiasi gani au mpango gani Serikali inafanya kujua ardhi kiasi gani inahitajika kwa wakulima na wafugaji nchini?

Tatu, nini mpango wa kuwagawa na kuwaonesha wakulima na wafugaji maeneo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo bora na cha kisasa hakitaweza kufikiwa na Watanzania 80% wanaotegemea kilimo kama hakuna watumishi wa kutosha katika maeneo yao (Maafisa Ugani). Upungufu huo ni mkubwa sana katika Halmashauri zetu. Ni kwa namna gani tutazalisha maafisa wa kutosha ili kukidhi upungufu huo? Nini mpango na mkakati wa Serikali katika jambo hili?

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja kuhusiana na Zao la Nazi. Kwa kuwa Zao hili linastawi sana katika Mikoa Kanda ya Pwani na kuwa Zao hili ni muhimu sana katika Pato la Taifa na chakula kwa Wananchi walio wengi; na kwa kuwa Zao hili halitegemei sana upatikanaji wa mvua; na kwa kuwa Zao hili limebabwa na ugonjwa wa kuuwa minazi na kudhoofisha uchumi wetu; na kwa kuwa katika Hotuba ya Waziri sijaona kutilia maanani sana Zao hili muhimu; napenda kuiuliza Serikali ni mkakati gani umewekwa ili Zao hili liweze kurudi katika hali yake ya kawaida ili kuimarisha juu ya upandaji minazi mipya labda maeneo husika na unyunyiziaji wa dawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali inipatie majibu mwafaka juu ya tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba nzuri. Nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo ni Wizara muhimu sana maana zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanategemea uchumi wao kupitia kilimo.

Nilipokuwa napitia Bajeti hii sijaona mpango wowote wa Kilimo cha Umwagiliaji katika Jimbo la Busanda, Wilaya ya Geita. Zipo simu za umwagiliaji ambazo zimeanzishwa lakini bado hazijakamilika. Ninaomba maelezo juu ya Skimu ya Umwagiliaji ya Nyamalulu itakamilika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni Kilimo cha Pamba; ninaomba maelezo ya kina juu ya mbegu za pamba ambazo hazikuota. Serikali ina mpango gani kwa msimu ujao kunusuru wakulima ili tatizo hili lisijirudie tena? Vilevile Serikali ina mpango gani wa fidia kwa wakulima ambao waliathirika na mbegu za pamba kutokuota?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita vijiji vingi havina Maafisa Ugani. Tunaomba tatizo hili lishughulikiwe angalau kila Kijiji tuwe na Afisa Ugani. Tunaomba vijana waliomaliza masomo yao wapewe ajira ili watumikie Taifa na tutaweza kuongeza Pato la Taifa na pato la familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo machache. Naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa maelezo au mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nkasi ni mzalishaji mkubwa wa mazao ya nafaka hasa mahindi. Tumekuwa tukipata matatizo yafuatayo katika kuendeleza kilimo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamekuwa na uchelewashaji mkubwa wa pembejeo za kilimo; mbolea, mbegu na madawa, vimekuwa vikicheleweshwa kuwafikia wakulima. Mara nyingi mbolea za kupandia zinawafikia wakulima mwezi wa kwanza, wakati msimu huanza Novemba; jambo ambalo halina tija kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa na Wilaya zake zote ni maeneo ambayo yanakubali kilimo kwa hali ya hewa na rutuba pia kuwa nzuri kwa kilimo. Fursa hii ingetumika kikamilifu na Taifa kuleta Mapinduzi ya Kilimo kwa kuleta matrekta ambayo yanahitajika sana na Wananchi wa Mkoa huu, lakini hayapo. Huu ni uzembe wa sisi Viongozi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iamue kuleta Viongozi wenye kupenda kuendeleza Kilimo ili Kilimo kishamiri na kuleta usalama wa chakula nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iamue kwa makusudi kupanga maeneo ya namna hii kupewa kipaumbele katika zana za kilimo, pembejeo na utaalamu ili yaweze kuleta tija katika kilimo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya barabara ni muhimu sana katika kuendeleza kilimo na wakulima ili kupeleka pembejeo, kusafirisha mazao kwenda kwenye masoko na pia kuwezesha miundombinu ya kuongeza thamani ya mazao kuanzishwa katika maeneo ya kilimo. Kwa hiyo, katika Jimbo langu la Nkasi Kusini, barabara zifuatazo ni muhimu kuboreshwa kwa manufaa ya kilimo na wakulima.

Barabara ya Kasu – Katavi – Chonga – Myula ni muhimu kujengwa katika kiwango cha lami kwani inaunganisha wakulima wengi katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa.

Barabara ya Kitosi – Wampemba, Nkana – Kala na Namanyere – Ninde ni muhimu kutengenezwa ili mazao yaweze kupelekwa Mwambao mwa Ziwa Tanganyika ambako nafaka zinahitajika sana. Soko la bure ambalo lingestawisha kilimo kama barabara zingejengwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vocha za pembejeo ni eneo lenye wizi kubwa. Lazima kuleta utaratibu utakaonusuru hali hii isiendelee. Sioni kama kuna msaada mkubwa kwa Wananchi wa chini kama lengo lake lilivyo, badala yake wananufaika wafanyabiashara watumishi na watu wengine ambao siyo walengwa. Watu wakopeshwe tu mbolea kupitia vikundi vya wakulima ambao wanaweza kujidhamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri uwepo utaratibu wa masoko ya mazao ya wakulima. Kwa sasa uzalishaji umeongezeka na *NFRA* hawataweza kukidhi hitaji la soko. Masoko yatafutwe nje na ndani ya nchi ili kuweza kuwafanya wazalishaji kuongeza juhudi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NFRA* pia wasambaze huduma zake katika maeneo yanayozalisha katika Jimbo la Nkasi Kusini. Maeneo ya Vijiji vya Nkundi, Ntuchi na Sintali, yanatakiwa kuwekwa vituo vya kununulia mazao na *NFRA*. *NFRA* hawalipi ushuru kwa Halmashauri zote ili kuboresha kilimo kwani kilimo kinasimamiwa na Halmashauri zenyewe.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kutoa maoni na mapendekezo yangu katika Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kufanikiwa kupitia *Programme* mbalimbali za Kilimo kwa kukuza kipato cha Mtanzania, kupitia Sekta hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijajua hadi sasa Serikali ina mpango gani kudhibiti wimbi la migogoro ya wakulima na wafugaji. Ninazungumzia suala la mifugo kuvamia mashamba na kula mazao. Binafsi sioni usalama wa chakula kwa watu wa Jimbo la Chalinze na kwa namna nyingine inaashiria kuwa Serikali iandae mpango wa kuleta chakula Jimboni Chalinze.

Pili, kutokana na kuongezeka kwa chakula na udogo wa hifadhi ambao umepelekea Mheshimiwa Waziri Mkuu, kusema mbele ya Bunge kwamba, amelazimika kuuza tani laki moja na nusu. Je, Serikali haioni sababu za kujenga sehemu mpya ya Hifadhi ya Chakula *(SGR)* katika maeneo mbalimbali ya nchi?

Tatu, kutokana na Mji wa Chalinze kuwa sehemu ya kiunganishi cha Miji ya Kaskazini mwa Tanzania na Miji ya Nyanda za Juu Kusini, Kati na Kanda ya Ziwa; je, Serikali haioni sababu ya kujenga maghala makubwa ya chakula Chalinze ili kupunguza wimbi kubwa la magari yanayokwenda Dar es Salaam kufuata chakula na kusababisha uharibifu mkubwa wa barabara kati ya Chalinze na Kibaha kwa upande mmoja na foleni zinazotokana na magari kusimama kwenye mizani Kibaha, hali inayopelekea watu kutumia muda mwingi barabarani kwa umbali mdogo.

Nne, Wilaya ya Bagamoyo ina wakulima wa mazao mbalimbali. Jimbo la Chalinze, Kata ya Mandela ilikuwa ni moja ya maeneo yaliyokuwa yanalimwa pamba hata ukienda pale kuna masalia ya *Ginnery*. Je, ni mpango gani Wizara imeandaa ili kurudisha tena zao hili ambalo linaweza kuwanyanyua Wanachalinze kiuchumi?

Tano, kuhusu kubadilisha kilimo kutoka jembe la mkono kwenda kwenye matumizi ya trekta. Ushauri wangu, wachaguliwe mawakala wengi na kuleta matrekta ili kuweza ku-*control* bei ya matrekta, lakini pia kuwezesha upatikanaji wa haraka wa vifaa hivi muhimu kisekta. Pia mawakala wachaguliwe kule mawilayani ili kurahisisha upatikanaji wa pembejeo hizi na tatu, kulinda bei za ajabu. Serikali iunde utaratibu wa ku-*control* bei za matrekta hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MARTHA M. MLATA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu kwa njia hii ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Wizara kwa juhudi kubwa katika kusimamia shughuli za kilimo na hadi kuleta mabadiliko makubwa katika

Sekta ya Kilimo. Matunda yake yameonekana wazi pale Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipotangaza kuwa, uchumi au pato la Mtanzania limeongezeka. Hiyo yote ni kutokana na kilimo. Pia akiba ya chakula ni kubwa kiasi cha kutaka kuuza ili kupisha nafasi ya chakula kipya kitakachovunwa. Kweli matokeo makubwa sasa yanadhihirika. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi wa yafuatayo:-

(a) Inaonekana mazao yaliyopewa kipaumbele kutengewa Maghala ya Taifa ni Zao la Mahindi peke yake. Je, nafaka zingine kama maharage, karanga, dengu, ufuta, kunde, alizeti na kadhalika inakuwaje na Wananchi wanalima lakini soko ndiyo tatizo?

(b) Zao la Alizeti limekua sana kwa watu kuongeza maeneo ya kulima, lakini bado kuna utata wa bei ya zao hili. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Bodi ya Zao la Alizeti ili kuwe na utaratibu wa kusimamia Kilimo cha Zao la Alizeti na bei?

(c) Ni lini Serikali itautoa kifungoni Mkoa wa Singida katika zuio la kutokulima Zao la Mahindi hata kwenye maeneo yanayostahili kulima Zao hilo? Zao hili limezuiwa na hata likilimwa pato linalotokana na mahindi halihesabiwi katika kukua kwa uchumi wa Mkoa au Wilaya. Naomba Waziri utusaidie ili Mkoa utoke kifungoni.

Je, Wizara imefikia wapi kuhusu matrekta ya SUMA JKT ambayo Wananchi waliyahitaji na mara yakaisha, hadi sasa bado wanasubiri na wengi walishajaza fomu katika Halmashauri zao?

Naomba Waziri anisaidie; hivi katika Wilaya za Mkalama na Iramba, ni Miradi ipi ya Umwagiliaji Wizara inayoitambua na naomba orodha hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusiana na Serikali kutilia mkazo Kilimo cha Umwagiliaji, kwa sababu ni kilimo cha uhakika na wakulima wanaweza kuzalisha zaidi ya mara moja kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Ukanda wa Ziwa Rukwa ni Ukanda maarufu sana kwa Kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu inayotumika ni ya kienyeji, pamoja na Wananchi kuomba Miradi ya Umwagiliaji kupitia Halmashauri zao. Miradi hiyo ni Maleza uliombwa toka mwaka 2005; Msia uliombwa toka mwaka

2005; Uzia uliombwa toka mwaka 2006; na Mradi wa Nkwilo ulioombwa toka mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Miradi hiyo ipewe fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mafuriko ya msimu huu, eneo maarufu la kilimo cha mpunga katika Kijiji cha Ilemba, miundombinu ya umwagiliaji ya kienyeji imeharibika baada ya Mto Mkanga waliokuwa wakiutumia kwa umwagiliaji kuhama njia yake. Wananchi walishatoa maombi kwa Halmashari na Halmashauri iliingiza katika Mpango wa Bajeti ya 2014/2015 na walishaleta katika Ofisi ya Wizara. Tunaomba wasaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Katibu Mkuu wa CCM Taifa alipokwenda aliwaahidi Wananchi kulileta kwa Waziri ili awape kipaumbele kwa sababu ni eneo kubwa la uzalishaji wa Kilimo cha Mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge wa eneo hilo, nilimwona Waziri na nikamweleza; jibu, aliniahdi mimi na yeye kuwa tutatembelea eneo hilo akalione; hivyo, namwomba tufunge safari twende akajionee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja ya Waziri.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja hii. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Timu yake, kwa jitihada za kuboresha Sekta ya Kilimo. Pamoja na pongezi hizi, napenda kutoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupanua Kilimo cha Umwagiliaji, pamoja na hatua ya Serikali ya kuanzisha Tume ya Umwagiliaji na kutenga Shilingi 29.8 bilioni kwa ajili ya Tume hiyo, bado fedha hizi hazitoshi. Kilimo cha kutegemea mvua kimepitwa na wakati hivyo Serikali lazima iongeze fedha za umwagiliaji ili Taifa letu liondokane ne kilimo cha kutegemea mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida hususan Wilaya ya Manyoni ni eneo kame na kila mwaka Serikali inapeleka chakula cha msaada wa njaa, lakini ardhi yenye rutuba ipo tatizo ni ukame. Ili kutatua tatizo hili, Wilaya ya Manyoni imebuni Mradi wa Bwawa la Mbwisa kwa ajili ya umwagiliaji. Tunaishukuru Wizara ilimleta Naibu Waziri, Mheshimiwa Zambi, kukagua maandalizi ya Mradi huu. Ombi letu ni kwamba, Wizara iunge mkono Mradi huu kwa kutenga fedha katika bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliitembelea Skimu ya Umwagiliaji ya Kijiji cha Chikuyu (Manyoni) ya Kilimo cha Mpunga, mwaka 2010. Baada ya kutembelea alitoa ahadi kuwa Serikali itasaidia yafuatayo:-

(i) Kwamba, banio (*intake*) litapanuliwa ili kupitisha magari ya kusomba mazao mashambani.

(ii) Kwamba, mifereji mikuu itajengwa kwa sementi ili isiendelee kupoteza maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ahadi hiyo, kila mwaka Wilaya huomba fedha kwa ajili ya utekelezaji, lakini haijapewa na Halmashauri haina uwezo kifedha wa kutekeleza Mradi huu. Naomba na kuikumbusha Serikali kupitia Wizara hii, skimu hii ikarabatiwe na maji machache yanayopatikana yasiendelee kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Manyoni yenye vijiji 99 ni nusu tu ya vijiji ambavyo vina Maafisa Kilimo wa Vijijii na nusu ya vijiji havina Maafisa Ugani. Naomba Wilaya ya Manyoni ipate mgao wa kutosha wa Maafisa Ugani watakaoajiriwa hivi karibuni. Aidha, Serikali iongoze fedha za kuajiri Maafisa Ugani kama moja ya mikakati ya kusaidia wakulima walime kilimo chenye tija na waondokane na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni tegemeo kubwa kwa maisha ya Watanzania wafikao zaidi ya asilimia 70. Kwa msingi huo, Serikali ilipaswa ielekeze fedha nyingi kwenye sekta hiyo ili mahitaji karibu yote yanayohitajiwa na wakulima yaweze kupatikana. Bahati mbaya, hizo fedha kidogo zinazoidhinishwa na Bunge hazipatikani zote. Kutokana na hali hiyo siyo rahisi kilimo chetu kuwakomboa wakulima wetu. Ipo haja basi Serikali ifanye marekebisho kuhusu changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 62 wa Hotuba ya Waziri unasema Serikali inataka kuanzisha Mfuko Maalum wa kufidia bei ya mazao. Pia inaeleza kuwa, Muswada wa Sheria utawasilishwa ndani ya Bunge hili kwa mwaka 2014/2015. Ninachoshauri, Muswada huo kabla ya kuletwa Bungeni uwepo ushiriki mkubwa wa Wadau wa Kilimo ili Sheria hiyo isije kulalamikiwa mara tu hapo itakapokuwa imeshapitishwa na Bunge. Pia ipo haja kwa vile kunatakiwa kuanzishwa Soko la Bidhaa na Masoko ya Mazao, kuangalia uwezekano wa Mfuko huo kuwafikia wakulima ambao pia watauza mazao yao katika soko hilo na wao wafidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa 71 wa Hotuba ya Waziri, unazungumzia migogoro iliyopo baina ya wakulima na wafugaji. Migogoro hiyo inahatarisha usalama wa nchi yetu na kusababisha Wananchi kupoteza maisha na mali kuteketea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inasema katika kukabili tatizo hilo ni kuanzisha umwagiliaji wa mazao na malisho ya mifugo. Kwa kweli inasikitisha kuona Serikali hii haielewi inachokifanya. Mwaka 2010 Bunge hili lilipitisha Sheria mbili; moja inahusu chakula cha mifugo na sheria ya pili mifugo kuwekwa kwenye maeneo maalum na kuna idadi inayokidhi malisho yaliyopo. Katika eneo hilo, Sheria mbili hizo ndizo tulizoambiwa kuwa ndiyo ukombozi wa migogoro ya wakulima na wafugaji. Leo tunaambiwa umwagiliaji wa mazao ya malisho ya mifugo ndiyo ufumbuzi wa migogoro ya wakulima na wafugaji. Ni bora Serikali iwe na msimamo thabiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Watanzania wote ili kujiinua Kiuchumi, tunahitaji Sekta ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuwa na bajeti ya kutosha, wakulima wa sasa wanahitaji kupata Wataalamu wa Kilimo katika vijiji, Kata, Wilaya na Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wataalam hawa wafanye kazi na wakulima vijijini na ili wafanye kazi vizuri lazima wapewe vitendea kazi kama vile usafiri angalau pikipiki kwa wale wa vijijini na wale wa Wilaya na Mikoa magari ya Idara ya Kilimo wapewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Iringa tunategemea sana Kilimo hasa katika Wilaya ya Mufindi, tunaomba tuletewe matrekta katika vikundi vya wakulima, pia tupewe mbolea kwa wakati kuanzia mwezi wa tisa. Tunaomba tuletewe mbolea katika Jimbo la Mufindi Kusini ili wakulima wapande mazao yao kwa muda unaotakiwa kwa Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mufindi tunalima sana chai na soko la Zao la Chai ni viwanda vya watu binafsi au makampuni ya *Uniliver Tea Company* na *Mufindi Tea*. Wakulima wanauza majani mabichi kwenye viwanda hivi kwa bei ndogo ambayo haiwasaidii sana wakulima wa chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna umuhimu mkubwa wakulima wa chai Mufindi kujengewa Kiwanda cha Chai waweze kusaga majani mabichi na kuuza chai *(finishing product),* badala ya kuuza majani mabichi na hii itasaidia kuboresha bei ya chai kuwa kubwa na mkulima kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nashauri Waziri wa Kilimo aitembelee Wilaya ya Mufindi hasa Jimbo la Mufindi Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kauli mbiu ya Kilimo Kwanza ni muda mrefu sasa nchi yetu imekuwa ikija na kauli mbiu mbalimbali juu ya Kilimo. Kilimo tangu miaka ya 70 wakati wa "Kilimo cha Kufa na Kupona" mpaka sasa "Kilimo Kwanza" hakuna jitihada za kuridhisha kuonesha kwamba sasa kilimo ndio njia mbadala ya kuinua uchumi wa nchi yetu.

Ni kwa nini mpaka sasa bajeti ya miradi ya maendeleo bado ni tegemezi kutoka kwa wahisani? Hivi ni kweli kwamba Serikali iko makini kwa vitendo kukifanya kilimo kuwa ni msingi wa kuinua uchumi wetu? Ni kwa nini Serikali haitoi fedha za ndani kwa wakati na pia haiachani na bajeti ya kutegemea wahisani kwa jambo muhimu kama kilimo? Je, kilimo nacho kinafanywa siasa katika nchi yetu? Serikali itoe majibu ya kina ni kwa nini miradi ya maendeleo bado ni tegemezi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ruzuku kwenye Pembejeo za Kilimo. Ni kwa nini pembejeo za ruzuku kwenye kilimo zimekuwa ni kero kwa wakulima kote nchini kwa kutokufika kwa wakati na ni kwa nini hata zikifika huwa ni pungufu na wakati mwingine kupitwa na muda wa matumizi hususani mbolea na mbegu? Je, tunaamini kwamba suala hilo lilikuwa la kisiasa zaidi na si dhana ya Taifa, kama maneno mengi yanayozungumzwa? Hatma ya ruzuku hii ni nini ili wakulima waelewe na wasiendelee kunyonywa kama ilivyo sasa? Naomba majibu kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zao la alizeti Mkoani Singida. Mkoa wa Singida kwa sasa unaongoza kwa kulima zao la alizeti ambalo umuhimu wake ni mkubwa katika kuinua pato la Taifa na kulinda afya ya Watanzania kwa ujumla. Mafuta ya alizeti ni mafuta ambayo hayana kemikali za kudhuru afya ya mlaji na husaidia magonjwa ya kisukari, moyo na mafuta mwilini. Hivyo basi, kwa umuhimu huu, ni muhimu sasa Wizara ione umuhimu wa kupeleka pembejeo na ruzuku kwa wakati ili kuwaletea tija wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Vyama vya Ushirika vya kununua alizeti. Kumekuwa na mgogoro usiokwisha juu ya uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika Mkoani Singida ambao kwa kiasi kikubwa umetawaliwa na wanasiasa wasioutakia mema Ushirika. Ni wakati sasa wa Serikali kuona umuhimu wa kuingilia kati suala hili la Ushirika kama ambavyo niseme kwamba wanasiasa wasiwe viongozi, pia hata hao watakaochaguliwa wasiwekwe kwa shinikizo la wanasiasa maana wana mchango mkubwa katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utafiti wa Kilimo *(R&D)*. Utafiti ni jambo la msingi sana katika kuinua kilimo na kukifanya cha kisasa zaidi na kutoa mazao mengi bila kutumia nguvu kubwa. Kwa umuhimu wa utafiti, wakulima

hawataweza kujua aina ya mbolea, udongo, mbegu na kadhalika nzuri kwa ajili ya kilimo na hivyo kuvuna zaidi na kuinua pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni busara sasa Serikali iendelee kutenga fedha zaidi kwa ajili ya kazi hii ya utafiti, maana kwa ilivyo hivi sasa, bajeti ya *R&D* haitoshi na hivyo itakwamisha shughuli nzima ya utafiti au kufanywa nusunusu. Vituo vya utafiti vilivyopo vitaweza kufanya kazi yake vizuri na kwa wakati pindi vinapopata fedha za kutosha na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na Naibu wake Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi kwa jitihada zao za kukabiliana na changamaoto mbalimbali za Wizara yao. Aidha, nawapongeza watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Bibi Sophia Kaduma kwa kuwasaidia Waziri na Naibu Waziri kukabiliana na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maoni yangu kuhusu Wizara hii:-

Mosi, katika utekelezaji wa mfumo wa stakabadhi ghalani kwenye korosho. Jambo moja lililo wazi na kero ni gharama za magunia. Kwa kuwa Wizara hutoa ruzuku kwa pembejeo kwa nini Serikali haioni haja ya magunia kuwa ni pembejeo na hivyo ruzuku ikatumika pia kwenye magunia ili kumwongozea pato mkulima?

Pili, kwa nini Wizara ya Kilimo kwa muda mrefu imekuwa ikifanya kazi za maghala (leseni) kwa kujibu na kutoa maelezo mbalimbali kiasi cha kuonekana kazi hizo ni za Wizara ya Kilimo badala ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Ningependa kupata maelezo Wizara ya Kilimo inanufaikaje kwa kulisimamia jukumu hili badala ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwa nini isiweke wazi mwenye jukumu hili?

Tatu, Sheria ya Ushirika ya 2013 imeweka wazi baadhi ya viongozi kama vile wa kisiasa mfano Madiwani, Wabunge, Wenyeviti wa Serikali ya Vijiji na kadhalika kutohusika kwenye uongozi wa Vyama vya Ushirika. Napenda kupata maelezo ni kwa kiasi gani Mrajis wa Ushirika amesimamia jambo hili maana bado tunawaona viongozi hao wakifanya kazi za Ushirika, mfano wa wazi ni kwenye Chama Kikuu cha Ushirika cha Tandahimba na Newala *(TANECO)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho uongozi wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika unashauriwa kuiangalia kwa umakini Ofisi ya Mrajisi. Ofisi hii imekuwa ikilalamikiwa kwa kukosa uadilifu. Mara nyingi hutoa siri ya mdau mmoja

kwenda kwa mdau mwingine lakini pia rushwa. Ni vyema macho yaliyo makini yaangazwe na viongozi kwa ofisi hii ya Mrajisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara kwa juhudi zao kwa kuandaa hotuba hii na kuleta kwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa kufuatilia kwa karibu Vyama vya Ushirika vya Mkoa wa Tabora na hata kuagiza *CAG* kufanya ukaguzi maalum. Ningependa Serikali itamke hapa Bungeni leo ni lini ripoti ya *CAG* itakuwa tayari ili matatizo makubwa yaliyovikumba Vyama vya Ushirika yapatiwe ufumbuzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wengi wa tumbaku Mkoa wa Tabora walibambikwa madeni makubwa na mabenki wakishirikiana na watendaji na viongozi wa Vyama vya Msingi. Kutokana na madeni makubwa, wakulima wengi kuanzia mwaka jana walikosa sifa ya kukopesheka na hivyo kukosa pembejeo na kushindwa kulima. Serikali itasaidiaje wakulima wa Mkoa wa Tabora ili kwa kupitia Vyama vya Ushirika wakopesheke na hivyo waweze kulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imewapa Mawakala wa mbolea 460 leseni za kufanya biashara ya mbolea. Hata wafanyabiashara ni watoa huduma tena kwa wakulima wadogo, kwani wamekuwa kibiashara zaidi mbolea *kilogram* 50 mfuko mmoja pale Dar es Salaam ni sh. 49,500/=, ikifika Mkoani Tabora inauzwa sh. 81,500/= wanadai ni gharama za usafiri. Serikali ieleze Bunge ni maagizo gani au maelekezo wanayopewa hawa Mawakala wa pembejeo ili wawe watu wa huduma na sio biashara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013 Serikali ilibuni utaratibu mpya wa kutoa pembejeo kwa wakulima wadogo kwa mfumo wa kutumia Vyama vya Ushirika na *SACCOS*. Serikali ilitakiwa kutoa dhamana ya 50% ya mahitaji ya pembejeo na wakulima kutoa 20% ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima walihamasika wakatoa 20%, Serikali haikutoa hata shilingi moja Benki, hivyo mpango huu haukutekelezwa. Serikali ieleze Bunge ni kwa nini haikutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huu ambao ulibuniwa na Serikali yenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ameeleza uzalishaji wa tumbaku unatarajiwa kupanda kutoka tani 47,240 mwaka 2013/2014 hadi tani 100,000 mwaka 2013/2014. Kwa sababu ya ongezeko la bei ya soko la dunia, tunayo

historia ya wakulima wa Tabora kuambiwa na makampuni wazalishe zaidi kwa sababu bei imepanda na bei itaongezeka. Baada ya kuvuna tu makampuni wanapanga bei wanayotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna urasimu mkubwa sana kwenye soko la tumbaku. Wakulima wameendelea kuwa maskini kwa kulima zao hili. Serikali iwaangalie sasa wakulima wa tumbaku. Vyuo vya Kilimo vyote vimechoka na miundombinu yake imechakaa. Haya ni maeneo yanayozalisha taaluma na Wataalam wa Kilimo. Serikali ihakikishe Vyuo vya Kilimo vinatengewa fedha za kutosha ili kuboresha miundombinu ya Vyuo, hivyo kuweza kutekeleza majukumu yao ya kitaaluma na kuzalisha wataalam wenye ujuzi wa kutosha.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, usahihi wa Uongozi unapaswa kuwa kwa maslahi ya jamii na kwa kuwa asili ya uongozi ni watu na haki na kwa kuwa pana mzozo wa kififikra kati ya wakulima na Utumishi wa ma-*DC* na ma-*RC*. Kwa hiyo, sasa naomba kushauri Serikali na kuishauri Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji waje kukutana na *TACOGA* (Chama cha Maono ya Wakulima).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ma-*RC* hawana masikio sikivu kwa wakulima, hivyo hakuna mfumo wa Mikoani na katika Wilaya wa kukuza majadiliano ya kukabiliana kwa tija dhidi ya kasoro zilizopo katika *sector* ya pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimya wa Serikali ni kitanzi kwa imani ya wakulima ya kuhusu kuamini Sera ya Utawala Bora wa kuwa ukombozi na uokovu kwa wakulima wa zao la pamba. Upembuzi yakinifu unabainisha kwamba pana mfadhili wa *TGT* hapa Tanzania, kwa hiyo, sasa naomba Serikali ipambanue yafuatayo:-

(i) *TGT* na *TCB* hivi sasa ni uoto wa hamaki za wakulima kwa sababu hawana faida dhahiri za msaada huu, je, una faida zipi za kutiririshwa katika kuonekana una mashiko ya kukabiliana na kero za wakulima, mfano, katika mahitaji ya maghala mbona hakuna chochote, kuchangiwa ujenzi wa karakana kwa mahitaji ya *workshop* za *tractor*.

(ii) Tangu *TGT* aje Tanzania nufaisho lake katika kuwa ni mchango wa MKUKUTA kwa mkulima, ni dhahiri matokeo yapo kwa uwazi na ukweli, wapi? Naomba nisipewe majibu ya nadharia.

(iii) Kwa nini *TGT* na *TCB* wamejiajiri kuwa shurti za kutumia Ma-*RC* wawe ndio amri ya kulazimishwa kilimo cha mkataba ambacho hadi leo, pesa ya wakfu ya mkulima ndio kizunguzungu cha *c/farming*.

(iv) Wakulima wa pamba wanataka kukuza kipato chao wajitegemee kukuza uchumi wa kaya, hivyo hivyo wakulima walijikomboa dhidi ya kuwa vibarua na wanunuzi wa pamba wa kabla ya Uhuru wa Tanganyika. Sasa wakulima wanataka kurejea ukombozi wa Victoria *Federation*. Mfumo wa c/*farming* sio wokovu hasa kuna nguvu kazi yao kutopata thaminisho wakati vibarua hulipwa ajira pale wanapokodishwa kulima katika shamba la mtaka vibarua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM ya Nyerere na Karume ilikuwa ya kujenga wakulima washike hatamu za uchumi. Je, Mheshimiwa Rais Dkt. Kikwete ameleta *TGT* izae mfumo wa kubinafsishwa wakulima wa pamba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, C/*farming,* je, inahusisha vipi wakulima wa pamba? Serikali ina sera ya soko huria vipi C/*farming* ni zuio la soko huria? Je, kwa nini *passbook* hairejeshwi? Bodi ya Pamba utumishi wake hauna sikio sikivu kwa maono ya wakulima na maazimio ya mikutano ya sekta ni yapi yametekelezwa ya kikao cha 2013?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ombi la fidia ya mbegu mbovu za *Quton* kwa nini wakulima wasilipwe pesa tasilim kwa hasara hizo. Mbegu za manyoya zimekuwa na matokeo ya kilo nyingi kwa eka kwa kilimo bora, je, *Quton* hadi sasa wana sifa zipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi wa UK atuambie mwongozo wake kwa *TGT* ni utumishi gani hadi unakuwa nyenzo ya fitina dhidi ya *TACOGA* na atake ifutwe, *TGT* vipi wanataka Mfuko wa Wakulima wa Wakfu ufutwe hasa dhamira ya *TGT* Tanzania ni maono ya kutokana na mavuno ya fikra za wadau wapi? Je, mwongozo wa Serikali kama upo kwa *TGT* unatokana na mwongozo ya watu gani?

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Nia ya kufanikisha malengo yake ipo ingawa tatizo ni uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida ni mmoja wa Mikoa ulioitikia kulima mazao yanayostahimili ukame kama vile mtama na uwele na mwaka huu mavuno ni mazuri. Tatizo la mazao haya ni kushambuliwa na ndege waharibifu wa *quelea quelea*. Usumbufu huu hushusha mavuno ya mazao haya na usimamizi wake kugeuka kuwa *Labour intensive,* Serikali isipotafuta ufumbuzi juu ya kukabiliana na tatizo hili wananchi wa maeneo haya watakata tamaa kulima mazao haya na watakimbilia kulima mahindi bila mvua za kutosha na pia kukiuka maelekezo ya Serikali ya Mkoa ya kulima mazao yanayostahimili ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo cha tumbaku, naiomba Serikali iendelee kuwabana na kuwachukulia hatua Maafisa Ushirika wanaokula njama na viongozi wa Vyama vya Msingi kuhujumu wakulima wa zao hili muhimu linaloingizia Serikali fedha za kigeni. Aidha, namshukuru Waziri wa Kilimo mwenyewe kwa kufanya ziara maeneo ya Mgandu, Mitundu na Mwanapembe kujionea matatizo haya yanayokatisha tamaa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko Itigi kutoka kwa baadhi ya wakulima kwamba mbegu ya mtama waliyopewa msimu uliopita haikuota. Wakulima wakubwa wa eneo hilo kama Bwana Kachema (0754 820989) wamelalamika sana baada na kuambulia patupu walipopanda mtama huo kuitikia kilimo cha mazao yanayostahimili ukame. Nashauri Serikali iwasiliane naye, awape uhalisia wa tatizo hili ili na wao waone kwamba Serikali inawajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia malalamiko haya yapo kwenye zao la pamba kwa mikoa jirani. Inakatisha tamaa kwa wakulima wanapolima na kupanda mbegu kukosa kabisa kwa kutoota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani bado ni wachache mno. Hawatoshi kupita Vijijini kutoa mafunzo ya kitaalam kwa wakulima wetu hasa kwa mbegu mpya zinazosambazwa. Naishauri Serikali ifundishe kwa wingi wataalam na kuwaajiri watalaam hawa kwa kilimo kwa wingi waweze kuwasaidia wakulima wetu walime kilimo cha kisasa chenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wako. Naomba yafuatayo yazingatiwe katika utekelezaji wa malengo ya Wizara yako.

Kwanza, ununuzi wa mazao/nafaka kwa ajili ya ghala la Taifa hukutaja zao la mtama, naomba msisahau kuweka zao hilo linunuliwe pia na *NRFA*.

Pili, kuhusu Kilimo cha mboga na matunda. Hotuba yako haikutaja kwa undani wakulima wa mazao ya mboga na matunda watasaidiwaje? Naomba maeneo ambayo yanalima mazao hayo hasa Wilaya ya Lushoto, tupatiwe pembejeo za ruzuku na ikibidi Serikali iwawezeshe kwa kuwapa mikopo kupitia vyombo vya fedha, madawa ya mimea na mbolea ni muhimu sana kwa uzalishaji mboga na matunda.

Tatu, ununuzi wa mazao mchanganyiko. Shirika la Ununuzi wa Uboreshaji wa Mazao Mchanganyiko, liimarishwe linunue mazao ya wananchi, litafute masoko ya mazao hayo, wasiendelee kuhangaika na usindikaji wakati hawajaimarisha masoko na ununuzi wa mazao.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilianzishwa kwa malengo mazuri. Inasikitisha kwamba Bodi hii hivi sasa haifanyi kazi kwa sababu muda wake umekwisha. Napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri ateue Bodi mpya haraka na kuhakikisha inafanya kazi. Kwa kuwa Bodi hii kisheria inaruhusiwa kukopa katika mabenki, Serikali iwasaidie kupewa dhamana ya mikopo ili iendeleze mikakati yake ya kuinua pato la mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza Bodi hii ishauriwe kuwa, kujenga *Strategic Grain Silos* yaani Vihenge vya Kimkakati na baadaye katika *Community Exchange* kwa mfano katika maeneo ya mipakani, bandarini na kadhalika. Hali hii itasaidia kuwa na masoko ya mtandao kwa mfano, wafanyabiashara kutoka nchi jirani kama Kenya, Malawi, Zambia hana haja ya kuja nchini kununua mazao badala yake ataagiza kimtandao na kusafirishiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia Bodi kufikiria kuweka bandarini vifaa vya kuhifadhi mazao mabichi kama maparachichi, ndizi mbichi, viazi na matunda ili viweze kusafirishwa kwenda masoko ya nchi za nje kwa njia ya meli ambayo ni rahisi kuliko usafirishaji wa ndege ambao ni gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti wa mabadiliko ya tabia nchi. Napenda kusisitiza Wizara hii kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuhakikisha kuna mipango thabiti ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Bila kufanya hivyo, ukame mkubwa na mafuriko yanayoendelea hivi sasa hapa nchini ni tatizo kubwa na yataendelea kuchangia njaa inayojitokeza mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine litakalosaidia kuongeza uzalishaji wa chakula ni Serikali kuweka utaratibu wa kuwapatia vijana wanaomaliza mafunzo ya kilimo katika vyuo vyetu, mitaji na kudhaminiwa mikopo ili waweze kuzalisha chakula cha kutosha. Vijana wengi kutoka Chuo Kikuu Sokoine, Uyole na kadhalika wamezagaa mijini kutafuta ajira za maofisini ambazo hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho bila kusahau, napenda kuwapa pole wananchi hususan wakulima wa mpunga na migomba Wilayani Kyela kwa maafa ya mafuriko yanayoendelea kutokea hivi sasa. Naamini Serikali kupitia Wizara hii itaangalia namna ya kuwasaidia chakula watu wa Kyela kwani mazao yao yameathirika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ushauri huo mfupi, narudia kuunga mkono hotuba ya Wizara. Nawatakia utekelezaji mzuri.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Stakabadhi Ghalani. Kwa muda mrefu tumekuwa tukipiga kelele kuhusu "Stakabadhi Ghalani" hususan wakulima wa korosho Serikali iliahidi kushughulikia suala hili takribani miaka mitano sasa, lakini hadi leo haijachukua hatua yeyote. Nahitaji ufafanuzi ni hatua gani imechukuliwa hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mashamba ya mkonge. Wakulima wakubwa wanaendelea kumiliki maeneo makubwa ya kilimo na wananchi kushindwa kupata ardhi yenye rutuba kwani maeneo hayo yenye rutuba yapo mikononi mwa wawekezaji ambao hutumia hati hizo kukopea fedha katika taasisi za fedha na kuendeleza miradi mingine ya kibiashara na sio kilimo. Tumeshauri mara kadhaa hati miliki hizo zifutwe, hatua hazijachukuliwa, naomba ufafanuzi ni namna gani Serikali inashughulikia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zao la mnazi. Kama inavyofahamika mnazi ni zao la biashara/chakula kwa wananchi wa Mikoa ya Pwani. Minazi mingi inaathirika na gonjwa la kunyauka (mchwa) katika maeneo mengi katika Mkoa wa Lindi/Pwani. Matokeo ya utafiti hayajafanyiwa ufumbuzi hadi leo na Serikali imekuwa kimya tunahitaji ufafanuzi wa hoja.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo mmeshugulikia ununuzi wa zao la choroko baada ya wafanyabiashara pamoja na sisi Wabunge kuleta utaratibu mbovu uliopangwa katika ununuzi wa choroko msimu huu, nasema asante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu jitihada za ziada zinahitajika kwa Mkoa wa Mtwara katika kusimamia ununuzi wa mazao hasa choroko, mbaazi na korosho. Hali ya chakula katika Wilaya ya Masasi kwa msimu huu mavuno hayatakuwa mazuri kwani mvua nyingi zinazoendelea hadi sasa mashamba mengi ya wakulima yamejaa maji, hivyo rai yangu kwa Wizara wapeleke watalaam ili tathimini ifanyike mapema kubaini upungufu wa chakula utakaokuwepo ili wakulima watakaobainika kuwa na upungufu wa chakula wasaidiwe chakula mapema, hasa ukizingatia bei ya chakula kwa sasa inapnda sana kutokana na miundombinu mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara isimamie kuwasukuma maafisa ushirika wetu kuvisimamia Vyama Vikuu vya Ushirika kutoa malipo ya pili na bonasi katika zao la korosho kwani Vyama vimekuwa vikiuza korosho wakulima wamekuwa wanacheleweshewa malipo yao na kupata zaidi ya miezi mitatu. Huu ni wizi na uonevu kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wakulima hivi sasa wameamua kupeleka korosho zao katika vyama vya msingi bila kulipwa naomba wakulima hawa mara baada wanapouza korosho basi walipwe fedha zao zote, kwani hawakukopa katika mabenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pembejeo ndio mkombozi kwa mkulima, naomba sana Vyama Vikuu vya Ushirika kufuatilia kwa karibu sana upatikanaji wa pembejeo kutoka Mfuko wa Wakulima wa Korosho ili pembejeo za wakulima kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wengi zaidi ya asilimia 80 ni wakulima, wafugaji na wavuvi, wengi wanategemea kilimo na wengi ni maskini. Ili kuondoa umaskini wa mtu mmoja mmoja, inabidi sekta ya kilimo iendelezwe, ili kipato cha mtu mmoja mmoja kiongezeke na pato la Taifa lizidi kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuondoa umaskini kwa kuendelea kutegemea jembe la mkono. Kilimo cha jembe la mkono hakina tija. Naipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuagiza na kuingiza matrekta mengi nchini, lakini sehemu kubwa ya Tanzania matrekta hayo hayakufika na kwa sasa hayapo vile vile utaratibu wa kuyapata haukueleweka vizuri. Naiomba Serikali iendelee na juhudi hizo na kuleta matrekta mengine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itueleze ni lini matrekta mengine ya bei nafuu yataletwa nchini? Je, ni utaratibu gani utatumika ili kuyapata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania iliridhia Azimio la Maputo la mwaka 2013, juu ya Kilimo na Usalama wa Chakula *(Agricutule Food and Security)* Azimio hili linataka kila nchi mwanachama wa Umoja wa Afrika kutenga angalau asilimia 10 ya bajeti za nchi zao na kuzielekeza kwenye Sekta ya Kilimo na kilimo kiweze kukua kwa angalau 6%. Hadi leo bajeti ya Tanzania haijafikia asilimia 10% na hivyo hatujafikia lengo. Nchi kama Burkina Faso, Ethiopia, Ghana, Malawi, Senegal wamefikia na kuzidi asilimia kumi. Inabidi sisi kama nchi wananchama wa *AU* tutekeleze hayo makubaliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani na lini itatekeleza Maputo *protocol* na *CAADP - Comprehensive Africa Agricultre Development Programme* ili bajeti ya Kilimo ifike asilimia kumi ya bajeti ya Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera umekumbwa na ugonjwa hatari wa migomba uitwao mnyauko/unyanjano. Mara kadhaa mmesikia kilio cha Wabunge wa Mkoa wa Kagera kuhusu ugonjwa huu. Wakazi wa Mkoa wa Kagera wanategemea ndizi kama chakula na zao la biashara, ugonjwa huu umerudisha maendeleo ya watu nyuma sana. Ugonjwa huu ulianzia kwenye Wilaya moja na sasa umesambaa kwenye Wilaya zote nane na ni ugonjwa ambao hauna tiba. Mgomba ukishaathirika watalaam wanashauri kuwa wang'oe, watu wameng'oa migomba iliyoathirika hadi wamebaki na nusu au robo ya shamba. Inatia uchungu sana kwa mkulima yeye kila siku kung'oa tu lakini tatizo haliishi, watu wanapoteza chakula, kipato na umaskini unaongezeka.

(i) Naiomba Serikali iwekeze zaidi kwenye Chuo cha Utafiti Maruku ili waendelee kutafiti jinsi bora ya kuondoa tatizo la unyanjano/mnyauko.

(ii) Naiomba Serikali iwaonee huruma wakazi wa Mkoa wa Kagera. Iwasaidie katika *operation* ya tokomeza mnyauko/unyanjano. Mkoa unaendesha *operation* ya mwaka mzima ya kuondoa gonjwa la mnyauko. *Operation* hii ina gharama kwa Mkoa na kwa mtu mmoja mmoja kwani kuna vifaa na madini vinahitajika.

(iii) Je, Serikali itawasaidiaje Mkoa wa Kagera ili waweze kutekeleza *operation* hii ya kutokomeza mnyauko kwa ufanisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ushirika ni mkombozi kwa watu hasa wenye kipato cha kawaida. Nimesikitishwa na taarifa ya Mheshimiwa Waziri kuwa sasa Vyama vya Ushirika na *SACCOS* badala ya kuongezeka baadhi vimekufa vimepungua. Kila mwaka Serikali mnaeleza kuwa mnaziwezesha *SACCOS* na mnatoa elimu mbona hiyo elimu inayotolewa na Serikali hatuioni? Mkifanya semina ya siku mbili, hii ndiyo elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa kufanyika mzitambue, muwe na mpango *structured*, unaoeleweka wa kutoa mafunzo kwa wanachama wa Vyama vya Ushirika, Uongozi/Bodi na watendaji. Pili, waweze kupata mikopo ya masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijaandaa mazingira, Mfuko au benki zinazoweza kutoa mikopo yenye riba nafuu na masharti nafuu. Je, ni wapi *SACCOS* za Mkoa wa Kagera wanaweza kupata mikopo ya riba kati ya asilimia nne mpaka tisa na ya muda mrefu miaka miwili, mitatu na kuendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara ya Kilimo kwa juhudi zinazofanywa kuinua hali ya kilimo, lakini katika mazingira magumu ya bajeti finyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuiweka Ngara katika orodha ya Wilaya zinazopata ruzuku ya pembejeo. Bado ni Kaya 5,000 zinafaidika na ruzuku hiyo. Naomba niongezewe Kaya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo bado ruzuku hiyo inachelewa msimu wa kupanda. Ombi langu la Serikali kuboresha mabonde Wilayani Ngara halijajibiwa. Naomba tuharakishe ombi la *Grant* kutoka *ADB*. Rais wa *ADB* yuko tayari kutoa *grant* ili mradi upate ombi kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipato cha wananchi wa Ngara bado kiko chini sana, ni kati ya sh. 170,000/= na 280,000 kwa mwaka. Bado wana uwezo mdogo, kununua trekta kwa bei ya sasa. Naomba bei ya trekta ipunguzwe ili wananchi waweze kujiunga katika vikundi na kununua trekta.

(a) Hatuwezi kuinua kilimo kwa jembe la mkono.

(b) Kwa kuwa kilimo ni sekta ambayo ni ya kipaumbele na iko chini ya *Big Results Now (BRN)*, basi *mechanisation* ya kilimo iwe ni kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ngara ina Vijiji 72, kila Kijiji kinatakiwa kiwe na Afisa Ugani mmoja. Kwa sasa hivi tuna Maafisa Ugani 22 tu. Naomba Wizara isaidie kutuongezea Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani hao wanahitaji vyombo vya usafiri kama vile pikipiki, *DADP* haitoi msaada tena.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala la korosho liangaliwe kwa umakini wa aina yake katika Mikoa ya Kusini kumekuwa wa migogoro kutokana na tofauti ya bei na wanunuzi wadogo wadogo. Kubwa zaidi ni kuwekwa vizuri kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kudhibiti mfumko wa bei ya vyakula katika Jiji la Dar es Salaam. Niombe na msimu huu tuendelee kudhibiti bei hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Ushirika vimekuwa vingi sana, lakini hatuoni Serikali kama wanasaidia Vyama hivi vya Ushirika? Kumekuwa na *SACCOS* nyingi za wakulima, lakini wanajipa nguvu wenyewe kwa wenyewe kwa kukopeshana. Hakuna msaada mkubwa kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MWENYEKITI:** Nampa sasa Naibu Waziri dakika 20 na Waziri utakuja kuhitimisha kwa dakika 40.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye bajeti yetu ya Wizara ya Chakula, Kilimo na Ushirika, ambayo Mheshimiwa Waziri amewasilisha asubuhi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kujibu hoja naomba niseme mambo machache yafuatayo:-

Kwanza, napenda nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ajili ya imani aliyoonesha kuniteua katika nafasi hii ya Naibu Waziri, Kilimo, Chakula na Ushirika, lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Pili na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao najua na wenyewe walikuwa na mkono wao katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Mhandisi Christopher Chiza kwa namna ambavyo alinipokea Wizarani pamoja na Katibu Mkuu na Wataalam wote na wananipa ushirikiano mzuri sana na naahidi kwamba, nitaendelea kuwapa ushirikiano mkubwa sana ili kuweza kutekeleza malengo ambayo yako chini ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana wana Mbozi ambao wameendelea kuniamini na ambao wamenileta hapa Bungeni mwaka 2005 na baadaye mwaka huu Mheshimiwa Rais akaniamini na kunipa nafasi aliyonipa leo, naomba niwaambie wana Mbozi kwamba hawajapoteza kunichagua na waendelee kuniamini na nitaendela kuwatumikia kwa kadri ya uwezo wangu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wanaopita pita kule Jimboni, wanajitangaza kwamba dhambi ana kazi nyingi, lakini naomba niwambie, kuwa karibu na viongozi unakuwa na nafasi pia ya kupata mengi na kwa maana hiyo una nafasi nzuri pia ya kusukuma maendeleo katika Jimbo lako. Naomba niwahakikishie wana Mbozi kwamba, nitaendelea kufanya kazi kwa ushirikiano sana kwa ajili ya kuwatumikia wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme mambo machache sana ambayo siyo rasmi sana kwenye Wizara hapa, lakini alisema mdogo wangu Silinde Mbunge wa Mbozi Magharibi, Wilaya ya Momba, lakini bado iko Jimbo la Mbozi Magharibi, alisema kwamba umepewa nafasi hiyo lakini Mbozi kuna hati mbaya. Mimi peke yangu Mheshimiwa Silinde sina miujiza, lakini wewe na mimi Wilaya ile ni yetu wote, kwa hiyo ukionyoosha mkono kwangu na wewe pia linaweza likawa linakuhusu. *(Makofi)*

Hata hivyo, Mheshimiwa Silinde unajua jitihada zangu nilizozifanya na wewe umechangia na mimi nimechangia tumewasukuma sana viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ili kuwa waadilifu katika utendaji wa kazi na yale tuliyokuwa tunayafanya sasa yalitugawa tukaonekana kwamba wabaya, sasa haya ndiyo matokeo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaahidi kwamba, niko Serikalini, wako viongozi ambao wanahusika na wale wote ambao wamehusika na hujuma katika Wilaya ya Mbozi mpaka tukapata hati mbaya, lazima mkono wa Serikali uwafuate kwamba hawatakuwa salama hata kidogo, kwa sababu naomba nikubaliane kwamba, pesa ya Serikali inapokwenda kule lazima zifanye kazi na hili sitalikubali kwa sababu, kama kiongozi ningependa Serikali yangu ifanye vizuri.

Kwa hiyo, wale viongozi ambao wataonekana ni tatizo na hizi ndizo salam nataka nipeleke kwa viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. Kama wameendelea kuiba hii *honey moon* sasa ya kuiba imekwisha wala haiwezi kuendelea tena. Hivyo hivyo kwa wataalam wote ndani ya Wizara, niko tayari na niko imara sana kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, lazima tuchukue hatua kuona kwamba hela za Watanzania, hela za walipa kodi, hela za Wafadhili zinafanya kazi sawa sawa. Kwa hiyo, hili naomba niwape ahadi.

Rafiki yangu Mheshimiwa Ndassa pia alisema, wewe ulipinga sana mbolea ya minjingu, leo unasemajekwamba uko ndani ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika?

Ndugu zangu, naomba niseme; hata siku niliyoteuliwa na Mheshimiwa Rais, waandishi wa habari walinihoji; unasemaje kuhusu mbolea ya minjingu uliyokuwa unaipinga sana? Mimi nikasema hivi, msichanganye mambo.

Moja, wakulima ndio waliokuwa wanasema kwamba mbolea hii haitufai! Sasa mimi nilikuwa kisemeo na ninaendelea kuwa kisemeo cha wananchi wale. Hivyo hivyo ndipo nilipoingia Wizarani nikamwambia Mheshimiwa Waziri, bado kule Mbozi na Mbeya kuna malalamiko ya mbolea hii ya minjingu. Sisi Wizarani tukachukua hatua, tukawaita wataalam. Wataalam wametupa taarifa. Sasa taarifa za wataalam, kiutafiti, wanasema ile mbolea maeneo mengi haina matatizo. Hizo ndizo taarifa za kitaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupata taarifa hizo za wataalam, nilifunga safari nikaenda kiwanda cha mijingu. Baada tu ya kuteuliwa kama wiki tatu, nikaenda kwenye kiwanda pale, nikazungumza nao, nikawaambia mnasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kiwanda kilikiri kwamba bado mbolea yao siyo sawa sawa; bado ina matatizo katika katika baadhi ya maeneo na kwamba zipo jitihada ambazo wanaendelea nazo kuhakikisha kwamba mbolea ile inakua vizuri na waliniambia kwamba wanaendelea kufanya utafiti katika Chuo cha Utafiti kule Mlingano, Tanga, ili wahakikisha kwamba ile mbolea yao inakuwa *perfect*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata wananchi wa eneo la Mijingu pale na wenyewe walisema, baadhi ya maeneo katika lile eneo, mbolea ile pia haitumiki vizuri.

Sasa tunachosema na kikubwa zaidi tulichoamua Wizarani, tumesema wananchi wasilazimishwe kutumia mbolea, wachague wao wenyewe ni mbolea gani wanataka kuitumia.

Mheshimiwa Waziri wangu, kabla sijateuliwa, tulipolalamika sana, aliandika barua kule Mbeya, kusimamisha utaratibu wa kulazimisha wananchi kuchukua mbolea ile ya mijingu chini ya utaratibu wa ruzuku ya Serikali. Kwa hiyo, wananchi na wakulima walikuwa huru kuendelea kutumia mbolea ambayo wanaitaka wao wenyewe na huo ndiyo utaratibu ambao utaendelea kubaki hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nimesema suala hili la mbolea, niseme pia kidogo suala ambalo amesema Mheshimiwa Machali na lilitokea sana kwenye bajeti ile ya upinzani, linalohusu wizi. Wao wanasema mbolea ziliibwa, hazikufika kule Kasulu, Kijiji cha Ruhita na Kijiji cha Asante Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri mimi nimetembelea Mkoa wa Kigoma, nimefika kule Kasulu, nimekutana na baadhi ya Viongozi wa Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma, nimekutana na Uongozi wa Kasulu, tukazungumza nao, pamoja na Wilaya ya Buhigwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, malalamiko haya pia yaliletwa kwetu na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum CCM Mkoa wa Kigoma. Kwa hiyo, mimi niliamua kuyafanyia kazi yote kwa pamoja, kwa sababu unapopata malalamiko kama Kiongozi, ni vizuri pia kuyafanyia kazi. Kwa hiyo, tulifika pale, tunakiri kwamba upo upungufu mkubwa katika utekelezwaji wa zoezi zima la mbolea ya ruzuku katika Mkoa wa Kigoma, na kwa kweli siyo Mkoa wa Kigoma peke yake; na Mikoa mingine pia.

Sasa zipo hatua ambazo tumechukua kwa baadhi ya viongozi ambao watabainika kwamba wamehusika, na mahali pengine viongozi hawa wamepelekwa Mahakamani. Sasa linapokwenda Mahakamani, linakuwa siyo la kwetu tena.

Naomba nikuthibitishie ndugu yangu Mheshimiwa Machali, ile ya Kigoma na Vijiji vya Ruhita na Ahsante Nyerere, tayari tumeshafanya uchunguzi na taarifa tayari imeshafika Mezani kwetu na wale ambao mlilalamika, tutafanya jitihata kwamba mpate taarifa hii. Sasa hayo ni matukio ya wataalam, tutawapa. Mnaweza mkaridhika, msiridhike, lakini ndiyo matokeo, vinginevyo tunaweza tukaendelea kushauriana.

Kama nilivyosema, siyo azma ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kulinda wezi hata kama wako ndani ya Srikali, siyo azma yetu hata kidogo! Kwa hiyo, hilo tutaendela kulifanyia kazi kwa sehemu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba baada ya kusema hilo, niseme suala la ndugu yangu Mheshimiwa Kangi Lugola. Ndugu yangu Kangi Lugola alisema hapa ndani kuniambia kwamba,"ulipokuwa huku ndani kama *back bencher* ulikuwa unapiga kelele sana." Sasa naomba tu nimfahamishe rafiki yangu Mheshimiwa Kangi Lugola kwamba, nakuwa na nafasi kubwa zaidi nikiwa ndani ya Serikali kuusema zaidi upungufu ambao unawezekana upo. Nakuwa na nafasi kubwa zaidi kuliko hata nikiwa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, lazima tukubali, kuna kukua pia. Sasa unaweza ukawa baba ndani ya nyumba, mama analalamika unga, na wewe baba unalalamika unga, haiwezekani! Kama mama anakwambia unga umekwisha, baba wewe chukua jembe ukalime au nenda katafute chakula.

Sasa mimi nimeingia shambani natafuta chakula, kwa hiyo, siwezi kuendelea kupiga kelele wakati wote. Ni azma yangu kuendelea kumshauri na kumsukuma Waziri na wataalam kwamba tunayapeleka haya mambo sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme mambo mengine machache; najua dakika 20 siyo nyingi sana, nikipata nafasi nitaendelea kuyasema, kwa sababu yako mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeulizwa suala la viwanda vya korosho vilivyobinafsishwa, kwamba Serikali ina mpango gani? Kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, baada ya kuteuliwa, muda mfupi Waziri wangu akanituma nihudhurie Mikutano kule Ofisini kwa Waziri Mkuu; Waziri Mkuu aliniomba, au alinielekeza, nisimamie suala hili la namna gani tunaweza tukaboresha Sekta ya Korosho kwa maana ya viwanda.

Kwa hiyo, tulichofanya sasa, tulichagua baadhi ya viwanda vya kubangua korosho vya sekta binafsi, tukakaa nao pamoja, tukawauliza matatizo yao nini? Wakatueleza, tukaita pia mabenki, tukakaa nao pamoja, tuone kama yanaweza yakawa tayari kukopesha baadhi ya vile viwanda ili viweze kukarabatiwa na kuweza kufanya kazi ya kubangua korosho.

Sasa hilo tulilifanya. Viwanda hivi ambavyo tulikuwa tumevitizamia, kimoja kinaitwa *Agro Focus,* ambacho kiko Newala, kingine Buko Lindi, kingine kinaitwa *Lindi Farmers*, kule Lindi; na kingine kinaitwa Buko kule Masasi.

Sasa hivyo viwanda tunaendelea kuzungumza, na tumetengeneza utaratibu ambao unaweza ukavifanya hivi viwanda baadaye vikapata mikopo au vikaingia katika ubia na watu wengine ili viweze kukarabatiwa na kwa maana hiyo viweze kubangua korosho ambayo ni changamoto kubwa sana katika Sekta ya Korosho kule Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, Mfuko wa *CIDTF* (Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho) pia unakusudia kujenga viwanja kadhaa huko kusini. Kimoja kinatarajiwa kijengwe Mkuranga, kingine kinatarajiwa kijengwe Mtwara na kingine kinatarajiwa kijengwe kule Tunduru. Sasa huo ni Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, kiko kikosi kazi ambacho kiliteuliwa, kilifanya jitihada pia na kiliwasiliana na baadhi ya Vyama vya Ushirika. Kwa mfano, ushirika wa *TANECU***,** ambao unakusudia, na kwa kweli umeshafika mahali pazuri pa kujenga kiwanda cha kubangua korosho, ambacho kikijengwa kitakuwa na uwezo wa kubangua tani 35,000 za korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna kampuni nyingine ambayo inakusudia ijenge kiwanda cha kubangua korosho, inaitwa *Amama Farmers,* lakini kiwanda hicho kitajengwa kule Tandahimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaweza kuona kwamba ziko jitihada za kutosha kabisa za kuhakikisha kwamba tunaweza tukawa na viwanda vya kutosha vya kubangua korosho. Kwa maana hiyo, korosho tunayozalisha nchini leo karibu asilimia 70 inayopelekwa nje na kubanguliwa nje, basi inaweza ikabanguliwa hapa nchini na faida zake, moja itakuwa ni kuzalisha ajira, lakini pia yale mabaki ya korosho zilizobanguliwa, yanaweza yakatuimika kwa ajili ya kutengeneza bidhaa nyingine ambazo pia zinaweza zikawa na faida kubwa sana kwa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa pia, tutakuwa tunaongeza ajira kwa Watanzania, kwa sababu tukiwa na viwanda vingi, maana yake tunazalisha ajira nyingi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika Sekta ya Korosho Serikali imejipanga vizuri, tuhakikishe kwamba tunaweza tukabangua sisi wenyewe hapa nchini, lakini pia kwa faida ya wananchi wetu.

Sasa hili suala limeunganishwa pia na suala la Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Kama ambavyo amesema Mbunge wa Masasi, dada yangu Mheshimiwa Kasembe; ni kweli utaratibu wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani,

kama utaratibu, hauna ubaya hata kidogo. Tatizo ni wale watekelezaji sasa wa jambo lenyewe hili.

Kwa hiyo, tusije tukawakatisha wananchi tamaa, kwamba sasa mbaki wenyewe, halafu waende mmoja mmoja. Tukifanya hivyo Waheshimiwa, hakutakuwa na maana hata ya kuwa na; kwa mfano kuwa na ushirika, hakutakuwa na maana yoyote ya kuwafanya wananchi waje pamoja; na wote tunajua, kwamba ukimwacha mwananchi mmoja mmoja, wafanyabishara watatumia nafasi hiyo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanawanyonya zaidi wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, faida ya kuwa na Stakabadhi ya Mazao Ghalani, moja, ni kuhakikisha kwamba mwananchi huyu anaweka mazao yake pale ghalani akisubiri bei ya mazao yake iwe nzuri. Hiyo ni faida kubwa zaidi. Pia, anaweza akatumia stakabadhi anazozipata, akaenda kukopa benki, na hiyo ni faida nyingine.

Sasa suala la ucheleweshaji wa malipo yale ya pili, hilo ndilo suala la kuzungumza. Sisi kama Wizara na wataalam wetu wanasikia, na vyombo vinavyohusika vinasikia, tunategemea hili jambo liondoke, ili wananchi waweze kupata faida kubwa zaidi kwa maana ya kutumia utaratibu wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mengine ambayo naona niyazungumze sasa, yanayohusiana na Sekta ya Ushirika kwa ujumla. Nawashukuru sana wote ambao wamechangia Sekta ya Ushirika. Moja, niwaambie kwamba kama Wizara, tumejipanga sasa kuhakikisha kwamba ushirika unaweza ukaenda vizuri.

La kwanza, ili tuhakikishe kwamba ushirika unaweza ukaenda vizuri, ni kwamba tumetunga sheria mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili; ninyi Waheshimiwa Wabunge, ndio mmetunga Sheria mpya ya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013. Madhumuni ya kutunga hii sheria mpya, ni kutaka kuona kwamba ushirika sasa unahuishwa, ushirika sasa unakuwa na manufaa kwa mkulima, ushirika huu unaweza ukamwondoa mwananchi huyu kwenye umaskini. Hiyo ndiyo azma ya sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii inawapa nguvu kubwa sasa, wale ambao watakuwa wanasimamia ushirika wenyewe. Moja, kama tunavyojua sheria ya nyuma, ilikuwa na udhaifu pia kwenye adhabu, lakini sheria hii inaweka adhabu kali sana kwa wale wote ambao watahujumu ushirika wenyewe. Wanaweza wakafungwa miaka miwili, wakalipa faini ya Shilingi milioni mbili, lakini pia adhabu zote mbili zikaenda pamoja, wanaweza

wakafilisiwa mali zao pale watakapobainika wamehujumu ushirika, na mambo ya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, watu wamezungumza kuhusu udhaifu. Udhaifu huu tumeuona na sheria hii ya sasa inau-*address* udhaifu huu ambao uko kwenye sheria hiyo.

Moja, sasa tumefufua Idara ya Ukaguzi ya Ushirika, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameshauri. Yote hii ni kuupa ushirika nguvu ili uweze kwenda kufanya vizuri zaidi. Pia tumehakikisha kwamba *COASCO* ambalo ni Shirika la Ukaguzi la Vyama vya Ushirika, tunalipa nguvu zaidi, lakini tunataka wawe na wataalam wazuri zaidi ili waweze kusimamia sana ushirika na kwa maana hiyo wananchi wakauona ushirika unakuwa na manufaa kwao kuliko ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze jambo lingine la *KNCU* limezungumzwa sana, Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro wamekuwa wanazungumza sana; mzee wangu Mheshimiwa Mrema amezungumza sana, lakini rafiki yangu Mheshimiwa Selasini amekuwa anazungumza sana, wanaupigia kelele sana na Wabunge wote wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla.

Naomba niwaahidi kwamba Wizara iko tayari kabisa kusimamia Vyama Vikuu vya Ushirika, ikiwepo *KNCU* pamoja na vyama vingine. *(Makofi)*

Kwa kweli naomba niwaeleze na niwafahamishe Viongozi wa Vyama Vikuu vyote vilivyoko nchini, kwamba kama walizoea kuupeleka ushirika kama mali yao binafsi, muda huo haupo tena. Nami nimepewa kusimamia Sekta ya Ushirika. Nimemwambia Waziri na ameniruhusu; lazima nifanye kazi, lazima niende huko nione matatizo yao na tuchukue hatua kwa wale wote ambao watakuwa wanafanya vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa nimeshaenda kule Mtwara, nimeshaenda Kigoma, tumeenda maeneo mengine kule Arusha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunausimamia ushirika na kwamba unafanya vizuri na tunaendelea kwenda katika maeneo mengi zaidi ili tuhakikishe kwamba Ushirika huu unafanya vizuri. Nimekwenda kule Mwanza, *Nyanza Cooperative Union,* inalalamikiwa sana. Lazima tunataka tuhakikishe kwamba nani hasa ambaye ni tatizo kwenye ushirika, ili tuwape wananchi imani na ushirika wao, ambao sisi tunaamini unaweza ukawaodoa katika umasikini.

Zile nyumba za Moshi pale zilizotaka kuuzwa tumesimamisha, lakini pia shamba la NGararagua ambalo lilitaka lisimamishwe, tumesimamisha utaratibu huo na wale wote ambao wanahusika, lazima tuchukue hatua.

Kule Mtwara kulikuwa na Chama ambacho wamehodhi soko la mazao kwa kampuni moja; tumesema siyo kazi ya Vyama Vikuu au Vyama vya Msingi kuhodhi soko kwa ajili ya kumnunulia bidhaa mtu mmoja. Tumesema wananchi wafanyabishara wote ili kuruhusu ushindani wa kweli. Ili mwananchi apate bei nzuri, lazima wanunuzi wawe wengi, washindane, na ni jukumu letu sasa kusimamia kwamba bei ya mazao ni nzuri. Hilo ndilo tunalisimamia, kuhakikisha kwamba linaweza likafanyika vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala amezungumza hapa rafiki yangu Mheshimiwa Rage, Rais wa Simba, sijui kama yupo humu ndani, na wengine, wamekuwa wanasema kwamba ni vizuri mazao haya ya wakulima, kwa mfano tumbaku, wanasema wakulima wengi hawataki kulipwa kwa dola. Sasa sijui. Inanishangaza! Kwenye kahawa wanaweza kusema hivyo hivyo, kwenye tumbaku wanaweza kusema hivyo hivyo na mazao mengine makuu. Wanasema hawataki kulipwa kwa dola kwamba wao wanaona wananyonywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niwaarifu kwamba Serikali iliajiri Mshauri Mwelekezi. Huyu Mshauri Mwelekezi, alifanya kazi yake, akatupa taarifa. Kimsingi taarifa aliyotupa ni kwamba, kinyume chake ndiyo sahihi, kwamba ukiuza kwa dola una faida zaidi kuliko kuuza kwa Shilingi. Sasa wananchi na wakulima wanasema, wao wanaona ni faida kuuza kwa Shilingi. Sasa hili jambo tunaweza tukaendelea kushauriana, tuone ukweli wenyewe uko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba…

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Kengele ya mwisho? Ya pili?

**MWENYEKITI:** Ya pili.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru kwa kunisikiliza, naunga mkono hoja ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, dakika 40.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii ili niweze kuhitisha hoja yangu ambayo nimetoa asubuhi.

Naomba nianze kwanza kuwashukuru wote ambao wamechangia hoja hii, kwanza waliochangia kwenye hotuba ile ya Waziri Mkuu na Waliochangia hoja hii kwa kuzungumza humu ndani na wengine kwa kuandika, wote tutaendelea kuwashukuru. Sasa kwa sababu siwezi kuwataja hapa, nitaomba wenzangu tujitahidi, hata kwa barua tutawaandikia angalau kuwashukuru, maana yake sasa hatuwezi tena kuwataja hapa. Lakini tutawaandikia hata barua angalau kuwashukuru kwamba mmetuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya wachangiaji tukianzia wale waliochangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, waliogusa kilimo na hawa wa leo, wamefikia 118. Nazungumzia Sekta ya Kilimo; hii inaonyesha jinsi gani sekta hii ilivyo muhimu sana kwa kila mmoja. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa jinsi mnavyokiona kilimo kwamba ni sekta ya mhimili wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru wale ambao wamechangia kwa kujenga. Kwa sababu kuna wengine wamechangia kwa kujenga wakiwa wanatoa kabisa hotuba zao, wakiwa wanatoa hoja na michango mizuri, wakilenga kuboresha kilimo. Pia wako wengine ambao wamechangia kwa kubeza tu. Ni haki yao nao kubeza. Nao nawashukuru kwa sababu wameonyesha uelewa wao kwamba kubeza ndiyo kazi. Lakini sidhani kama ndiyo kazi nzuri, kwa sababu kama unabeza tu na huna mchango wowote wa kuboresha, nawe huna maana vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tabia kwa kweli ya kutukana tukana, lakini mimi natarajia uniambie Waziri ungefanya hivi na hivi, tunaweza tukaenda mbele. Sikatai mchango wa mtu yeyote. Mimi siku zote nasikiliza michango, Mzee Shibuda akizungumza, Mzee Cheyo akizungumza, nikona hapa kuna mantiki, tunazungumza na yeye yuko hapa. Mahali ambapo tunakubaliana, tunakubaliana. Lakini mtu ambaye anasimama tu kusema, hapa hakuna kitu, hapa ni hivi; ah, basi na wewe ni bure vilevile. Maana yake huna msaada wowote wa kunisaidia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie wakati huu kusema kwamba, inawezekana pia hotuba yangu muda haukutosha kuisoma vizuri kutokana na muda wenyewe, mnaona ratiba za zamu hii. Nitoe mfano tu wa ndugu yangu Mheshimiwa Kangi Lugola pale, yeye amesema, mimi sijaona mahali ambapo Waziri amezungumzia habari za *Price Stabilization Fund,* wakati ukurasa wa 62 unasema na hatua tuliyoifikia. Maana yake ni kwamba alikuwa hajapata muda wa kusoma, akaelewa. Kwa hiyo, namsamehe bure tu, kwa kuwa alikuwa hajaisoma vizuri. Mambo yake yale ya mzigo, wala hakuna mzigo wala kiroba hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nakubaliana na michango yake. Ninachoweza kusema ni hivi, niwaombe wote kwa ujumla, kwamba badala ya kusema walete wapiga kura wako, wamzomee Waziri, hutapata lolote! Kikubwa, tuchangie kuboresha, tupitishe bajeti, halafu Mheshimiwa Mbunge sasa, wewe ni mwishoni twende wote, Wabunge wote, wawe wa Upinzani, wa CCM, twende kwenu, tukaangalie matatizo ili tuangalie tunayatatuaje kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko tayari kwenda Majimbo yote, kwa akina Kangi Lugola, kote, ili tuweze kuyatatua mtatizo ya wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, naomba niseme kwamba haiwezekani tukawapa majibu yote. Kwa kweli michango ilikuwa mizuri, yenye afya; tutakachokifanya, ni kuhakikisha kwamba tunawaandikia majibu yote, halafu tuwaletee. Sasa nitajitahidi tu labda nijibu baadhi ya hoja kwa bango kitita hiki kwa ujumla wake. Maana nikisema nianze moja mpaka nyingine najua kengele itagonga tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na Kamati yangu ya Kilimo, Maji na Mifugo. Kwa kweli Kamati hii naishukuru sana kwa sababu inaonyesha ni Kamati pevu maana tangu ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho wao kazi yao ni kuchambua udhaifu na kutoa *solution*. Kwa hiyo, yote ambayo wametushauri, nataka niwahakikishie kuwa tumeyachukua, tumeyapokea, na kwa kweli walianza tangu tukiwa Dar es Salaam kule wakati wa kuchambua ile hotuba yangu na randama. Yote waliyotushauri tumeyapokea.

Nashukuru pia kwa kuona kwamba tunastahili kuongezewa fedha ili kilimo kiweze kuongeza juhudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme pia kwamba hapa hakuna habari ya kusema; hawa sijui ni wa Chama Cha CCM, sijui fedha zimewekwa hapa kwa ajili ya kulinda hiki, hapana! Mbona katika Kamati ile ya Kilimo wamo Wabunge wanaotoka Upinzani? Ninathubutu kusema kwamba walichangia vizuri na wanatoa hoja nzuri, na mmoja ni Mheshimiwa Sakaya. Yeye hachangii kwa ushabiki tu! Akichangia unaona kabisa kwamba huyu mtu anaelewa Sekta anayoizungumzia. Kwa hiyo, kwa kweil nampongeza sana Mheshimiwa Sakaya kwa sababu kazi anayoifanya inaonesha kwamba kazi anayoitaka ni kilimo kiweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nizungumze moja baada ya nyingine katika mambo ambayo tumeyaweka kwa *clusters*. Hoja moja ambayo ilitolewa ni hoja ya *stimulus package*, naomba mnisikilize sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja inasema inahitaji ufafanuzi wa matumizi ya Sh. 48,000,000,000/= za *stimulus package* zilizotolewa na Benki Kuu kwa ajili ya kuchochea uchumi katika kukabiliana na msukosuko wa uchumi ulioikumba dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niweke wazi na niweke vizuri hapa kwamba fedha zile za *stimulus package* hazikuwa kwa ajili ya Sekta moja ya Kilimo, ilikuwa ni *stimulus package* ya mdororo wa uchumi kwa Sekta nyingi zaidi ya Kilimo. Sasa majibnu yangu ni kama ifuatavyo:-

Serikali kupitia Benki Kuu ilitekeleza mpango wa kunusuru uchumi kwa kuweka utaratibu wa vigezo kwa wale wote walioathirika na mdororo wa uchumi duniani. Waombaji walioathirika na mdororo walitakiwa kuwasilisha maombi yao kupitia benki zilizowapatia mikopo kama uchambuzi wa awali kabla ya kupeleka Benki kuu.

Kutokana na mdororo wa uchumi uliotokea msimu wa mwaka 2008/2009, Serikali kwa kutambua jukumu lake la kuwalinda wakulima na wafanyabiashara, ilitenga fedha kwa ajili ya kuwafidia wafanyabiasha waliopata hasara kutokana na kukosa soko la mazao yao.

Mazao makuu yaliyohusika katika utaratibu huo ni pamoja na pamba, kahawa na zao la mwani. Nadhani ndiyo maana zao la pamba hapa nimeamua kuli-*pick* lakini pamba, mwani na kahawa, mazao yote haya yalihusishwa katika shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliweka vigezo stahiki kwa waathirika pamoja na muda maalum wa kuwasilisha madai yao. Hata hivyo, kasoro zilizojitokeza katika zoezi hilo ni pamoja na baadhi ya wafanyabiashara kuwasilisha madai yasiyokuwa sahihi, wafanyabiasha kuwasilisha madai yao baada ya muda uliotolewa kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo maelezo ambayo mpaka sasa ninayo. Kama kuna hoja ile inayosema tunataka tuyaone orodha ya makampuni, nakumbuka hoja hii ilishaletwa hapa Bungeni na mlimwomba Waziri wa Fedha atoe orodha ya hayo Makampuni ambayo hasa hasa yanahusika na Sekta ya Kilimo yaliyonufaika na *stimulus package*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yangu kwa Mheshimiwa Gekul, sijui kama ndiye Waziri Kivuli lakini nadhani leo anakaimu tu.  Unakaimu! Nitakuwa nakuonea, lakini ukishakuwa Kaimu, unakaimu kweli kweli. Wewe ndiwe Waziri Kivuli, kwa hiyo lazima nikujibu tu.

Orodha ya makampuni katika Sekta ya Kilimo yaliyonufaika na fedha za *stimulus package,* kiasi cha Shilingi bilioni 20 kati ya Shilingi bilioni 48 ipo. Waziri wa Fedha aliahidi atawapa. Sasa kama wewe ndiwe Waziri Kivuli, uwe kivuli kweli kweli sasa; mwulize Waziri wa Fedha atakupa orodha hiyo, usiniulize mimi kwa sababu mimi sisimamii sekta zote. Waziri wa Fedha aliahidi atakupa orodha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yalitakiwa pia maelezo kuhusu kasoro zilizobainika katika ukaguzi wa matumizi ya fedha hizo, na majibu nadhani ni hayo hayo kwamba taarifa kamili mtaipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya bajeti ya fedha za maendeleo kwamba kwa kiasi kikubwa zinatolewa na wahisani: Je, ni hadi lini kilimo chetu kitaendeshwa na wahisani? Kulikuwa na hoja pia kwamba licha ya kuongezeka kwa bajeti ya Kilimo kuanzia mwaka 2003 ambapo tulikuwa na Shilingi bilioni themanini na nne na nusu hadi 2011/2012, Shilingi bilioni 926 ukuaji wa sekta hiyo umekuwa ni mdogo kwa wastani wa 4% tu kwa mwaka.

Mheshimiwa mwenyekiti, hii najumuisha pamoja na hoja nyingine. Nataka niwaeleze tu kwamba ukuaji wa Sekta ya Kilimo, ni kweli Sekta ya Kilimo inakua kwa asilimia 4.3. Lakini ukuaji wa Sekta ya Kilimo, mimi sio mtaalam sana wa mambo haya, lakini najua kabisa ukokotoaji wa ukuaji wa Sekta ya Kilimo huwezi kuukokotoa tu kwa sekta moja tu ndogo ya mazao. Ukuaji wa Sekta ya Kilimo unaathiriwa na mambo mengi zaidi tu ya mazao, zaidi tu ya fedha za umwagiliajki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima uangalie mambo mengi ambayo yanasaidia kilimo kikue. Hata barabara zinasaidia kilimo kikue, hata usindikaji unasaidia kilimo kikue. Sasa ukichungulia tu zile fedha zinazoingia kwenye kilimo ukasema hizi ndizo zitakazokokotoa na kuonesha ukuaji wa Sekta ya Kilimo naamini utakuwa hututendei haki kwa kuchukua fedha zile tu zilizoingia kwenye Kilimo ukasema hizi ndizo zimesababisha Sekta hii isikue. Kwa hiyo, nadhani hapo ingetazamwa kwa mtazamo mpana kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sasa nitumie nafasi hii kujibu hoja inayosema, mgawo wa fedha kwa Sekta ya Kilimo umekuwa unaongezeka kwa takwimu tu, lakini fedha halisi zinazotolewa ni kidogo. Vile vile kulikuwa na hoja ya kwamba, tumefikia wapi katika kutenga asilimia 10 ya fedha, yaani ile *Maputo Resolution*. Serikali katika kipindi cha miaka minne kuanzia 2009/2010 hadi 2012/2013 tumekuwa tukitenga fedha kwa mtiririko ufuatao:-

Mwaka 2009/2010 tulitenga jumla ya Shilingi bilioni 722 sawa na asilimia 7.6; mwaka 2010/2011 tulitenga Shilingi bilioni 903.8, sawa na asilimia 7.8; mwaka 2011/2012 tulitenga Shilingi bilioni 926.2, sawa na asilimia 6.8; na mwaka

2012/2013 zilitengwa Shilingi bilioni 1,103, sawa na asilimia 7.4. Sasa utaniuliza, hela hizi ziko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Sekta ya Kilimo tunazozikokotoa kuonesha kutenga kwa Sekta ya Kilimo ni fedha zote zile ambazo zinakwenda Wizara ya Kilimo, nyingine zinakwenda TAMISEMI, nyingine zinakwenda Mifugo, nyingine zinakwenda kwenye misitu. Yaani *sub-sectors* au sekta zote zile ambazo kwa *definition* ndizo Sekta ya Kilimo; ndizo hizo wanakokotoa wanakupa *figures* hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipenda kupata ufafanuzi zaidi, basi uende Wizara ya Fedha, watakupa mikokotoo hii. Hata mimi mwenyewe nazipata kutoka Wizara ya Fedha. Hivi ndivyo tunavyokokotoa sasa mchango huu kwenye Sekta ya Kilimo. Msije mkafikiri labda ni fedha hizi ambazo kwa kweli nawashukuru mnanipigia debe kwamba ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba pia wakati mwingine tusije tukawa tunalaumu tu; tuishukuru Serikali nayo, wakati inapofanya vizuri tuipongeze. Kwa sababu mimi mwenyewe nimekuwa nashiriki, nakwenda vikao vingi vya *FAO*, na swali hili linaulizwa vikao vingi. Ukitulinganisha na nchi nyingine inawezekana wengine wametupita, lakini nchi nyingi hizi tulizo pamoja, wala sitaki kuzitaja lakini katika *region* hii, wote hakuna ambaye ametufikia. Sisi tumejitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kutulinganisha sisi na nchi kama Burundi huitendei haki Tanzania. Wewe tazama hata Tanzania yenyewe, *size-wise, nine hundred forty five thousand square kilometers.* Wanaotufuatia kidogo ni Kenya, nafikiri wako kwenye *five hundred forty eighty*. Hizi nchi nyingine ni ndogo ndogo, *population-wise* sisi tuko juu. Kwa hiyo, *resources* zetu vile vile hata kujitahidi kutenga angalau kiasi hiki, mimi nasema tumejitahidi kiasi, lakini bado kuna kazi ya kufanya.

Sasa ninachotaka kusema hapa ni nini? Ndiyo maana nilisema, tusibeze tu kwamba hatujafanya chochote, nadhani pale ambapo Serikali ikifanya inastahili nayo ipongezwe kwa jitihada ambayo imeonyesha. Kwenda kwenye asilimia 7.8 kuelekea kwenye 10, naamini kwa mwaka 2015/2016 tutakuwa tumefika kwenye asilimia 10.

Mheshimiwa mwenyekiti, kulikuwa na hoja inasema katika fungu namba 43, Wizara imepanga kutumia Shilingi bilioni 271.6. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 2,765.1 ni kwa ajili ya usafiri peke yake. Kati ya hizo Shilingi milioni 877.2 ni za ununuzi wa magari, Shilingi milioni 994.9 ni za ununzi wa mafuta na vilainishi na Shilingi milioni 893 ni kwa ajili ya nauli ya ndege. Hoja ilikuwa kwamba fedha hizi zimetenga kwa vitu ambavyo havina *direct relationship* na ukuaji wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua alichokifanya Waziri wangu Kivuli ni kukokotoa fedha zote kutoka kila kifungu na kuzijumlisha. Sasa jibu langu hapa ni hivi, Wizara ina majukumu mengi. Kwa mfano, tumezungumzia masuala ya kufundisha, mkasema hivi Wizara hii haiajiri wataalam mpaka wawe wanatumia fedha nyingi kwenda kusomesha?

Ndugu zangu gharama za kusomesha, kwa mfano kusomesha mwanafunzi mpaka apate *Ph.D,* na hapa tumezungumzia utafiti, kila mahali tumesema utafiti, tutenge 1% kwa ajili ya utafiti. Watu wanaofanya utafiti kwa sehemu kubwa ni hawa watu ambao wanasomeshwa mpaka wanapata *Ph.D*. Kuwasomesha watu hawa mpaka warudi hapa siyo lelemama, ni gharama kubwa.

Kwa hiyo, fedha hizi zote ukizikokotoa, siyo fedha tu ambazo zimekuja kwa ajili tu ya kusafiri kwenda kusoma kozi na kurudi. Ni pamoja na kusomesha watu kwa taaluma mbalimbali waende wapate mpaka shahada za uzamivu. Kugharamia watu wote hao pamoja na safari zao, kuwalisha, na utekelezaji wa miradi ambayo inatekelezwa katika ngazi za Wilaya; fedha zote hizi tunagharamia sisi.

Sasa tumetenga hela kwa ajili ya pikipiki; kwa ajili ya usafiri. Hapa tumekuwa tunajenga hoja kwamba tupeleke wataalam. Tuna vijiji zaidi ya 12,000; tunataka Wagani 15,082, kila Kijiji kipate Afisa Ugani. Tumekubaliana kwamba tupeleke huduma za umwagiliaji mpaka kwenye ngazi ya Halmashauri. Yuko mmoja amelalamika kwamba hizi Ofisi za Kanda zinafanya nini? Sasa tumejitahidi tukasema tunataka tupeleke huduma hii mpaka kwenye Halmashauri. Tumeamua kwamba tupeleke huduma za ushirika mpaka kwenye Halmashauri.

Watu hawa ndugu ndugu zangu hawawezi kufanya kazi bila kutengewa fedha za vitendea kazi, ndiyo maana ya kusema tuweke huduma hii, tuwape pikipiki, tuwape magari, tuwape vitendea kazi.

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani fedha tulizoweka hapo siyo kwa ajili ya kujifurahisha tu, tumeziweka makusudi kabisa na tumeziweka baada ya kufanya mahesabu. Bahati nzuri wataalamu wangu ndani ya Wizara ya Kilimo, naomba Mheshimiwa Gekul nikwambie kabisa, katika Wizara ambazo zimebarikiwa na Mwenye Mungu kuwa na wasomi, Wizara ya Kilimo wapo. Nami sitaki kubeza uwezo wao kwamba baada ya kufanya ukokotoaji na kuwasiliana na wenzao, wamefikia mahesabu haya. Siyo kwamba labda wameweka tu, wamechukua makaratasi na kujibandikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie mfumo wa vocha za pembejeo za mazao. Hili nadhani nilizungumzie kwa ujumla tu. Ni kweli utaratibu ule wa vocha za pembejeo umekuwa na athari kubwa. Lakini niwakumbushe tu, tulipoanzisha utaratibu wa vocha za pembejeo hatukusema Watanzania wote tunawapa ruzuku. Lengo ilikuwa kwamba tutoe ruzuku kwa baadhi ya wakulima ili wakulima hawa wakishazoea vizuri matumizi ya pembejeo wawe vichocheo halafu tutafute utaratibu mbadala wa kuwapatia, na hasa wao wenyewe waweze kujinunulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siamini hata kidogo kwamba inawezekana Serikali ndiyo ikatoa mbolea, mbegu na pembejeo zote kwa wakulima wote wa Tanzania. Hilo haliwezekani, tutakuwa tunajidanganya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda changamoto ambayo imejitokeza ni kwamba mfumo ule wa vocha za mazao kwa kweli umetuathiri, ndiyo maana ndugu yangu Mheshimiwa Machali pale akisimama, na kwa yaliyompata kule Kasulu lazima apige kelele. Nakubaliana naye kwamba kweli utaratibu wa vocha umetuathiri.

Baadhi wameutumia utaratibu huu kujitajhirisha wenyewe, wengine wametumia mwanya huu kwa kuwa wakulima hawaelewi vizuri, kuwarubuni wakawapa Sh. 5,000/=. Ni kweli wamefanya hivyo! Ndiyo maana tumefika mahali tukasema, tuubadilishe utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ambao tumeona mbadala ni huu ambao tumejadiliana na ninyi wenyewe, tukasema tuangalie utaratibu.

Kwanza, uwe mbadala, tuokoe fedha za Serikali, lakini utaratibu huu uwe endelevu. Utaratibu wenyewe ndiyo huo tumebuni kwamba, sasa tutumie vikundi, tutumie Vyama vya Ushirika, tutumie *SACCOS*, tutumie *AMCOS*, lakini hizi nazo zina vigezo mbalimbali. Zinatakiwa zenyewe ndizo zikope kutoka kwenye mabenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Serikali katika utaratibu huu itakuwa ni kuweka fedha; kwa mfano, Serikali ikiweka Shilingi bilioni moja, basi benki nayo inaongezea Shilingi bilioni moja halafu inamkopesha mkulima. Sasa mkulima kupitia kwenye Chama chake aende mwenyewe akanunue pembejeo. Tunadhani utaratibu huu unaweza ukawa mzuri.

Kwa kweli nataka nikiri kwamba msimu uliopita tulitarajia uanze, haukuweza kuanza, kwa sababu kubwa mbili. Moja, mabenki yalitaka Serikali itoe fedha *up-front* na mabenki hayakupenda dhamana ya kuandikiwa karatasi. Lakini unajua tunapoanza utaratibu mwanzo wa mwaka kabla fedha za Serikali hazijaanza kukusanywa, inakuwa ngumu kidogo. Hapo kidogo kulikuwa na changamoto, lakini tumeamua sasa, tumefanya mazungumzo na

Waziri wa Fedha, kama tulivyofanya kwenye ununuzi wa mazao, tukapewa fedha mapema, vivyo hivyo tunatarajia Serikali sasa itatoa fedha mapema, tutaingiza kwenye mabenki haya, na utaratibu huu tunaamini utaweza kuwasaidia wakulima.

Vile vile tunaanza kubuni njia nyingine kwamba kama *fall-back position;* katika maeneo mengine tumeanza mazungumzo na makampuni. Makampuni ambayo yatakuwa tayari, yenyewe kwa ridhaa yao kwenda kuwakopesha wakulima pembejeo kwa utaratibu tutakaokubaliana nao, hayo nayo tutayapa nafasi. Lakini lengo letu ni kufuta utaratibu huu wa vocha, tuangalie jinsi tunavyoweza kutumia utaratibu huu wa kukopa kupitia kwenye vikundi vya wakulima.

Mimi naamini kama tukifanikiwa, utaratibu huu utakuwa ni endelevu zaidi kuliko utaratibu ule tuliokuwa nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko swali lilisema, asilimia 40 hadi 70 ya pembejeo za ruzuku haifiki kwa walengwa, na upotevu wa Shilingi bilioni 58.4 mpaka bilioni 102 kwa takwimu; sina hakika na *figures* hizi. Ninachoweza kusema ni hivi, tulimwomba *CAG* kwamba atufanyie ukaguzi wa mfumo mzima wa ruzuku ya pembejeo kwa kutumia vocha, ule mfumo tulioutumia huko nyuma.

Pamoja na kwamba huo tumeufuta lakini haina maana kwamba matokeo ya ukaguzi wa *CAG* yakisema mfumo ule haukuwa mzuri, na kweli inaonesha kwamba kulikuwa na *anomalies* hapa na pale. Haina maana kwamba wale watakaobainika kwamba walithibitika kwamba wao wamepona sasa kwa sababu tumeingia kwenye mfumo mwingine, bado wale watakaobainika kwamba walihusika kufilisi au kuiba fedha kwa utaratibu uliopita, wengine tumeshawachukulia hatua, lakini wengine ambao bado hatujawakamata au hawajathibitishwa, matokeo ya utafiti au ukaguzi yatakapotoka wao nao sheria itachukua mkondo wake.

Bado ziko kesi mbalimbali ambazo ziko Mahakamani, nami siwezi kwenda kuwalazimisha Mahakama kwamba zitoleeni hukumu haraka kwa sababu najua kuna taratibu za kufuatilia kesi za namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hili kwa sababu kulikuwa kuna hoja inayosema, "Serikali kutowachukuliwa hatua walalamikiwa wa wizi wa Pembejeo."

Ndugu zangu siyo kwamba Serikali haijachukua hatua yoyote ile. Kesi kama ziko Mahakamani, ninyi wenyewe ni muhimili hapa, sisi ni Bunge hapa, tunasema tunasimamia Serikali, lakini naamini hata sisi kama Bunge hapa,

sidhani kama mna mamlaka ya kwenda kule Mahakamani na kusema, sasa hivi tunataka hii kesi iishe. Sidhani! Maana ule ni muhimili mwingine, unaendelea kufanya kazi.

Kwa hiyo, sisi kwa kufanya hivi ni kwamba tunaheshimu tu ule muhimili, wale watakapomaliza kazi yao, uchunguzi ukikamilika, watatupatia matokeo na Serikali itachukua hatua ili angalau haki itendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo nafikiri kwa kifupi tu yako mengi, lakini nadhani muda wetu hauwezi ukawa mrefu kiasi cha kupitia mambo yote. Naomba niende kwenye mambo mengine machache ambayo ni ya kiujumla niliyoyachukua wakati mnachangia.

Katika suala zima la usalama wa chakula, nilisema mwanzoni kwamba, hivi kila kitu jamni ni lazima kulaumu? Yaani mninyime raha tu, kwamba Waziri wa Kilimo! Kila kitu, Waziri wa Kilimo! Hata nilipofanya vizuri, hamsemi hapa umefanya vizuri? Muwe mnasema bwana. Ina maana hata mimi nitawaambia na ninyi pale mlipofanya vibaya na nyinyi mmefanya vibaya vile vile. Muwe mnanisifu! *(Makofi)*

Sasa mimi ninawaambia mwaka huu. Ndiyo, msifu! Tumejitosheleza kwa chakula asilimia 118, bado mnakataa! Tunakwenda kuuza chakula sasa, mpaka tumefika mahali tumeanza kuwauzia *World Food Program*. Hivi sasa tunafanya mazungumza na Serikali ya Sudan, kupitia Ubalozi wetu uliopo Nairobi ili tuwapelekee chakula wenzetu wale, wana taabu. Yako Makampuni mengi yaliyoniletea maombi, "tunaomba Waziri uturuhusu tukauze." Nikawaambia rukhsa! Mradi mfuate taratibu za Serikali tu.

Sasa hili nalo la kuuza; hivi kupata asilimia 118 ni balaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Selesini, eh, afadhali ufanye namna hiyo! Mimi nadhani hapo tumefanya vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Haya, kuhusu upatikanaji mzuri wa chakula; Taarifa ya Benki Kuu, Taarifa ya Serikali, inasema upatikanaji wa chakula umechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza mfumuko wa bei kutoka asilimia 12.1 mwezi Jananuri, 2013 hadi asilimia 6.1 mwezi Aprili, 2014, mwulizeni Gavana wa Benki. Ni kwa sababu ya upatikanaji wa chakula. Pigeni makofi basi! *(Makofi/Kicheko)*

Ndiyo. Hapo ni kwenye Usalama wa Chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 14 Aprili, *NRFA* ilikuwa imelipa madeni yote ya wakulima na Mawakala waliouziwa nafaka hizo. Lakini kwa

sababu ya ufinyu wa Bajeti, *NRFA* haijaweza kulipa madeni ya ushuru wa Halmashauri mbalimbali zinazoidai na nimesikia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maneno ya faraja kwamba tumewaruhusu *NRFA* kukopa kutoka Benki ya *CRDB*. Pia tumewaruhusu wauze chakula hiki kwenye *World Food Program*. Sasa fedha zitakazopatika, ambazo zimekwishaanza kupatikana, zitatumika kulipa madeni haya. Kwa hiyo, tutaanza kuyalipa pole pole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Waziri wa Fedha, nimeongea naye, ameniambia kabisa kwamba najitahjidi kukutafutia fedha ili umalize madeni yako ya *NRFA*. Nami naamini hanidanganyi. Kwa hiyo, nadhani hiyo ni habari njema kwa wale ambao wanaidai *NRFA*.

Ndugu zangu, lingine ni kwamba tumeamua tuuze, kwa sababu kama nilivyosema katika hotuba yangu, kuna kila dalili kwamba katika mwaka huu au msimu huu wa mwaka 2014/2015, hali ya chakula kama mambo hayabadilika itakuwa nzuri zaidi kuliko hata msimu uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hali itakuwa hivyo, hatuna budi kupunguza kwenye maghala yetu ili angalu tupate mahali pa kuweka tena chakula kingine kinachokuja. Lakini nimewaeleza pia kwamba kwa mara ya kwanza basi hatuishia kununua mahindi tu, tutanunua pia na mpunga. Maana hatujawahi kununua mpunga, na kumekuwa na kelele sana kutoka kwa wale wanaolima mpunga. Kwa hiyo, wenzangu wale wanaolima mpunga; mipunga mizuri ile, Shingo ya Mwali, Tule na Bwana, Nikamate Sawasawa, ya kila aina kama itaonekana inafaa *NRFA*, itainunua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia kengele ya kwanza imegonga, naomba nimalizie na eneo langu la umwagiliaji. Ni kweli kwamba iko miradi mingi ambayo haijakamilika. Iko miradi, siwezi kuitaja yote, lakini wako Wabunge kama vile Mheshimiwa Aza Hamad, Mheshimwia Silinde, ameitaja kwa majina; miradi ya Ishololo, Masengwa, Naming'ong'o, nami ninaijua miradi hii yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie jambo moja ambalo naomba na nyinyi mnisaidie, maana yake wote ninyi mnatoka katika Halmashauri zenu. Halmashauri nyingi zinazo fedha ambazo ni *carry over funds,* ambazo ni za Umwagiliaji na ziko ndani ya Halmashauri zenu. Hebu na nyinyi basi mnisaidie. Maana mimi kwa haraka haraka, nilivyotizama, nimegundua kwamba, hizi fedha ambazo tumepeleka na hasa zinatoka Mfuko wa *District Irrigation Development Fund,* tukazileta huko kwenye Halmashauri, fedha nyingi bado hazijatumika na ziko chini yenu, na ninyi Wabunge ni Madiwani kama

mimi. Sasa msitarajie kwamba Waziri ndiye atakayekuwa anaingia katika kila Halmashauri zote hizi.

Nanyi mnisaidie mnapokwenda kule, hebu ziulizieni kwamba fedha za Umwagiliaji zilizokuja kwenye Halmashauri, zimetumika kujenga Miradi hii? Kama hazijatumika vizuri, ziko wapi? Ikiwezekana, nanyi mnisaidie, mniamie ili angalau sisi kwa pamoja tuzifuatilie. Sasa mikikaa tu kunilaumu, wakati mimi kazi yangu wakati mwingine ni kuwaleteeni huko kwenye Halmashauri; mnaniomba fedha, nawaletea, halafu mambo yasipokwenda vizuri kule, mnaningoja kuja kuniambia hapa, mtakuwa hamnitendei haki. Maana mtakuwa mnaniuliza nami tena nawauliza. Mkisema mnawaleta Wakulima kunizomea, nami nakuja nawaambia, mwazomee huko huko! *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, hebu tusadiane, hizi fedha ambazo ziko kwenye Halmashauri, tuhakikishe kwamba zinatumika.

Naomba niwahakikishie kwamba miradi ile ambayo kwa bahati mbaya haijakamilika, Serikali tumejipanga kutafuta fedha hata nje ya vyanzo vya Serikali. Viko vyanzo vingine hapa huwezi kuviona. Kwa mfano, fedha zinazotoka kwenye Mfuko wa *Food Aid Counter Part Fund,* zile hazijadiliwi humu, kwa sababu zinakuja wakati wowote ule. Zinapotokea, basi tuna-*allocate* kwenye miradi. Nami nimesema fedha za namna ile, mwaka huu tumepata Shilingi bilioni nne, bado tunapata tena fedha nyingine. Zote hizo tutazielekeza kuhakikisha kwamba ile miradi ambayo ni viporo, haikukamilika, nayo angalau tuhakikishe kwamba tunaifanyia kazi ili ikamilie.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Silinde, usiwe na wasiwasi Mradi wako wa Naming'ong'o ule utakamilika, *inshallah* na Waheshimiwa Wabunfge wote naamini mtaweza kupata kile mnachokihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala huhitaji kuniambia bado ni dakika sita, maana najua hoja ni nyingi kweli! Hata nikisema nizijibu zote, sitaweza kuzimaliza.

Mheshimwia Mwenyekiti, labda nimalizie tu na jambo moja la pamba. Mambo mawili; pamba imezungumzwa sana humu ndani. Mimi mwenyewe nalima pamba pia. Kwa hiyo, nawaomba wale wanaolima pamba katika Mikoa hiyo inayozalishwa pamba, dhahabu nyeupe, wala msifikiri kwamba mimi nina bei za zao la Pamba. Mzee Cheyo, Mzee Shibuda na wengine wote, mimi sibezi zao la pamba.

Mheshimwia Mwenyekiti, tamaa yangu ni kuona kwamba changamoto; *and this has been my spirit, always!* Changamoto zote zinazosibu zao la Pamba tunazishughulikia. Mkizungumzia habari za Kilimo cha Mkataba, mimi sisemi

kwamba Kilimo cha Mkataba, hakina changamoto. Kama vile ninavyosema stakabadhi ghalani, sisemi kwamba haina changamoto, ziko changamoto.

Ninachokisema ni kwamba changamoto zile ambazo zinakisibu Kilimo cha Mktaba, tunatakiwa tuzitazame ni zipi. Nimesema pale kwanza. Kuwapa Elimu, maana ukimwambia mtu ingia kilimo cha Mkataba, kama mwenyewe hajui mkataba ukoje, anasaini nini? Hilo ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotamani kuona ni kwamba watu wanaelewa wanachokifanya kabla hawajakifanya. Ndiyo maana nimesema, tutaendelea kuwaelimisha.

Nimeahidi hata baada ya Mkutano huu, natamani tukae na wadau wa pamba, tuzungumze mustakabali wa zao la pamba, tuwaite wakulima wa pamba *per se,* wale wakulima ambao ndio wazalishaji wa pamba. Wala sio wakulima *fake fake!* Maana wakati mwingine nikiagiza wakulima wa pamba, mnaniletea wakulima mliowachagua kuja kunipa maelezo. Tuwapate wakulima ambao ndio wenyewe, *they put their fingers* kulima pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kule Mtwara niliwahi kuulizwa kwamba huyu Stakabadhi Ghalani, ni nani hana hata mkorosho hata mmoja? Kwa hiyo, hiki kilimo cha pamba, wale wakulima wote wa pamba. Naomba kabisa mniamini, dhamira yangu ni kuhakikisha kwamba tunatoa changamoto zote.

Mimi nimekwenda kule nimeangalia dawa zisizoua wadudu, ni mimi ndiye niliyesimamisha zile *Agriculture Packs* zote kwamba zisiingizwe sokoni mpaka zifanyiwe tathmini, na zilifanyiwa tathimini. Zile zilizoonekana hazifai, ziliondolewa Sokoni. Mpaka sasa hivi ninavyozungumza, tutaendelea na zoezi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mbegu ya *Quton,* mlipo nilalamikia kwamba hii mbegu ya *Quton* mahali pengine bei kubwa, nikasema kama bei ni kubwa lakini inafaa, wakulima wanaitaka, ni Sh. 1,200/=; ninachoweza kufanya, basi tuingeize ruzuku. Ndipo tukaingiza ruzuku ile ya Shilingi bilioni 4.8, bei ikashuka mpaka Sh. 600/=.

Pamoja na hayo ikaonekana kwamba mahali pengine mbegu hiyo haikuota. Sasa taarifa tumeipata kwamba maeneo yote ambayo mbegu hii haikuota vizuri; unajua ilikuwa siyo rahisi kuwahukumu watu kwamba sasa tutamwambia nani? Kama ni yule aliyetoa, afidie, bila kujua ni wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitabu namwonyesha Mzee Cheyo na Wakulima, ndiyo tathmini ya orodha ya Wakulima wa pamba ambao mbegu haikuota katika msimu huu. Kazi hii imekamilika, sasa *this is a good starting*

*point,* ili uweze kusema sasa hawa watu tunazungumza nao namna gani. Lakini msimu ukiisha tu unaanza kusema sasa, tunakwenda, haikuota mpifidie huyu, haiwezekani. Hata namna ya kuzungumza kwamba tunafanyaje; *Quton* mwenyewe tunamlipaje; ilikuwa ni ngumu.

Kwa hiyo, hatua ya kwanza ambayo nimeichukua ni hivi. Tumefanya *evaluation* tukakuta, hawa ambao mbegu haikuota, dhamani yake ni Shilingi bilioni 1.7.

Kwa hiyo, nimesimamisha, fedha hizi hazitalipwa kwa *Quton* kwa sababu kumlipa ni sawa na kulipa bure. *(Makofi)*

Kwa hiyo ndugu zangu, ninaomba nimalizie tu kwa kusema tutaendelea kufanya hivyo, na wale wote ambao watepeleka pembejeo feki, bado naamini tunao utaratibu mzuri ambao tunaweza tukafikia. Kwani kuna kazi gani?

Kama tumemthibitisha huyu kwamba ndiye aliyepeleka hiki feki, madawa ni feki, naye amesababisha, tukahakikisha kisheria kwamba ndiye aliyesababisha, bila shaka kutakuwa na mfumo fulani kwamba yeye atafidia. Lakini sasa tukisema tu jumla jumla kwamba Serikali ije ifidie, nadhani tutakuwa hatuitendei haki Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niwashukuru tena Ndugu zangu wote kwa michango yote mizuri, kwa kuwa wasikivu, naomba mwendelee kuniami, mni-*support* ili angalau nami niendelee kuwasaidia katika muda huu uliobakia nikiwa Waziri wa Kilimo.

Nami nawaahidi sitawaangusha, nitashirikiana na nyinyi, naomba mniite.

Kwa bahati nimepata Naibu Waziri Mchapa Kazi, muda ni mfupi lakini ameshazunguka Mikoa mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 5 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kif. 1001 –*Admn. and HR Mgt* … … … ... Sh. 108,600,00/=
Kif. 1002 – *Policy and Planning* … … … … Sh. 30,000,000/=
Kif. 1003 – *Finance and Account* … … Sh. 15,000,000/=
Kif. 1004 – *Legal Service Unit* … … … … Sh. 15,000,000/=
Kif. 1005 – *Internal Audit Unit* … … … … Sh. 15,000,000/=
Kif. 1006 – *Procument Mgt Unit* … … … Sh. 20,000,000/=
Kif. 1007 – *Mgt Inform. Syst. & Data Base*... Sh. 6,400,000/=
Kif. 1008 – *Environ. and Social Mgt Unit* … Sh. 10,000,000/=
Kif. 1009 – *Educ. Inform. & Comm. Unit* … Sh. 10,000,000/=
Kif. 2001 – *Irrig. Plan. Design & Privates*… Sh. 41,520,000/=
Kif. 2002 – *Irrigation Infrast. Dev..* …. Sh. 103,480,000/=
Kif. 2003 – *Irrig. Research & Techn. Prom*… Sh. 50,000,000/=
Kif. 2004 – *Irrigation Operations and Support Services* … ... ... ... … Sh. 50,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 24 – Ushirika**

Kif. 1001 - *Administration and Mgt* … Sh. 1,581,461,000/=

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi katika Kifungu kidogo 221300 - *Educational Material, Supplies and Services.* Naelewa kwamba Ushirika unahitaji sana *Educational Materials,* lakini nimeangalia vifungu vyote vidogo, kwenye *Sub-votes* nyingine sioni kama kifungu hiki kimetengewa hela hata kidogo kwenye vifungu vyote, wala hakipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua ni kwa nini? Je, watu wa Ushirika wakati tunapiga kelele sana kwamba watu wanahitaji kuelewa kupata mawasiliano na kujua mambo yanayoendelea katika Ushirika, lakini hakuna. Naomba kupata maelezo kutoka kwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Kifungu gani hicho?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Kifungu 221300 – *Educational Materials, Supplies and Services.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kifungu anachokisema Mheshimiwa Susan Lyimo, zimesambazwa

kwenye sehemu na Vitengo vingine. Yaani tuliona kila Idara ifanye kazi hizo yenyewe badala ya kuwa kwenye sehemu ya Utawala.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu nimeuliza, kwa sababu ukiangalia katika vifungu vingine vyote vinavyofuata hiyo *Sub-vote* haipo, ndiyo sababu nimeulizia ni kwa nini? Kwa sababu anachokisema Naibu Waziri ni kwamba imesambazwa kwenye vifungu vingine lakini ukiangalia vifungu vinavyofuata pia haipo. Ndiyo maana nilikuwa nataka maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, shughuli ya kutoe elimu kwenye ushirika kwenye *Vote* hii ambayo iko chini ya Utawala inaonekana kwamba haikuwa na hela, kama tulivyosema, zinaweza zikafanywa kwa maana ya kwamba kwa sababu kinakuwa hakijatengewa fedha, basi ni jukumu la Katibu Mkuu wa Wizara kuhakikisha kwamba eneo hilo la ushirika linaweza pia kwa maana ya kufanya *reallocation* ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kimesababisha hivyo ilikuwa ni *ceiling*. Sasa inapokuwa *ceiling* imefika, inabidi sasa muamue ni eneo gani lipate fedha na eneo gani lisipate fedha. Lakini bado nasema kwamba elimu hiyo inaweza ikafanyika kwa maana ya kufanya *reallocation* ndani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sussan!

**MHE. SUSSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubaliana naye lakini ni kwamba alikuwa amejichanganya mwanzoni baada ya kuwa amesema kwamba hicho kifungu kiko kwenye vifungu vingine, lakini ni wazi kwamba hakipo. Kwa sababu nimepitia vifungu vingine vyote, hilo fungu halipo. Kwa hiyo, labda anavyosema kwamba Katibu Mkuu atafanya *reallocation, well and good,* lakini mwanzoni alikuwa amechanganya.

**MWENYEKITI:** Ahsante!

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi ya Bunge Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 Finance and Accounts Unit... ... ... Tshs. 80,775,000/=

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - Planning, Monitoring & Evaluation
Unit… ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Tshs. 245,660,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika sasa ugonge basi, huwezi kuwa unasimama kama unasoma Albadir, siwezi kukuona! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naanza kusoma sasa!

Kifungu 1003 Kasma 270200 - *Current Grant to International Organizations*. Kifungu hiki kinapendekezwa kuongezeka kutoka Shilingi milioni 190 za mwaka wa fedha uliopita mpaka Shilingi 360 kwa mwaka wa fedha unaofuata.

**MWENYEKITI:** Hebu soma tena kifungu chenyewe! Tupo ukurasa wa 98!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ukurasa wa 98, *okay* shukrani!

**MWENYEKITI:** Si umeona Abdadir hizo? *(Kicheko)*

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 Legal Service Unit… … … … … … Tshs. 43,750,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Najielekeza kwenye kasma ya 221000 – *Travelling – in – Country* ambayo tunaona kwamba hii ni *Section* ya *Legal Service Unit.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja tu kwa Mheshimiwa Waziri naomba anisaidie. Kwa kuwa fedha hizi ambazo ni *Travelling - in - Country* zinatumika katika kutatua au kushughulikia mambo mbalimbali ndani ya Ushirika hapa nchini na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri unafahamu wazi, nilikuletea barua moja kutoka Chuo cha Ushirika Moshi ambapo ushirika wa pale ulikumbwa na matatizo; kulikuwa na ufisadi mkubwa ambao ulijitokeza na baadhi ya watu wamenyanyasika.

Naomba kupata ufafanuzi, suala lile limefikia wapi? Kwa sababu kuna fedha hata hapa zilitengwa mwaka jana, 2013 naomba nipate ufafanuzi kama fedha hizi zimetumika kikamilifu katika kutatua matatizo pale Moshi, ikiwezekana na maeneo mengine.

**MWENYEKITI:** Majibu!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya ukaguzi imefanyika, ni kazi endelevu, lakini sasa hivi itakuwa ni vigumu kukwambia nikupe *report* ya ushirika. Zipo nyingi kweli! Hapa nina *report* za ukaguzi nyingi, lakini nina hakika hiyo kazi imefanyika. Kwa hiyo, kwa wakati muafaka naweza kukwambia. Lakini sasa hivi ukisema nikupe taarifa za ushirika Moshi na wapi na wapi, itakuwa siyo rahisi kukupatia sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba anipe *specific time* labda wakati nimwone anipe labda hapa pengine kuna *information* ambazo hawezi kuzi-*disclose*. Naheshimu suala la *privacy,* lakini anipe *time* ambapo nitamwona kwa wakati wangu ili kusudi aweze kunipa tujue kinachoendelea ni kitu gani.

**MWENYEKITI:** Mtakutana Jimboni, wote mnatoka Kigoma nyie!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala la Kilimanjaro, aniahidi tu basi kwamba nimwone wakati gani ili aweze kunipa *information* hizo. Kama sivyo, basi nitaondoa Shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ahadi!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Shilingi unaondoa ya nini Mheshimiwa Machali? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Mheshimiwa Machali anakuja kwangu wakati wowote hata...

**MWENYEKITI:** Mpe muda Waziri!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Wewe njoo tu hata kama ni kesho ofisini, maana haya ni mambo ya kiofisi, utapata majibu.

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007 -Management Inform. Unit… … … Tshs. 53,840,000/=
Kif. 1008 - Internal Audit Unit… … … … … … Tshs. 42,885,000/=
Kif. 4001 - Promotion Service Section… … Tshs. 492,350,000/=
Kif. 4002 - Coop. Micro Finance Sect.… … Tshs. 495,100,000/=
Kif. 4003 - Cooperate Banking and Investment
Section… ... ... ... ... ..... ... ... ... ... Tshs. 170,515,000/=
Kif. 4004 - Cooperative Marketing and
Information Sect... ... ... ... ... ... ... Tshs.164,775,000/=
Kif. 4005 - Registration Service Section… …Tshs. 416,185,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 4006 - Inspection and Supervision Service
Section… ... ... ... ... ... ... ... ... ... Tshs. 2,998,822,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chilibunje! Chibulunje! Ah, haya majina mengine! *(Kicheko)*

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu ni Hezekiah Chibulunje! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki, kifungu kidogo cha 220800 - *Training –Domestic,* asubuhi nilisisitiza sana suala la *cooperative of inspectorate,* sasa naona mwaka uliopita, huu unaokwisha kimetengwa pale Shilingi milioni 90, mwaka tunaouombea sasa imeteremka mpaka Shilingi milioni 57 ambapo nilitagemea kwamba Tume ndiyo inaanza na *Cooperate of inspection* ndiyo ilitakiwa iimarishwe kwenye *training*. Nataka maelezo, ni kwa nini kifungu kimeteremshwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mafungu yote ambayo kimsingi Waheshimiwa Wabunge mnaona yamepungua ni suala la kibajeti kama tulivyosema awali. Mnakuwa mmepewa *ceiling,* sasa ni jukumu lenu kama Wizara kuona kwamba pesa ambazo mmepewa kama *ceiling* mnazipanga namna gani.

Kwa hiyo, mnapofika kwenye vifungu vingine kama hiki ambacho Mheshimiwa Chibulunje anakisema kwamba tumepewa *ceiling* hii, kwa hiyo, kwenye *training* ni lazima muweke pesa kiwango hicho. Kwa hiyo, hatuna maelezo mengine zaidi ya hayo kwamba ni suala la kibajeti na hicho ndicho tulichoweza kupewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaafiki eh! Mheshimiwa Susan!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wakati wanachangia pamoja na mimi tuliongelea suala la ukaguzi na tumesema kwamba katika Vyama vyetu vya Ushirika vingi vinaanguka au vinafilisika kwa sababu ya kutokufanyiwa ukaguzi. Sasa niko kwenye kifungu kidogo 220300 ambacho kinahusiana na mafuta ya magari, yaani *fuel, oil and lubricants.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri ameshazungumzia habari ya *ceiling* kwamba Wizara inapaswa kuyapa vipaumbele maeneo ambayo wanaona ni muhimu sana, lakini ukiangalia kwa mwaka huu fedha zimepungua kwa zaidi ya Shilingi milioni 30 na wote tunajua kwamba hawa Wakaguzi hawataweza kwenda kukagua kama hawana magari au mafuta ya magari. Kwa hiyo, nadhani ni muhimu basi hata Wizara ikaona kwamba pamoja na hiyo *ceiling* kuwa ndogo, bado kuna maeneo nyeti ambayo wangeweza kuyaongezea hasa hili la magari ili Wakaguzi waweze kwenda kukagua.

Kwa hiyo, naomba ufafanuzi ni kwa nini kifungu hiki kisiongezwe ili Wakaguzi waweze kwenda kukagua kama ambavyo kilio cha Wabunge wengi, kwamba Vyama vyetu vya Ushirika vimekuwa vikishindwa kujiendesha kwa sababu havifanyiwi ukaguzi wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Ukaguzi wa mara kwa mara!

**NAIBU WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Susan kwa *concern* yake. Nasi kama Wizara, tungefurahi iwe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba kama Mbunge angetaka kuleta mabadiliko, kwa vyovyote vile angekuwa ameleta mabadiliko hapa ili Bunge liweze kuyakubali, lakini katika hatua hii tunachoweza kufanya ni kuliomba Bunge liidhinishe hizi fedha halafu baadaye tunapokwenda kwenye utendaji wa kazi, basi tunafanya *internal reallocation* ili kazi hizi zisiweze kusimama. Mara nyingi tunaweza tukafanya hivi ili kuhakikisha kwamba kazi hizi hazisimami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan!

**MHE. SUSSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawa, nakubaliana naye kwamba wanaweza kwenda kufanya *reallocation*.

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 43**

**Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika**

Kif. 1001 Admin. and HR Mgt… … … ... ...Tshs. 4,569,276,400/=.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyokuwa tumekubaliana kuna orodha ambayo tayari nilishapewa na Vyama vyenu vinavyohusika. Nitawaita wale ambao walichaguliwa na kama kutakuwa na muda, basi nitafikiria na wale wengine.

Tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema.

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Waziri kwani mwaka jana, 2013 alinipatia Shilingi milioni 300 kwa ajili ya umwagiliaji kwenye Jimbo langu la Vunjo, mfereji wa Mchomba. Kwa hiyo, vijiji vilivyonufaika ni Sembeti, Rauya na Matala. Hilo la kwanza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili lililoniamsha hapa ni kwamba Mheshimiwa Waziri amesema sasa hivi kwenye Chama Kikuu cha Ushirika Kilimanjaro amechukua hatua ya kusimamisha uuzaji wa nyumba katika kiwanda cha kukoboa Kahawa; nyumba tatu ambazo zilitakiwa ziuzwe kwa ujanjaujanja, namshukuru sana.

Jambo lingine amesema kwamba amechukua hatua ya kuzuia shamba la Gararagua lisiuzwe kiujanja ujanja, nakushukuru sana. Lakini kwa hatua mlizochukua ni kama mnatibu *symptoms,* yaani ni kama mnatibu dalili, ugonjwa uko pale pale.

Mheshimiwa Waziri kuna kazi nzuri mnazofanya wakati mwingine, sijui inakuwaje. Nikiangalia bajeti ya mwaka jana, 2013 kuhusu *KNCU* ulisema, ili kudhibiti ubadhilifu katika Vyama vya Ushirika, uchunguzi na ukaguzi maalum ulifanyika katika ngazi mbalimbali za Vyama vya Ushirika, ndiyo ukataja *KNCU*. Kwa hiyo, sisi wakulima wa Kahawa tulifurahi sana, tukajua kwamba kweli kazi imeanza. La kwanza!

La pili, kuna taarifa ya Wakaguzi, hapa tunalalamika kwamba Vyama havikaguliwi kutoka *Cooperative Audit and Supervision Cooperation* inayosema kama ifuatavyo:-

Kwamba, *KNCU* imepata hasara ya Shilingi bilioni 3.4 huku ikiwa na madeni yenye thamani ya Shilingi bilioni nne. Tukaona basi hii *report* ya ukaguzi ilishafanyiwa kazi. Nashukuru mwaka jana ulituletea sheria ambayo ni vizuri nikaikumbusha. Inasema: "Bila kuathiri vifungu vidogo moja, mbili, tatu, nne, saba na nane, Bodi itawajibika kwa hasara yoyote iliyopatikana kwenye Chama na kila Mjumbe aliyehusika na hasara hiyo atashitakiwa kwa kosa la jinai na akipatikana na hatia atatozwa faini ya Shilingi milioni tano pamoja na kulipa fidia kwa hasara iliyopatikana."

Sasa Mheshimiwa Waziri, kama mngechukua hatua, wale viongozi wanaotusumnbua kule Kilimanjaro ungekuta sasa hivi wako Gerezani. Lakini mmewaachia, madeni wanadaiwa *four billion* za *CRDB,* sasa hayo madeni wameyapataje? Hakuna anayejua. Sasa wanachofanya ni kwenda kuuza rasilimali. Ndiyo wakaenda huko *TCC* kuuza hizo nyumba na kwenda Gararagua.

Sasa ninachosema, hii sheria mmesema kwamba Bodi inayohusika, hao wahusika watakamatwa, watatiwa adabu, watafikishwa Mahakamani, watalipa, watafungwa; mbona Kilimanjaro hilo halitekelezwi? Ndiyo hilo tu uniambie Mheshimiwa Waziri. Wakulima wa Kahawa wafanyeje? Hawa watu waliowazingira hawa wanaowasumbua na *report* zipo, *report* yako ya bajeti na *report* ya *COASCO*. Ukishalijibu hilo nitajua kama nikamate Shilingi au niachie.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mrema na viongozi wengine wote wa ushirika. Lipo jambo moja ambalo nadhani mnalichanganya. Vyama vya Ushirika siyo Idara za Serikali. Vyama vya Ushirika ni vyenu, ni mali zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina maana kwamba nakataa wajibu wa Serikali, lakini mnapokuwa ndani ya ushirika, watu wanafanya madudu humo ndani ya Ushirika halafu mnaogopana kuchukuliana hatua, mnatupa mzigo sisi wengine. Kwa sababu kama mko pale Moshi, fulani kafanya madudu pale, halafu mkaogopana kwamba hebu msimchukulie hatua, nenda mkamwambie Chiza kule, inakuwa ni tatizo mnaniletea mzigo.

Mnatakiwa ninyi kwanza muanze pale pale Wanaushirika, kwa kuwa mali ni yenu, mkatae jambo lile. Pale ambapo mmezidiwa kwamba kuna mtu

anakaidi, ndiyo mnakuja kwangu. Kwa sababu mambo mengine yanakuja kwangu baada ya ninyi wenyewe kuwa hamkutoa taarifa.

Kwa mfano, nilikuwa sijui kama mnauza hayo mashamba, wale wa *Coffee Curing* walianza kufanyafanya utaratibu wa kuuza, mali ni yao, siyo ya Msajili wa Hazina. Lakini kama wamekubaliana wao mimi bila kujua na hawajaniambia, nitajuaje? Mnaponiambia sasa, ndipo sisi tunaingia kama Serikali.

Sasa narudi kwako kwamba pale ambapo tumetuma Mrajisi kwamba nenda kakague, tuletee taarifa na pale ambapo tunaona kwamba sasa hawa watu wamezidi, lazima tuwasaidie au wengine wamezidiwa nguvu, ndipo tunaingia. Kwa mfano, sasa zile mali za *Coffee Curing* zote, baada ya kuona kuna ujanja ujanja niliandika barua kwamba 'simamisha mchakato huo.'

Haya mambo ya kuuza shamba la Gararagua nimejua siku tatu zilizopita baada ya ninyi kuniambia, lakini mchakato unaendelea huko kimya kimya kwa Washirika. Nao nimewaambia hawatauza kwa sababu kwanza hatuna uhakika kwamba shamba hilo ni lenu au mlikuwa mmepewa na Serikali ili mlitumie tu.

Sasa naomba tu mnapofika mahali mmeshindana huko mtoe taarifa haraka ili na sisi tuchukue hatua. Kwa hawa *KNCU*, ukaguzi umekamilika na Mrajisi atatumia rungu lake kiserikali kuchukua hatua pale ambapo Wanaushirika wenyewe wamesema tusaidie Serikali. Nakuhakikishia tutachukua hatua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mrema!

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mambo yenyewe ndiyo hivyo, nimeridhika. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Mwijage!

**MHE. CHARLES MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika kuchangia Bajeti ya Kilimo nilizungumzia juu ya ugonjwa wa mnyauko ambao umeathiri sana migomba Mkoani Kagera. Lakini mwaka jana, 2013 katika kupitisha bajeti ya kilimo nilikuwa miongoni mwa Wabunge ambao waliiomba Serikali iongeze bajeti na nikawa nimeeleza bayana kwamba ningependa kiasi cha pesa kitakachoongezeka kiende kufanya kazi ya kupambana na ugonjwa Mnyanjano Kagera. Niliahidiwa hivyo na mimi mwenyewe nikaandika andiko la mapendekezo yangu namna gani Serikali ingeweza kupambana na ugonjwa ule. Lakini leo wakati nazungumza nimeelezea kuwa tunachotaka kutoka Serikali Kuu ni Serikali kuchukua nafasi ya Kiongozi, kuongoza *operation* za Wilaya na Mkoa. Lakini Serikali kuangalia namna ya kuwasaidia wale watu ambao migomba yao itafyekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anatoa majibu, suala hili ambalo ni muhimu ambalo watu wa Kagera sasa hawana chakula na hawana chanzo cha mapato ya pesa, hakulizungumzia. Napenda maelezo ya Serikali namna ya kuwasaidia watu wale na ninakusudia kutoa Shilingi iwapo sitaridhika kwa sababu najua kwetu kuna njaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba mtani wangu Mwijage aamini kwamba hili suala wamelizungumza hapa na Wabunge wenzake walilizungumza na mara ya kwanza nilitoa jibu ambalo halikuwaridhisha mwaka jana nikasema tutawaletea mbegu bora za kisasa  na walinijibu hapa kwamba mbegu bora za kisasa hazitatusaidia kwa sababu sisi tunataka Inshakara, Intobe, hatutaki  hizo nyingine.

Kwa hiyo, nikasema, pamoja na yote hayo, tutakachokifanya na ndiyo hatua ambayo tumeifikia Mheshimiwa Mwijage naomba nikupe taarifa; Idara ya Utafiti tayari imefikia mahali ambapo napata matumaini kwamba tunataka sasa tuanzishe *program* ya kuzalidha mbegu hizo hizo za kwenu za asili; Intobe na Inshakara, zile zile za Bukoba ili zizalishwe kwa utaratibu wa *tissue culture*. Tunaamini zikizalishwa kwa utaratibu wa *tissue culture,* tukiweka na ruzuku kwenye mbegu hiyo, wakulima wengi sasa watapata mbegu ile, japokuwa na yenyewe wanasema kama wasipofuata utaratibu na zenyewe baadaye zinaweza zikaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ambayo tumeifikia ni hiyo kwamba tunataka sasa tuangalie kama tunaweza kuweka *program* ya kuzalisha mbegu zile zile za wakulima lakini zizalishwe kwa utaratibu wa *tissue culture* na tunaamini inaweza ikaleta nafuu kwa wakulima wa migomba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage!

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika Mheshimiwa Waziri na Serikali hawakunielewa.

Nilichosema ni kwamba Kagera sasa kuna njaa, migomba imeathirika. kinachopaswa kufanyika kwa sababu huu ni ugonjwa wa mgusano na Mheshimiwa Waziri katika mchango wangu kama wataalamu wako wamenisikia, nilisema nilikuja ofisini kwako na sijui kama walinielewa. Sikuja na mikono mifukoni, nilikuja na andiko, na andiko hilo likachapishwa hata kwenye magazeti nini kifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwamba kinachopaswa kufanyika kwa sababu huu ni ugonjwa wa mgusano yaani *contagious diseases*, mimea yote

iliyoathirika inapaswa iwe *uprooted* na iwe *destroyed*. Wakati unai-*uproot* wataalam wanawaelekeza wananchi kulima mazao ya muda kama viazi; wakati huo huo migomba hiyo unayoisema inapandwa; wakati huo huo kutoka kwenye *Strategic Grain Reserve* tunapata chakula hata kwa bei pungufu. Ndiyo maana Mheshimiwa Mushashu akasema Kagera kuna maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni majanga kama yale ya ukame, kama yale ya kwenye mafuriko kwamba hatuna chakula, lakini ni kwa sababu ya ugonjwa. Kama mnavyowasaidia wale watu waliokumbwa na baa la nzige, ndiyo kitu ninachozungumza. Kama unavyo-*respond* kwenye nzige, sasa na kwetu kuna nzige wengine wanaitwa mnyauko, *how are you responding*? Ndiyo *issue* iliyoko mbele yetu kwamba kwetu kuna njaa. Hatukupenda njaa, migomba yetu imeambukizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza programu na andiko liko kwenye Ofisi ya Waziri. Serikali inasema nini kuhusu hili? Serikali inasema nini kuhusu mapendekezo yangu; yalikuwa hayafai? Mimi niliomba wataalam, nime-*borrow experience* kutoka nchi za jirani.

Kwa hiyo, nauliza, Serikali inasema nini kusaidia mamlaka za Wilaya na Mkoa kuondoa Mnyauko? Wataalam wa Waziri wanasema kutoka Ofisini kwake kwamba kwa miezi mitatu tukifuata hiyo programu ugonjwa wa Mnyauko utakwisha? Serikali inasema nini kuhusu hilo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tu pengine jibu lilikuwa nusu, nimesema tutaweka program. Labda kwa sababu sikwenda zaidi, nimekwenda moja kwa moja nikajikita kwenye kuandaa mbegu za migomba mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo programu anayoizungumza kwa kweli ni programu ambayo hata mimi mwenyewe ilinitia matumaini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hoja ya Mbunge ni kwamba kuna njaa sasa hivi.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, lakini yeye amesema ameandaa programu.

**MWENYEKITI:** Sasa ukiishaanza programu, njaa ndiyo hamna tena!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema tuki-*uproot* wakati huo huo tunatengeneza programu ya kupanda,

lakini tunawatafutia chakula wakati wanaandaliwa hiyo migomba. Kwa hiyo, nakubaliana naye kwa kweli, ni *proposal* nzuri, sidhani kama ina ubaya wowote kwa sababu ni programu ya kutusaidia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage, chakula kiko tayari, onana na Waziri, umeridhika?

**MHE. CHARLES MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natangaza kuondoa Shilingi, sijaridhika yaani ulichojaribu…

**MWENYEKITI:** Ondoa Shilingi tuendelee.

**MHE. CHARLES MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naondoa Shilingi.

**MWENYEKITI:** Kuna yeyote mwingine anayekuunga mkono? Mheshimiwa Mshashu.

**MHE. BERNADETHA K. MSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mwijage. Wakati nachangia nimeeleza hali hiyo hiyo kwamba kuna huo ugonjwa na ni zaidi ya miaka saba huo ugonjwa umejitokeza Mkoani Kagera. Wataalam wote wamejaribu, wameshindwa na sasa hivi wanasema kuweza kuuondoa ni kung'oa ile migomba na labda kupanda mingine.

Sasa tunauliza wale ambo migomba tayari wameshaing'oa, wana njaa, wanahitaji chakula, tulitegemea Mheshimiwa Waziri aseme, tutatenga fedha au tutapeleka chakula kusudi wale ambao migomba yao imeishang'olewa waweze kupata chakula. Tulitegemea kwamba wakati hii operesheni ya kuendelea kung'oa migomba inaendelea wasije wakafa. Haya mambo ya kupanda mpaka huo mgomba uweze kuzaa ni *two years*! Sasa hiyo miaka miwili watakuwa wanakula nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Serikali itupe *commitment,* watafanya nini kusaidia hiyo operesheni? Vilevile watafanya nini kusaidia chakula kwa watu ambao wamepata njaa kwa sabahu ya Mnyauko?

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Mheshimiwa Waziri unatakiwa useme tu, unapeleka chakula ili Shilingi yako ukatumie na mkeo, basi. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tu, sijui tumepishana na watani zangu hawa. Chakula kipo, kama ni hilo suala la kupeleka chakula…

**MWENYEKITI:** Lini? Lini kinakwenda? Watu wana njaa sasa hivi, lini chakula kinakwenda?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Sasa hivi, walete maombi chakula kipo, tunacho kingi tu.

**MWENYEKITI:** Haya, tunakushukuru.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Maombi kwa kawaida yanapita kwenye Halmashauri.

**MWENYEKITI:** Basi Mheshimiwa Waziri,. Mheshimiwa Mwijage chakula kipo peleka maombi.

**MHE. CHARLES MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa jitihada zako. Nitawasiliana na mamlaka na kesho asubuhi Jumapili nitawasilisha maombi ya Mkoa wa Kagera, sehemu zote zenye migomba wananchi wakate migomba, chakula kinakuja. Ahsante kwa Serikali sikivu.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Mheshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo moja ambalo nilikuwa napenda pengine Serikali iweze kutoa kauli yake. Suala hili linahusiana na *issue* ya pembejeo za ruzuku ambazo zinatolewa na kwa kiasi kikubwa imeonekana ni *deal* ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la mbolea ya ruzuku inaonekana ni biashara ya watu, kiasi ambacho sishawishiki na mikakati ya Serikali ya sasa kwamba ile mbolea izidi kuendelea kupelekwa kwenye Mikoa yetu katika maeneo mbalimbali, kwa sababu kuna *experience*. Kwa mfano ukichukua miaka minne iliyopita kwa misimu tofauti ya kilimo, unakuja kubaini kwamba, kwanza mbolea inaenda kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mmoja katika mkoa wa Kigoma peke yake, na imeelezwa hapa kwamba wakulima wanaanza kupanda mwezi wa Kumi, lakini unakuta mbolea inakuja kuanzia mwezi Desemba, Januari pamoja na Februari. Maajabu ni kwamba; Afisa mmoja wa Kilimo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu alipata kusema kwamba, hata kama walishapanda na mahindi yamefikia kimo fulani kikubwa, bado unaweza ukachukua mbolea ya kupandia ukaenda ukaweka kwenye mazao yale, jambo ambalo kidogo hata watu wengine wanalipinga kwamba siyo sahihi.

Mbolea ya kupandia kwenda kuweka kwenye mahindi ambayo yamefikia pengine nusu yangu mimi, ni jambo la ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema, naomba kauli ya Serikali kama hawana mkakati mbadala ambao ni *very scientific*, ni kwanini wasisitishe suala la kupeleka mbolea katika msimu wa kilimo unaokuja nchini kote mpaka Serikali itakapokuwa imefanya *review* na ituhakikishie hakutakuwa na suala la uporaji wa mbolea kama ambao unaendelea hivi sasa? Zimetolewa takwimu kwenye hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Kwenye kijiji cha Lwita peke yake, badala ya kupata kwa mfano mbolea ya minjingu mifuko 500, walipata mifuko 100. Mifuko 400 yote iliporwa. Mbolea ya *ADP,* badala ya kupata mifuko 500 walipata mifuko 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni wizi mkubwa na tatizo hili limekuwa linaendelea. Mamlaka za kiuongozi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na chini ya Mkuu wa Wilaya ambaye ni Mwenyekiti wa Pembejeo, wameshindwa kudhibiti suala hili. Vyombo vya ulinzi na usalama, wakiwemo na TAKUKURU nao wameingia kufanya uchunguzi lakini hakuna *improvement* yoyote kuelekea katika mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Serikali: ni kwanini haitaki kupeleka mbolea ili kusudi mkae na mjipange na mkipata mbinu mbadala mpeleke ili kuepusha suala la wizi wa mbolea, kwa sababu mfumo umekaa kifisadi mno ukiangalia kwa sehemu kubwa. Naomba kauli ya Serikali, kama hakuna majibu ya ushawishi, nakusudia kuondoa Shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza nilipokuwa nilipokuwa na- *wind up* kwamba, mfumo wa vocha ulighubikwa na huo ubadhirifu anaousema Mheshimiwa Machali. Sina kabisa kipingamizi, na ninakubaliana naye. Siyo kwake tu, ni sehemu nyingi, hata kwangu yametokea. Ndiyo maana sasa tumekuja na mfumo mbadala. Huu mfumo hauruhusu mtu yeyote tena kwenda kudanganya mkulima kwa kumpa vocha, kumpa Sh. 5,000/=, maana yake tukiishafanikiwa na huu mfumo, mkulima mwenyewe kupitia *SACCOS* yake anakopa benki anakwenda kununua mbolea yeye mwenyewe, hakutakuwa tena na mtu wa kumchakachua au kumdanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatuwezi tena kuwa na mtu hapo katikati. Sidhani kama hayo yatajirudia tena. Ni mfumo ambao utakuwa ni mzuri, utaondoa mianya hii ya ubadhirifu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, mmeshakubaliana hapa mnakutana kesho, huoni kama utapata majibu mazuri Ofisini kwake kesho? Haya dakika mbili.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilikuwa naomba tu kwamba pengine Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali atueleze ni kwa kiasi gani huyu mkulima asiyekuwa pengine na *assets*, kwa sababu najua kwamba mikopo inawasumbua watu wengi; wengi wangependa kwenda kukopa mikopo kwa ajili ya shughuli nyingine.

Kuhusiana na suala la kuweza kukopa pembejeo, kuna masharti mepesi kiasi gani ili yule mkulima wa kutoka kule kijijini asije kwenda kukutana tena na utata mwingine, bali wale watu ambao ni matajiri ndio watakaokuwa pengine wanakwenda wanakopa mikopo hiyo, wanapata mbolea na bado wataendelea tena kwenda kuwauzia wananchi kwa bei ambayo mkulima hawezi ku-*afford*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pengine niweze kufahamishwa vizuri.

**MWENYEKITI:** Umeeleweka. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kusema kwamba labda *model* hii yangu sasa itakuwa ni *perfect hundred percent*, sijawahi kuona *model* ambayo ni *hundred percent*, lakini ninaamini itakuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kujibu swali lake tu ni hivi, wakulima watakopa kupitia Vyama vyao. Kwa hiyo, tulichokifanya ni kupitia *AMCOS* na *SACCOS* ambazo zinakopesheka Benki. Kwa hiyo, wataalam wamepita kwanza, hata Kasulu wamepita kuzitafuta *AMCOS* na *SACCOS* ambazo zinaweza kukopesheka. Lakini kama *follow back position* tumeanza pia mazungumzo na makampuni na nimeeleza hapa; tunataka makampuni ambayo yataweza kukopesha moja kwa moja. Hilo hatujalifikia muafaka.

Pia makampuni ambayo yanaweza yakakopesha wakulima moja kwa moja bila kupitia benki, nazo tunataka tuone kama tunaweza kuzipa fursa hiyo. Hii imetokea kwenye upande wa korosho, imeenda vizuri Mkoa wa Pwani, watu hawakukopa benki na wamefanya vizuri na ndiyo maana pamoja na kelele za Korosho, unaona mwaka 2013 sikupigiwa kelele za Korosho mahali pengine. Sasa tunataka tujaribu hivyo, tutajitahidi wakope kupitia kwenye vyama vyao vya ushirika (*SACCOS* na *AMCOS*). Ndiyo maana tunataka tuziboreshe hizi *AMCOS* na *SACCOS* zikopesheke.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaridhika na maelezo hayo. Naomba kuondoa Shilingi tu kwa sababu kinachofanyika hapa ni kwamba, leo unaondoa kampuni, unasema unaingiza *SACCOS,* kesho unakuja unaingiza sijui kuna Chama gani kingine cha Ushirika, lakini suala la mfumo bado binafsi sioni pengine kama kutakuwa na tija zaidi ya Serikali kusema ngoja iache, iende ikae tena pengine iweze kushirikisha na watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niondoe Shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Machali. Ukisoma kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 11 kinataja idadi ya *SACCOS* mpaka mwezi Machi mwaka 2014 kwamba kuna *SACCOS* 5,000 na kinaeleza *SACCOS* ambazo nyingine zimekufa, nyingine zimedorora, lakini ukurasa unaofuatia wa 12 kinataja Vyama vya Ushirika wa mazao kwa maana ya *Agricultural Marketing Cooperatives* (*AMCOS*) na kwamba ziko 368.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema ni nini hapa? Tafsiri hii ni kwamba siyo kila mkulima yuko katika *SACCOS* na siyo kila mkulima yuko katika *AMCOS*. Maana yake ukiishatengeneza kwamba msingi wa kukopa benki ni *AMCOS* au *SACCOS* umeshatengeneza chujio kwa wakulima ambao wengine hawatapa fursa hiyo ya kuweza kupata pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Waswahili wanasema ukitaka kuruka ni lazima uagane na nyonga. Kama Serikali inataka kuja na *model* mpya ni lazima kwanza ifanye maandalizi ili hiyo *model* iweze kutekelezeka. Jambo hili lina tatizo, siyo kwa sababu tu ya mfumo wa utoaji wenyewe wa ruzuku, tatizo la msingi ni Menejementi, Uongozi; tatizo ni ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina azimio la Arusha hapa, lilikuwa linazungumza wakati ule kuhusu masharti ya Uongozi kwa sababu hii kashfa ya matumizi mabaya ya fedha za pembejeo; za ruzuku ni kubwa. Mheshimiwa Waziri amesema ana ripoti nyingi za ukaguzi, zikiletwa hapa ni kashfa kubwa kweli kweli!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika fanya haraka umalize, unajua wewe ni dakika tatu tu, na umeishazimaliza.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa hiyo, naunga mkono hoja ya kwamba mfumo huu usikubalike mpaka kwanza

utaratibu uweze kuwekwa ili wakulima nchi nzima wasiathirike na mianya ya ufisadi isiwepo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niwaelimishe pia hawa wasemaji kwamba, hata kwenye utaratibu uliopita, mimi nadhani ni *misconception* kwamba Serikali sasa inatoa ruzuku kwa wakulima wote wa Tanzania. Haikuwa nia yetu hiyo, hata kwenye utaratibu ule wa vocha ilikuwa siyo wakulima wote wa Tanzania. Tulianza na wakulima wachache na tulikuwa tunasema ni utaratibu tu tunauweka wakulima wazoee halafu baadaye wao wenyewe ndiyo watakuwa wanajiendesha. Sasa siyo kwamba Serikali inaweka mabilioni kwamba wakulima wote wote wa Tanzania wakakope kila mkulima, hata kidogo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye huu utaratibu tunaouingiza humu, fedha mtakazozipitisha siyo kwamba ni za wakulima wote wa Tanzania, ni wakulima ambao watakuwa ni wachache tu na ndiyo maana tunaanza na *AMCOS* na *SACCOS*. Hata tungesema tufikie wakulima wote, hakuna bajeti hapa ingekwenda kwa wakulima wote wa Tanzania kupata ruzuku ya mbolea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, hitimisha.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa *concern* ya Mheshimiwa Waziri kwamba sio kila Mtanzania ni mkulima. Haiwezekani wote tukawa wakulima kama ambavyo haiwezekani wote tukawa Wabunge. Lakini ninachokisema, tatizo ni mfumo uliopo na inawezekana wewe kwa nia yako Mheshimiwa Waziri huna tatizo kabisa wala huhusiki huko! Lakini watu wake na nimetoa mfano, kwa mfano katika Wilaya ninayotoka mimi, nawe unajua kuna matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea kuwa na mfumo huo ndiyo maana nikasema ni bora basi m- *stop* kwanza huo mchakato ili kusudi tuweze kushirikisha wadau, inawezekana tukapata mawazo mengine ya watu ambao watatusaidia kuja na suluhisho la tatizo ambalo lina-*exist* kwa miaka siyo chini ya mitano. Tangu mfumo huu umeanza, ni matatizo, wizi, ufisadi wa kila namna ambao ukiangalia kwenye maeneo mengi watu wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri pia amekuwa analalamikia suala hilo wakati bado ni Mbunge mwenzetu pamoja na wengine hapa. Mheshimiwa Kangi Lugola amelalamika hapa! Kuna sababu gani ya kuendelea kuwa na haraka juu ya mambo haya ambayo ukiyaangalia kimsingi, wananchi, mkulima aliyekusudiwa hanufaiki? Hizo ni takwimu kidogo ambazo nimewapatieni. Kati

ya mifuko 500, ni 100 tu ndiyo imefika; mifuko 500, ni 80 tu ndiyo imeenda, kwa miaka mitano mfululizo imepita wamepora mbolea kiasi gani? Kwanini wasisimamishe suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sikubaliani na mawazo ya Mheshimiwa Waziri, naomba suala hili lisimamishwe kama ambavyo nimeshauri. Sina la ziada, kama wanaona kwamba inafaa, Bunge liamue.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri tulipoanzisha utaratibu huu siyo kwamba, tumeamka tu asubuhi tukaja hapa. Tuliujadili kwa kina, tuliwaita Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, tumefanya mazungumzo na Vyama vya Ushirika na wakakubali na ndiyo walio-*suggest* kwamba tuanze na *SACCOS* na *AMCOS* ambazo ni *viable*. Kwa hiyo, siyo kwamba ni jambo limeanza leo.

Kwa hiyo, kama leo hii tukisema kwamba tuache kwa Kasulu tu wakati wengine wote ukiwauliza, mimi nina hakika ukiwauliza Wabunge wengine hapa, nakumbuka tuliposema tupitie kwenye *AMCOS* na *SACCOS* walipiga makofi namna hii. Sasa leo tena ukisema eti wamekataa, siwezi kukuelewa. Ni jambo tulikubaliana hapa msimu uliopita kabisa kwamba tuanze na *SACCOS* na *AMCOS* tunadhani inaweza ikatupeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naona ni utaratibu unaoweza ukatufaa.

**MWENYEKITI:** Basi, kaa chini. Sasa nitawahoji.

*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Shilingi imebaki. Mheshimiwa Gekul!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mambo mengine kwa kweli yanasikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nizungumze suala zima la sera kuhusu bajeti ya Wizara ya Kilimo na Mheshimiwa Waziri ulisema nakaimu, ni kweli; Waziri husika amepata dharura lakini nimeitendea haki hotuba hii na bajeti hii kwa kusoma vitabu vyote; kitabu cha maendeleo, kitabu cha matumizi ya kawaida, randama, kitabu chako na hotuba zote mpaka za Kamati.

Mheshimiwa Waziri, ni kweli hawajafikia lile Azimio la Maputo au makubaliano yale ya 10%, ninyi mmefikisha 7%. Ni kweli bajeti yako ni ndogo, lakini naomba nipate ufafanuzi, ni vipaumbele vipi kwenye Wizara yako ambavyo sasa unavikazia? Kwa sababu ninachoona, kinachofanyika kwenye

kitabu cha matumizi ya kawaida ni fedha za *per diem,* unakutana na Shilingi milioni 500, fedha za usafiri Shilingi milioni 500, lakini kibaya zaidi ukienda kwenye kitabu cha maendeleo mambo ni yale yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwe tu mkweli. Wakati nasoma bajeti ya Wizara hii pamoja na kwamba nilikuwa nakaimu, niliogopa sana kwamba, hii *Vote 43* upande wa Wizara wanatenga fedha nyingi za mafunzo. Nilikuwa najiuliza kuna sababu gani mpaka leo Wakuu wa Idara huko Wizarani wanaendelea kupeana mafunzo wakati matatizo ya kilimo katika nchi hii ni wakulima kwa 70% wanatumia jembe la mkono na trekta ni 10% tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi na nitoe hoja ya kuondoa Shilingi kama hatanieleza vilivyo, ana vipaumbele gani katika Wizara hii ya Kilimo tofauti na posho na *per diem* ambazo naziona katika Wizara hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumsahihisha, sio kumsahihisha kumsaidia tu. Hiyo asilimia 10 unayosoma wewe ni ripoti ya mwaka 2001 maana na mimi nimesoma taarifa zako, kwenye kilimo cha kutumia zana baada ya *interventions* hizi za Serikali ambapo ndio vipaumbele vyenyewe hivi, kuingiza matrekta nchini, tumeshusha asilimia 70 ya jembe la mkono mpaka 64, tumepandisha kilimo cha matrekta kutumia zana za kilimo kutoka asilimia 10 unayosema wewe mpaka 14. Sasa mimi nakupa taarifa kwa sababu najua hizo unazozisoma ni za mwaka 2001, ni miaka ya nyuma kabisa, sasa sisi hatuwezi kuwa *static,* hizo *figure* ndio tunakupa sasa baada ya kuwa tumefanya *evaluation.(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye mambo ya *training,* Mheshimiwa Kaimu Waziri Kivuli ni hivi, elimu mimi naamini sio *static*. Unajua mambo mengi yanakuja kila siku, kila wakati kuna mambo mapya yanakuja. Kwa mfano sasa kuna magonjwa yameingia ya mnyauko, huwezi kusema wewe uliyosoma mwaka 1900 ni yaleyale. *There so many new innovations* zinakuja. Kwa hiyo, watu wetu lazima wawe *up to date,* wakutane na watu wengine wajifunze vitu vipya lakini wakikaa tu wakasema tulishasoma tumemaliza basi tutakuwa *dormant*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli suala la kusoma ni endelevu sidhani kama tutakuwa tumewatendea haki kwamba wakae tu wasiendelee kujifunza vitu vipya.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu niseme kwamba naondoa shilingi na Wabunge wenzangu wasaidie kuchangia katika hili kwa sababu zifuatazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikatai hizo *training* zifanyike katika fedha za kawaida lakini nazungumzia fedha za maendeleo, ndiyo maana nikauliza vipaumbele vyako ni vipi? Ukiangalia fedha za ndani niache za nje katika Wizara yako fedha za ndani ni shilingi bilioni 25 lakini fedha za nje za maendeleo ni bilioni 22. Kwenye hizo shilingi bilioni 25 za kwetu tu Mheshimiwa Waziri ni shilingi bilioni 8 tu zinakwenda kwenye miradi mfano ya ujenzi wa maghala na ukarabati lakini kutoka shilingi bilioni 25, shilingi bilioni 8 ukatoa zingine zilizobaki ni mafunzo, ni semina ambayo inaenda kwenye kitabu cha matumizi ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba kwangu mimi ningeona kwamba Mheshimiwa Waziri angekuwa muungwana akakubaliana hizi fedha tukazi-*reallocate* kwenye Kamati ya Bajeti ziende kwa wale wakulima walioathirika na mbegu zile ambazo hazijaota, nimesema kwenye hotuba kule Hai, Manyara lakini pia wakulima wa pamba maeneo mengi na wale wa migomba wa Kagera wanazungumza. Mheshimiwa Waziri, kwa nini fedha hizi unaendelea kuzipigania wakati unajua kabisa hizi fedha zinatumika visivyo, zinaenda kwenye matumizi ya kawaida haziendi tena kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shilingi na Wabunge wenzangu waonyeshe jinsi gani ambavyo Wizara hii inatumia vibaya na wanaomba tena fedha zingine, tusiwaongezee, nashauri bajeti yao tupeleke kwenye Kamati ya Bajeti iangalie upya, ifumuliwe na fedha zitapatikana kwa kuwalipa wakulima wetu walioathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, dakika tatu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anataka tumpongeze, hatuwezi kukupongeza kwa sababu Ilani ya CCM ya chaguzi tatu zilizopita mlisema itakapofika mwaka 2010 kilimo kitakua kwa asilimia 10. MKUKUTA ulisema ifikapo mwaka 2010 kilimo kitakua kwa asilimia 10. Sasa hivi tuko mwaka 2014 kilimo kimekua kwa asilimia 4 licha ya maneno mengi ya bajeti imeongezeka na porojo nyingi. Alipita mzee wangu wa Bunda, akapita Mheshimiwa Maghembe, umekuja wewe maneno yaleyale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema hapa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Gekul, ukiangalia fedha hizi fungu la maendeleo wanatenga shilingi bilioni 1.3 kulipia gharama ya mtoa huduma na manunuzi ya gari ya *Four Wheel Drive* wakati huohuo kusaidia kuanzishwa vikundi ya vijana kwa masuala ya kilimo wametoa shilingi milioni 35. Hii ni aibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija mfano mwingine huku, hii ni mifano midogo tu kwa sababu dakika zenyewe ni tatu. Kumwajiri mtoa huduma binafsi shilingi bilioni 1.4 wakati huohuo, yaani hivi vitu, mafunzo kwa wakulima ni shilingi milioni 200. Sasa hivi hao wakulima ambao ni asilimia 80 ya Watanzania huu uchumi ambao mnasema unakua kwa nini usiwe *reflected* huku kwa sababu hamuwekezi. Mnasema uchumi unakua kwa asilimia 7 ukienda kwa mkulima wamechoka chokani kwa sababu fedha ambazo mnatakiwa muwekeze kwa wakulima wadogo wadogo mnamalizia kwenye matumbo yenu huku, tukisema kwenye matumbo tunamaanisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani fedha za ndani ambazo tuna uhakika nazo shilingi bilioni 25 ni shilingi milioni 8 tu ndio zinakwenda kwenye maendeleo. Fedha za maendeleo, hapo hatujazungumzia matumizi ya ambapo na kwenyewe kuna vihoja vyake na tunajua fedha za nje zile shilingi milioni 20 asilimia zaidi ya 80 za fedha za wafadhili ni mafunzo mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike kipindi tubadilike, ifike kipindi tuache kuwadanganya Watanzania, tusitumie kuwanyima elimu Watanzania kuja Bungeni kutumia Bunge hili kupeleka porojo za uongo. Kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja Kamati ya Bajeti sisi tuelekeze ifanye *reallocation* tujibu mahitaji ya Wabunge humu ndani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mnyika.
**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Dakika tatu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wakakumbuka Azimio la Arusha. Mheshimiwa nitaomba ninukuu ndani ya dakika hizohizo tatu wakati huo wanapewa masharti viongozi wa TANU. "Kiongozi wa TANU au wa Serikali sharti awe mkulima au mfanyakazi na asishiriki jambo lolote la Kibepari au la Kikabaila". Kiongozi huyohuyo wa TANU ambaye ndio kiongozi wa CCM kwa sasa ni Wajumbe wa Halmashauri Kuu, Mawaziri, Wabunge na kadhalika. Kwa maana yake ilitarajiwa kwamba chama hiki cha wakulima na wafanyakazi, wakulima na wafanyakazi wa kwanza kabisa ingekuwa ni Waheshimiwa Wabunge na wangejali kweli maslahi ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa hapa tunajadili kuhusu maslahi ya wakulima na ndiyo maana naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Pauline Gekul ya kuondoa shilingi ili tuondoe fedha kutoka kwenye matumizi yasiyo ya lazima tuelekeze kwenye matumizi ya msingi ya kuwajali wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukikipitia hiki kitabu cha maendeleo utadhani kwamba ni bajeti ya maendeleo kumbe ukweli ni kwamba ni bajeti ya kuendelea kulipana posho, bajeti ya matumizi ya kawaida badala ya bajeti ya miradi ya maendeleo na hii iko katika vifungu mbalimbali. Ukikisoma kifungu kwa kukiangalia juu juu kimeandikwa *expand rice production project* utafikiri ni kweli wanaenda ku-*expand rice production* lakini *the devil is in details,* ukiingia ndani kinasema kuratibu, sio kwenda kulima, sio kwenda kusaidia vikundi vya wakulima, yaani kuna vituko humu. Kuna mahali kuna shilingi milioni 248 zinatengwa kwa ajili ya kikundi kidogo cha watendaji kununua bodaboda halafu bodaboda moja shilingi milioni 3.1, bodaboda ya wapi hiyo inauzwa shilingi milioni 3.1 halafu haiendi kwa mkulima, haiendi kwa wananchi wa kawaida kuwasaidia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii bajeti ya maendeleo inatakiwa kufumuliwa haya mabilioni hasa haya, unajua Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kusimamia analipwa shilingi bilioni 1.5 yaani shilingi milioni 1,500 kusimamia!

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halikubaliki kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi wamesema tu lakini labda…

**MWENYEKITI:** Kama mengi yamesemwa acha basi Waziri ajibu. *(Kicheko)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Nahitimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipeleke swali moja tu kwa Serikali. Hivi hamuoni aibu na maajabu kuweza kutenga kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni moja halafu kwenye maeneo mengine kama kutoa mafunzo kwa wakulima mmetenga pengine shilingi milioni mia moja, milioni mia mbili, hamuoni ajabu kwamba mnaiingiza nchi yetu kwenye maajabu ya dunia, hamuoni maajabu? Shilingi milioni 600 ukienda kule kwenye randama kazi zinazofanywa kwa mfano kwenye hiyo *rice production* mmetenga shilingi milioni 600 *plus* ni fedha za utafunaji, hamuoni aibu! Wabunge wenzangu wa Chama cha Mapinduzi hili suala sio kwamba nakwenda kunufaika mimi, siendi kunufaika mimi, tuone aibu! Kama kweli tuna dhamira ya kuwasaidia wakulima wakati ndio huu kwamba tufanye maamuzi waende wakakae hizo fedha zipelekwe kwa ajili ya kwenda kuwasaidia wakulima. Suala hili kama mnafanya hivyo basi muache kuwa

mnalalamika mahali hapa ooh, wakulima wananyanyasika, wakulima wa mahindi mbolea haziendi wakati fedha zinapelekwa kwenye utafunaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ione aibu na iridhie kwamba hizi fedha zifanyiwe *reallocation.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niwaeleze wenzangu, ninyi mnasema kuona aibu, mambo mengine ni kwa sababu na nyie hamjui vilevile. Kwa sababu ukilichukulia suala la *training*, kwa mfano humu ndani tumezungumzia *systems of rice intensification*, nikikuuliza Mheshimiwa Machali unaijua hata maana yake? Ni jambo ambalo lina mambo mengi ndani yake. Ni jambo jipya la kufundisha namna ya kulima mpunga bila ya kumwaga maji. Kuna wataalam ambao wamebobea katika masuala haya, kuna vifaa ambavyo pia wanatumia wanapokwenda kwenye shughuli hizi, ni utaalam ambao ni *package* ya kutosha sio kwamba ni kwenda tu kumwagia shilingi bilioni 8 unawapa wakulima halafu tayari ule utaalamu unakwenda kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka vitu vingi, tumesema pikipiki kama unakumbuka wamepiga mahesabu au wamekokotoa wakasema *three million shilings.* Hivi kweli unataka kusema unampelekea pikipiki Bwana Shamba kule uchukue *Sun LG* halafu inakufa kila siku haiwezekani! Lazima tupeleke pikipiki ambazo zinaweza kufanya kazi kule vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hii miradi naomba tuelewane hii kitu ambayo mmeisoma ya watoa huduma, hii ni *package* ambayo tumeianzisha chini ya *Big Results Now*. Tumeamua kwamba wakulima wakishakuwa na miradi tunataka watoke kwenye kulima tu lakini waingie kwenye *managements* ya zao, mambo ya masoko, sio suala tu la kulima. Kwa hiyo, hawa ma-*consultant* ambao wameteuliwa kwanza ni wataalam wa shughuli hizi, wakati tumeweka matangazo hawakupatikana hapa, tulitaka saba wakapatikana wawili, uone kwamba hilo sio somo tu la kwamba unaenda unamwaga mamilioni, unampa mkulima tayari analima anapata. Kwa hiyo, kuna vitu ambavyo wataalam wamefanya sio kwamba tu wamekwenda wanataka kujitafunia fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sioni aibu kwamba eti wataalam labda wametafuta kwenda kutafuna hela tu. Hii kazi kabla hatujakubaliana kwanza wako wafadhili wetu ambao nao wamekubali kuweka fedha zao hawangeweza kukubali kuweka fedha hizi bila ya miradi hii kupitia kwenye mchakato na mradi huu kabla ya kupitia hapo imepita kwenye *Planning Commission* ikawa *approved.* Ukisema leo mimi nione aibu sioni Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hitimisha hoja yako

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nihitimishe kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wabunge wenzangu wa Chama cha Mapinduzi kwa wingi wao…

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Kwa sababu tunapotaka kufunga magoli kwa Serikali mnahamisha magoli, naomba msihamishe. Tuiambie Serikali kwamba kwenye miradi ya maendeleo, nimezungumzia *vote* tu ya Waziri, ana *vote* tatu kwenye Wizara yake, kuna ile ya Ushirika, kuna ile ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na kuna ya kwake. Nazungumzia kwenye ngazi ya Wizara, fedha hizi bilioni zilizotengwa za maendeleo zimetumika kwa mambo mengine tena ya *perdiem* ya mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa anazungumza kuhusu hili la upande wa umwagiliaji, inasema kumwajiri mtoa huduma, kwa lugha ya Kiswahili mtoa huduma ni mtu mmoja, shilingi bilioni 1.4. Ndiyo maana nimeomba hivi kwa kweli bajeti yako Mheshimiwa Waziri kwa upande wa maendeleo tunakusaidia, tunakupenda, tunaomba ipelekwe kwenye Kamati ya Bajeti ikafumuliwe na sisi Wabunge wote tulioko humu ndani tunaowakilisha wakulima na tunaowapigania twendeni siku hiyo kwenye Kamati ya Bajeti tufumue hii bajeti kwa pamoja ili hii miradi ya maendeleo na wale wakulima wetu walioathirika wapewe fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, kwa hili tunakusaidia na ukubaliane na sisi kwa sababu haiwezekani kwenye kitabu cha matumizi ya kawaida kuna mafunzo, kila kitu kimewekwa huko. Unaenda kwenye kitabu hiki cha maendeleo unakutana na lugha hiyohiyo, nyimbo hizohizo, mafunzo sijui kusafiri sijui kitu gani. Pia niseme tu miradi ambayo imetengwa kwenye Wizara hii ni ujenzi wa ghala lakini pia skimu za vijana shilingi milioni 200. Mheshimiwa Waziri unasema unaenda kuwasaidia wagani kuwapa mafunzo umetenga shilingi milioni 85 tu nimeona kule hakuna chochote kwenye bajeti ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuamue kwamba sasa bajeti hii ya maendeleo ya Waziri, posho zako wala mimi sigusi, kwenye maendeleo tukafumue na tuangalie upya tuwasaidie wakulima walioathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lukuvi.

**MBUNGE FULANI:** Wewe hukusimama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Nimesimama, si tunajadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tukumbushane utaratibu, hiyo Kamati ya Bajeti wanayoitaka ikutane ilishakutana kuchambua Wizara zote. Utaratibu ni kwamba tunaanza kwenye Kamati na kwenye Kamati tuna Wabunge wa CHADEMA *unless* watume watu wenye akili upeo kidogo waweze kutambua, lakini walikuwepo…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Subiri nitakupa nafasi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Lakini kila Kamati kabla bajeti haijasomwa hapa, Kamati ya Bajeti imeshapitia lakini kuna Wizara zingine Kamati ya Bajeti zimezishika mashati sasa hivi, tunajua kuna Wizara zingine zimeshikwa mashati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachotaka kusema ni kwamba hakuna sababu ya kutumia *phrase* za Azimio la Arusha na CCM katika kujenga hoja, tumieni akili yenu, msisome maneno ya CCM, tumieni akili yenu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kumalizia ni kwamba mafunzo, hapa tulikubaliana mwaka jana hata mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ni maendeleo.

**WABUNGE FULANI:** *Yes.*

**MBUNGE FULANI:** Huku haipo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Huwezi kusema kwamba utafiti kwa sababu ni mambo ya utafiti huyaoni au hayafanani na vitu halisi vinavyoweza kushikwa sio maendeleo. Huwezi kusema kwamba mafunzo kwa ujumla ya wataalam wa kilimo sio maendeleo.

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Jana Mheshimiwa Spika ametuambia hivi, haya tunayopitisha haya ni *provision*, upitishaji wa mwisho utafanywa kwenye Bajeti ya Serikali. Sasa mkilijua hilo inakwenda bila hata kusema kwamba mahitaji yatakapokuja tutakapokuwa tunajadili bajeti ya Serikali ambayo itakuwa imeshapitishwa na kina Mheshimiwa Mbatia Wajumbe wa Kamati ya Bajeti, mahitaji haya ya kufumua hizi Wizara yanaweza yakaletwa kulingana na maelekezo ya Kamati ya Bajeti. Hilo linakuja bila ya kuhitaji Kamati moja moja hapa kusimamisha kwa sababu Mheshimiwa Spika jana ametuambia upitishaji huu ni kama wa muda lakini upitishaji wa mwisho utakuja baada ya bajeti ya Serikali kupitishwa.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kaeni, mimi nina-*manage* hapa, nikiona kuna mashimo nayakwepa, nikiona kuna mafuriko nayakwepa, sasa nahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Barwany.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ndugu yangu Mnyika ulijaribu kuwakumbusha hawa juu ya Azimio la Arusha lakini Azimio la Arusha walilifuta Zanzibar hawa miaka kadhaa iliyopita lakini hata Baba wa Taifa alishasema kwamba kukumbuka Azimio la Arusha ni sawasawa na uwendawazimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja yangu ya maandishi nilizungumzia suala la zao la mnazi. Zao la mnazi kama ilivyoelezwa katika hoja zetu Wabunge zaidi ya tatu hapa, tulitegemea Mheshimiwa Waziri angetoa maelezo angalau tu kwa kutupa matumaini ni namna gani Serikali inaweza kuweka mkakati wa makusudi kabisa katika kuhakikisha kwamba zao hili linarudi katika ubora wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la mnazi leo limeathirika kwa kiasi kikubwa. Hatujapata taarifa yoyote ya utafiti uliofanywa katika kulinusuru. Leo ukitembelea katika maeneo ya Mikoa ya Pwani ambako zao hili linalimwa utaona minazi mirefu tu imesimama tayari imeshaathirika kwa kiasi kikubwa. Utafiti gani umefanywa katika kuhakikisha zao lile linaboreka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la mnazi kama inavyofahamika ni uchumi mkubwa kwa Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani pia ambao tayari imezungumzwa hapa watoto wamesoma kupitia zao hilo lakini sio zao la chakula tu pia ni zao la biashara. Ndani yake mle tulikuwa tunapata mbata, kulikuwa na viwanda mbalimbali lakini katika hatua iliyofikiwa sasa hivi leo kijana

wa miaka 20 au 30 ukimwambia habari ya mbata haelewi mbata ni kitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka Mheshimiwa Waziri atuambie anatupa matumaini gani na ana mkakati gani ndani ya kipindi chake hiki, tupo ndani ya mwaka wa tano tunazungumza habari ya nazi hapa lakini bado Serikali haija-*respond* juu ya hili. Mimi nakusudia kuondoa shilingi kama bado hajanipa jibu la kufaa ili wananchi wangu wakapate matumaini kwamba Serikali ina mpango maalum juu ya zao la mnazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Barwany kwamba utafiti ni jambo endelevu na kweli utafiti huo wa minazi umechukua muda mrefu sana, wengine wananikumbusha imeshafika hata miaka 30. Huwezi ukasema kwamba kwa nini hamjapata jibu labda hamna akili, si kweli, maana hata UKIMWI haujapata majibu lakini watatifi hawajasimama, kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa habari njema Mheshimiwa Barwany ni hivi, tayari wataalam wamekwishagundua ugonjwa wenyewe wa minazi unaita *Coconut Litho Disease* na hatua tuliyoifikia, mimi mwenyewe nimekutana na Waziri wa kutoka Serikali ya Sri Lanka tumetengeneza utaratibu kwa sababu wao wanasema wamekwenda mbali kidogo na hivi sasa ninavyozungumza na wewe tumeshaandaa mpango kupitia *COSTECH* kwa ajili ya kuendeleza utafiti wa zao hili la nazi ili tuweze kuangalia njia bora za kuutokomeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wataalam wetu wanashirikiana na wataalam wa Sri Lanka kwa ajili ya tatizo hili la nazi. Sasa zaidi ya hapo ukisema kwamba mlete majibu leo leo asubuhi, haiwezekani lakini huo utaratibu tayari tunao na tumeuanza mwaka huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Barwany.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kufananisha tatizo la nazi na tatizo la UKIMWI, tatizo la UKIMWI ni la kujitakia lakini suala zima la nazi ni suala la kiuchumi na maendeleo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hii ni ya muda mrefu, mwaka jana kauli hii imetolewa, mwaka juzi na mwaka wa nne sasa Wizara hii inazungumzia juu ya utafiti huu ambao umefanywa na watu wa Sri Lanka lakini kama kungekuwa na matarajio makubwa tungeambiwa sasa kupitia taratibu hizi, baada ya kusema tu ndiyo taarifa hii inakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Mheshimiwa Waziri hajatoa jibu la kuwapa matumaini wananchi kama jambo hili linashughulikiwa.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo?

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Kwa hiyo, bado naendelea kushika shilingi yake.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanyika ni utafiti. Unajua utafiti ukisema kwamba leo Waziri leta matokeo ya utafiti utakuwa hanitendei haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachoweza kusema sasa Mheshimiwa Barwany kama kweli na wewe una *interest* na jambo hili, ningekualika basi hata ofisini kwangu ukutane na watalaam ili wakuoneshe ni kitu gani kinafanyika lakini ukiniambia sasa hivi kwamba toa matokeo ya utafiti, *results* zimekuwaje hapa kwenye *desk* hili siwezi kukupa Mheshimiwa Barwany lakini utafiti unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii habari ya kukutana na wenzetu wa Sri Lanka, mimi mwenyewe nakuambia nimekutana nao wala siyo zaidi, miezi mitano iliyopita alikuja Waziri wao akasema tuendeleze utafiti huu. Sasa tunaufanya siyo sisi peke yetu, tunafanya kwa kushirikiana na *COSTECH* na tunafanya kwa ajili ya kutafuta njia za kunusuru zao la nazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitumie nafasi hii nikukaribishe Mheshimiwa Barwany uje angalau uone tumefikia wapi na utakutana na watalaam wangu ndiyo watakupa maelezo mazuri zaidi kuliko mimi unionee hapa kwamba leta majibu hapa hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Barwany, ushauri mzuri!

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima yako nakubali tu kama ni ushauri mzuri lakini mimi siwezi kuja ofisini kwako, tunataka taarifa hiyo ulete hapa ndani ya Bunge, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na nakushukuru. Mheshimiwa Jitu Soni!

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi katika mchango wangu wa maandishi niliuliza, je, ni lini na ni kiasi gani Serikali itaongeza bajeti katika sekta ya maendeleo katika vituo vyetu vya utafiti, elimu ya kilimo ikiwa pamoja na Chuo Kikuu cha Sokoine ili kiweze kuboresha zana, miundombinu na vifaa vya kufanyia kazi na utafiti. Pamoja na hiyo, pia hivyo vituo vyetu vya utafiti vina mashamba makubwa ya kuzalisha mbegu

viwezeshwe ili viwe na fedha za kuingia ubia na makampuni au watu wengine ili tuweze kuzalisha mbegu ya kutosha, mbegu bora ndani ya nchi badala ya kuagiza mbegu kutoka nje. Pia bajeti ya vifaa vingine vya kupimia dawa na mambo mbalimbali ambapo sisi leo tunaletewa sokoni vitu mbalimbali, vyakula ambavyo vimepigwa labda dawa ambayo inaathiri afya zetu. Ni lini Serikali itaweka bajeti hiyo na kwa kiasi gani na pia je, ni lini tutafikia ile asilimia moja tuliyokubaliana ya bajeti yote ya taifa iende katika utafiti?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Jitu Soni kwa swali lake lakini niseme Bunge hili ndilo linalopitisha bajeti ya Wizara zote na tunajitahidi kila mwaka kuleta bajeti ambayo Wabunge mnaipitisha. Tunakiri kabisa tunalo tatizo la fedha kwenye sekta hiyo lakini ni azma ya Serikali na kufuatia pia Azimio la Adis Ababa nadhani la mwaka 2007/2008 makubaliano yalikuwa ni kwamba tutenge asilimia moja ya *GDP* kwa ajili ya kwenda kwenye shughuli za utafiti. Hiyo ndiyo hatua ambayo tunaendelea nayo na mimi nadhani tunapoleta bajeti ya jambo hili, Waheshimiwa Wabunge mtusaidie kuipitisha, lakini hiyo ndiyo azma na mimi nadhani tunaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye suala la vyuo vya utafiti kama alivyosema Mheshimiwa, tunajua hali ya vyuo vyetu na Jitu Soni kama Mjumbe wa Kamati yetu anajua jambo hili, wao wenyewe wamekuwa wanashauri Kamati mara kwa mara, wamekuwa wanashauri Serikali kwa maana hiyo. Sisi hata kwenye bajeti ya mwaka huu tunatenga fedha kidogo kwa ajili ya ukarabati wa vyuo vyetu.

Mheshimwia Mwenyekiti, lakini suala la mashamba makubwa ya mbegu, hili tumeishalizungumza sana hata Mkurugenzi Mkuu wa *ASA* tumeishamwagiza kabisa ahakikishe kwamba analitangaza jambo hili kwenye vyombo vya habari, ahakikishe kwamba analitangaza kwa maana ya kwamba kuna kuingia kwenye *PPP (Public Private Partnership)* kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu. Wote tunajua kwamba iko changamoto tungependa tuzalishe mbegu zaidi hapa nchini na kwa kweli hawa wenzetu wa *ASA* wameanza na mimi nimetembelea baadhi ya mashamba, hili jukumu kimsingi wameishalianza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nadhani kwa mipango tuliyonayo Wizarani katika mwaka unaokuja tunaweza tukawa tumefika mahali pazuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Soni!

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama nilivyoelewa ni kwamba tunakubaliana wote na Wizara itaunga mkono ikiwa ni upande wa Serikali kwamba bajeti nzima ya Serikali ikiletwa hapa wakati tunapitisha kwa

ujumla, kama hakuna asilimia moja ambayo itaenda kwenye utafiti ambayo itasaidia magonjwa ya minazi, ya migomba na utafiti mbalimbali ambapo tuna matatizo makubwa na hali mbaya ya miundombinu huku katika taasisi zetu za utafiti, wote tukubaliane kwamba kipindi hicho tutaikataa bajeti hiyo na hatutakuwa na msamaria mwema kwamba bila utafiti hii nchi haiwezi kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mtukubalie kwamba hiyo ni kauli na ninyi mtatuunga mkono kipindi hicho kama ni Waziri wa Fedha anasimama, ninyi mtatuunga mkono sisi Wabunge wengine wote.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, umeridhika na majibu na umeweka *conditions* zako?

**MHE. JITU V. SONI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** *Okay*. Ahsante. Mheshimiwa Cheyo!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kabla sijaendelea, naomba yule dada *DC* aniache nifanye kazi ambayo nimepewa na wananchi na yeye aendelee kutumia zawadi aliyopewa na Rais kufanya mambo ambayo anapaswa kufanya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati nachangia nimemwomba Mheshimiwa Waziri, msimu unaanza. Tulishakubaliana kilimo cha mkataba si lazima na hakuna *by definition* mkataba kuwa lazima. Hili tulilizungumza hata mwaka jana. Wewe umesema ni watu wachache sana ambao wamo katika kilimo cha mkataba. Sasa pamba imeiva, kwa nini hawa watu washurutishwe kwamba wawauzie tu watu ambao wana mkataba na watu mbalimbali? Mimi naona dhana nzuri ni wale wote ambao wana *ginnery* na ambao tumewapa leseni ya kuchambua pamba, wapewe nafasi na leseni ya kununua hiyo pamba ili pawe na ushindani bila sasa ku-*ring fence* watu kadhaa kadhaa kwa kisingizio kwamba wana vikundi na vikundi hawana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema, sisi pia tuna marafiki Uingereza, huyu Lord Salisbury ambaye anaweza kuwa rafiki labda wa viongozi wa nchi hii, hiyo pesa yake isituharibie zao letu la pamba kwa kuleta sheria mbalimbali ambazo haziwezekani. Kama umesema mkulima wa mahindi anaweza kuwa huru kuuza mpaka Zambia na popote pale, ni kwa nini mkulima wa pamba unamshikilia lazima amuuzie mtu fulani ambaye anachaguliwa na *DC*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili siyo haki, haiwezekani, mimi nataka majibu. Mimi ninachotaka useme kwamba wote wenye *ginnery* wanunue

pamba. Nisipopata majibu, si kawaida yangu kutoa shilingi, lakini zamu hii nitatoa shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Cheyo wewe ni shahidi unajua kabisa hata msimu uliopita, *intervention* niliyofanya mimi nilipokuja kwenye kilimo cha pamba na hata mahali pengine nililaumiwa. Mimi labda nikuahidi tu, changamoto zilizoko kama unasema sasa msimu ndiyo unaanza, nimezijibu hapa kwamba na mimi najua huo mfumo siyo kwamba ni *perfect a hundred percent*. Hata zile *farmer business groups* ambazo ndizo zimo katika kilimo cha mkataba, zingine ni *non-existent,* najua hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachoweza kukuahidi ni hivi, msimu bado uko *on* na sisi tuko hapa, jambo lile haliwezi kuharibika wakati sisi tupo. Kwani mbona ni rahisi tu, tunakuja tukae na ninyi na wakulima wenyewe husika kule tulizungumze mpaka tulipatie majibu kabla hata ya msimu haujaenda mbali. Mimi nakuahidi kabisa, nitakuja, twende kule tuzunguke pamoja, tupate majibu. Mbona nimefanya *intervention* wakati mlisema Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa wamesema ukileta mbegu ya fazi nakuweka ndani, mlisema hivyo lakini nimekwenda kule nikasema haiwezekani, msiwaweke ndani watu isipokuwa wape *benefit of doubt*, waachie wanaoweza kutumia fazi watumie, wanaoweza kutumia *quton* watumie, wale watakaoona hii inatufaa watakuja wenyewe. Hiyo ndiyo *principle* ya ugani, huwezi kulazimisha mtu kwamba usipotumia hiki nakutia pingu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hata hii kitu mimi sioni kama kuna kitu chochote kinachoweza kutupa tabu. Bado msimu ndiyo unaanza na sisi tuko hapa kwa ajili ya kutatua matatizo hayo. Hebu mniamini, nakuja twende tuhangaike na jambo hili ili msimu uende vizuri.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Waziri, huendi tu kesho ukanunua pamba, kuna maandalizi, maandalizi yenyewe ni pamoja na kuomba leseni. Leseni sasa ambazo wenye ma-*ginnery* wanaomba, ma-*DC* wanakataa eti kwa sababu lazima wawe na vikundi na wewe mweyewe umesema vikundi hivyo ni *non-existent*, havipo. Sasa kama tunajua hilo, kwa nini Mheshimiwa Waziri uwe na kigugumizi, si sema tu kwamba wote wenye ma-*ginnery* wapewe leseni washindane kwenye soko ili bei ya mkulima wa pamba iwe nzuri. *It is simple*, *we do not need* ku-*meet.* Kwa hiyo, kwa misingi hiyo sijaridhika natoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shibuda.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni masikitiko makubwa sana Mheshimiwa Waziri anapozungumza kwamba hakuna matatizo wakati yeye ni shahidi na shuhuda wakati wa kilimo alipokuwa akizuia kilimo cha mkataba, ma-*DC* hawakumheshimu, Wakuu wa Mikoa hawakumheshimu, hata kauli ya Waziri Mkuu haikuheshimika hadi Rais alipokuja kwenye ziara Simiyu. Sasa mimi nashangaa wakati tumefika katika msimu wa kuuzwa pamba unaongelea lugha ya tabia kifuniko kwenye uovu ambao ni patanifu na Serikali ya uasi ya ma-*DC* na Wakuu wa Mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri atambue Lord Salisbury katika nchi hii ni nchi huria, hizi ni amri za *TGT*. Leo nimezungumza hapa hujajibu wala hujajielekeza kutoa ushuhuda wowote wa kutengua mawazo ya *TGT* ambayo ndiyo inatoa amri kwenye Bodi ya Pamba na Bodi ya Pamba wamekuwa ni mawakala na makuhani wa uzandiki dhidi ya wakulima wa pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema Bodi ya Pamba ni laana, nimekwambia na Wakuu wa Mikoa wapo ambao hawakuheshimu mpaka Katibu Mkuu wa CCM Kinana wanamwita gunia tupu lisilosimama mbele ya Wakuu wa Mikoa na wanamwita Waziri Mkuu na yeye hana kauli yoyote hakuwateua, mpaka Rais anapotoa kauli sasa kama wewe umeshindwa kuzungumza, toa kauli.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shibuda kaa chini. Mheshimiwa Kirigini!

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningefurahi sana kama wazungumzaji wanaozungumza wangeweza kuwa *specific* kwa niaba ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri. Mimi ninayezungumza hapa jana nimeruhusu vibali vianze kutolewa na kwa wateja mimi mwenyewe nawafahamu, kuruhusu vibali vianze kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukianza kusema Waheshimiwa ma-*DC* wanakataa vibali visitolewe, Waheshimia ma-*DC* wanakataa sijui pamba isifanya nini, si kweli Mheshimiwa. Ningewaomba, Mheshimiwa Cheyo nakuheshimu sana, kama tunataka kumsaidia Mheshimiwa Waziri tuwe *specific*.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shibuda siyo utaratibu, kaa chini.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Tuwe *specific* kwenye maeneo ili Mheshimiwa Waziri aweze kujua wapi sasa anajielekeza kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wetu wa pamba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa hapa na ni tatizo la kimfumo. Kwa kuwa mfumo wetu hauweki bayana kuhusu hiki kilimo cha mkataba ambapo ni makubaliano kati ya pande zote na wakubaliane kwa hiari yao na ni lazima kitekelezeke na wakishakubaliana matokeo yaonekane. Sasa hapa huwezi ukaruhusu wakulima wa upande mmoja wafanye kilimo cha mkataba na wakubaliane pande zote, upande mwingine uwakatalie. Hii ndiyo inayoleta tatizo kwa wakulima wa pamba na ndiyo *contradiction* iliyotokea kati ya Mheshimiwa Cheyo na *DC* pale. Sasa *DC* akisema ametoa *may be* ni kwa wale anaowafahamu na siyo *system* nzima iliyo ya uwazi na ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiangalia haya matatizo ya stakabadhi ghalani na mambo yote ambayo yamezungumziwa hapa kama ni mfumo umewekwa na huo mfumo unaonekana una matatizo, inakuwa ni jambo la busara mnakaa mnauangalia ule mfumo namna ya kurekebisha yale yaliyotokea. Huwezi ukasema mfumo huu niliouweka mimi ndiyo nafikiria uko sawasawa, wakati Waheshimiwa hapa ni wawakilishi wa wale wakulima, ndiyo wanaotoa hayo matatizo yako moja, mbili, tatu, nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu kwamba kuna tatizo kubwa na hii ni bajeti ya kilimo. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, ni kwa muda mfupi sana nimpe taaifa Mheshimiwa Lukuvi, kwa bahati mbaya kwenye Kamati yetu ya Bajeti hatujaichambua hii wala tukaona matatizo gani yanayotokea, hatujaichambua. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Cheyo ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, hatujafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu kwamba Mheshimiwa Waziri akubali kwamba hili tatizo la pamba na tatizo la kilimo cha mkataba, akubaliane na Waheshimiwa Wabunge ili utaratibu huu ambao unaolalamikiwa uangaliwe, ndiyo uungwana wa uongozi ili tuwe *pro-active rather than being reactive*. Tusisubiri mpaka janga litokee ndiyo tuanze kuangalia lile janga, ile *crisis* inasuluhishwa vipi. Sisi viongozi tuwe *pro-active* tuweze kuzuia hayo matatizo yanayotokea huko mbeke ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Mheshimiwa Wasira!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni-*declare interest*, mimi natoka katika Wilaya inayolima

pamba, kwa hiyo matatizo ya pamba yanayoongelewa nayafahamu vizuri. Vilevile nimewahi kuwa Waziri wa Kilimo na mikataba inayozungumzwa tuliianzisha nikiwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani jambo hili haliwezi kuwa *resolved* humu Bungeni. Hiki ni kitu ambacho tunaweza tukazungumza wadau wa pamba, Wizara ya Kilimo na Bodi ya Pamba, tukapata jibu, halafu tuka-*implement* kile tutakachokubaliana. Kwa hiyo, kukaa hapa kwa kweli tu-*resolve* namna tutakavyofanya mkataba, namna tutakavyouza pamba, namna tutakapopata leseni kwa mwenye *ginnery* ni kitu ambacho siyo *practical* hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pendekezo langu ni kwamba jambo hili liachiwe Wizara iitishe mkutano wa wadau wa pamba, twende tukae tukubaliane namna tutakavyoendesha msimu na haki za wakulima zitapatikana nje kuliko hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nahitimisha hapa nimewaahidi kabisa hawa wazee wa pamba, tena nikamwambia mzee Cheyo kwamba katika mkutano huu, kama vile niliota atauliza, nikasema kwamba tutaitisha mkutano wa wadau wa pamba. Mheshimiwa Shibuda amekuja ofisini kwangu tukazungumza kabisa tena leo mchana, nikamwambia na *this time* nataka wakulima *perse* na siyo wale wakulima wa kubabaisha, tujadili suala la mustakabali wa pamba na ndivyo tulivyokubaliana. Mimi sijui ni wapi nimewakatalia! Haya anayosema Mheshimiwa Wasira ndiyo *exactly* nimewaambia hawa wazee. Sasa labda kama ni jambo lingine linatakiwa lakini ndiyo tumezungumza hivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mheshimiwa Wasira amezungumza, nilitaka kuongezea kwamba kama alivyosema Mzee Wasira kwa kweli kama kuna vikundi vimeingia mkataba kwa hiari yao kuanza kuivunja hapa ni ngumu na jambo hili linawagusa sana wakulima wa pamba na wadau wao. Kama Mheshimiwa Waziri amekubali wakachambue wale ambao wamefunga mikataba kama anavyosema Mheshimiwa Mbatia kwa hiari bila ya shaka kuna vifungu ambavyo vinawabana, wale ambao wako huru watafunguliwa minyororo. Hiyo sasa si ndiyo Waziri anavyosema? Sasa Waziri yuko hapa, anamaliza bajeti leo, pangeni mkutane kesho.

Mheshimiwa Mbatia, Kanuni zetu, Sehemu ya Tatu, ukurasa wa 137, inawapeni ninyi majukumu mawili yafuatayo, sasa kama hamkukutana ni shauri yenu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa ushauri wa jumla kuhusu bajeti ya Serikali kwa Bunge na Kamati za kudumu za Bunge lakini pili kuchambua hoja zitakazojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta kama hii wakati wa kujadili bajeti ya Wizara kwa ajili ya kuishauri Serikali. Huu ndiyo utaratibu wa kawaida ni lazima mzichambue, sasa ukiona hamkufanya hiyo kazi ni jukumu lenu au vinginevyo Kamati hii imeona haina matatizo yoyote lakini Kanuni hii...

**MBUNGE FULANI:** Wewe ni Waziri wa Sera, Uratibu na Bunge, Serikali inapaswa kupeleka hizo bajeti.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Kanuni hii inawataka Kamati ya Bajeti wachambue Kamati za Kisekta kabla hazijaja hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Selasini kaeni chini, Mheshimiwa Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuzungumzia mambo ya *Budget Committee* lakini ni mantiki tu huwezi ukachambua kitu ambacho hakijaletwa mbele yako, *simple*! *Unless* tumeletewa huwezi ukasema sasa unachambua tu *from there,* mimi naona tuache Kamati ya Bajeti ifanye kazi yake. *I think we are trying to do a good job* na hatuhitaji *criticism* ya Waziri juu ya jambo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo umeridhika?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Sasa kwenye pamba.

**MWENYEKITI:** Sababu kama tulivyosema hii ni *provisional* bado iko nafasi hii inaweza kuchambuliwa na Kamati hiyo, sasa umeridhika?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Sikiliza.

**MWENYEKITI:** Ninazungumza na mtoa hoja wengine kaeni chini.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ngoja basi niseme Mheshimiwa Mwenyekiti. Mimi ninasema hivi swali ambalo tumemuuliza Waziri ni rahisi sana wale ambao hawana mikataba wawe *free* kuuzia mtu yeyote, *is so simple,* hakuna hata haja ya kukutana, kulizungumza maana ni jambo ambalo linajulikana. Sasa kama amepata kigugumizi, najua hapa litapigiwa kura itakuwa Ndiyo au Hapana lakini jambo linabakia palepale hii ni *crisis,* tunaomba Waziri akubali tukutane hata na Wabunge wa kanda hiyo tukutane Jumatatu ili tuone *the way forward* kwa misingi hiyo nitakubali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa upendeleo siyo utaratibu lakini kwa kuwa ni *crisis* jibu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Lakini mimi nilikwisha jamani…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jibu unakutana nao acha mazungumzo mengine, waambie tu utakutana nao.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Lakini sasa wananilazimisha kwamba kesho tukutane wanajuaje ratiba zangu?

**MWENYEKITI:** Hawakulazimishi ni watu wa busara.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Maana ukiniambia lazima Jumatatu unajua ratiba zangu?

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba…

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Taarifa Mwenyekiti, Bunge liheshimiwe siyo ratiba yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu, Machali kaa chini, Mheshimiwa Waziri kaa chini, Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI - KAIMU WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hatuna haja ya kuendelea kuvutana kwa kitu ambacho kwa kweli wakulima wetu wanasubiri. Kwa hiyo, ninaagiza kwamba kati ya Jumatatu na Jumanne uwepo Mkutano wa Wadau na haya mambo yaishe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana. Mheshimiwa Benardetha Mushashu.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisharidhika nilikuwa ninazungumzia mambo ya mnyauko.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mchango wangu nilimshauri Waziri kwamba kutokana na matatizo yaliyoikumba Wizara yake takribani miaka mitatu, minne iliyopita ya kushindwa kudhibiti usambazaji wa mbolea, inapelekwa feki, kushindwa kudhibiti usambaji wa dawa kwa wakulima yanapelekwa feki, kushindwa kudhibiti usambazaji wa

mbegu zinapelekwa feki na mbaya zaidi mbegu ya *quton* nikasema aliizundua yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri lakini bado ameshindwa kudhibiti suala la vocha za ruzuku za pembejeo, zinachakachuliwa. Nikasema kwa sababu kilimo ndiyo mwajiri mkuu katika nchi yetu na wananchi wanaendelea kuwa maskini hatuwezi Bunge tukawa tunatenga fedha hapa halafu wakulima wanachakachuliwa katika maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikamshauri Mheshimiwa Waziri kwamba achukue hatua ya kujiuzuru kwa sababu amekuwa mzigo kwa wakulima. Hata hivyo katika hitimisho hakuna mahali ambapo amenipa majibu kwamba sasa anachukua hatua ya kuachia ngazi ili kilimo hiki kiendelee kuwa na tija na zaidi alichokifanya ni kulaumulaumu tu anasema ni kebehi, hatuwezi kuacha kukuambia maneno mazito Mheshimiwa Waziri wakati Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ndiyo Wizara ambayo ni kimbilio la wananchi wa Tanzania zaidi ya 80%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninamtaka na kwa kweli nitaondoa shilingi na nilimpa mfano wa Mchina ambaye alichukua hatua za kujinyonga kwa sababu alijenga daraja lisilo na kiwango ili asije akaenda kupigwa risasi kule China. Nikamuuliza yeye anasubiri nini wakati sisi tunataka Wizara hii iboreshwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba majibu kwa nini hachukui hatua ya kauchia ngazi vinginevyo mimi natoa shilingi na nitaomba Wabunge wenzangu na wakulima wote nchi nzima mnaonisikiliza kama kuna Wabunge hawataki kuniunga mkono muwaogope kama ukoma kwa sababu hawataki muishi kwa mapaenzi ya Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi majibu yangu ni rahisi tu kwamba mimi nilidhani ananishauri sasa nilisema hapo kwamba ukitoa ushauri kwamba Mheshimiwa Waziri nakushauri hivi ninaupokea sasa kama ananishauri, ushauri wa kuendeleza sekta naupokea lakini kama ni ushauri wa kusema ondoka, jiuzulu kwani sasa ndiyo sekta imekwenda mbele? Mimi nadhani kama alivyosema kuboresha utoaji wa pembejeo na kufanya haya ya kuboresha sekta, hayo mimi ninayakubali na wala siyakatai Mheshimiwa Lugola ni ushauri mzuri na kama ndiyo ushauri wako mimi ninaupokea huo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuniambia kwamba amepokea ushauri wakati ushauri wangu ni wa kuachia ngazi maana yake amepokea kuachia ngazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba anieleze ni lini sasa anaachia ngazi? Aseme lini maana amesema nimemshauri aachie ngazi amesema amepokea, sasa ninamtaka aeleze ni lini anaachia ngazi kwa ajili ya ustawi wa wakulima wetu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hili simkebehi, sina chuki naye, simtanii Bunge hili hatuwezi tukawa kila mwaka tunapiga kelele kwenye pembejeo mpaka hata maiti na marehemu na wenyewe wanakuwa na vocha za pembejeo. Kila mwaka tunapiga kelele hapa dawa feki, kuna mkulima wangu mmoja anaitwa Mussa Alfayo yuko pale Namhura alikuwa na dawa ambazo ni feki, zina *label* mbili za ku-*expire*…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lugola, subiri dakika moja tu. Kwa mujibu wa Kanuni ya 104 (1), ninaongeza muda wa dakika thelathini kama Kanuni zinavyoniruhusu, endelea.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima hawa wamekopa benki, wanalipia pembejeo matokeo yake wanafilisika. Leo Waziri hapa anabaki kuonyesha kitabu anamuonesha Mzee Cheyo kwamba tumetathmini, tumehakiki, hatuwezi kuendelea na lugha hizihizi, hatuwezi kuendelea na namna hiihii ya utendaji. Kwa hiyo, mimi kwa uchungu kabisa Wizara ya Kilimo, ni lazima tuwe na Waziri ambaye anakaba maeneo yote ambayo tunayalalamikia kila siku. Mbaya zaidi ambayo ni aibu utazinduaje mbegu ya pamba aina ya *quton*, mbegu ambayo haioti halafu bado uko ofisini, hii ni aibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi namuomba, suala tu la kuliambia Bunge kwamba amepokea ushauri wa kuachia ngazi halafu hatuambii ni saa ngapi au lini anachia ngazi ni kama ananipa majibu ya kunikejeli, ameliarifu Bunge amepokea sasa ni lina anaachia ngazi? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lugola asiniwekee maneno mdomoni, mimi nimesema nimepokea ushauri ule wa kujenga, hata nilipokuwa ninahitimisha hapo nilisema wale wote wanaotoa ushauri wa kujenga wote nimeupokea. Sasa hayo ambayo ninayapokea ni yale ya kujenga sekta. Sasa kama yeye anachotaka ni kingine huo siyo ushauri nilioupokea kwake ila ushauri wa kuendeleza sekta hii niko tayari hata na yeye na nikasema niko tayari hata kwenda kwake akiniambia hapa Mheshimiwa ulikosea tutashauriana, tutasaidiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo pia ninalikata mimi sikwenda kuzindua kule, mimi sidhani kama ananitendea haki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lugola, Waziri ameomba mkutane, umpe ushauri, umwelekeze sehemu alizokosea halafu utamuelekeza atajifunza, nakuomba ulikubali hilo, *please!*

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningekubali lakini ajue pia kwamba kuachia ngazi ni sehemu ya kuboresha, ni sehemu ya kujenga. Siyo kwamba kutoachia ngazi hajajenga anaijenga ile Wizara, anaitendea haki. Kwa hiyo, anaponiambia kwamba ni yale tu ya kujenga kana kwamba kuachia ngazi siyo kujenga mimi simuelewi. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Sasa unaondoa shilingi?

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mimi ninaondoa shilingi na ninaomba Wabunge na wakulima kule, nimeongea nao nimewaambia washike sehemu ya kifua kuonyesha kwamba maisha yao leo Bungeni hapa ni lazima wapate mwelekeo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wa kila mahali ninawaomba tusifanye mzaha na kilimo, ninaomba mnyanyuke mniunge mkono, ninashika shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lugola waliokuunga mkono ndiyo hao, mwacheni amalize kufafanua halafu mtachangia.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sikupata Mbunge hata mmoja wa CCM wa kuniunga mkono.

**MBUNGE FULANI:** Nkumba!

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Aaah, Nkumba.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Haya ninaomba hoja yangu tuendelee kujadili maana nimeungwa mkono pia na wenzangu wa CCM.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nkumba.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa masikitiko makubwa sana, naomba nikuambie Mheshimiwa Lugola mimi sikuungi mkono kabisa katika jambo hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, simuungi mkono kwa sababu kubwa mbili. Sababu ya kwanza katika kujenga hoja yake, anataka kutugombanisha sisi Waheshimiwa Wabunge na wapiga kura wetu. Yeye hakuwa anajenga hoja

zake, amejenga hoja zake kwa kutaka sisi Wabunge tugombane na wapiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba Mheshimiwa Kangi Lugola hawezi akawa msemaji wetu sisi kwa Wabunge ambao…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Anajadili nini wakati hajaunga mkono?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Tufuate Kanuni hajaunga mkono anajadili nini?

**MWENYEKITI:** Amesimama kama mlivyosimama ninyi, siyo lazima aunge mkono.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Haungi mkono halafu anajadili hoja.

**MWENYEKITI:** No, no, siyo lazima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Huo ndio utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kaa chini, *behave yourself.* Endelea Mheshimiwa Nkumba.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** We Halima unanitafuta mie wewe? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba hoja alizozijenga ni hoja za kutugombanisha na wapiga kura. Nataka niseme kwamba hawezi Mheshimiwa Lugola ndiye peke yake msemaji wa wakulima nchini. Sisi hapa tunawatetea wakulima katika mambo ya msingi, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, hivi yeye Mheshimiwa Kangi Lugola toka achaguliwe amekwishakamilisha yote ambayo aliwaahidi wananchi wa Jimbo lake? Kwa hiyo, suala la kumlazimisha Mheshimiwa Waziri ajiuzulu, uanze kwako wewe ujiuzulu kwanza Ubunge ndiyo uanze kuzungumza habari ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie, kazi ya Uwaziri siyo kazi nyepesi, kazi ya Ukuu wa Mkoa, kazi ya Ukuu wa Wilaya, kazi ya Ubunge siyo kazi nyepesi, ni kazi nyepesi kuja kumwambia mtu jiuzulu jipime na wewe mwenyewe una mambo mangapi ambayo uliwaahidi wananchi wako umewatimizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi siungi mkono na naomba kabisa hoja yake hii mimi ninaiita hoja dhaifu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lugola hitimisha hoja yako.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MWENYEKITI:** Kaeni chini.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ambayo nilikuwa nimeitoa siyo tu kwamba mimi ndiye nimekuwa msemaji wa wakulima nchi nzima, Wabunge wengi tu humu wamewazungumzia wakulima. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba mimi ndiyo nimewazungumzia wakulima peke yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili sijawagombanisha Waheshimiwa Wabunge pamoja na wapiga kura na kama mimi sijafanya kazi kwa wapiga kura wangu, wao ndiyo wanajua kama nimefanya au hapana na siyo Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nahitimisha hoja yangu, Makaburu walipitisha Sheria Bungeni ya kuwaua na kuwatesa watu weusi na walikuwa wengi sana lakini pamoja na wingi wao walifanya dhambi kubwa ya kuwaua na kuwatesa watu weusi. Kwa hiyo, siyo kila watu wengi wanapokuwa wanakataa kama ambavyo Mheshimiwa Said Nkumba anajaribu kusema, haimaanishi kwamba hoja niliyokuwa nimeitoa haina mashiko. Ni hoja yenye mashiko na mimi nitaendelea kusimamia kwenye shilingi yangu na nitakwenda kushindwa kwenye kura kwamba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika ameshindwa na amekuwa mzigo mkubwa kwa wakulima kusimamia sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niko tayari kushindwa kwenye kura lakini siko tayari kuondoa shilingi. Kwa hiyo, ili nitendewe haki ninaomba twende kwenye kura.

**MWENYEKITI:** Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Kifungu Kilichotajwa hapa juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002- *Finance and Accounts…........... Shs.1,442,002,700/=*

*(Kifungu Kilichotajwa hapa juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1003 – *Policy and Planning … ….. …. Shs. 1,838,813,900/=*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kasma 270200, *current grants to international organizations* ambayo mwaka uliopita wa fedha ilitengewa Sh.190,000,000/= mwaka huu wa fedha zimeongezeka mpaka Sh.360,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilipohoji kuhusu kifungu hiki nilielezwa kwamba ni kwa ajili ya kulipia ada za taasisi za Kimataifa za FAO na *IFAD*. Mwaka huu kwenye mkokotoo wa fedha hizi, inaelezwa kwamba ni kwa ajili ya kutoa fedha vilevile kwa taasisi moja inaitwa *ACT* kama sehemu ya sekta binafsi kwa ajili ya masuala ya kilimo cha hifadhi na masuala mengineyo lakini maelezo yana utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kupewa ufafanuzi ya sababu za hizi fedha kuongezeka kwa kiwango hiki na nini hasa hii taasisi inayoitwa *ACT* ambayo ni ya sekta binafsi inakwenda kufanya na sababu za msingi za taasisi hii kuwekwa peke yake kwenye jambo hili. Kama sitaridhika na maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri atayatoa, nitaomba kuondoa shilingi katika sehemu hii ili tujadili jambo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo kifungu kinasema kwamba ni michango kwa ajili ya taasisi za Kimataifa, pesa hizi zimeongezeka kwa sababu kifungu hiki pamoja na kulipa hiyo michango lakini pia kulikuwa na michango ya nyuma ambayo ilikuwa ni sehemu ya malimbikizo ndio sababu pesa hizo zimeweza kuongeza. Kama ungeweza kusoma kwenye randama yetu, utaona haya ndio maelezo ambayo tumeyatoa. Kwa hiyo, tusingekuwa na sababu ya kusema vinginevyo na hiyo *ACT* ambayo unaisema haikuwa sehemu ya *vote* hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninayo randama hapa, kwa hiyo, nimeisoma randama yote. Ningeomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu sijaridhika bado na asiponiridhisha kweli nitaondoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana niliuliza sikuambiwa hayo masuala ya madeni, nilitajiwa taasisi kwamba ni *FAO* na ndio maana nazitaja kwa majina, *FAO* na *IFAD*. Nielezwe katika hizi Sh.360,000,000/= *FAO* wanalipwa

ngapi, *IFAD* wanalipwa ngapi ili tusiuziwe mbuzi kwenye gunia, kusipenyezwe pesa kuelekea uchaguzi zisizoeleweka.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, sema hoja yako, wewe kila siku hoja yako ni ya uchaguzi tu?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hiyo ina msingi kwa sababu kuna mambo ambayo hayatolewi majibu. Kuna mambo yanafichika ndani ya bajeti ya safari hii.

**MWENYEKITI:** Kaa wewe!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kama hamna jambo la maana hizi fedha zipelekwe kwenye miradi ya vijana ya kilimo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, nilishakuambia ukae, Waziri ndio anajibu sasa.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, usiogope Jimbo lako, wewe kajipange vizuri tu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikiri tu ile *ACT* ni *Agricultural Council of Tanzania*. Ile *ACT* ni *NGO*, miaka ya nyuma tuliitengea katika kuijengea uwezo, mwaka huu tumesema yenyewe inasimama *on its own*. Kwa hiyo, hata kama imeingia kwenye randama itakuwa imeingia tu kimakosa yenyewe haipati *subvention* lakini kwa mashirika haya ya *IFAD,* fedha za *IFAD* ni Sh.160,000,000/= na *FAO* ni Sh.200,000,000/= kwa hiyo, ukijumlisha zitakuja hizo Sh.360,000,000/=.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru Mheshimiwa Waziri alichokieleza ni tofauti na Naibu Waziri angalau maelezo ya Mheshimiwa Waziri yanaridhisha kidogo kuliko ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumkumbusha Mheshimiwa Naibu Waziri maneno ya Baba wa Taifa kwenye jambo hili.

**MBUNGE FULANI:** Aaaah!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kwa maana moja sasa hatuna Serikali, tuna Mawaziri tu, Serikali ni timu na timu halisi ina dira na rubani. Mkusanyiko wa

Mawaziri bila mwelekeo, bila mwongozo, bila mshikamano, bila uongozi, kila Waziri na lake hauwezi ukaitwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu ni mpya akazingatia uwajibikaji wa pamoja na aka-*consult* na Waziri wake katika mambo ambayo yanahitaji ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nairudisha shilingi.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 - *Agriculture Training Institute*……Tsh.7,768,934,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pareso!

**MHE. CECILIA D. PARESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika kasma ya 220800 kuna kifungu cha *training domestic* na kama sitaridhika nitatoa shilingi. Nilikuwa naomba maelezo ya kutosha fedha hizi zimetengwa kwa nini kwa sababu ongezeko ni kubwa ukilinganisha na mwaka jana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ukiangalia mwaka uliotangulia utaona kwamba tulikuwa na fedha kubwa zaidi kwa maana tulikuwa na karibu shilingi bilioni 4.7, mwaka uliofuata zikapungua zikawa shilingi bilioni 2.7 na mwaka huu zikaongezeka kwa maana ya kuwa shilingi bilioni 3.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hizi zinaongezeka kwanza ni kwa ajili ya kugharamia mafunzo ya Vyuo vya Kilimo pamoja na mafunzo ya muda mfupi kwa waajiriwa wapya na mafunzo ya vitendo kwa ajili ya wanafunzi. Pia tunaongeza udahili kwenye vyuo vyetu na mahitaji kimsingi hayabaki palepale. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba *figure* hiyo inakuwa inaongezeka. Kama mwaka jana hatukupata maana yake linakuwa ni suala la kibajeti, tunapoomba zaidi tukapata hivi na hata tulipokuwa tumeomba tulikuwa tumeomba kiwango kikubwa zaidi lakini tukaweza kupata hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema na wote mmesema kwamba vyuo vyetu vipo katika hali mbaya. Pesa hizi zinazokwenda kwenye mafunzo wakati mwingine wanafunzi wamekuwa wanataka kukosa vyakula, wanafunzi wanashindwa kwenda kwenye mafunzo ya vitendo, kwa hiyo, kimsingi tukihoji

hizi pesa na kwa maana kwamba Wabunge wakiwa na wazo kwamba wazipunguze maana yake tunataka tuhakikishe kwamba vyuo vyetu vinaendelea kuwa na uwezo mdogo kwa ajili ya kutoa mafunzo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pareso!

**MHE. CECILIA D. PARESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasikitika majibu hayaridhishi kwa sababu ukisoma randama wametoa mchanganuo pale na Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba kasma hii ni kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi na mafunzo kwa vitendo. Ukienda kwenye mchanganuo wa kasma *tuition fee* ya haya mafunzo anayoyasema ni Sh.1,263,000/= lakini *accommodation* ni Sh.2,625,000,000/= halafu ukienda kwenye *training allowances* ni Sh.606, 714,000/= lakini unaenda kwenye *training materials* Sh.320,000/=, *training aids* Sh.28,000,000/=, *hiring of training facilities* Sh.1,400,000/=. Sasa ufafanuzi huu unakinzana na maelezo yako ya muda mfupi na muda mrefu, *accommodation* hii ni ya namna gani ambayo inagharimu Sh.2,625,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitaridhika nakusudia kutoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Waheshimiwa Wabunge watajenga tu picha kwamba kila kinachokuja hapa hakina maana lakini ukweli ni kwamba tunataka kujenga uwezo wa vyuo vyetu kwa maana ya mafunzo zaidi ndio maana pesa hizi zinaongezeka, lakini pia tumesema pesa hizi kimsingi hata hizi tunazoomba bado ni kidogo. Unaposema Sh.2,000,000,000, hivi fikiria vyuo vyetu tulivyonavyo na kwamba unalipia kwa maana ya vyakula, hela hizi haziwezi zikawa zipo nyingi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anaweza kuamini. Pia kuna vyuo vingine vipya ambavyo kwa kipindi kilichopita havikuchukua wanafunzi kwa mfano Chuo cha Mbondo ambacho kipo Kasulu lakini mwaka huu tunataka tufanye utaratibu kwa maana ya kwamba tukiongezee pesa ili kiweze kuchukua wanafunzi kwa maana hiyo ile nia ya kuongeza wataalam iweze kutimia. Hata hivyo kama Wabunge watajenga picha hiyo maana yake hata nia njema ya Wizara pote wanapoona watakuwa wanahoji kwamba ni jambo ambalo sio zuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pareso!

**MHE. CECILIA D. PARESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi. Tupo hapa Bungeni kwa ajili ya kuuliza na kupata ufafanuzi lakini majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri anasema ni kwenda kujenga uwezo wa taasisi na kulipia chakula, sasa kwa nini kuna *accommodation* ya Sh.2,625,000,000/=?

Ndio hiki ambacho tunauliza. Kama yangeelezewa masuala ya kujenga uwezo wa taasisi sawa lakini haimo kwenye randama na hii randama ni ya Wizara yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kuna jibu lolote *sundries, accommodation,* chakula, hospitali, jazeni tu humo. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, timu ilizunguka na hata Kamati kwa kumbukumbu zangu, wamezungukia vyuo vyote vya Kilimo na taarifa waliyoileta ni kwamba vipo katika hali mbaya kwa kila hali, kwa majengo, *training* na kadhalika. Hiki Chuo alichosema cha Mbondo kimeshindwa hata kudahili, bado wapo nyuma kwa sababu hata maeneo ya kuwaweka wale wanafunzi hayapo. Sasa tukisema kwamba hizi hela ni nyingi na mchangiaji mmoja namkumbuka sijui ni nani alikuwa anasema *training institute* hizi lazima tutenge hela kwa ajili ya ku-*train* na wanafunzi wapewe hela za vitendo, nashangaa tena wanajipinga wao kwa wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nadhani maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri ndio *valid* na tusipoziweka vyuo vingine vitashindikana. Natoa sasa mchanganuo. *Accommodation* (chakula) 2,600,000,000/=, kulisha wanafunzi shilingi bilioni mbili sio hela nyingi sana kulisha wanafunzi wote. *Tuition fees* 1.63 bilioni, *training allowances* maana lazima uende kwenye *field practical three hundred and twenty*, tena hizo hata hazitoshi inabidi tuwabinye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu Mheshimiwa Pareso akubali, angekuwa ni yeye ange-*operate* katika mazingira magumu. Mbona mara nyingine mnaenda kuwaambia *UDOM* kataeni hamlipwi, hamlipwi leo tunataka tutenge ili watu wasome sasa mnasema haiwezekani tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Pareso akubaliane na mimi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pareso, kuna *rehabilitation*, kuna mambo mengi ambayo *accommodation* inabeba vitu hivyo. Kwa hiyo, mimi nafikiri ungekubali yaishe tu. Mheshimiwa Pareso! *(Makofi)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia maelezo yanajichanganya ya Manaibu Waziri na Waziri.

**MBUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Ni haki yangu kusema, naomba Waheshimiwa tuvumiliane kama tunavyowavumilia, mnyamaze!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa muacheni mtoa hoja aendelee na hoja yake.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mchanganuo wa kasma hii, *tuition fee* 1,200,000, ni watu wangapi? *Accommodation* ni Sh.2,000,0000,000/= na kitengo ni *Agricultural Training Institutte, which means* labda ni chuo au kitengo kimoja. Sasa hapa kuna mchanganyiko, huku mnaeleza mnataka kujenga uwezo wa taasisi, mafunzo ya muda mfupi ndio maana tunasema haturidhiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono kwenye suala hili, natoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko!

**MHE. ESTER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni dhahiri kweli tunataka tupate Wakufunzi na Wataalam wengi lakini tunachohoji hapa, hatuhoji idadi ya hela, tunahoji mchanganuo halisia. Kwa sababu haiingii akilini mtu anakwambia kwamba *training domestic 3.62 billion* ambapo anakuambia *accommodation is 2.6 and then tuition fee 1.2 million not billion*? Ndio maana tuna-*raise* hoja hii, kuna nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu ukiendelea wanakuambia *hiring of training facility is 1.4 million, so even the hiring of training facility is higher* kuliko *tuition fee. So, tuition fee* hii ni kwa wanafunzi wangapi? Hatujaishia hapo! Ukiendelea anakwambia *the training allowance is 600,000,000 rationale* hapa ipo wapi? *Rationale* hapa haipo! Sawa mnasema mtajenga majengo na nini kama utalipa *tuition fee* ya 1.2, ukaweka *training allowance* ya 606,000,000, ukaweka *training aids* ya 28,000,000/=, sasa kama utamwekea *training aids* ya shilingi 28,000,000/= na *tuition fee 1.2 millions,* jamani! Watu wengine tumepita kwenye hizo *institution* tunaona kama ni kitendawili, tufumbulieni tuelewe, ndio hilo tu! Tunataka hela ziende nyingi sio kwamba hatutaki lakini mfumbue ieleweke tujue hela zinaenda wapi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko muda wako umekwisha, Mheshimiwa Ester Bulaya!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hapa wote ni Wabunge na sisi wote hapa ni viongozi. Mimi namheshimu sana wajina wangu kwa sababu tunatoka wote kule nyumbani, namheshimu sana na Mheshimiwa Pareso. Hivi kweli ni majibu gani mnayoyahitaji zaidi ya aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, yapi!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuwa tunalalamika hapa kwamba sekta ya kilimo ipo nyuma, leo fedha zimetengwa kwa ajili ya kwenda kusaidia katika hivyo vyuo ambavyo vinatuletea wataalam ili waende kuwafundisha wakulima wetu huko ambao wanalima kilimo ambacho sisi tunataka walime kilimo cha kisasa.

**MBUNGE FULANI:** Hujaelewa.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Taarifa!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Kaa chini.

**MWENYEKITI:** Kaa chini.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Kaa chini mimi sio saizi yako!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali kaa chini.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Tunapoteza muda bure. Hivi hapa tunachokihitaji hapa ni nini? Mheshimiwa Waziri ametoa majibu ya kutosha kuhusiana na hizo fedha zinaenda kufanya kazi gani katika vyuo ambavyo tunahitaji sisi wataalam? Amesema kwamba kulikuwa na fedha kwa ajili ya Kamati ambazo zimezungukia katika hivyo vyuo vingine, ndio hiyo *accommodation* ambayo tunaisema, sasa tunataka nini tena? Ni sawasawa na mtoto anaomba chakula unampa anasema hiki akina chumvi, kachukue chumvi mwenyewe uweke!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Huvisa.

**MHE. DKT. TEREZYA P. L. HUVISA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Mimi naamini kabisa mawazo aliyotoa Mheshimiwa Waziri ni sahihi kwa sababu tunaona kabisa hii ni *agricultural training institute* na siku hizi ada mara nyingi kuna kuchangia na kuna *sources* nyingi za ada lakini *accommodation* wanafunzi wengi wanakuwa wanalala pale na unaweza ukakuta mabweni yetu miaka mingi sana yanakuwa hayajahudumiwa. Kwa hiyo, hizi pesa moja kwa moja zinaenda ku-*rehabilitate* hizo *accommodation facilities* kwa hiyo, hela nyingi zitatakiwa. Ahsante! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pareso. Hitimisha hoja yako.

**MBUNGE FULANI:** Hakuna *rationale* hapo kwenye uchangiaji.

**MWENYEKITI:** Jamani mimi ndio ninayepanga watu hapa kwa mujibu wa Kanuni.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hata baadhi ya wachangiaji hawakuelewa *concept* iliyopo ni nini. Kwa sababu tunachohoji hiyo *tuition fee* iliyopo Sh.1,263,000/= kwa mwaka inahusiana vipi na *accommodation* ya Sh. 2,625,000,000/= kwa mwaka na kwa wanafunzi wangapi? Ndio tunachouliza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pareso tumekubaliana itakwenda kuchambuliwa tena kwenye bajeti hiihii.

**MBUNGE FULANI:** Mmekubaliana saa ngapi?

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Tupate kauli Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Kuna mtu yeyote upande wa Serikali, Waziri! Machali kaa chini!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee yale niliyoyasema hapo mwanzoni na kabla sijaenda huko naomba nijaribu kutoa ufafanuzi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala tulilozungumzia mwanzoni kabisa maana naona kuna *concept* sasa ndio unataka kuileta. Kwa mfano, kule mwanzo tulipokuwa tunazungumzia mtoa huduma nyie mkajua wakati mwingine ni mmoja wakati mtoa huduma anaweza kuwa ni *consultant* ana timu kubwa, sasa anazungumzia *concept* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa narudi hapa, nimeeleza kwamba kwenye vyuo vyetu hivi chakula peke yake ni 2.6, *tuition fee* ni 1.63 *billions*…

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Sikilizeni basi, sasa mbona mnaniingilia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanafunzi wetu wanalipiwa na Serikali *perse*, hawajilipii wao wenyewe.

**MBUNGE FULANI:** Wangapi?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *field practicals* ndio fedha tumeweka hizo hapo.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tunalazimika ku-*hire* Walimu kutoka *SUA* kwa ajili ya kutusaidia katika vyuo vyetu kutokana na ufinyu wa bajeti na lazima watakapokuja tunawalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijajua hiyo *concept* inayokupa tabu leo hii kwamba tusiongeze fedha za kuwadahili lakini upo tayari kuwaambia watu wa *UDOM* kwamba mgome, mgome kwa sababu hamna hela, mimi siwaelewi kwa kweli.
*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea kwa sauti za juu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pareso, hitimisha hoja yako, *please!*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado maelezo ya Mheshimiwa Waziri hayajitoshelezi na yana mkanganyiko. Hapa sasa hivi anatoa maelezo kwamba kuna ku-*hire* Walimu hakuna maelezo ya ku-*hire* Walimu kwenye randama na randama ni ya Wizara yao hii hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uhusiano gani bilioni mbili inaenda kufanya nini wakati *tuition fee* ni 1,263,000/= halafu *accommodation* au *definition* ya *accommodation* ni nni, ni bilioni mbili, hili halieleweki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pareso bado unashikilia shilingi ya Mheshimiwa Waziri?

**MHE. CECILIA D. PARESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, meza hapa sio kocha ni *referee* ndio kazi nayofanya mimi hapa.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, *concept* haijaeleweka!

**MWENYEKITI:** Nikisimama mimi, wewe *sit down!*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Tunaingia kwenye *guillotine* sasa, kaeni chini.

**MBUNGE FULANI:** Tuhesabu kura! Randama iko tofauti.

**MWENYEKITI:** Machali kaa chini, wote kaeni chini.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Hamsomii vitabu.

**MWENYEKITI:** Machali nakupa *warning* ya mwisho.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Nipe hata tano.

**MWENYEKITI:** Uwe na adabu humu ndani.

Kif. 1005 – I*nternal Audit unit* …......................Tsh.282,177,200/=
Kif. 1006 – *Procurement Management Unit*..Tsh.727,145,300/=
Kif. 1007 – *Government Communication Unit*................................................Tsh.261,235,700/=
Kif. 1008 – *Legal Unit*…………….....................Tsh.354,789,400/=
Kif. 1009 – *Management Information Systems Unit* ....................................Tsh.216,780,400/=
Kif. 1010 – *Enviromental Management Unit*..Tsh.152,166,600/=
Kif. 2001 – *Crop Development*…………..Tsh.121,010,887,100/=
Kif. 2002 – *Agricultural Mechanization*……Tsh.3,969,728,100/=
Kif. 2003 – *Agriculture Land Use Planning and Management* ......................Tsh.713,615,500/=
Kif. 2004 – *Plant Breeders Unit*…………………..Tsh.181,129,800/=
Kif. 2005 – *Irrigation and Technical Services*…..……………Tsh. 0
Kif. 3001 – *Research Development*……..Tsh.16, 033, 397, 500/=
Kif. 5001 – *National Food Security*……….Tsh.112,136,328,400/=

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 05- Tume ya Umwagiliaji**

Kif. 1002 – *Policy and Planning* ………………Tsh.393,862,000/=
Kif. 1004 – *Legal Services Unit* …………………Tsh.74,410,000/=
Kif. 1007 – *Management Information System*

*and Database* .................................Tsh.130,000,000/=
Kif. 1008 – *Environmental and Social Management Unit* ……...................Tsh.307,400,000/=
Kif. 2001 – *Irrigation Planning Design and Privates* …….......................Tsh.9,121,212,000/=
Kif. 2002- *Irrigation Infrastructure Development* ……......................Tsh.16,023,682,000/=
Kif. 2004 – *Irrigation Operations and Support Service* ……...................Tsh.2,882,454,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika**

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ……………Tsh.7,669,352,000/=
Kif. 1004 – *Agriculture Training Institute*……Tsh.2,407,913,500/=
Kif. 1009 – *Management Information Systems Unit*….........Tsh.0
Kif. 2001 – *Crop Development* ……………..Tsh.5,405,377,500/=
Kif. 2002 – *Agricultural Mechanization* ……Tsh.7,899,685,600/=
Kif. 2003 – *Agriculture Land Use Planning and Mgt*…….................Tsh.8,500,000,000/=
Kif. 2005 – *Irrigation and Technical Services* ……………...Tsh.0
Kif. 3001 – *Research Development* …….Tsh.6,025,085,700/=
Kif. 5001 – *National Food Security* ………Tsh.9,172,855,700/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mjadala mkali, napenda kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limepitia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Fungu 43 – Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Fungu 05- Tume ya Umwagiliaji na kuyapitisha bila mabadiliko. Kwa hiyo, naomba makadirio haya sasa yakubalike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI - KAIMU WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo yoyote, naipongeza Wizara na Wabunge wote, yote yanayotokea humu ndani ni changamoto za Bunge na ndio Mabunge yote yalivyo. Kwa hiyo, naliahirisha Bunge mpaka Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.26 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 12 Mei, 2014 Saa Tatu Asubuhi)*